MPATANISHI

By richard MWAMBE

SURA YA KWANZA

April 1984

UKUMBI WA RAILWAY GEREZANI

"Ina maana unafurahia kwa ushindi wake?"

"*Of course yes!* Jamaa anapiga ngumi za kilo nyingi, yaani kamtwanga Kibwana mpaka

kamwacha na meno ishirini na nane…”

“Na uhai kamwondoa!”

“*What?* Unasemaje wewe?”

“Ndiyo maana nikakuuliza unafurahia ushindi wake?”

Badala ya kujibu swali lile

MPATANISHI

By richard MWAMBE

Stella aliamua kuinuka na kutoka nje ya ukumbi huo uliosheheni watu waliokuwa wakishangilia kwa kelele na mbinja zenye kukera masikioni mwa wasiopenda. Ijapokuwa alipata upinzani mwingi kupita katikati ya mashabiki hao wa mchezo wa ngumi, mwishowe alifanikiwa kutoka kabisa na kujikuta nje. Baada ya kujikuta nje akagundua kuwa hana pa kwenda zaidi ya kusimama na kushangaa magari

yapitayo kutoka Kurasini kwenda Shule ya Uhuru.

“Stella! Stella!” sauti ya kiume ikasikika nyuma yake ikiita kwa mbisho. Stella hakugeuka nyuma zaidi ya kuikusanya mikono yake kifuani na kutulia kimya kabisa.

Mtu mzima, ambaye ngozi ya mashavu yake tayari ilianza kujikusanya na kufanya makunyanzi alisimama kando ya binti huyo. Hakuwa mtu mzima bali msichana mwenye kadiri ya

miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi.

“Sasa kilichokutoa nje ni nini?” kule mtu mzima akauliza.

“Sasa si pambano limeisha, nikae nifanye nini?” Stella akajibu.

“Sidhani kama umetoka kwa sababu hiyo!” Yule mtu mzima akaonesha shaka.

“Mzee taksi, twende!” dereva wa taksi alimwita mzee huyo kwa sauti kwa kuwa yeye alikuwa

upande wa pili wa barabara ile. Gari yake aina ya Volvo ilikuwa bado inaunguruma.

“Tuondoke na hii….” Yule mtu mzima akamwambia Stella. Msichana huyo hakujibu zaidi ya kubetua mabega ‘sitaki’.

“Tunapanda UDA, sasa hivi litakuja…”

“Utapandaje UDA na mimi nipo? We ni malkia wangu watakiwa kutumia kebu mama kufika kwako…”

“STAKI EH!” Stella akajibu kwa sauti ya juu wakati huo tayari watu walikuwa wamezagaa kila upande nje ya ukumbi huo, wakitoka kushuhudia pambano la ngumi kati ya Joseph Marwa na Kibwana Mtwana. Pambano hilo lililokuwa gumzo katika kona za Jiji la Dar es salaam lilimalizika kwa raundi tatu tu baada ya Kibwana Mtwana kupigwa kwa K.O. Kila aliyetoka alikuwa akizungumzia mchezo huo. Dakika chache za ukimya

zikamfanya Stella na yule bwana wajikute mbele ya basi kubwa jekundu lenye maandishi 'UDA' ubavuni mwake. Basi hili aina ya Leyland lilimeza watu wa kutosha akiwamo Stella na yule mtu mzima.

Safari nzima ilikuwa ni ya ukimya kati ya wawili hawa, zaidi ya mazungumzo ya abiria wengine walikuwa wakisikia mlio mkali wa basi hilo. Haikuchukua muda kufika katika kituo cha

Shule ya Uhuru, wakateremka kwa kuwa safari ya basi hilo iliishia hapo.

“Tunaelekea wapi?” Yule mtu akamwuliza Stella.

“Ukitaka tuelewane nipeleke DDC Kariakoo nikacheze muziki wa NUTA,” Stella akamwambia mshikaji wake huku akiweka sawa nywele zake alizochoma mchana wa siku hiyo.

“DDC hakuna NUTA leo! Twende Mlimani Park tukaburudike,” akamwambia.

“Aaaaaa sawa!” Stella akakubali, wakavuka barabara na kuingia katika taksi iliyokuwa mbele yao, nayo ikaondoka kwa kasi. Yule dereva akafungu droo katika dashboard ya gari hiyo na kuchomoa bahasha ya khaki, akam[atia mtu huyo. Yule mtu mzima akashangaa kabla ya kuipokea.

“Yangu?” akauliza.

“Ndiyo! Yako”.

Yule mtu mzima akaipokea na kuigeuza, upande wa juu ilikuwa imeandikwa *‘ON TANZANIA GOVERNMENT SERVICE’* na pembeni yake karibu na kona ya kuia juu iligongwa mhuri wa rangi ya zambarau wenye neno moja tu la Kiingereza, *‘CONFIDENCIAL’*.

Akaichukua na kuifutika ndani ya koti alilovaa, kisha akashusha

pumzi ndefu na kujiegemeza katika kiti cha nyuma, akauinua mkono wa Stella na kuuweka juu ya paja lake.

“Bora umenilipa pesa zangu!!!” Yule mzee akamwambia dereva mara baada ya kuona Stella akitaka kumtwanga swali, akamkatisha na tayari akawa amempa jibu kwa swali lake.

“Mzee unafika wapi?”

“Mlimani Park!” akajibu.

“Unaonaje nikikupeleka Magomeni Lango la jiji?”

“Kuna nini?”

“Kuna taarab ya JKT inapiga pale…”

“Aaaaaaaa! Ewe njiwa, ewe njiwa, peleka salaamu…” Mtu mzima akamalizia.

Muda wote wa mazungumzo kati ya dereva huyo na Yule mtu mzima, Stella alikuwa kimya kabisa huku mkono wake ukiwa juu ya paja la mzee huyo. Ile

Peugeot ikasimama mbele ya mlango mkuu wa ukumbi huo maarufu katika jiji la Dar es salaam.

"Twende mrembo wangu," akamwambia Stella.

"Mzee!" Yule dereva akaita na mtu mzima huyo akasogea karibu, akainama kidogo kwenye usawa wa kioo cha mbele upande wa abiria.

"Kaa meza ile ile ya siku zote!" akamnong'oneza kisha akaondoa

gari kwa kasi na kumwacha mzee huyo akiwa kasimama pale pale.

“Inaonekana unamjua vyema kijana huyu,” Stella akamwambia mzee huyo mara baada ya kufika pale aliposimama.

“Ah! Ni mdeni wangu,” akamdanganya kisha akamkamata kiuno na kuingia naye katika ukumbi huo uliofurika watu.

Ukumbi huo ‘ulitapika’, wasemavyo watoto wa mjini, taarabu ya JKT ilikuwa

ikitumbuiza huku watu wakijipatia vinywaji na mishikaki. Stella aliketi katika moja ya viti vimgi ndani ya ukumbi huo na kufuatiwa na mzee wake. Kidogo tu, mhudumu aliwafikia na kuwasikiliza na baada ya maagizo wakaletewa vinywaji. Huyu mtu mzima hakuwa na utulivu hata kidogo, macho yaliyofunikwa na kofia ya *'Mungu Usinione'* yalikuwa yakiutalii ukumbi ule. Stella alikuwa akiburudika na muziki huo laini huku akinywa kinywaji

chake taratibu na huku akifuatisha maneno matamu ya wimbo huo kila apumzikapo.

“Mbona hutulii?” Stella akamwuliza mtu mzima.

“Aaaa nimebanwa kidogo…”

“Si uende chooni” Stella akashauri na Yule bwana akashukuru moyoni kwani alitaka kufanya hivyo muda mrefu isipokuwa alikuwa akimwogopa msichana huyu mrembo.

Stella alikuwa msichana mbembe, alipenda wazee na watu wazima wenye pesa, penzi atakupa ilimradi tu ushikishe kibunda chake. Kwa mzee huyu alinasa, pesa iliyotakata aliipata, hakuwa na shida na mabwana mengine zaidi ya zee lake hili. Mapenzi aliyopewa mtu mzima huyu yalimfanya asahau shida na familia yake. Alibebwa, akaogeshwa, akapet-petiwa na kufanyiwa kila aina ya mahaba, akaridhika.

Mwanamke si ndiyo huyu! Akajisemea kila alipomtazama akiwa kama alivyozaliwa. Kutokana na haya yote, mtu mzima huyu hakuwa na kauli juu ya ratiba yake ya maisha, akiamuliwa hivi hufuata, akiamuliwa vile hutii. Mara hii alipewa bahasha ya kikazi, lakini alijikuta akishindwa hata kutafuta nafasi ya kuisoma kwa kumwogopa Stella. Mtu mzima akatabasamu na kuvuta hatua kuelekea choo cha wanaume.

Ndani yake, akajifungia, akapachika mkono wake ndani ya koti na kuitoa ile bahasha, akaigeuzageuza na kuichana kisha akaisoma taratibu sana. Haikuwa na maandishi mengi isipokuwa machache ambayo yalichapwa kwa mashine ya kupigia taipu ya Oliveti. Alitambua hata upangaji wa maneno na kujua kuwa mwenye mtindo huu si mwingine zaidi ya Fatuma Beka ambaye alikuwa akifanya kazi katika afisi

ya Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa.

'Ikukutapo bahasha hii, fika Lango la Jiji,

meza ya kwenye kona kushoto mwa ukumbi,

Ukitakiwa kusoma gazeti, sema ndiyo, kisha soma kurasa ya 11'

'D'

Asante

Kijasho chembamba kikamtiririka, akaikunja ile

karatasi na kuitia kinywani, akajiweka sawa na kuifutika bahasha katika mfuko wa nyuma wa suruai yake ya dengiriz kisha akatoka nje. Alipopiga jicho katika meza aliyomuacha Stella, hakumuona.

Kaenda wapi? Akajiuliza kisha akasonya na kupiga hatua nyingine kadhaa mpaka katika ile meza, alichokikuta ni chupa yenye bia nusu, basi. Tayari kwa kutoweka msichana huyo, mtu

mzima akasahau majukumu ya kikazi, akaketi katika kile kiti na kutulia kimya kwa nukta kadhaa. Alipokumbuka barua ile imemwambia akakurupuka kama mbwa aliyefurumushwa sehemu, akaiendea ile meza na kuketi.

Dakika chache tu, mhudumu wa baa hiyo akamsogelea na kumsabahi.

“Karibu sana, kinywaji gani?” akauliza.

“Pilsner tafadhali…”

“Unapenda kusoma gazeti?”

“Yap,” akajibu na Yule mhudumu akapotelea.

Mtu mzima Yule aliendelea kuzungusha macho yake huku na kule kama atamwona Stella, hakumwona, akasonya na kupiga ngumi mezani.

“Vipi kaka?” akashtushwa na sauti kutoka nyuma yake, kabla hata hajageuka mgeni huyo akajikaribisha mwenyewe na

kuketi katika kiti kilichokuwa mbele yake, wakatazamana.

“We n’nani?” mtu mzima akauliza.

“Huna haja kujua, ila nilitaka kukujulisha tu kuwa kasichana kako nimekachukua na ninakwenda kukahifadhi mpaka utakapokaidi kazi utakayopewa,” yule kijana akamwambia mzee huyu. Macho makali yam zee huyu yalimtazama yule kijana kwa nukta kadhaa.

“Unamjua unayemwambia maneno hayo na kujitamba mbele yake kuwa umemchukua msichana wake?” akamwuliza.

“Sina haja ya kumjua!” Yule kijana akajibu.

“Sawa, basi nimesikia, mchukue huyo msichana… kwa taarifa yako, maisha yako hayana thamani kama msichana huyo…”

“Bullshit!” yule kijana akang’aka na kuinuka, kisha akaanza kuondoka.

“Unasikia kijana, kama hujawahi kunisikia, mimi ndiyo Chameleon!” akamwambia, na wakati huo huo Yule mhudumu akawa tayari amefika na kumwekea gazeti mezani. Chameleon akamtazama kijana Yule akipotelea kwenye kundi la watu huku akielekea mlango mkubwa. Haraka akanyakua lile gazeti na kuelekea upande wa chooni huku akiacha kinywaji chake bila kukigusa.

* * *

Nje ya ukumbi ule kulikuwa na magari mengi sana yameegeshwa huku na huko, walevi na wanaouza miili yao walikuwapo pia. Yule kijana alipotoka tu ndani ya ukumbi ule akayapita magari kadhaa na kuingia ndani ya *Volks Wagen* moja jeupe, *Transporter*. Katika kiti cha mbele, kushoto, akaketi, kisha akageuza uso wake nyuma na kutazama.

“We are going for honeymoon baby!” akamwambia Stella.

Stella hakuweza kujibu chochote kutokana na gundi la plastiki liliobandikwa midomoni mwake, miguu yake na mikono vilifungwa kwa kamba katani. Hakuwa kwenye kiti, kwani gari hiyo ilikuwa na viti viwili tu, cha dereva na abiria wake mmoja. Kila alipojaribu kujikukurusha hakufanikiwa kwani mfungaji wa

kamba zile aliijua vyema kazi yake.

“Let us go!” akamwambia dereva naye akaliondoa lile gari kwa kasi mpaka watu wa nje wakaanza kupiga kelele. Akiwa katika mwendo huo, kabla hajamaliza kuupita wigo wa ukumbi ule, Yule dereva akakanyaga breki na gari ikasimama ghafla.

“Vipi?” Yule kijana akamuuliza dereva.

“Kuna mtu mbele!” dreva akajibu ndipo yule kijana.

Naye alipotazama vizuri, kweli, akaona mtu aliyesimama katikati ya barabara akiwa na koti refu la rangi ya chai ya maziwa akiwa amejishika kiuno, kichwani mwake alikuwa kavalia kofia ya *Mungu Usinione*.

“Mgonge!” akamwabia. Yule dereva akaiondoa tena ile gari kwa kasi kwa minajiri kumpamia Yule mtu lakini ghafla lile gari

likayumba na kugonga nyumba iliyokuwa pembeni mwa barabara. Chameleon akashusha mkono wake wenye bastola kubwa aina ya *Revolver*. Kishindo kilichosikika kilifanya watu waanze kukimbilia eneo lile kujua kulikoni.

Ndani ya gari yule kijana akamtazama dereva wake na kumkuta akiwa na jeraha baya kabisa la risasi kisogoni mwake. Tayari watu walikwishajaa katika

eneo lile, Chameleon alijichanganya na kufanikiwa kulifikia lile gari lakini zaidi ya mwili wa yule dereva hakuona mtu mwingine. Vurugu za watu zikamfanya atoke haraka eneo lile na kusimama kando akitazama huku na kule kama atamwona yule kijana au Stella.

Amenizidi akili! Akawaza kisha akavuta hatua na kuvuka barabara mpaka kwenye moja ya kibanda cha simu, akaingia na

kuchukua lile gazeti, akalifungua ukurasa aliotakiwa kusoma. Hakukuwa na kipya zaidi ya makala ndefu iliyojaa upande huu mpaka ule. Makala ile ilikuwa ikizungumzia juu ya kilimo cha kisasa kilichoanzishwa na walowezi huko Rhodesia. Akapitisha macho na kuhesabu maneno machache ambayo yalikuwa ymezungushiwa miduara kwa kalamu nyekundu. Kichwani mwake akayakusanya maneno yale ambayo

yamezunguziwa na kuyaunganisha kwa akilia yake na kupata sentensi kamili.

Kamati ya mapatano itakutana jijini Harare kesho.

Fika bila kukosa katika Hoteli ya Zim maagizo utayakuta hapohapo.

Baada ya kuunganisha maneno yale, akapata ujumbe huo.

Rhodesia! Akawaza.

Niende Rhodesia au nimtafute Stella? Akajiuliza bila kupata jibu.

'Huna haja kujua, ila nilitaka kukujulisha tu kuwa kasichana kako nimekachukua na ninakwenda kukahifadhi mpaka utakapokaidi kazi utakayopewa," alipoikumbuka kauli hii aliyoambiwa na yule kijana, akameza funda kubwa la mate.

Ina maana huyu kijana alikuwa anajua juu ya kazi hii kabla yangu? Akajiuliza.

Anachotaka nisiende Rhodesia ndiyo anipe Stella wangu, huu

mtihani! Akatia shaka moyoni. Alipoinua saa yake na kutazama, ilimwonesha kuwa ni saa nne za usiku. Na mara hiyohiyo ile simu pale kibandani ikaita. Si kawaida kwa simu za vibandani kuita, kawaida hutumiaka kwa kupiga tu. Chameleon, akageuka na kuitazama, kisha akainyakua na kuiweka sikioni bila kuongea lolote.

Usipokaidi namkata kichwa, na kitakachotokea Rhodesia hutoamini,

na serikai yako itapoteza matumaini na wewe!

Go or do not go…. Is up to you!

Ile simu ikakatika na kumwacha mzee huyu akiwa kaduwaa hajui nini cha kufanya. Akatoka ndani ya kile kibanda cha Post na Simu na kuingia mitaani. Mtaa kama wa tatu hivi akachukua taksi na kumtaka dereva amfikishe Kawe Mzimuni. Chameleon akamlipa dereva huyo kisha akasubiri aondoke, ile

taksi ilipopotea kabisa, ikapita gari nyingine *Ford Angria* kwa mwendo wa taratibu kabisa na kwenda zake. Hatua chache zikamfikisha katika nyumba yake kubwa aliyoijenga miaka kadhaa nyuma. Ndani ya nyumba hiyo alimkuta mkewe akimsubiri sebuleni huku akisikiliza kipindi cha Lala Unono kutoka RTD.

"Karibu mume wangu!" akamkaribisha. Mzee huyo

akajitupa kochini na kushusha pumzi ndefu.

“Vipi, nikuandalie maji uoge?”

“Hapana, muda umenitupa mkono, nahitaji kusafiri usiku huu kuelekea Rhodesia, vipi umesikiliza kipindi cha ATC Hewani?” Chameleon akamuuliza mkewe.

“Eh! Mume wangu safari tena, si juzi tu ulikuwa Misri? Unakumbuka kuwa keshokutwa

ni kumbukumbu yetu ya ndoa?" Mkewe akmwuliza.

"Najua, lakini nitafanyaje nawe unajua kazi zangu! Nijibu basi…"

"Nimesikiliza, ndege ya nje ipo inayokwenda hapo hapo Rhodesia!" Yule mama wa Kizigua akajibu.

Chameleon akiendea simu mezani, akavuta kiti na kuketi, akinua mkonga wa simu ile na kukoroga namba kadhaa kisha

akweka sikioni. Simu ile ikapokelewa na opereta wa idara ya Posta na Simu.

"Naomba niunganishe Uwanja wa Ndege tafadhali…" akamwambia opareta yule.

"Subiri kidogo!" akajibiwa.

Sekunde kama thelathini hivi akasikia sauti ya kume ikiita na kutambulisha kuwa hapo ni Uwanja wa ndege.

“Nahitaji usafiri wa kufika Rhodesia usiku huu…” akamwambia.

“Nafasi ipo, lakini ndege inaondoka dakika tisini zijazo…” mtu wa upande wa pili akajibu.

* * *

Dakika kumi kabla ya ndege ile kuondoka, Chameleon alikuwa mtu wa mwisho kuketi kitini, akafunga mkanda tayari kwa safari hiyo ya dharula. Mpaka dakika hiyo alikuwa akijua tu

kuwa anakwenda kwa ajili ya mkutano wa kamati hizo. Ulikuwa mkutano muhimu sana kati ya Serikali ya Tanzania na Makaburu kutoka Afrika Kusini. Mkutano huu ulipangwa kufanyika katika Jiji la Harare nchini Rhodesia na wajumbe wa pande zote mbili walitakiwa kufika siku hiyo.

Masikini Stella wangu! Akajiwazia wakati ndege ikiwa inakaa sawa angani.

Wacha nifanye kazi kwanza, na nikirudi watanikoma kama watakuwa wamemuua! Lakini wana uhusiano gani na kazi hii ninayoifanya na wamejuaje kama mimi ninatumwa huko? Maswali mengi yakampitia kichwani mwake asipate jibu. Muziki wa Kilwa Jazz ulikuwa ukitumbuiza kwa sauti ya chini, hakuna aliyekuwa anaongea, wengine walionekana kusinzia na wengine kusoma vitabu ili mradi tu kuifanya safari hiyo kuwa fupi.

SURA YA PILI

RHODESIA…

Usiku wa saa tisa Chameleon aliwasili jijini Harare kwa ndege ya hiyo kubwa ya ATC. Moja kwa moja akapitia katika vitengo vya ukaguzi na kuhakikisha kamaiza vyote. Akatoka nje ya uwanja huo na kuingia msalani,

huko alichukua dakika kama tatu hivi na kujibadili muonekano kidogo, kisha akatoka nje na kuingia katika taksi tayari kwa safari ya mjini.

Hoteli ya Zim ilijengwa nje kidogo ya Jiji la Harare, ilipendwa na watu wote ambao hawapendi kuishi karibu na mjini. Hakuwa yeye ameichagua hoteli hii bali ujumbe ule alioupata ulimwelekeza hivyo. Ndani ya taksi aligubikwa na mawazo

mengi sana, mojawapo ni kuwa ‘vipi kama jamaa wale wanaoijua safri yake pia wanajua hoteli atakayofikia?’ jambo hili lilianza kumtia wasiwasi. Kila alipojaribu kulifukuza kichwani mwake bado lilimng’ang’ania, mwisho akakumbuka kuwa kwa kazi yake anatakiwa kuitii *sense* hiyo ya sita.

“We are here my brother! Zim Hotel,” yule dereva akamwambia mteja wake mara tu baada ya

kuegesha gari katika lango kuu la hoteli hiyo.

"Oh, thank you, how much?" Chameleon akamwuliza yule dereva.

"Just Five Dollars…"

Akatoa pochi yake na kumpatia kiasi hicho cha pesa alichosema na Yule bwana akaondoka zake. Hatua chache zikamfikisha katika mapokezi ya hoteli ile, akamsabahi mwanadada aliyeketi hapo.

“Paulo Kalesa, kutoka Zambia,” akajitambulisha.

“Welcome Mr. Paul, welcome to Harare…”

“Thanks, thank you very much,” akamtania.

Yule mwanadada akamkabidhi mteja wake funguo na kutaniana kwa maneno machache kisha wakaagana. Lakini hatua kama mbili mbele, akasimama, kisha akageuka na kurudi pale mapokezi.

“Yes Mr. Paul!”

“Any message for me….”

“Oh I’m sorry…” akaomba msamaha na kumkabidhi bahasha. Chameleon akatumia lifti ku[anda ghorofa ya saba ambako ndiko hasa kilikokuwapo chumba chake. Akili yake ilikuwa ikifanya kazi harakaharaka, alikumbuka kuwa pale mapokezi alimwacha mtu mmoja akisoma gazeti, lakini ushikaji wa gazeti

hilo haukuwa wa kisomaji bali *danganya toto*.

Alipofika chumbani, hakuingia badala yake aliingia lifti nyingine na kushuka mpaka ghorofa ya kwanza, akachukua korido na kutokea mlango wa dharula mpaka nje. Kwa kutumia njia hiyo akatoka nje ya hoteli usiku huo na kuchukua taksi kurudi mjini.

* * *

Mara baada ya Chameleon kutoka pale kaunta, Yule jamaa akashusha gazeti lake taratibu na umtupia jicho mzee huyo wakati akiingia katika lifti na kuondoka. Akanyanyuka na kuliacha lile gazeti pale chini mezani kisha taratibu akazikwea ngazi kwa mtindo wa kukimbia. Kwa kuwa alikuwa ni mtu wa mazoezi, haikumchukua muda kufika katika ghorofa ile ambayo alisikia Yule mhudumu akimtajia mgeni huyo. Akajitokeza koridoni na

kuangaza macho upande huu na ule, hakuna mtu.

Akavuta hatua taratiu kwa mwendo ambao nyanyo zake hazikufanya ukelele wowote ukizingatia muda huo kila mtu alikuwa amelala. Akachomoa jisu lake kubwa lililokuwa limefichwa ndani ya koti lake na kulishika barabara kwa kono lake lenye nguvu. Jisu lile la makali kuwili iikuwa iking'aa kwa mwanga wa taa za koridoni na kufanya

kujionesha wazi makali yake. Huyu jamaa akavuta hatua za kimyakimya mpaka akafika katika ule mlango ambao kwao alikuwa na uhakika kabisa kuwa mgeni wake ameingia.

Ni kumcharangacharanga tu! Akajiwazia huku akikamata kitasa cha ule mlango, umefungwa. Akajaribu tena, hali ileile, akajaribu kusikiliza kwa makini lakini hakusikia dalili ya kuwa na mtu ndani ya chumba kile.

Akachomoa funguo zake na kupachika mojawapo katika mlango huo nao ukafunguka bila taabu. Yule jamaa akatulia kwanza na baadae akatanguliza kichwa kutazama. Kila kitu kilionekana kipo kama kilivyokuwa. Akaingia mzimamzima na kuanza kutazama hapa na pale. Kila alipofunua hakuna mtu, chooni, bafuni, kabatin, chini ya kitanda, peupe.

“Come on!” akasema kwa sauti ndogo, “where is he son of bitch?” akashikwa na hasira. Baada ya kujiridhisha kuwa hakuna mtu mle ndani, akatoka taratibu na kurudi kaunta ya mapokezi kwa yule dada.

“Vipi?” yule mwanadada akauliza.

“Hayupo!” akamjibu kwa sauti ndogo.

“Hayupo kivipi, si katoka hapa sasa hivi…”

“Hayupo…”akasisitiza.

Baada ya kuongea mawili matatu na mwanadada huyo, wakaagana na Yule kijana akapotelea kwenye mataa ya mjini, hatua kama mia tano hivi akaingia ndani ya kibanda cha simu kilichokuwa kando tu mwa barabara. Akakoroga namba kadhaa kisha akaiweka sikioni simu hiyo.

“Jamaa katutoroka!” akamwambia mwa upande wa pili.

“Unatorokwaje kizembe hivyo?”

“Si kizembe, bali inaonekana jamaa ni mjuvi sana, labda amenigundua!” akaendelea kujieleza.

“Sikia, fanya juu chini umpate maana kazi yetu ya kesho haitakiwi kuingiliwa na mtu yeyote…”

“Yes Sir!”

* * *

Mataa ya barabarani katika Jiji la Harare yalikuwa yaking'aza kila kipitacho. Kiukweli mji ulipendezeshwa na mataa hayo. Chameleon alikuwa amepumzika katika kiti cha nyuma akimwangalia dereva wa taksi hiyo alivyokuwa akikata mitaa kwa umahiri wa hali ya juu.

"Which hotel bro?" dereva akamwuliza mteja wako.

“Nipeleke Flamingo!”

Chameleon alimwambia kijana yule naye akabadilisha njia mara moja na kuchukua barabara nyingine ambayo iliwafikisha katika hoteli hiyo. Akamlipa pesa yake kisha akamwacha aende. Dakika mbili baadae akaifikia kaunta ya hoteli ile na kupokewa na mwanadada mwingine. Akalipia chumba na kuchukua ufunguo kisha akaingia ndani katika ghorofa ya nne akajifungia na kutulia kimya.

Shenzi sana hawa! Wanafikiri watanipata kizembe kama bata bandani! Akawaza. Na hapo ndipo akaikumbuka ile bahasha aliyopewa pale kaunta katika hoteli ya Zim, akaichukua na kuichana, ndani yake kulikuwa na karatasi ya rangi ya *cream* na maandishi machache.

Baadhi ya watu wetu wapo jijini Harare kwa ajili ya mkutano maalumu wa mapano kati ya

Tanzania na Makaburu wa Afrika Kusini.

Kikao hicho kinategemewa kufanyika katika ukumbi wa Mugabe Square nje ya jiji hilo. Tunahofia usalama wa watu wetu ndo maana tumekutuma uhakikishe hilo. Msafara huo unaongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi Bwana Kitwana Selemani.

Kazi njema!

Chameleon akashusha pumzi na kujibwaga kitandani kisha

akachukua dakika kadhaa za kufikiri. Aliuelewa ujumbe ule vizuri sana, kati ya watu hao ambao hakuyapata majina yao alimjua huyo waziri tu kwa sababu aliandikiwa jinale karatasini. Licha ya yote hayo hakujua ni wapi kafikia na ni katika hoteli gani.

Kazi ngumu kuwalinda watu usiowajua, na je nipo peke yangu au kuna wengine kwa kazi hii? Akajiuliza kwa maana alijua kuwa

kazi kama hiyo mara nyingi huundwa timu na si kutumwa peke yake.

Mchezo gani huu? Akajiuliza kisha akakurupuka na kutoka kitandani, breki ya kwanza ilikuwa bafuni, mbele ya kioo kikubwa, akajitazama, duh, uzee umekwishamchukua.

Tutapambana na hawa jamaa mpaka lini? Maana wanataka kutumia kila njia kututawala tena! Akawaza kisha akarudi tena

chumbani na kupanda kitandani tayari kujipa usingizi wa dakika sitini na tano tu kwani ilikwishatimu saa kumi na moja alfajiri.

* * *

“Kwani Tanzania ni nani hata ijifanye kuwa mbele katika kila jambo la ukombozi wa Afrika? Maana wamefanya mengi, sawa, na wametutia hasara nyingi sana kwa kuwatumia wale vijana wao kwa nyakati tafauti. Hii vita ni

kubwa na ni vita ambayo haina mwisho mpaka Afrika isalimu amri na kukubali nkuwa wao ni watumwa wa watu weupe tu!" Kaburu Jeremy Waltergard aliwaeleza wajumbe wa kamati maalumu iliyoundwa tayari kukutana na ile ya Tanzania.

"Kweli Comrade! Wametutia hasara na hasa kupitia hawa vijana wao, huyu nani huyu…"

"…Joram Kiango na Willy Gamba," akaingilia mazungumzo

ya mwenzake maana alijua wazi kuwa amesahahu watu hao matata ambao walilisaidia taifa katika kupambana na makaburu hao kwa nyakati tafauti. Wakamkumbuka marehemu Von ambaye Joram Kiango alifanya kazi kubwa kuiangusha ngome yake kule Afrika Kusini katika sakata ambalo mwandishi maarufu Ben Mtobwa aliliita *Tutarudi na Roho Zetu?*. Lakini pia walikumbuka makaburu wenzao waliotumia nchi ya Zaire

kujificha na kuendesha shughuli zao kwa mwamvuli wa umiliki wa magereji huku chinichini wakiendesha kundi hatari la White Power (WP) ambalo Willy Gamba na vijana wengine kutoka Nigeria na Zaire yenyewe walilitikisa na kulisambaratisha na hii ilimvuta sana mwandihi maarufu Tanzania naye akaandika mkasa huu na kuuita *Kikosi Cha Kisasi.*

“Hatuwezi kuvumilia, na hao tulio nao hatuwaachii, najua ni watu hao hatari sana, sasa tunao sisi na ndiyo maana wanataka mazungumzo nasi,” akaongea kiongozi wao aliyeteuliwa kuongoza jopo hilo la watu hatari. Tofauti na Tanzania, tume hii kwa upande wa Afrika Kusini ilikuwa na watu weupe tu, tena wenye weledi wa mambo ya juu. Ndani yake kulikuwa na majasusi hatari kama The Cobra, Blastas Duker na Margaritha Casbarai

mwanamke hatari sana katika medani za vita, majasusi awa walikuwa bado vijana sana na waliendesha shughuli zao katika nchi ya Zimbabwe, Botswana na Namibia. Pia alikuwepo Waziri wa Ulinzi wa serikali hiyo ya makaburu na wajumbe wengine wa kidiplomasia ambao wana uwezo wa kujenga hoja isipingike.

Tanzania wao waliteua Waziri wa Mambo ya nje, wanasheria

waliobobea na watu wachache wa idara ya Uhamiaji kwa kuwa daima serikali yetu iliamini katika mazungumzo.

Asubuhi hii kikao kizito kilikaa katika moja ya hoteli ya gharama jiji ni Harare, kikao cha *Top Rankin* wa WP yaani White Protection ambao walijibadili jina kutoka White Power baada ya kusambaratishwa na kule Zaire, bado machungu yale waliyakumbuka na hii ilipelekea

kujenga chuki kubwa na Tanzania tena hasa Rais wa wakati huo Mwl. Nyerere. Waliamini kuwa mtu huyu sit u mtu wa kawaida bali ni mwenye ubongo wenye nguvu kubwa ya kushawishi na kufikiri, kwa upande wao walimhesabu kama Jasusi namba moja wa Afrika mwenye ulinzi usioonekana kwa macho.

“Mpango wetu ni uleule, hakikisheni unakamilika kwa

ustadi wa hali ya juu sana. Watu wetu kule Tanzania wametuletea majina ya wajumbe waliokuja, hakuna hata wa kututisha wote ni kama mende tu…" Yule kiongozi akasema huku wengine wakiwa kimya kabisa kusikiliza, nidhamu ya utii.

"Comrade, Tanzania ni nchi isiyotabirika, tusiiamini hata kidogo kusema kwama imetuma watu hawa tu na tuwaona hawana hatari kwetu, kumbuka nchi ile

kila mtu ni mwanajeshi na mpelelezi… isitoshe, katika kazi mliyonipa tayari nimegundu kuna mtu ameingia nchini alfajiri ya leo, nilipanga auawe lakini mtu huyo ametoweka katika mazingira ya kutatanisha mpaka sasa hajulikani alipo…" Blastas Duker akawapa taarifa ambayo ilizua minong'ono kati yao.

"Silent!!!!" Margaritha akawaambia wenzake.

“Sidhani kama ana hatari kama wale wengine, ila naomba afuatiliwe na ihakikishwe ametiwa nguvuni kisha ajumuishwe na wenzake. Wapelelezi wao hatari wote tumeshawadhibiti na hao Willy na Joram sasa hawana lolote, hawasikiki kabisa,” Stewart Mc Clain, Waziri wa Ulinzi akawaeleza.

Baada ya mazungumzo marefu na kujiridhisha kwa mipango yao,

kikao kikavunjwa na tayari wakajiandaa kuelekea katika ukumbi huo wa Mugabe Square kwa ajili ya mkutano. Kila mmoja alichukua usafiri wake na kurudi hoteli aliyofikia kujiandaa kwa kazi hiyo ambayo kwao walitegemea kuimaliza hata kabla ya kikao.

* * *

Ilikuwa ni kama pango au handaki ambapo Chameleona aliketishwa chini baada ya

kupewa kipigo kikali kilichomwacha nusu mfu. Mtu mweupe sana kana kwamba alijipaka chaki usoni mwake na mwili mzima alisimama kariu yake akiwa na ndoo kubwa. Kisha akaja mwingine wa jinsi ile ile na kitu kama kata mkononi mwake, akaitumbukiza katika ile ndoo na kukoroga. Hapo Chameleon alihisi wazi kabisa harufu ya damu, damu nzito.

“Kunywa damu ya ndugu zako kabla wengine hawajanywa ya kwako!” akasikia sauti tu na asione mtu, mara Yule mtu akachota damu katika ile kata na kumwekea kinywani kwa lazima anywe. Chameleon alijaribu kukataa kwa kujitikisa.

Ghafla akashtuka usingizini na kukaa kitako kitandani akihema kama mbwa aliyekimbizwa. Ilikuwa ni ndoto mbaya sana kwake, kijasho chembamba

kikamtiririka, hakujua nini maana yake. Akainuka na kuelekea chooni huko akatapika sana maana alihisi kabisa kuwa amekunywa damu ile lakini ukweli ni kwamba ilikuwa ndoto tu. Alipotazama saa yake aina ya Motima ikamwambia kuwa ni saa moja kasoro robo asubuhi. Akajiswafi haraka haraka na kubadili nguo, akavaa jinzi lake na fulana nyekundu kwa ndani, akapachika bastola zake tatu zilizojaa vyema na silaha nyingine

nyingine mwilini mwake ambazo huwa si rahisi kutambulika kwa mtu asiye na ujuzi wa mambo kama hayo. Kisha akachukua koti lake na kulivaa juu yake, na lile kubwa kabisa akaliweka begani na kutoka nje ya hoteli hiyo.

Kabla hajaenda sehemu yoyote, kwanza akanujnua gazeti la siku hiyo na kulitumia macho. Lilikuwa gazeti la *The Sun* ambalo lilibeba habari nzito juu katika kurasa ya kwanza kabisa.

‘TANZANIA NA MAKABORU KUKUTANA KATIKA MEZA YA UPATANISHI’

Habari hii ilimvutia sana, akavuta kibenchi kidogo na kuketi juu yake akisoma gazeti hilo huku pembeni yake kukiwa na vijana na watu wengine wakiendelea na mazungumzo. Habari ile ilieleza kwa kina sana juu ya kikao hicho na vile vya nyuma ambavyo

vilikwishafanyika bila muafaka wowote. Aidha ilizungumzia juu ya usalama mzima wa wajumbe wa kikao hicho kwani uhalifu katika jiji la Harare ulikuwa umeshika hatamu na Afrika ilikuwa katika hali ya kutokujielewa kwa mauaji ya viongozi mbalimbali na watu wengine maarufu. Zaidi sana mwandishi alijaribu kuuzanisha tume hizi mbili yaani ile ya Tanzania na Afrika Kusini na kuwaeleza wasomaji kuwa lolote

linaweza kutokea kwani Tanzania inajulikana kwa ushawishi wa kimazungumzo na makaburu wanajulikana kwa ubabe wao na kutokumthamini mtu mweusi.

Chameleon alipomaliza kusoma habarai hiyo, akajikuta moyo ukimwenda mbio, akakunja lile gazeti na kulifutika ndani ya koti lake refu, akainuka na kundoka zake taratibu. Baada ya kukata mitaa miwili mitatu akachukua taksi na kuketi katika

siti ya nyuma. Bado alijikuta moyo ukienda mbio bila kumtulia, hakuielewa hali hiyo na mishtuko kadhaa ilimtokea kila alipoikumbuka ile ndoto aliyoota.

"Safari wapi kaka?" Yule dereva mtu mzima akauliza. Ndipo Chameleona akakumbuka kuwa yupo ndani ya gari na hajasema wapi anaelekea. Kutokana na habari aliyoisoma alijua ni wapi tume ya Tanzania imefikia na kuweka kambi yake.

Akamtazama dereva Yule mtu mzima, ambaye kichwa chake kilifunikwa kwa kofia maridadi lakini ilishindwa kuficha nywele zake nyeupe. Hii ilimfanya Mtanzania huyu kutabasamu na kuachia cheko la moyoni.

"Charlemagne Hotel!" akamwambia, na yule dereva akaondosha gari kuelekea hoteli hiyo.

“Inaonekana wewe si mtu wa hapa kabisa!” dereva taksi akaanzisha mazungumzo.

“Yeah mimi ni Mzambia, nimekuja kutalii…”

“Kutalii? Ina maana wewe ni mtalii?”

“Ndiyo. Kwani haiwezekani?” Chameleon alizidi kuzungumza na dreva huyo.

“Aaaaa sijawahi kuona mtalii mweusi…”

“Ndo mimi sasa!”

“Unajua Charlemagne ni hoteli kubwa sana na ya kisasa, watu kama mimi hatuwezi kuingia… pale ni watu wazito tu, marais, mawaziri au matajiri wakubwa, itakuwa nawe ni mmojawapo?” Yule dereva akazidi kuchimba na Chameleon alikuwa kimya akiendelea kumsikiliza kwa kila analoliongea huku akili yake ikjariu kichanganua mambo kujua

kama mtu huyo ana maneno yaliyojawa hila au la.

“Nina rafiki yangu nataka nimwone, amefikia pale…”

“Ooooh ok! But you need to be smart aaanh!” akaendelea kubwabwaja, “asubuhi hii patakuwa na ulinzi sana kwa sababu kuna wajumbe wa mkutano ule wa upatanishi kutka Tanzania…” akaongeza kusema.

“Kwani wamefikia hapo?” Chameleona akajifanya hajui lolote.

“Ndiyo! Si nimekwambia ni hoteli ya hadhi ya nyota tano… mi nawaomea heri ila Harare imechafuka siku hizi!” akaeleza. Wakati mazungumzo yakiendelea tayari taksi hiyo ilikuwa ikiengeshwa katika megesho ya Hoteli ya Charlemagne. Chameleon akashuka na kumlipa mzee huyo kisha akaondoka

zake. Hakuelekea hotelini bali kwa mmoja wa wauza magazeti ambaye alikuwa ameyapanga chini si mbali na lango la kuingilia hotelini hapo.

Haikupita muda kikasikika king'ora cha pikipiki ya polisi kikasikika na mara ikaonekana ikitoka ndani ya hoteli hiyo kwa kasi na kufuatiwa na magari kadhaa, yote yakienda mwendo ule ule.

“Haoooooo wanenda sasa, ngoja tusikie Stewart Mc Cain atamshinda Nyerere?” alisikika mtu mmoja aliyekuwa jirani na eneo hilo. Chameleon, akaacha kutazama yale magazeti na kupotelea katikati ya majengo yaliyo jirani na eneo hilo. Mtaa wa kwanza, wa pili, wa tatu, akakuta pikipiki zimeegeshwa na kufungwa kwa mnyororo. Akatazama huku na kule hakuna anayemwona, akachuka funguo yake isiyoshindwa kitu,

akafungua kufuli na kuuondoa mnyororo huo kisha akachagu Honda kubwa na kulikalia juu yake. Kiki ya kwanza, mashine ikakubal, akavuta klachi na kukanyaga gia, lile pikipiki likachomoka kwa kasi. Haikumchukua muda kuifikia barabara kuu, akakunja kushoto na kuvuta mafuta kwa nguvu. Ile Honda ikawa katika mwendo wa hatari sana kwa kasi yake, dakika kama tatu hivi akaanza kuuona ule msafara mbele yake,

akaongeza mwendo na kuukariia sana kisha akapunguza na kuhakikisha hazidishi wala hapunguzi.

Katika njia panda kubwa ya mbele, msafara ukakunja kulia na kuingia katika barabara yenye maghorofa mengi, ukawa ukipita katikati ya majengo hayo kwenda kutokea upande wa pili ambapo ndipo haswa ukumbi wa Mugabe Square ulipo. Naye akakunja na kuwa nyuma kwa takribani mita

mia moja hivi. Kati yake na ule msafara kulikuwa na pikipiki nyingine kubwa ya polisi. Mara ghafla, kitendo ambacho hakukitegemea, alishuhudia pikipiki nyingine ikiibuka katika barabara ya mtaa na Yule askari akachomoa basto na kumtungua huyu wa kwanza akiwa juu ya pikipiki, akaanguka vibaya na kuburuzika chini. Kitendo hiki kilimshtua Chameleon, hakuwa na muda wa kujiuliza mawili matatu, akajua wazi kuwa hapo

hakuna usalama. Akaongeza mwendo lakini mara akaona ile pikipiki iliyokuja mara ya pili badala ikae nyuma ya msafara sasa ikawa inaupita msafara huo huku Yule dereva akitazamatazama kwenye vioo vya gari.

Chameleone akiwa anakalikaribia gari la mwisho, alihisi mvumo wa ajabu kando ya sikio lake, akageuka asione kitu, kabla hajarudisha macho mbele

akasikia kishindo kikubwa, akageuka kutazama kulikoni, alichokishuhudia hakuamini. Gari ya mwisho ilikuwa ikibingilika hewani huku ikiwaka moto kisha ikatua chini kwa kishindo. Akafunga breki ya ya ghafla na kuweka mguu chini kisha akaizungusha ile pikipiki na kutazama juu ya yale majengo. Akamwona mtu akikimbia juu ya lile jengo huku begani mwake akiwa na RPG. Akili yake ikasoma haraka kuwa hapo tayari

walikuwa hatarini, akachomo bastola yake, akaiweka sawa huku akiliacha lile pikipiki lijitupe chini. Mara akshuhudia gari ya mbele nayo ikitupwa upande wa pili kisha kutoka kwenye madirisha ya zile nyumba watu wakatokeza mitutu ya shotgun na kuanza kumwaga njugu, kizaazaa. Milio ya risasi ilisikika ikijibishana kutoka upande huu na ule, Chameleon tayari akiwa na bastola yake mkononi aliazna kuwatungua kwa shabaha ya

ajabu, alihakikisha kila risasi yake inaanguka na mtu. Alipoona kuwa sasa wanamgundua, aliingia nyuma ya gari moja lililokuwa limeegeshwa eneo hilo, nakutumia kila upenyo kuendelea kuwapunguza jamaa hao huku akutazama kama kuna yeyo aliyebaki hai ndani ya magari yale.

“From this side, this sideee!!!” akasikia sauti zikitoka juu ya jengo moja wapo bahati nzuri a.iweza kumwona aliyekuwa

akihimiza wenzake. Akamweka kwenye shabaha na kumtungua vizuri kisha akaendelea kuwatungua wengine. Bastola yake ya kwanza, Revolver ikaisha, akaipachika kiunoni na kuchukua nyingine, kazi ikaendelea. Moshi ulitapakaa kila upande na moto ukaendelea kuyateketeza magari yale. Chameleon akalifikia gari la pili kutoka mbele na alipochunguia ndani akamwona Mheshimiwa Waziri akiwa bado anapigania uhai wake,

akaipachika bastola kiunoni na kuuvuta mlango kwa nguvu, akamvuta nje na kuanguka nay echini. Wakati huohuo lile gari la mbele likapigwa roketi moja na kutupwa upande wa pili. Bahati kwa Chameleon kwani wingi wa moshi ulikuwa ukimpa kinga, akajitahidi kumvuta kando Waziri Kitwana kisha akamsaidia kuinuka na kumweka mkono mmoja begani, wakakokotana mpaka kwenye gari lile alilotumia kujikinga, akatikisa mlango

ukafunguka akamtupia waziri Yule kiti cha nyuma kisha yeye akakaa myuma ya usukani.

“They are running!!!!” akaisikia sauti hiyo kutoka kwenye yale majengo, hakuijali, akachukua funguo zake na kupachika, jino moja mashine ikawaka, akakanyaga klachi, akaweka gia rivasi na kushusha breki ya mkono kisha akaachia klachi na kuipa mafuta, lile gari likarudi nyuma kwa kasi na alipofika

kwenye pacha, akakunja kona kali huku akiondoa mguu mafutani na kukanyaga tena klachi, akatoa gia rivasi na kutupia namba mbili, akaweka mguu kwenye akseleleta na klachi akapiga norinda ya maana na kusugua barabara, moshi uliotoka hapo ukawachanganya waliokua wanamfuata. Lile gari likaondoka kwa kasi na kupotelea katikati ya majumba.

Breki ya kwanza aliikanyaga dakika ishirini baadae, akiwa tayari kilomita nyingi nje ya Jiji la Harare, akalitoa pembeni na kusimama, akateremka na kufungua mlango ule ambamo alimtupia Yule waziri, akakuta tayari amekwishakata roho, akaweka mkono wake kwenye mshipa mkubwa wa damu, hakuna kitu.

“Shiiiiiit, aaaaaaaiiiiggghhhh!!!!!” akajikuta

anapiga kelele peke yake, “kwa nini? Kwa nini?” akaongeza kusema kisha akautikisa kwa nguvu ule mwili, hauna uhai.

Nimefeli? Hapana! Nimefaulu? Sijui! Akajiuliza na kujijibu mwenyewe, Chameleone akaegemea gari na kuangusha chozi.

Wakati tayari Chameleon ametoweka katika mtaa ule uliotokea mapigano, milio ya risasi ikakoma na ving’ora vya

magari ya wagonjwa pamoja na yale ya polisi na zima moto vikasikika na dakika chache eneo lote likazingirwa.

Hakuna kilichokutwa zaidi ya miili isyo na uhai ambayo mingine ilitobolewa kwa risasi na mingine iliungua kwa moto. Ndani ya jengo la upande mwingine ambako ndiko haswa mashambuizi mengi yalitokea kuliokotwa maiti saba zote zikiwa

na jeraha la risasi katika paji la nyuso zao.

“Yalikuwa mapigano makali,” afisa mmoja wa polisi akamwambia mwenzake.

“Huu ni uhalifu mbaya kabisa wa kimataifa, lazima ijulikane nani anahusika,” huyu mwingine akajibu. Nusu saa baadae, miili yote iliondolewa na kupelekwa katika hospitali kubwa ya jijini hapo na kuhifadhiwa.

* * *

Katika moja ya taasisi ya kiserikali jijini hapo, maafisa wa ngazi za juu za jeshi walikutana kikao cha dharula kuzungumzia shambulio hilo la karne.

“Afrika hatujafikia huku!” akang’aka mmoja wa maafisa mwenye nyota nyingi begani na tepe zinazoning’inia kifuani mwake. Kwa mwonekano wake tu ilijulikana kuwa ni mkuu wa jeshi.

“Hii ni hatari, yaani inaonekana tumeshindwa kuwapa ulinzi wageni wetu?” mwingine akauliza, kisha ukimya ukatawala kati yao, hakuna aliyekuwa anazungumza.

“Watu sita wameuawa kutoka Tanzania na madereva wetu wane, lakini hatukuuona mwili wa minister, je amefanikiwa kutoroka au?” Yule mkuu akauliza tena na kila mmoja akaandika kwenye kijitabu chake.

“Hilo ni shangazo la kwanza, lakini kumbuka ndani ya lile jengo tumeokota miili saba, na hawa si watu wetu… je nani aliyewashambulia?” akauliza mwingine, nalo wakaliandika ili uchunguzi uendelee.

“Hawa ni makaburu tu! Hakuna mwingine hapa wa kumhisi…”

“Point!! Nalitaka kusema, itakuwa wameogopa kushindwa kwa hoja za mezani wameamua

kutumia mtutu kuwafutilia mbali!" akaongeza mjumbe wa pili.

"Hata wafanye nini, hawawezi kuizuia nguvu ya mtu mweusi. Sasa na tuone jinsi ya kuliweka swala hili vizuri ili taarifa imfikie Mkuu wa Nchi," yule mkuu wa majeshi akawaeleza wenzake kisha mazungumzo yakafuatia kujadili hili likaaje na lile liwekweje, kwa maana waliona pamoja kuwa kabla ya kulifikisha

kiafisi kwa Rais wan chi hiyo basi tayari wawe na majibu ya maswali watakayoulizwa. Kingine kikubwa kilichokuwa kinatazamwa ni vipi kuhusu uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Rhodesia.

* * *

Upande mwingine, WP walikutana nao kutazama hali hiyo. Mara tu baada ya mkutano kuahirishwa katika ukumbi wa Mugabe Square, kamati hiyo

iliondoka na kudai kuwa inakwenda kufanya kikao cha siri ili kujaribu kuona nani anaweza kuwa amehusika katika mashambulizi hayo ikiwezekana waingine katika uchunguzi wa kujua sakata zima limeanzia wapi. Wakarudi katika ukumbi uleule waliofanyia kikao alfajiri na kujifungia upya, iikuwa ni kama walikwenda mapumziko tu.

"Well done Margaritha!!" Stewart akampongeza

mwanamke pekee aliyekuwa katika jopo hilo kwa kazi nzuri iliyofanyika.

“Thank you sir!” akaitika kisha akaketi kitini.

Blastas Duker akaonesha ishara ya kutaka kuzungumza kitu, akaruhusiwa na kujiweka tayari kwa kusafisha koo.

“Tumefanikiwa kwa asilimia tisini, kati ya watu saba tuliyowadhamiria tumeangusha watu sita na tumehakikisha hilo,

lakini kiongozi wa msafara huo ambaye ni waziri katika serikali ya Tanzania ametoroka!" akawaambia.

"Ametoroka? Ina maana alikuwa anajua kuhusu huu mpango na kwa nini asiwaambie wenzake…?" Stewart akauilza kwa mshangao.

"Usiseme ametoroka, sema ametoroshwa!" Margaritha akarekebisha kauli hiyo. Mpango huu wa shambulizi la ghafla

ulikuwa umepangwa vyema na Bi. Margaritha na Blastas Duker.

“Kuna jambo nililotaka kukwambieni, katika wapiganaji tuliowakodi, mategemeo yetu katika mpango ule ni kuwa hatutapoteza hata mmoja lakini saba wamekufa kwa kupigwa risasi katika paji za nyuso zao, ina maana mpigaji alikuwa mwenye shabaha sana, nafikiri kulikuwa na mtu wa nane katika msafara huu ambaye sisi hatukumjua

kabisa na alikuwa hatari sana kwetu, je si huyu kamtorosha waziri? Kumbukeni niliwaambia kuwa Tanzania sin chi ya kijinga sana kwa vyovyote ilisuka mpango huu ikijua wazi nini kitatokea, kama alikuwapo na kafanikiwa kumtorosha waziri huyo nini kitafuata kama si vita kali kati yetu na taifa hilo?" Blastas akaongea kisha akatulia kitini akiwa kajishika mikono kichwani.

“Haijalishi, White Protection kinajua nini cha kufanya, The Cobra, now is your turn, hakikisha unajua waziri huyo alipo na aliyetekeleza kumwoko uniletee kichwa chake…”

“Yes Sir!” The Cobra akajibu kwa utii. Kijana huyu mwenye mwili mpana wqenye nyama nyingi alipewa jina hilo la kificho *‘The Cobra’* kutokana na macho yake jinsi yalivyo, wengi waliyafananisha na nyoka huyo

aina ya swila. Huyu alikuwa ni jasusi aliyefanya kazi zake nyingi katika nchi tafauti duniani, wazazi wake walikuwa walowezi katika nchi ya Afrika ya Kusini miaka nenda rudi, wakati wa mtu mweusi alipokuwa katika harakati za ukombozi wa bara lake ndipo weupe nao walipoongeza nguvu kwa kutawanya majasusi wao kila pembe Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Na hasa hasa walikuwa wakiiangalia sana Tanzania kwa sababu waliamini

harakati za ukombozi wa Bara la Afrika hususan Kusini mwa Jangwa la Sahara zinaendeshwa katika taifa hilo. Walimwogopa sana Mwl. Nyerere, hawakujua wafanyeje badala yake wakaimarisha ngome yao kwa kutawanya majasusi katika nchi hizo wakiwafanya *'residents'* na wengine *'undercover'* ili mradi tu wajue mipango na mbinu zinazosukwa. Kule Afrika ya Kusini walijua na kumhofu Nelson Mandela, wakamkamata

na kutupa jela huko Kisiwa cha Roden, wakamhofu Samora Machel, wakamtungua akiwa ndegeni karibu kabisa na mpaka wa nchi hizo.

Katika kujenga na kuimarisha nguvu yao ndipo wakajitokeza watu hatari kama Jasusi Von, akina Papa Dimistriou na wengine wengi wakaweka makazi Zaire, Botswana, Zambia, Namibia, Malawi na Tanzania kwenyewe ambako wapigania

uhuru wengi walijificha na kufanya kambi ya kujifunza maswala ya kisiasa ili kuwa tayari kuzitawala nchi zao. Ni katika miaka hii The Cobra akaibuka, Margaritha Kasbarai, mwanamke hatari sana anayekuua huku anacheka na wengine kama akina Mc Cain na wenzake. Ilipoangushwa ngome yao ya White Power wakaanzisha White Protection na kuendeleza kazi zao.

* * *

23 Baines Avenue, Harare

Katika afisi za ubalozi wa Tanzania nchini Rhodesia hali ya sintofahamu ilishika hatamu, taarifa za vifo vya wanatume ya upatanishi zilimwacha Balozi George Kerege akiwa hana fahamu, ni mshtuko uliompelekea kuanguka vibaya afisini mwake.

Chameleon alisimamisha gari alilokuwa akiendesha mbele ya

geti la kuingia katika afisi hiyo iliyopo katika Jengo la Ujamaa. Baada ya kupiga honi mara mbili tu lango likafunguliwa naye akaingiza gari ndani taratibu na kuliweka kwenye maegesho. Askari aliyekuwa akilinda eneo hilo alimfikia wakati akishukantu kwenye gari hilo. Mgeni huyu kabla hata hajaulizwa lolote akamwonesha kitambulisho chake halisi kabisa cha kazi. Yule askari naye hakuongea kitu zaidi

ya kumruhusu kuingia ndani ya jengo hilo.

Katika dirisha la mapokezi akakaribishwa na mwanadada wa Kirhodesia aiyekuwa akihudumu hapo.

“Karibu sana nikusaidie nini?” akamwuliza.

“Nahitaji kuonana na Bwana Maige, mwambie Chameleon yuko hapa!” akamwambia huku tayari akiwa amegeukia upande mwingine. Yule mwanadada

akachukua simu na kupiga namba fulani kisha akamruhusu mgeni huyo kupita ndani. Ngazi mbili tu zikamfikisha Chameleon katika afisi hiyo aliyoihitaji.

"Karibu sana Mr. Chameleon," Maige alimkaribisha mgeni wake na kumpa mkono wa salamu.

"Asante nimefika!" Chameleon akajibu huku akiketi, kisha akashusha pumzi ndefu na kujiegemeza akiangalia juu ya dari

kana kwamba kuna kitu anachokitazama huko. Baada ya sekunde kama ishirini hivi akashusha uso wake na kutuliza macho kwa Bwana Maige.

"Maige!"

"Yes braza!"

"Mheshimiwa yupo?" akauliza.

"Asee kaka, hapa kuna tatizo kubwa, hata mimi nimeingia sasa hivi nilikuwa hospitalini kumpeleke huyo unayemuulizia…"

“Nani… balozi?”

“Yes! Kama upo hapa Rhodesia basi utakuwa umesikia juu ya shambulio baya lililowapata wanatume ya upatanishi, watu sita wameuawa wakiwamo madereva na mpaka sasa mkuu wa msafafra yaani Waziri Kitwana Selemani hajulikani alipo,” akamweleza. Chameleona akajikuta akibutwaika bila sababu ya msingi kwani alijua kila kitu nay

eye ndiye ambaye angeweza kumweleza Maige ni nini hasa kimewakuta wanatume wale.

“Hali yake…”

“Mbaya… hapa tunafanya utaratibu arudishwe nyumbani Tanzania kwa check-up zaidi, amepata mshituko mkubwa sana kwa taarifa hizo!” Maige akaeleza.

“Maige! Let us break the rules…”

“Yes…”

“Nimefika jana hapa Rhodesia, na nilitumwa kuja kuhakikisha usalama wa wanatume hawa, kukweli sikutakiwa kabisa kujileta kwenu kabla wala baada…”

“Ndiyo, najua mambo yetu ni siri sana…”

“Yes… sasa nimekuja kwa sababu maalum, katika shambulizi lile nilikuwepo lakini nimeshindwa kuwaokoa jamaa kwa sababu ilikuwa ni hali ambayo sikuitegemea lakini

isitoshe wale jamaa wlitumia silaha nzito za kivita. Kwa shabaha yangu nimeweza kuua kama sio watu sita basi watano kwa upande wao, lakini nia yangu ilikuwa nimpate Kitwana kwa sababu ni gari yake iliyokuwa bado haijashika moto, na kama ujuavyo mkuu wa msafara ndiye mwenye maagizo na kabrasha zote…"

"Sasa Kitwana ndiye hatujaona hata mwili wake, isitoshe

mashuhuda wanadai ametekwa…” Maige akaongea kwa wasiwasi.

“No! ninaye mimi…”

“Unaye? Wacha kunidanganya… na ni kweli alikuwa na faili confidencial,” Maige akaongezxa kusema.

“Yuko wapi sasa?” Maige akauliza kwa shauku.

“Yupo, lakini hawezi kuongea, na moyo wake umesimama… hili ndo limenileta kwako,

tunamhifadhi vipi na wapi?” Chameleon alitumia maneno hayo akimaanisha kuwa Kitwana amekufa tayari na sasa alikuwa anatafuta msaada wa kuhifadhi maiti hiyo.

“Aisee, umepata hiyo faili?” Maige akauliza.

“No, sijapata chochote…”

Mazungumzo marefu kidogo yakafuata baada ya hapo lakini Chameleone aliweza tu

kumweleza yale yanayomhusu ila mengine yote alimficha kabisa.

“Ok, mwii utahifadhiwa, na wewe sasa unatakiwa uje ukae hapa ubalozini maana kama wamekumaki sura, sijui kama utafurukuta…”

“No! ninaondoka usiku leo hii kwa ndege ya ATC, sina kazi mpaka nitakapotumwa tena,” Chameleon akajibu huku akisimama na kumpa ishara Maige kuwa amfuate. Wakatoka

nje mpaka kwenye maegesho ya magari ya wageni, akafungua mlango kidogo na Maige akauona mwili wa Kitwana ukiwa umeketishwa kitini huku umefungwa mkanda kama abiri wa kawaida.

"Kapigwa risasi kadhaa mwilini mwake, kupona ingekuwa ni kudra za Mwenyezi Mungu," kamwambia. Maige akabaki kimya kwa jozi la sekunde kisha akampa ishara

Chameleon ya kuwa aingie ndani ya gari hiyo. Wakaingia na kuketi huku Maige akiwa nyuma ya usukani.

“Hii gari umepata wapi?” akauliza.

“Nimeiba! Pale kwenye mapigano niliondoka na jingine nimeliacha huko mashambani nikachukua hili kwenye maegesho ya mgahawa mmoja hukohuko…” akaeleza.

Maige akawasha na gari lile likawaka kisha akaligeuza na kuliondoa taratibu na kupotelea mjini.

* * *

The Cobra, akaipachika miwani yake usoni na kuingia garini kisha akatulia tuli nyuma ya usukani. Mbele yake alikuwa akiiona hoteli ya Zim ambayo huyo anyemtafuta ndipo alipofikia kadiri ya hesabu zao kumbe alisahau kuwa anacheza

na kinyonga anayejibadili rangi kadiri ya mazingira. Saa mbili zilipita akiwa palepale na asione dalili za kiumbe huyo. Ndani ya gari hilo aina ya Jeep, jamaa huyu alikuwa peke yake. Hakuamini tena mtu kuifanya kazi hiyo kwa sababu aliyemwamini alikwishashindwa.

Anaweza kuwa kabadili hoteli! Akawaza huku akitia moto injini ya gari lake na kuondoka taratibu.

Cha kufanya ni kumbania njia tu! Akazidi kuongeza mikakati ya kumkamata mtu huyo. Mwendo wa gari ake hata kama ulikuwa wa wastani barabarani, bado aliweza kufika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Harare. Kutokana na kazi yake, The Cobra alikuwa akifahamiana na watu wengi sana katika jiji la Harare, safari yake ya kuja hapa uwanja wa ndege ni kumtafuta rafiki yake ambaye alikuwa akifanya kazi katika mamlaka

hiyo na alimtumia sana katika kazi zake kama hizi.

Katika moja ya afisi nyeti ndani ya uwanja huo, mzungu huyu ambaye rangi yake ilikwishafifia kwa jua la Afrika alikweti kitini huku akitazamana na swahiba wake.

“Mr. Kabele! Leo ndege gani inaenda Dar es salaam?” akamuuliza.

“Boeing 737 Ngorngoro mali ya Air Tanzania…” akamjibu.

“Mmmmm good! Unaweza kupata orodha ya wasafiri?”

Kwa swali hili, Bwana Kabele akaacha kazi aliyokuwa akiifanya na kumtazama mzungu huyo kwa mashangao, kisha akaikunjua sura yake kwa tabasamu.

“Kazi ndogo hiyo, vipi kuna mzigo?”

“Yes! Kuna mtu sitaki aiache ardhi ya nchi hii akiwa na roho yake… simjui kwa sura ila

naweza nikaliotea jina lake," The Cobra akasema.

"Ok, wait!" akamwambia huku akisimama na kutoka nje ya afisi hiyo, dakika kumi baadae alirudi na karatasi kadhaa mkononi mwake akamkabidhi mtu huyo naye akaanza kuzipitia. Yalikuwa majina kama 145 hivi yakiwa yameandikwa kamilifu yaani majina matatu, umri, atokako na aendako pia na muda aliyokata tiketi hiyo.

Katika majina matatu ya mwisho, The Cobra aiyatilia wasiwasi kwa kuwa yalionesha kuwa watu hao wamekata tiketi ndani ya saa tano za siku hiyo, akayaandika pembeni kisha akarudisha ile karatasi na kuagana na swahiba wake huku akimwachia *ZimDollar* kadhaa kama zawadi.

Baada ya kuuacha uwanja huo, akarudi tena katika hoteli ya Zim na mara hii akapitiliza mpaka

katika kaunta na kukutana na kijana wa Kirhodesia.

“Karibu!”

“Asante, aaaa kuna wageni wangu nawaulizi walifika jana hapa…” akaeleza.

“Majina yao na wanakotoka …” Yule kijana akamwambia mzungu huyo naye akatoa kijikaratasi na kumkabidhi. Yule kijana akatazama kwa makini na kupitia orodha yake kama kuna wageni wa aina hiyo, kisha

akamtazama tena Yule mzungu huku akimpa kile kijikaratasi.

“Wapo?”

“Mmoja nimeona kuwa yupo chuma namba 304…” akamwambia.

“Yupi kati ya hawa?”

“Paulo Kalesa kutoka Zambia…” akajibu.

“Asante sana nahitaji kumwona!”

“Panda tu hakuna shida kaka..” Yule kijana akamruhusu Cobra kuingi ndani kuonana na mgeni wake na mzungu huyo huku akipiga mruzi alikwea ngazi kwenda ghorofa ya tatu chumba namba nne. Haikumchukua muda akakipata, akasimama mlangoni kwa sekunde kusikiliza kama kuna mtu ndani yake. Ndiyo, akajihakikishia hilo kwani alisikia sauti za watu kwa mbali sana, akahisi wapo, akachomoa bastola yake na kuifunga

kiwambo cha sauti, kisha akachukua funguo zake na kutumbukiza, akanyonga haraka na kujitoma ndani.

Mawazo na hisia za Cobra hazikukosea, ndani ya chumba hicho kulikuwa na watu wawili, mwanamke na mwanaume wa Kiafrika. Viumbe hawa wawili walikuwa juu ya kitanda kikubwa wakiendelea kuvunja amri ya sita ya Mungu wakiwa kama walivyozaliwa.

“Come on who are you stupid!?” Yule jamaa pale kitandani aling’aka huku akijinasua kutoka katika kifua cha mwandada huyo na kugeuka mzima mzima. Kabla hajajiweka sawa, risasi moja kutoka katika boastola ya *Smith and Wesson* ikadidimia kwenye paji la uso na kubwaga kitandani akiwa hana uhai.

“Mbwa mweusi wewe! Unafikiri unaweza kuukimbia

mkono wa Cobra!?”
akaunguruma kwa sauti nzito.
Yule mwanamke akabaki kitandai
akiwa anatetemeka hajui nini cha
kufanya, machozi yalimtoka
lakini hakuweza kutoa sauti.
Macho ya Cobra yakatua katika
mwili wa mwanamke huyu
aliyekadiriwa katia ya miaka
ishirini na tano mpaka thelathini,
mwenye rangi nzuri ya
kupendeza na umbo la kiafrika.
Mzungu huyu akajikuta anameza
funda kubwa la mate kwa uchu

lakini katu asingethubutu kufanya lolote na mwanamke huyu kwani kwao ni marufukua kabisa kuchangamana na mtu mweusi.

"Nakuacha hai, ukisema na nikisikia nitakukamata tu, nakwambia nitakukatakata mwili wako, kunguni nyie!" Cobra akamwambia huku akitoka taratibu na kuondoka asijue haraka kosa alilolifanya katika uvamizi huo. Aliendelea kupiga mruzi kufuatisha melodia ya

wimbo unaojulikana kama *Yesterday* uliopigwa na *The Beetles* huku taratibu akiondosha gari lake kutoka eneo hilo.

* * *

Chameleon, mara baada ya kuachana na Maige alirudi Hoteli ya Flamingo na kujitupa kitandani huku mawazo lukuki yakimzonga kichwani. Moyoni mwake hakujisikia furaha hata kidogo na mara kwa mara tukio lile baya kabisa lilimrudia kwenye

fikra zake. Baada ya kuona kuwa akili yake haiwezi kupumzika, akaingia maliwato na kujimwagia maji ya baridi kwa dakika kadhaa akifikiri hili na lile. Alipojiona kidogo yupo sawa, akarudi chumbani na kuketi, akafungua redio yake ndogo na kusikiliza kinachotangazwa. Kwa bahati saa kumi jioni hiyo, taarifa ya habari ilikuwa inaendelea na ndipo alivutiwa na taarifa ya mauaji yaliyotokea asubuhi ya siku hiyo pia na yale ya hotelini.

‘…mauaji hayo katika Hoteli ya Zim yanahusishwa kwa ukariu nay ale ya watu sita katika shambulio la kigaidi lililofanyika asubuhi leo. Duru za usalama katika Jiji la Harare zinasema mfanyabiashara huyo aliuawa kwa kupiga risasi katika paji lake la uso sawasawa na miili sita iliyopatikana katika eneo la tukio la ugaidi…”

“Shiiit!” Chameleon akang’aka na kujishika kichwa.

Yaani Zim Hotel namba 304, walininuia mimi au? Akajiuliza bila kupata jibu na hapo akang'amua kuwa vyovyote atakuwa anasakwa na watu hao, na watakuwa wamepeleleza na kugundua hoteli hiyo. Kilichomfariji ni kuwa shabaha yao imekosea, kwa kuwa hawakuwa wakimjua kwa sura hivyo wameua mtu mwingine katika chumba kile kile.

Je; itakuwaje wakigundua waliyemuua si mimi? Swali hili likampiga kichwa na moyo wake ukaanza kudunda kwa nguvu, akachukua begi lake na kuanza kuchambua nguo ya kumfaa kisha akajibadili sura hapa na pale na kuwa na muonekano tafauti. Na hii ndiyo ilimfanya shushushu huyu kupewa jina la Chameleon kutokana na uwezo wake wa kujibadili kwa haraka na kumtoroka adui yake. Katika mafunzo yake ya kikachero huko

USSR chini ya taasisi ya kijasusi ya KGB miaka hiyo kabla haijasambaratika, Chameleon alibobea katika utundu huu, alikuwa na uwezo wa kujibadili mwanamke, mzee, kipofu au hali yoyote aitakayo. Baada ya maadui wake kugundua hila hiyo, kila walipojua kuwa mtu huyo alikuwa akiwapeleleza waliamua kuua mpaka mbwa au paka au hata kuku kwa maana waliamini kuwa jamaa huyu anaweza kujibadili hivyo.

Hapa pameharibika!
Akajisemea na kuweka kibegi chake tayari kwa safari, giza lilikuwa linaunyemelea mji na muda huo alitakiwa kufika uwanja wa ndege tayari kwa safari saa mbili zinazofuata. Kawaida yake katika kazi kama hizi ambazo hujua wazi kuwa anasakwa huwa hapendi kuondoka sehemu watu wakijua. Mtu mzima huyu akauendea mlango na kuufungua akatazama huku na huko hakuna mtu,

akatoka na kuurudishi kisha akatafuta mlango wa dharula na kutokomea kizani kwa kupitia kwenye vyumba vya usafi mpaka nyuma ya hoteli na kuruka wigo.

* * *

Upande wa pili, The Cobra alipiga teke redio aliyokuwa akiisikiliza kwa hasira mara baada ya kugundua kuwa aliyemuua si aliyemnuia. Kwa hili akajiona ni mjinga kuliko unavyofikiria, hapa ndipo akajiuliza kwa nini

alimlaumu kijana aliyempa kazi hiyo mara ya kwanza, ambaye alimwambia kuwa mtu huyo amemtoroka katika mazingira ya kutatanisha naye akamlaumu kwa ujinga huo, sasa akajikuta yeye ni mjinga zaidi kuliko huyo.

Akainua simu ya mezani na kukoroga namba fulani kisha akaweka simu ile sikioni.

“Yes! Nawataka uwanja ndege haraka sana, mtu wangu atakuwa

anafika pale mida hii kwa ajili ya safari," akamwambia mtu wa pili.

"Yes Sir," akajibiwa.

Dakika hiyo hiyo na yeye akaanza safari ya kuelekea katika uwanja huo akiamini wazi kabisa kuwa hapo lazima ampate adui yake, moyoni mwake aliapa kuwa hatokubali kiumbe huyo ambaye ameua vijana wake sita aiache ardhi ya Rhodesia na roho yake. Na hili alimhakikishia Margaritha Kasbarai ambaye kwa namna

nyingine alikuwa kama mkubwa wake katika medani za kiintelijensia ndani ya W.P

* * *

Chameleon aliwasili uwanjani hapo kama saa moja jioni hivi, akaiacha taksi iliyomleta na kuvuta hatua kuelekea katika jengo la wasafiri. Daima alikuwa akitembea kwa tahadhari ya hali ya juu sana kwani tayari alikuwa akijua huwenda anawindwa na aliamini msemo wa wahenga

‘Muwinda huwindwa.’ Ijapokuwa alimini kuwa kugundulika itakuwa ngumu kutokana na jinss alivyojibadili, hiyo haikumpa ujinga wa kubweteka kwani alijua wazi kuwa kuna watu ni wataalam wa utambuzi hata ujibadili vipi. Aliendelea kuvuta hatua huku macho yake yaliyofichwa nyuma ya miwani myeupe yakiendelea kupepesa huku na huku kuona kama atamshuku mtu yeyote kumfatilia.

Baada ya kupita hapa na pale, machale yakaanza kumcheza, mara kwa mara mwili wake ukamsisimka na nywele kusimama, akaheshimu hisia yake, maana tayari alijua kuwa eneo hilo si salama. Akasimama katika afisi mojawapo ya kuuza tiketi za makampuni mbalimbali, akaingia ndani yake na kujifanya kuuliza kama anaweza kupata ndege ya kuunganisha mpaka Muscat. Ilikuwa ni hila tu kwani tayari aliona vijana wawili

nyumaye wakimfuatilia kwa chati, akawatilia shaka na sasa akataka kuhakikisha kama hisia yake iko sahihi au la, hisia ya sita.

Baada ya kujibiwa kuwa ndege ya kuunganisha itapatika baada ya saa kumi na saba, akageuka nyuma tayari kwa kutoka, mara hii akagongana macho na wale vijana, mmoja alikuwa chotara na mwingine mzungu kabisa.

You are welcome! Akajisemea moyoni kisha akatoka katika afisi

ile na kuelekea chooni. Nao hawakusita wakamfuata kwa kugawana, huyu upande huu na huyu upande wa kule, wakijaribu kwa nguvu zao zote wasijulikane naye kumbe walikwishacheza patapotea, Chameleone hakuwa mtu wa kufuatwa kizembe namna hii.

Salamu nilizowapa haziwatoshi! Akajisemea huku akiingia ndani ya choo na kasha kwenye sinki lakunawia mikono,

akaweka begi lake chini na kufungua bomba la maji. Mara tu baada ya kufungua maji akajikuta hayuko peke yake baada ya kuona taswira ya mtu wa pili kwenye kioo.

“Usiumize kichwa, cha muhimu ni kufuata tu nitakachokwambia,” Yule jamaa akamwambia Chameleon .

“Itategemea natii amri yako wewe kama nani!” akamjibu

huku akiwa ametulia na macho yake yakiwa kwenye kioo.

“Napenda sana watu jeuri kama wewe, haya geuka utoke nje taratibu, boss anataka kukuona,”

“Boss?”

“Ndiyo, Boss ana shida na wewe, shida nyeti kasha atakuacha uende zako,” Yule kijana akamwambia Chameleon. Mtu mzima akabaki kimya mbele ya kioo kile, akimtazama kijana Yule kupitia kioo hicho

hakumwona kushika silaha ya aina yoyote, akaamini kwa vyovyote mtu huyo anajiamini sana kimapigano yaani mapambano ya bila silaha. Si kwamba mzee huyu hakuwa anajua michezo hiyo, la, ila alijiuliza kwa nini huyu *dogo* anajiamini namna hii. Akageuka na kumtazama kijana huyo.

"Sikia dogo! Kamwambie bosi wako, kama ana shida na mimi basi aje anifuate hapa hapa, ila

mimi sina muda wa kumfuata mtu, nina muda wa kujisaidia na kuondoka zangu basi. Tena kmwambie kuwa mkojo wangu una thamani kuliko yeye kwa hiyo asinisumbue…”

“Aaaaaa hah! Hah! Hah! Hah! Unajua unaongea na chatu ee, angalia asikumeze bila kukulainisha kwa mate…” akajitapa. Mtu mzima akaendelea kunawa taratibu kana kwamba hakuna hatari yoyote katika eneo

hilo lakini akilini mwake tayari alikuwa akifikiri ni jinsi gani atamwonesha kijana huyo kuwa *'mtu mzima dawa'*.

Wakiwa katika mazungumzo hayo mlango ukafunguliwa na yule kijana wa kizungu akaingia ndani ya chumba kile.

"Hey, boss is waitin enh!" akamwambia mwenzake na ni wakati huo huo Chameleon alipogeuka kwa kasi na kumshindili akonde zito kijana

wa kwanza. Konde ile lilitua sawia katika shavu la kushoto na kung'oa meno kadhaa. Yule kijana akayumba na kuanguka chini, huyu aliyeingia baadae, akachomoa bastola kwa minajiri ya kumshambulia mzee huyu, lakini alichelewa sekunde kadhaa, tayari Chameleoni alikwishamfikia na kuukamata ule mkono, akajigeuza na kugeuka na kijana huyo kumwelekea yule wa kwanza. Risasi iliyofyatuka katika bastola ile aina ya PPK ikazama

katikati ya paji la uso la kijana wa kwanza ambaye alikuwa anajaribu kuinuka kutoka pale sakafuni, akarudi chini akiwa marehemu.

Pigo moja la pepsi likatua mbavuni mwa huyu kijana wa kizungu, kisha Chameleaona akamwachia na kumsukuma kando. Kama kuna kosa ambalo alilijutia ni hilo. Yule kijana wa Kizungu, alijipanga kimapigano na kumteremshia kichapo hevi

mzee yule na kumwacha hoi sakafuni.

“Mi huwa siongei sana, simama twende!” akamwambia Chameleon wakati huo akiwa chini akijizoazoa. Yule jamaa akamsogelea kwa upande wa nyuma mzee mziama akamwona vizuri kabisa kijana huyo, kisha yeye akajifanya yuko hoi kweli kweli.

Jifanye mnyonge unapokuwa na nguvu na jioneshe una nguvu

unapokuwa mnyonge ili umshinde adui! Akaikumbuka mbinu hii ya kivita 'Art of War' ambayo ni moja katika hatua za mafunzo yake siku za nyuma. Chameleon akajiangusha tena chini huku akifuta damu kinywani mwake kwa kutumia mgongo wa kiganja cha mkono wake.

"Ujanja wako ni kwenye silaha tu ila kwa mikono hujiwezi, mbwa wa ndani we!" Yule kijana

akamwambia na kumsukumizi tusi. Kichwani mwake mzee huyu alikuwa akitamani muda wowote waingie ndani ya choo hicho lakini haikuwa hivyo.

“Inuka!” Yule jamaa akamwamuru, kisha akavuta hatua na kukamata kipande cha bomba ukutani hapo, akaking’oa na kukishika kwa mkono wake wa kuume. Pigo moja likatua mbavuni mwa mtu mzima, maumivu yake yalimwacha

akigugumia tu. Pigo la pili, la tatu.

“Inuka!” akamwamuru.

“Ni-ki-i-nu-ka hapa u-ju-e ndi-yo ki-ki-fo chako!” Chameleoni akajibu kwa shida.

“Hah! Hah! Hah! Inukaaaaa!!!!” akamtandika bomba lingine lililotua mgongoni mwake, mzee huyu akinuka taratibu na kutazamana na kijana huyu wa Kizungu.

“Where is my death?” akauliza huku akianza kumfuata na kuweka lile bomba vizuri kwa pigo lingine. Kinywani mwa Chameleon bado damu zilikuwa zikimsumbua. Akamtazama kijana huyo kwa vipimo vyote kisha akainua mkono wake, kwa kutumia mgongo wa kiganja chake akajifuta tena zile damu lakini mara hii kulikuwa na kitu kingine zaidi.

“You asked for your death? Here it is…” akamwambi huku akikunja ngumi kwa nguvu, na mkono wa kuume ukashika saa aliyokuwa ameivaa. Hii haikuwa saa kama saa, ilikuwa ni silaha inayobeba vitu kama misumari. Ukiitazama ni saa lakini ndani mkono wa shati kuna kitu kingine zaidi, akabonya kitufe kimoja na msumari wenye urefu wa inchi nne ukafyatuka na kuzama katikati ya paji la uso la

Yule bwana, akabaki katoa macho.

“Have a nive day!” akamwambia, na yule jamaa akajibwaga chini kama gunia, hana uhai. Mtu mzima akaendea lile sinki na kunawa harakaharaka kisha akainua mkoba wake na kutoka nje, akaufunga mlango na alipogeuka kuutazama ndipo akakuta kibao kimeandikwa ‘OUT OF ORDER’.

Ndiyo maana watu hawakuwa wakiingia! Akawaza. Akakamata kitasa kwa nguvu zote na kukivunja kisha akakitia kwenye ndoo ya takataka.

Huku nje The Cobra aliendelea kusubiri vijana wake, tayari gari yake alikuwa amecha buti wazi kwa ajili ya kumpakia mtu huyo. Akasubiri na kusubiri, kimya, kila mara alikuwa akitazama saa yake, hakuna mtu. Dakika kumi baadae, akasikia

sauti ya ndege inayoacha ardhi, alipotazama kwa makini akaona tu picha ya twiga kwenye mkia. Ndipo akakumbuka kuwa ni ndege hii iliyotakiwa kumbeba mtu wake. Akatoka haraka kwenye gari na kuubamiza mlango, hatua zake zikamfikisha katika eneo la wasafiri. Alishtuka baada ya kuona makundi ya watu na askari wakijazana katike eneo la vyoo vya nje.

“Mh!” akaguna, na yeye akaungana nao kwenda kushuhudia nini kilichomo. Vurugu ya askari na wananchi haikuwa ndogo kila mmoja alikuwa akitaka kushudia na kujua nini kilichotokea. The Cobra alitumia mabavu yake mpaka akafika karibu kabisa na mlango ule na alipopiga jicho ndani akashuhudia miili miwili imelala bila uhai huku askari wakichukua vipimo. Mzungu huyu mwenye mwili uliyoshupaa

hakuyaamini macho yake baada ya kushuhudia kuwa ni viajana wake aliyowatuma kumleta mtu huyo au kummaliza kabisa kama akileta ubishi.

Kati ya vijana wake wte anaopenda kuwatumia katika kazi kama hizi yaani za hatari, basi hawa walikuwa mstrai wa mbele kabisa. Lakini mara hii walizidiwa ujanja, The Cobra hakuamini na wala hakujua nini kimewapata, alichokishuhudia ni tundu la

risasi katika paji la uso la yule chotara na kitu kama msumari katika paji la yule mzungu.

* * *

Chameleon, alifungua mkanda wa isalama kwenye kiti cha ndege, akajiweka vizuri na mara hiyo mwanadada mhudumu wa ndege akamfikia.

“Unajisikiaje baba?” akamwuliza.

“Najisikia afadhali…”

“Labda unahitaji msaada wowote?”

“Hapana asante!”

Yule mwanadada akapita na kuendelea kuwahudumia watu wengine. Chameleone akasimama na kukiacha kile kiti, akaelekea nyuma kabisa ya ndege hiyo ambako kuna huduma ya choo. Akaingia na kujifungia ndani, akatumia kama dakika tano kusukutua kinywa chake kwa kuwa kilikuwa na mabaki ya

damu. Mwili wake nao ulikuwa na maumivu ya hapa na pale.

SURA YA TATU

DAR ES SALAAM

Katika Ikulu ya Dar es salaam, Rais wan chi alikutana na watu wake muhimu katika swala zima la usalama. Wote walibakia kupigwa na bumbuwazi baada ya kupokea taarifa hiyo ya mauaji yaliyotokea mapema asubuhi ya siku hiyo. Usiku huo kwao

ulikuwa ni muda tulivu wa kujadili na kuamua nini cha kufanya juu ya hilo. Mkuu wan chi, aliyekuwa ndiye mwenyekiti wa kamati hiyo ya Baraza la Usalama la Taifa alifikiri kufanya juu chini na kuwasaka wauaji hao. Lakini makamanda wake wakamshusha hasira na kumjuza ukubwa mzima wa adui wanayemfikiria.

“Ni vibaraka tu! Lazima wanatumiwa na makaburu, sasa

kwa uwezo wetu hatuwezi kuwavamia kivita kwa kuwa pia hatuna ushahidi kamili kwa kuwa hawakuonekana katika uwanja wa mapambanao," Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa akasema.

"Ni kweli, hata hivyo Yule aliyetumwa amefanya kazi kubwa ijapokuwa watu wote wameuawa lakini amefanya kazi, laity angejua nini kitatokea nahisi kama tungepoteza watu wasingekuwa

wote," IGP naye akaongeza katika hilo.

"Taarifa nilizozipata ni kuwa Waziri Kitwana amefia mikononi mwa mtu huyu, ina maana alishamwokoa ila sema tayari alikuwa na hali mbaya sana, asingeweza kupona!" Mwenyekiti wa kikao akatoa taarifa.

Wakiwa katikati ya kikao hicho mara mlango ukafunguliwa na katibu muhtasi wa Rais anayeratibu maswala mbalimbali

akaingia, moja kwa moja akamwendea Aide De Camp na kumnong'oneza kitu, na mwanajeshi huyo naye akaongea na Rais kisha Yule mwanadada akatoka ukumbini.

"Tuna mgeni wa dharula ninahitaji kuonana naye! Naomba tuahirishe kikao mpaka kesho asubuhi hapahapa, tuweze kufikia muafaka!" Rais akasema huku tayari akisimama na wengine wote wakasimama kwa

ukakamavu kisha yeye akaondoka na kuingia kwenye afisi nyingine nadi ya jengo hilo hilo.

Katika afisi hii alikutana na Chameleon. Mara tu baada ya kushuka ndegeni hakwenda popote kwani ilimpasa kufikisha taarifa hiyo kwa Rais hata kama ni usiku namna gani. Akamwelezea hali nzima iliyokuwa huko Rhodesia na alimhakikishia mkuu huyo kuwa wanapambana na watu wenye

ujuzi wa hali ya juu sana. Baada ya mzungumzo ya takribani saa tatu hivi, mnamo saa tisa usiku wakaagana na mzee huyu akarudi nyumbani kwake kwa mapumziko.

Asubuhi kulipokucha, majira ya saa tatu hivi ndipo kamati ile ilikutana tena kwa mazungumzo juu ya sakata zima la mauaji. Mwenyekiti wa kikao akatoa ripoti fupi aliyoipata kutoka kwa Chameleon, ilikuwa ripoti nzito

ambayo kila mmoja kama si kutetemeka basi alihisi BP ikipanda juu. Mwisho wa kikao hicho wakaamua mambo makubwa matatu; kwanza kushughulikia maazishi ya wapendwa wao saba waliokufa huko Rhodesia na kuwazika nyumbani kwa heshima zote, pili kutazama kwa mapana juu ya watu waliofanya shambulio hilo na tatu ni kufanya kila minu za kiintelijensia ikiwezekana

kuwakamata na kuwafikisha mbele ya sheria.

Kikao kikafungwa na majukumu yakagawanywa, kazi ikaanza. Kutoka Ikulu Chameleon akapangiwa kazi nyingine kwani yeye alikuwa akiwajibika kwa Rais moja kwa moja.

* * *

Katika ukumbi wa Lango la Jiji, Magomeni, Chameleon aliketi katika kiti kile kile

ambacha mara ya mwisho aliketi na msichana Stella. Alijariu kuvuta picha kujaribu kuona ni jinsi gani atampata msichana huyo ambaye siku kama tano nyuma alitekwa mikononio mwake. Kwa hili alihisi ana hatia, kama isingekuwa kazi basi hakika angeweza kumpata Stella. Mtihani uliokuwa ukimkabili ni kujuankama binti huyo yuko hai au ameshadhuriwa kwa sababu yeye alikiuka lile aliloambiwa na mtu Yule. Kila alipowaza hilo

alipata kiu ya kutaka kujua kuwa ni uhusiano gani upo kati ya watu hawa waliomteka Stella na wale waliofanya shambulizi lile kule Rhodesia.

Lazima nijue, na nataka nijue usiku huu. Na nikijua nitahakisha nawasafisha wote, ama zao ama zangu! Akawaza ndani ya nafsi yake huku akiweka sawa kofia yake kubwa. Alipotaka kuinuka akajikuta akishikwa began a kurudishwa kitini. Mbele yake

akaketi mtu ambaye sura yake haikuwa ngeni kwake ila hakukumbuka ni wapi aliwahi kumwona. Haikupita hata sekunde arobaini kati yao, mhudumu akaweka bia mbili mezani zikiwa zimefunguliwa.

"Karibu tusherehekee ushindi," mgeni Yule akamwambia Chameleon.

"Ushindi gani?" Chameleon akauliza kwa mshangao.

“Huujui? Si ushindi wa ngumi kati ya wale mabondia wawili hapo majuzi,”

“Huwa sishabikii ngumi!”

“Mbona ulikuwa pale?”

“Sikuwapo!”

Chameleone almstaajabu mtu huyo, hakumuona katika ukumbi wa Railway siku ya pambano lakini anajuaje yote haya. Kengele za hatari zikalia kichwani mwake, akamtazama kwa tuo mtu huyo.

“Karibu kinywaji!”

“Sinywi bia,” akajibu kijeuri huku akiisogeza ile chupa kwa mgeni wake na yeye kusimama. Hasira zikawaka ndani ya kichwa cha mzee huyu, alitamani amzabe makofi mtu huyo aliyekwenda kumwaribia siku yake lakini hakutaka kuanzisha vurugu ukumbini hapo kwani wanaomjua walimheshimu sana. Akavuta hatua na kupita kwenye meza kadhaa mpaka katika

mlango wa kutokea nje. Manyunyu ya mvua yalikuwa yakiendelea kunyurunyuta wakati mtu mzima huyu akiwa katika harakati za kufungua mlango wa gari yake aina ya *Ford Cortiner*. Mara baada ya kufanikiwa akaingia na kuketi nyuma ya usukani tayari kwa safari yake. Akatia injini moto nayo ikakubali pasi na shaka, akaondo taratibu katika maeneo hayo. Gari ilipokaa sawa nay eye kutulia kwenye usukani akisikiliza muziki

wa *Super Mnyanyuo*, akahisi kama kuna kitu katika siti ya nyuma yake, kabla hajafanya uamuzi wowote akajikuta kapigwa kabala maridadi kabisa. Kwa kabala ile mzee huyu akatulia, na kwa kuonesha kuwa jamaa wamejiandaa, tayari mwingine kutoka kiti hicho cha nyuma alikwishawahi kukaa mbele na kuanza kuendesha gari hiyo huku mwenzake akimvuta nyuma mzee huyo.

Baada ya kumweka sawa katika kiti cha nyuma, akamwachia, “tulia! Kama unayataka maisha yako usilete kokolo, maana ujue hapa upo jirani na kifo…” kijana huyo akamwambia. Chamelleone akatulia kama alivyoamuriwa maana tayari alihisi ubavuni mwake kuna domo la bastola limemgusa.

Kuna wakati wa masihara ila kama huu, hapana yapasa kuwa mpole kama kondoo! Akawaza

na kuendele kutulia huku akihisi kiu, maana kabali ile ilipigwa kiujuzi sana, zamani tuliita *'kabali namba sita'*. Yule bwana aliyemweka mtu mzima huyu nyuma akachukua kitu kama pafyumu hivi, akampulizia usona Chameleon kisha yeye akawahi kujizuia pua yake na mwenzake akafanya vivyo hivyo. Chameleon akajua tayari, hiyo ni dawa ya usingizi, hakufanya chochote, akatulia na kuchukuliwa na usingizi mzito akisindikizwa na

wazo moja tu, ‘anayetaka kukuua hawezi kukupa dawa ya usingizi’.

* * *

“Chameleeeeeeooonnn!!!! Chameleeoooonnnn!!!!!”

Sauti hiyo ya kuita kwa kilio ilimdikia mzee huyu kwa taabu sana akiwa chini sakafuni, akahisi akitikiswatikiswa kwa nguvu kana kwamba anaamshwa kutoka usingizini. Nje ya usingizi wake, Stella alikuwa akimtikisa mzee huyo ambaye alibwagwa ndani ya

chumba hicho akiwa hana fahamu kwa usingizi mzito. Binti huyu alikuwa akilia kwa kwikwi mpaka sauti yake ikaanza kukauka kwa kumwita bwana huyo aliyekuwa kama mfu hapo chini.

Masaa mawili yaliyopita…

Mlango wa bati gumu katika godown kubwa ulisukumwa na watu wawili wakaingia ndani ya cumba hicho wakiwa wamebeba mtu mzegamzega. Ndani ya

chumba hiki kisicho na kitu hata kimoja ndipo Stella alimotupwa siku tano au nne nyuma.

"Tumekuletea bwana 'ako, mle fungate kabla ya masaa mawili yajayo… maana mtakufa pamoja leo hii…" mmoja wa wale vijana akasema kisha wakamtupa chini mzee Yule pasi na huruma. Stella hakujua ni nani huyo kutokana na mwanga hafifu wa chumba kile, walipotoka na kuufunga mlango akausogelea mwili ule

kuutazama na ndipo alipopigwa na butwa kumwona Chameleon, akaanza kumwamsha na kumwamsha lakini mzee huyo alikuwa kimya. Upumuaji wake ulikuwa chini mno, kwa ujumla hakuonesha dalili za kuendelea kuishi. Alipoona hakuna dalili za bwana huyo hata kufumbua macho akaketi kwenye kona ya banda hilo na kuanza kulia kwa uchungu. Baada kama ya saa moja na dakika kadhaa kupita hivi, mlango ule ukafunguliwa

tena na vijana wale mara hii wakaingia wakiwa wanne. Binti huyu aliwatambua tu kwa sauti zao kwani daima walipenda kuficha sura zao, na isitoshe aling'amua kuwa si Watanzania kutokana na lafudhi ya Kiswahili waliyotumia.

Mara hii walikuwa kwenye suti safi na tai maridadi kabisa shingoni mwao, viatu vye kiwi safi vilivyong'azwa kwa mwanga wa kutoka nje.

“Sikia! Tunakupa maagizo ambayo utampa bwana wako mkishafika ahera. Mwambie kwa kukaidi agizo tulilompa, tunamuua yeye na wewe. Na pia kwa kulipiza kisasi kwa ndugu zetu huko Rhodesia kifo cha mtindo huu kinamhusu. Tunataka ufe naye ili umpe haya maagizo, sawa?” mmoja aliongea na wale wengine wakabaki kimya.

“Silowane, weka mtoto huyo…!” akatoa maagizo na

huyo Silowane akachukua kimkoba kidogo na kukifungua ndani, humo akatoa kitu kama saa hivi lakini kilikuwa ni bomu linalotumia saa. Akagusa hapa na pale akatega dakika thelathini zijazo kisha akaondoa pini ya usalama na kuliweka juu kiasi kwa kutumia ngazi, kisha akashuka na kuiondoa hiyo ngazi na kuiweka nje ya chumba hicho. Kisha kijana mwingine akachukua dumu la lita ishirini

lililoja petrol na kuimwaga kuzunguka eneo hilo.

"Goodbye!" Yule kiongozi akaaga na kisha waktoka na kufunga mlango kwa nje. Dakika moja iliyofuata, Stella akasikia mngurumo wa gari ikiondoka kwa kasi. Hakuna alichoweza kufanya zaidi ya kulia, kila alipomwamsha mwanaume huyu hakuamka hata kidogo. Ilipofika bado dakika tano mlipuko ule utokee lile bomu likaanza kupiga

alarm kila baada ya sekunde thelathini. Alarm hii ikamfanya Stella agundua hatari iliyopo, alikumbuka kuwa aliwahi kuona kitu kama hiki kikilipuka vibaya kwenye filamu moja ya *Charles Bronson,* akaogopa. Ndipo alipoanza kupiga kelele kwa nguvu na kumwita mtu huyo kwa fujo zote.

Rejea tukio…

"Chameleeeeeooooonnnn!!!!! Aaaaaaaiiiiiggggghhhhhh!" akaita

kuangusha kilio alipogundua kuwa dakika moja na sekunde chache zimebaki, hakutaka kuamini kama ni kweli uhai wake unakatika namna hiyo huku akijiona, ni heri hata kama ni yeye angekuwa ndiye aliyelaal hapo hana fahamu. Mara hii akaanza kuita huku akimpigapiga ngumi na makofi, akimfinya na kumsukasuka huku na huko akilia.

Ndani ya usingizi, Chamelleon alikuwa akihisi zile kelele nay eye aliona kama anaota, mwanzoni alikuwa anasikia kwa mbali na sasa alihisi zikiwa karibu zaidi, ghafla macho yake yakafumbuka kwa taabu, akapiga chafya kutokana na vumbi la sakafu hiyo. Akajaribu kugeuka lakini alihisi kichwa ni kizito sana.

“Chameleon! Asante umeamka, asante Mungu, tunakufa baba tunakufa!” Stella

alilia huku akionge amfululizo. Neno hili ‘kufa’ ndilo likamfanya mwanaume huyu mzee apate nguvu na hata kutambua kuwa ni Stella aliye mbele yake.

“Stella, wewe ni Stella au?” akauliza.

“Ni mimi, ni mimi kabisa!!!” akajibu huku akiinuka, na Yule mzee naye akajikongoja kuinuka akapepesuka kidogo kisha akatulia.

“Tunakufa! Tunakufa baba!” akamwambia huku akimwoneshea pale bomu lilipo. Chameleone aliposikia ile alarm ikianza kupiga kwa sekunde moja moja akajua kazi imekwisha. Haraka akili yake ikarudi kazini, akamsukuma Stella, “lala chiniiiiiiii!!!!” kisha yeye akapiga hatu mbili, za kukimbia, ya tatu akaruka na mguu mmoja ukakanyaga ukuta na mkono wake ukalifikia lile bomu, akalinyakua na kushuka chuini

kama mzigo, haraka akafungua mkanda wake na kupachika kile chuma cha kufungia mkanda sehe ya kukaa *'safety pin'* huku akifumba macho kusubiri nini kitatokea, kimya. Akafumbua macho taratibu na kutazama lile bomu mkononi mwake, kisha akauvuta ule mkanda taratibu kabisa na kufanikiwa kuuvua wote. Akageuka na kumtazama Yule binti akiwa kalala kimya sakafuni.

“Stella!”

“Be!” akitika.

“Tumepona!” akamwambia huku akitabasamu.

“Kweli?” Stella akauliza.

“Ee kweli,” akamjibu na binti Yule akasimama na kumkumbati kwa nguvu huku mzee huyu akiuweka mbali mkono wenye kile kilipuzi. Wakanyonyana ndimi kwa sekunde kadhaa kabla ya kukumbuka kuwa wapo hatarini.

“Tuondoke!” akamwambia na kuuendea mlango, akaujaribu na kugundua umefungwa kwa nje. Mara wakasikia tena mngurumo wa gari likisimama na milango kubamizwa.

“Mamaaaa wanarudi, wanarudi!” Stella akaanza kulia.

“Shhhhh!!! Tulia,” akamwambia huku akimvuta na kumweka nyuma yake kisha wakajibanza pembezoni mwa mlango.

“Wewe hukuseti muda vizuri, kwa sababu ni dakika tatu sasa ilitakiwa ilipuke…” wakasikia sauti zikisema haya kutoka nje.

“Hamna mi nimetega sawasawa, kwani hii ni mara yangu ya kwanza kutega!” mwingine akagoma.

“Fungua mlango!”

Mara mlango ukafunguliwa na yule jamaa akaingia ndani akifuatiwa na mwenzake, wote akilia yao ikiwa juu ya bomu lao,

pata potea. Ni nukta hiyo hiyo, alipingia mtu wa pili tu na kupita kama mita mbili hivi, Chameleona akamvuta Stella na kumsukuma nje kisha akafuatia yeye.

"Wanatorokaaa!" huyu mtu wa pili akasikia vishindo na kupiga kelele kwa mwenzake, haraka wakajaribu kuwawahi nje huku wakiwa tayari bastola mikononi. Mzee mzima alijirusha hewani na kumtandika kijana wa mbele

miguu ya kifua, Yule jamaa akaanguka ndani ya kile chumaba akimpamia mwenzake, wote wakaenda chini na bastola zao zikiwatoka mikononi.

“Funga mlango, usukume!” akamwambia Stella naye akajitahidi akaufunga na Chamelleona akautia kufuli iliyoning’inizwa hapo nje.

“Na sasa ni zamu yenu!” akawaambia kisha akamshika mkono Stella na kukatiza hapa na

pale mpaka karibu na mlango wa kutokea nje. Akatazama kile kilipuzi mkononi mwake, bado kipo salama.

Sekunde thelathini zinawatosha! Akawaza na kuiondoa ile pini ya mkanda na lile bomu likaanza kuhesabu sekunde za mwisho. Kwa nguvu zote akalirusha mpaka likaugonga ule mango kisha yeye akamvuta Stella nje na kuingia kwenye gari waliyokuja nayo hao jamaa,

bahati nzuri ilikuwa ikunguruma, akatia gia, ile anataka kuondoa tu, mlipuko mkubwa ukatokea, kishindo kikasikia, ule msukumo ukaitikisa gari na kuitupia upande wa pili, ikajibwaga vibaya. Wale vijana wawili na suti zao wakateketea mpaka mfupa wa mwisho. Godown lile likawaka na kuwaka ukizingatia walikuwa wamemwaga petrol.

* * *

Siku iliyofuata….

Hospitali ya Muhimbili

Chameleon alirudiwa na fahamu baada ya siku mbili, pembeni yake alimwona mkewe na mtoto wake mkubwa wakiwa wameketi.

“Nipo wapi?” akauliza.

“Muhimbili…” mwanaye akamjibu.

Mzee huyu akatulia kwa sekunde kadhaa, akifumba macho na kufumbua, akaifanya hivyo mara kadhaa. Aliporudiwa

na fahamu sawasawa, ndipo akagundua kuwa ana POP mkononi na mguuni.

“Hah! Nimevunjika? Na Stella yuko wapi?” akauliza.

“Stella ndiyo Yule mwanamke wako mlikutwa naye kwenye gari sivyo?” mkewe akaanza kulalama.

“Niambie yuko wapi, au niitie nesi,” akasema.

“Mwanaume Malaya wewe, hivi unaona mi sikutoshi, watoto wote niliokuzalia, mpaka una

tembea na hako katoto kadogo, ona sasa unapata ajali za aibu, watu wote wanajua umefumaniwa na mume wa huyo kasichana wako akataka kuwaua…”

“Mimi? Maneno gani hayo mke wangu? Enh! Yaani dah!” Chameleon akalalama na mara mashine ya kucontrol presha ikaanza kupiga kelele. Akajilaza kitandani kimya. Mwanaye akawahi kupiga kemgele ya

hatari, muuguzi akafika na kukuta hali mbaya, naye akaomba msaada kwa wengine, wakafikana na kukuta mapigo ya moyo yameshuka kiasi kwamba sekunde yoyote unasimama. Hakukuwa na jinsi wakajaribu kufanya *'mouth to mouth respiration'*, haikusaidia ikabidi waanze kumshtua kwa umeme!

SURA YA NNE

Dar es salaam, February 15, 1990

Utawala wa kibeberu wa Makaburu nchini Afrika ya Kusini uliionekana wazi kushindwa kuhimili vishindo vya mtu mweusi. Nchi za Kusini

mwa jangwa la Sahara zilikombolewa na kupata uhuru wake katika miaka tofauti zikisaidiwa hapa na pale na taifa la Tanzania ambalo ama liliwapa elimu ya kiuongozi na siasa viongozi wa vyama vya ukombozi katika nchi hizo au kutoa mafunzo ya kijeshi katika kupambana na vibaraka wa watu hao. Kambi mbalimbali zilifanyika nchini kama kule Mazimbu Morogoro na Frelimo mkoani Iringa n.k.

Mzizi mmoja ambao ulibakia kung'olewa mpaka mwaka huo ilikuwa ni Afrika ya Kusini pekee ambayo bado ilikuwa ikiongozwa na Rais mzungu, Bw. Frederick De Clerk huku mtu mweusi akinyimwa haki yake na kukandamizwa kila uchao. Si kwamba hawakupenda kuwa huru ila walikosa umoja wa kitaifa ambao ungewapa nguvu ya kupambana na kaburu. Weupe hawa kila walipoona au kugundua nani anaweza kuwaunganisha,

walimkamata na kumtia ndani au hata kumuua kabisa kama tunavyosoma katika vitabu vya historia.

Kati ya wengi wa waliokamatwa, alikuwamo Nelson Mandela ambaye ushupavu wake kisiasa na kupinga ubaguzi wa rangi vilimfanya awe kinara katika ukombozi wa Afrika ya Kusini. Makaburu walimhara na hawakuwa na njia nyingine zaidi

ya kumhukumu kifungo cha maisha mwaka 1964, tarehe 12 Juni. Kama wao walijua kuwa huo ndo utakuwa mwisho wa nguvu ya mtu mweusi, waliula wa chuya. Afrika iliamka, ikapiga kelele. Tanzania ilikuwa mstari wa mbele kabisa chini ya Baba wa taifa, kuitaka Afrika ya Kusini huru. Na mnamo tarehe 11 Februari ya mwaka 1990, siku ya jumapili, ‘mpiganaji’ huyo aliachiwa huru. Kwa Afrika ilikuwa kama nuru mpya,

pambazuko jipya, na kwa hili umoja wa kitaifa ulianza kuonekana.

* * *

Mwaka 1992 kabla Makaburu hawajaachia madaraka kwa weusi, ujumbe mzito ukatua katika Jiji la Dar es salaam, ikiwa ni hatua nyingine ya mazungumzo ya upatanishi kati yao na Tanzania. Katika ujumbe huu wa watu watano alikuwamo mwanamama Margaritha Kasbarai ambaye sasa

alikuwa akinyemelewa na utu uzima, si kigoli kama miaka ile. Mwingine alikuwa Waziri wa zamani, Mc Cain na wengine watatu ni wapya kabisa.

Tanzania ikaunda tume nyingine mpya baada ya miaka kadhaa tangu tukio la Rhodesia litokee, katika tume hii alikuwapo mwanasheria mkuu wa Serikali, afisa wa juu wa uhamiaji, mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa, Waziri wa Mambo ya

nje na wajumbe wengine wachache. Jumla walikuwa watu kama tisa hivi. Kikao hicho kilifanyika ndani ya Hoteli ya Kilimanjaro.

“Kuja kwetu hapa, kama mnavyojua ni kwa sababu ya swala ambalo hatujaliweka sawa mpaka sasa. Tunajua kuwa serikali ya Tanzania imefanya mengi sana katika kuzikomboa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, lakini katika haya mengi

pia imetutia hasara katika miundo mbinu mingi na isitoshe kuna watu wetu ambao inawashikiia katika magereza yake. Hatuna haja ya kurudia haya yote isipokuwa sasa tunataka kufikia muafaka na tupatane kwa hili, lazima Tanzania ifidie hasara tuliyopata na iwaachie huru watu wetu…" McCain akaeleza kwa sauti yake nzito, huku wenzi wake wakitikisa vichwa juu chini kama ishara ya kukubaliana na hayo. Upande wa Tanzania

walikuwa wametulia wakisikiliza yote hayo.

“Mnasema magereza yetu yamewashikilia watu wenu, hatukatai, lakini je mnaweza kutuambia kwa nini yamewashikilia? Na kama mnataka serikali yetu ifidie hasara mliyopata kwa kuharibu miundo mbinu mbalimbali, je mmewahi kufikiria kuhusu hasara ambayo mmetupatia Waafrika tangu mje hapa barani? Je mnaweza

kuifidia?" Wazirio wa Mambo Ya nje Bwana Njenje Kanjenjela akaijibu kauli hiyo kwa maswali.

"Ndugu…" akasimama Margaritha, "…hatupo hapa kutupiana maswali…" akazungumza kwa kiingereza safi, "…mnatakiwa mjibu hoja.

"Hakuna hoja ya kujibu!" akajibu mkurugenzi wa usalama wa taifa, "…hata ninyi mna watu wetu mikononi mwenu, na tunajua si kwamba hatujui,

tunawataka hao watu, mkiturudishia nasi tutawarudishia, mkilipa hasara mliyosababishia Mwafrika na sisi tutalipa… mkono kwa mkono…" akaendelea.

"Hilo haliwezekani!!!! Na wala hatuna watu wenu mikononi mwetu…"

"Msitufanye mabwege! Tunajua mna watu wetu na tunawajua mpaka majina yao, na isitoshe tunajua kuwa mlitufanyia

hujuma katika mauaji ya mwaka 1984 pale Harare…”

“Sisi! Sisi? Yaani tumewasaidia kupeleleza na kugundua kuwa waasi kutoka Angola, leo mnasema ni sisi…” Mjumbe mwingine wa tume ya Afrika Kusini akajibu kwa jazba. Kwa ujumla kikao hicho kikawa moto, mvutano na mabishano vikawa juu kiasi kwamba hakukuwa na uelewano kabisa.

“Msifikiri sisi hatuna akili, tulishachunguza na tunajua kuwa ni ninyi mliyopanga mauaji yale, bya the way hatuna haja ya kukumbuka machungu, tupatieni watu wetu kumi na moja mnaowashikili huko. Mkitupatia hao, tutawapatia wa kwenu kisha tutakutana kwa awamu ya pili ya mapatano, mlipe fidia na si tutalipa fidia…” waziri wa mambo nje akawa mbogo katika hilo. Sasa kikao kikawa ni

mabishano tu hakukuwa na uelewano kabisa.

“Tusikilizane, hatujaja kugombana, kama watu wenu tumewaacha huru, mmempigania Mandela, tayari yupo huru, sijui nani tena mnamtaka awe huru. Sisi tunataka tumalize haya kabla ya uchaguzi mkuu wa kidemokrasia utakaofanyika labda mwaka 1994, ili kila kitu kianze upya,” Mjumbe mwingine

aiyekuwa katika serikali ya kikaburu akangea kwa upole.

“Hatumzungumzii Nelson…. Nini mmewakamata Watanzania wetu kumi na moja, ndiyo tunaowataka…” yue waziri wa Tanzania akasema na hapo sasa almanusura ngumi zipigwe ndipo mkutano ukavunjika bila mapatano yoyote.

Sellina kutoka katika meza moja aliyekuwa akichapa taarifa yote hiyo kadiri ya mazungumzo

akaitazama saa kubwa ya ukutani, ikamwambia ni saa kumi na moja kamili. Na kwenye ratiba ilikuwa saa hiyo hiyo mkutano huo uwe umekwisha. Wajumbe wakatawanyika hata bila kupeana mikono, wale wa kutoka Afrika Kusini wakaingia kwenye magari yao na kusindikizwa na pikipiki ya polisi kwenda Uwanja wa Ndege tayari kwa safari maana ndege yao ilitakiwa kuondoka saa kumi na mbili jioni. Wajumbe kutoka Tanzania wakakutana

kwenye chumba kingine falagha kwa mazungumzo.

Selina, mwanamama wa umri wa kati, aliyekuwa akihudumu katika idara ya Usalama wa Taifa alikuwa mmoja wa wajumbe waliokuwa wakisikiliza kila kitu, zaidi ya hapo alitakiwa kuandika kila kinachzungumzwa kwa ajili ya kumbukumbu ya afisi. Mkononi mwake alikuwa tayari na karatasi kama ishirini na nne hivi zenye muhtasari wa kikao

hicho. Akamkabidhi bosi wake, kisha yeye akatoka na kuwaacha wakubwa hao wakiendelea na mzungumzo.

"Na sasa hivi inabidi tuimarishe ulinzi, hawajamaa wanaweza kutuma makomandoo kuja kuwatoa watu wao…"

"Thubutuuuu, hawawezi hata kidogo, tumeimarisha magereza na isitoshe tumefunga katika selo za siri kabisa, hata askari wenyewe wengine hawajui

walipo, wasitusumbue na wasitake kutupelekesha," akajibu waziri.

"Sasa kikao kimevunjika, nini kitafuata?" mjumbe mwingine akauliza.

"Tutapeleka taarifa hii kwa Mkuu wa Nchi na yeye ndiye atakayeamua juu ya hili, ataongea na De Klerk watajua nini cha kufanya lakini zana ya mkono kwa mkono ipo sawa kabisa…"

"Yeah of coz!"

* * *

Katika ukumbi mdogo wa Ikulu, Dar es salaam, Rais alikutana na tume hiyo siku mbili baadae kupokea taarifa ya kikao hicho. Taarifa ile ikasomwa na kisha akakbidhiwa mkuu huyo.

“Kwa hiyo hakuna muafaka?” akauliza.

“Hakuna muafaka uliofikiwa…” Yule waziri akajibu.

“Hawawezi kuwazuru watu wetu?” akatupa swali lingine.

“Nina uhakika hawawezi, kwanza wameshtuka sana tulipowaambia kuwa wana watu wetu na tunawahitaji…” akaongeza yule waziri.

“Sawa! Swala la fidia wasahau kabisa, ila kwa swala la watu wetu lazima tuwapate hata kama ni maiti zao tutazifukua na kuja kuzika nyumbani. Nitaongea na De Klerk kisha nitawaita tujue

nini tunafanya…” akawaambia na kikao hicho kikahairishwa, wajumbe wakatawanyika baada ya kupata kinywaji cha pamoja.

Bara la Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara, lililipuka kwa furaha baada ya mpigania uhuru mmoja aliyedhulumiwa haki yake na kutupwa gerezani maisha, kufunguliwa kwa nguvu ya mtu mweusi. Wengi wakamshukuru Mwalimu Nyerere kwa jitihada zake za

kupambana na mtu mweupe kwa maneno ya hekima na busara na si mtutu wa bunduki. Ndoto yake ya kuifanya Afrika huru ilizidi kuchanua na kuchukua nafasi katika mioyo ya Waafrika waliokata tama ya hilo.

Mara tu baada ya kuachiwa huru, kama shukrani kwa Watanzania, mwanamapinduzi huyu alitua nchini kuja kukutana nao na kwa mzungumzo na Mwalimu ambaye wakati huo

tayari alikuwa amekwishang'atuka na nchi ilikuwa mikononi mwa Rais mwingine.

Mwaka 1994 Afrika Kusini walipiga kura katika uchaguzi mkuu wa kihistoria na kumbwaga kaburu kisha mtu mweusi kuchukua madaraka na kuongoza taifa lake. Pamoja na yote hayo, bado kaburu alikuwa amewashikilia baadhi ya wapigania uhuru wa Kitanzania katika sehemu fulani fulani za

nchi hiyo, huku Tanzania ikiwa imewashikiliwa baadhi ya majasusi wa makaburu katika magereza yake. Waliwakamata watu hawa kwa kuingia nchini na kufanya ujasusi wao ili kujua jinsi ya kuzifisha nguvu za mtu mweusi, maana walijua kuwa chimbuko na vuguvugu la ukombozi wa Mwafrika ni Tanzania, lakini kwa ushupavu wa vyombo vya usalama vya hapa nchini, waligundulika na kukamatwa katika maeneo

mbalimbali nchini na wengine wakijikuta wanauawa baada kpambana na wapelelezi mahiri kama akina Joram Kiango, Willy Gamba, Mteko Vano na wengine wengi wa enzi hizo. Pia na mamluki kadhaa ambao walilaghaiwa na weupe hao kuziuza nchi zao kwao nao walitiwa ndani na wengine kuuawa kwa kutotii amri ya kujisalimisha.

SURA YA TANO

Aprili 2006

Katika Ofisi za AGI Investment

Kama kuna siku ambazo jua lilikuwa kali na joto la kutisha ni hii, kutokana na hitilafu ya umeme katika Jiji la Dar es salaam, hakukuwa hata naafisi moja yenye kiyoyozi kilichochafanya kazi kwa nishati hiyo labda kwa nguvu mbadala ya jenereta. Pilikapilika za huku na

kule ziliendelea kwa wakazi wa jiji hilo pasi na kujali hali hiyo.

Katika jengo refu la JM Mall, ghorofa ya sita, binti mmoja mrembo sana alikuwa nyuma ya kompyuta akiendelea na kazi ya kuchapa hiki na kile huku akisikiliza muziki laini wa Celine Dion katika mashine hiyo. Katika afisi ya pili chumba hicho hicho, kijana mmoja shababi alikuwa ameketi akiperuzi kitabu hiki na kile huku juu ya meza yake

kukiwa na magazeti kadha wa kadha ya zamani na ya sasa. Katika chumba hiki hakukuwa na sauti yoyote ya muziki, zaidi ni sauti hafifu ya kuchakura magazeti hayo. Huyu hakuwa mwingine bali Mkurugenzi wa kampuni hii, Amata Ric au Kamanda Amata kama wanavyomwita katika kazi yake. Ndani ya afisi hii palikuwa ndipo pa kupanga mambo yake kwa mwamvuli wa *Clearing and Forwading* na wengi walimtambua

kijana huyo kwa kazi yake ya biashara. Na chini tu ya jengo hilo vijana wengi walipenda kumwita anko. Tangu aingia kazi asubuhi ya siku hii, macho na akili yake havikubandukana na magazeti hayo ambayo alimwagiza katibu muhtasi wake akamtolee vivuli huko Makataba Kuu. Kila alichoona kinamfaa katika tafutishi yake alikiwekea mistari kuonesha kuwa kina uzito wa pekee. Akainua macho yake na kuitazama saa ya ukutani,

ikamwambia kuwa ‘sasa ni saa nane mchana’, ndipo akagundua kuwa hata kula hakula siku hiyo. Akayakunja magazeti hayo na kuyatia katika droo ya meza yake, akafunga na kutoka mpaka afisi ya pili.

“Sasa we hata muda wa kula hunishtui?” akamwambia Gina.

“Nikushtue kwani we huna saa?”

“Ushakua siku hizi… haya kwa heri!” akamuaga huku

akiuelekea mlango mkubwa wa kutoka nje. Huku nyuma Gina akabaki akimwangalia bila kusema lolote, alipohakikisha kapotelea nje, akaendelea na kazi zake.

* * *

Safari ya Amata haikuwa kwenda kula kama alivyoaga, nah ii ni kwa sababu wakati mwingine haitakiwi mmoja kujua nini mwingine anafanya vinginevyo iwe hivyo kiofisi. Gari lake likatia

breki mbele ya jengo la Wizara ya Ardhi, akaliacha hapo maegeshoni na yeye kutembea kwa mguu kuelekea afisi ndogo. Akiwa bado hajalifikia geti la afisi hiyo, Amata akagongana macho na kichaa aliyekuwa ameketi karibu kabisa napo. Haikuzoeleka mahali hapo kuwa na mtu wa aina hiyo. Akili ya Amata kasoma haraka na akaelewa kuwa hilo si la kawaida. Hakuonesha kujali lakini alikuwa akitembea kwa tahadhari kuelekea mlango huo.

Kutoka mbali alimwona kichaa huyo akitabasamu.

Simuelewi! Akawaza huku akiwa karibu kabisa. Na alipotaka kuushika mlango tayari kufungua akagutushwa na sauti ya kichaa huyo. Alikuwa ni babu wa umri kidogo, ukimwangalia tu utagundua kuwa hakuwa na meno ya kutosha kwani hata nyama za mashavu yake zilididimia kwa ndani, nywele

chafu, nguo chafu nay eye mwenyewe kwa ujumla mchafu.

“Kiyana! Kiyana!” akaita akimaanisha ‘kijana’.

Amata akasimama na kumtazama, “unasemaje babu?” akamwitikia kwa swali.

“Tangu asubui nipo hapa nakusubii wewe…” akamwambia.

“Mimi?”

“Yesh! Wewe, wewe kabisha…” aliposema sentensi hiyo akaingiza mkono ndani ya koti lake chafu na kutoa picha ndogo, akaitazama kwa ndani hukohuko, ila jicho la kidadisi la Kamanda lilikwishapenya na kuona kuwa ni picha. Akautoa mkono na kuiacha ile picha ndani, akamtazama Amata na kutabasamu tena.

“Yesh! Yesh! Yesh! You are the one I am looking for, Hah!

Hah! Hah!" akaongea, mara hii kwa kiingereza.

Kamanda Amata alijaribu kutafuta kichwani lafudhi hiyo ya Kiswahili ili kujua huyu ni mtu kutoka mkoa gani, ikawa ngumu kufahamu kwa sababu mara aliongea Kiswahili na wakati mwingine Kiingereza.

"Ok, mimi hapa nambie babu!" akamwambia.

"Come closer! Nataka nikwambie yambo," akasema na

Kamanda akachuchumaa mpaka pale alipoketi babu huyo. Yule babu akaingiza mkono ndani ya koti na kutoa bahasha ya kaki yenye ukubwa wa A5, akampatia.

"Shukua, kuna uyumbe kwa wewe hapo, na shi mutu mwinghine!" akasisitiza huku akimtazama Amata usoni.

"Ujumbe kutoka wapi?"

"Kashome baba, kisha ndo utaniuliza," akamwambia.

Amata akaichukua ile bahasha na kuitia ndani ya koti lake kisha akafungua geti na kuingia ndani, akalifunga kwa nyuma na kuvuta hatua mpaka kwenye ngazi za jengo hilo. Kabla hajaugusa mlango wa Madam S, akakumbuka kuwa hakumuuliza kichaa yule hata jina lake. Akaamua kurudi kwa minajiri ya kujua angalau jina, alipogeuka, hakumwona.

“Shiit!” akang’aka.

Akawahi pale getini na kutazama kwa nje, kushoto na kulia, hayupo. Akahisi kichwa chake kikimgonga kwa kutokujua sawia mtu huyo ni nani na kaenda wapi. Akaichomoa ile bahasha na kuitazama juu haikuwa na anwani yoyote, akaigeuza nyuma.

For your eyes only!

Upande wa nyuma ilisomeka hivyo, akatabasamu na

kumkumbuka 007 kwenye muvi yake yenye jina hilo.

“For my eyes only?” akajiuliza kwa sauti ndogo. Akaipachika tena ile bahasha ndani ya koti lake na kurudi afisini kuonana na bosi wake.

* * *

Madam S alikuwa ametingwa kwenye kabati lake la chuma akichakurachakura makabrasha mbalimbali, hakujua wala hakuhisi kama mlango

umefunguliwa lakini alimwona mtu akiingia ndani ya afisi hiyo kwa kutumia kioo kidogo kilicho katika pete yake.

“Karibu kiti!” akamkaribisha mgeni wake.

“Nimeshakaribia kabisa, nalijua hujaniona,” Amata akamwambia.

“Nimekuona tangu ukiwa unaongea na huyo kichaa hapo nje…” Madam S akamwambia Kamanda huku bado akiwa

anaendelea kuchakurachakura yale makabrasha.

“Kuna nini humo bibi? Achana na zilipendwa!” akamtania.

“Zilipendwa? Subiri, nitakachokutolea humu ndiyo utajua kama zilipendwa au za leo leo…” akamwambia.

Dakika moja baadae, akamaliza kazi yake na kuketi kitini akiwa na kabrasha moja mkononi, akalitupia mezani na

kujiegemeza kitini. Kabrasha lile halikuwa na maandishi yoyote juu yake zaidi ya rangi asili iliyopo. Amata albaki kimya maana alimjua bibi yake huyo haishiwi kazi za kumpa.

"Asee…" akaanza Madam S, "…nilikwambia asijue mtu kama unakuja hapa, ndivyo au sivyo ilivyo?" akamaliza kwa swali.

"Ndivyo!"

"Safi… siku hizi umekaa muda mrefu unakula maisha tu kwenye

mahoteli na fukwe tafauti, hujapata kash-kash!" Madam akamwambia.

"Kwa hiyo we unataka nipate kash-kash?"

"Ndiyo, kwa sababu ni kazi yako…"

"Aaahah! Hah! Hah! Hah!"

"Unacheka?"

"Ndiyo, nacheka kwa sababu hunitakii mema, ukiona hivyo

ujue hatuna maadui siku hizi…” Amata akasema.

“Haya bwana, we jipe moyo,” Madam akamwambia.

“Sawa, nimefika nipe habari, maana we huishiwi na umbea…” akamtania.

“Ipo hivi, kuna kazi ndogo ambayo unatakiwa ukaifanye Jijini Windhoek…”

“Namibia?”

“Eh! Kwani kuna Windhoek Misri au Libya?” Madam akamuuliza akiwa amekaza sura.

“Basi mama samahani,”

“Unatakiwa ufike Windhoek, kesho saa saba mchana, utapokelewa na mwanamke, aliyevaa fulana yenye picha ya Tina Tunner, utampa kipande hiki cha noti…” Madam akatoa ndani ya pochi yake kipande cha noti, pesa ya Kitanzania Sh. 1000.

“Nusu ya kipande hiki anayo yeye, zikilingana na ukijiridhisha, mfuate, atakupa maelekezo yote ya kazi inayokukabili huko. Si kazi kubwa na wala si ya siku nyingi. Ni kama ya siku tatu tu, then utarudi hapa…” Madam S akamuelekeza.

“Sawa, nimekuelewa…” Amata akamwambia Madam S huku akisimama kitini.

“Ni hilo tu Kamanda, cha muhimu ni hiki… uwe makini

muda wote, tabia yako ya kujiachia na wasichana nina uhakika safari hii itakugharimu kama usipokuwa makini…”

“Kwa nini Madam?”

“Nina maana kubwa kukwambia hivyo, na mimi kama mama yako lazima nikwambie,” Madam akasisitiza.

“Sawa mama! Nimesikia!” Amata akajibu. Madam S akavuta droo katika meza yake na kutoa

kitu kama bahasha kubwa ngumu, akamkabidhi.

"This is your ticket!" akamwambia na kumkabidhi bahasha ile. Amata akaifungua na kuchungulia ndani, tiketi na pasipoti mpya na pesa za Kimarekani zilikuwa ndani yake pamoja na kadi ya benki. Akatikisa kichwa juu chini na kumpa mkono bosi wake. Cha kwanza kukitoa ilikuwa tiketi ya ndege, Air Namibia. Cha pili

pasipoti mpya kabisa iliyosomeka ‘Johnson Chilewa’ kama ilivyokuwa kwenye tiketi. Akahesabu pesa zilizopo, Dola za Kimarekani 2500, kadi ya benki inayoweza kutoa pesa kwenye kiotomotela chochote kile duniani.

“Nimemaliza…” akamwambia kijana wake naye akatii.

* * *

Saa tisa kamili ya siku hiyo ilimkuta kamanda Amata uwanja

wa ndege wa kimataifa wa dare s salaam, tayari kwenye viti vya kutumia abiria akisubiri muda wake ndipo aondoke. Mpaka dakika hiyo alikuwa hajui chochote juu ya safari yake. Kwake yeye cha muhimu ilikuwa ni safari yake, na alijiuliza sababu ya kutoambiwa nini kinachomsubiri huko, hakupata jibu.

Liwalo na liwe! Akajisemea moyoni. Alipokuwa anaketi kitini

hapo na kwa muda mrefu kidogo, alikuwa peke yake. Lakini ni sasa alipogundua kuwa katika kiti cha pembeni yake kuna mtu mwingine, mwanamke mrefu, mwembamba mwenye nywele ndefu zilizomwagika chini ya mabega yake. Uso wake ulifichwa kwa miwani kubwa myeusi, midomo yake ilikuwa imepakwa rangi nyekundu sawasawa na suti aliyovaa. Kiumri alionekana mtu mzima isipokuwa tu mekapu alizojisiliza usoni zilimrudisha

kwenye ujana japo kwa asilimia chache. Hakuongea lolote ila daima alikuwa akitafuna jojo kinywani mwake.

Kamanda Amata akamtazama kwa chati na wizi, kuanzi miguuni mwake mpaka juu bila yeye mwenye kujua kama keshakaguliwa kwa macho ya kijasusi. Kwa kuwa hakusalimia, naye hakusalimiwa. Kila mmoja likuwa pale akisubiri safari. Nusu saa baadae tangazo la kuingia

ndegeni likatangazwa, akasimama na kunyanyua mkoba wake wa ngozi, akaupachika begani, pasipoti yake mkononi akavuta hatua kuungana na abiria wengine mpaka ndani ya ndege hiyo. Kama ambavyo huwa anapenda, kiti chake kilikuwa upande wa korido au kitaalamu huitwa 'Isle'. Akapachika mkoba wake katika keria ya juu ya na kuketi akiwa na kitabu chake mkononi akiendelea kujisomea. Kwa jicho la wizi akamwona yule

mwanamke naye akiwa ndani ya ndege hiyo, ameketi kama siti saba mbele yake. Hakumjali sana ila alijishangaa kwa nini macho na akili yake vimenaswa na kutekwa na mwanamke huyu anayeonekana mjuzi wa mambo.

* * *

Gina alikuwa afisini mpaka majira ya saa kumi na moja jioni akiwa hata hajuia kama bosi wake tayari yupo angani. Kila mara aliitazama saa yake na kujiuliza

kwa nini amechelewa namna
hiyo, alipojisikia kumpigia simu,
roho nyingine ikamkataza,
akaamua kuacha tu lakini moyoni
wivu ulimshika akijua tu kuwa
Amata atakuwa kapata kigoli
mwingine na si ajabu atakuwa
akiponda naye raha katika moja
ya hoteli nzuri hapa Dar es
salaam au nyumbani kwake.
Achilia mbali kuwa alikuwa akiact
kama katibu muhtasi wa Amata
huku akiwa katika idara hiyo
nyeti, Gina alitokea ,kumpenda

sana kijana huyu, hajawahi kupenda namna hii katika maisha yake. Alijikuta akiwaka wivu kila alipokuwa mbali naye, lakini kutokana na kazi yake ilimbidi kuvumilia.

Saa kumi na mbili jioni, akafunga afisi na kuingia katika gari lake, safari kwa Amata, Kinondoni . kama kuna siku ambayo alipania afumanie ni hii, alijiandaa kwa lolote na aliapa safari hii atamtia adabu kila

anayejifanya kutembea na bwana wake, si bosi wake tena.

Akawasha gari na kuondoka kwa kasi akifuata Barabara ya Samora mpaka Mnara wa Saa, akakunja kulia na kuchukua Barabara ya Uhuru mpaka Mnazi mmoja, pale akaiacha hiyo na kukamata ile ya Lumumba baada ya kuivuka ya Bibi Titi. Dakika kama tisini hivi zilimfikisha nyumbani kwa Kamanda Amata, akapunguza mwendo na

kuegesha gari yake nje ya geti lakini si mbali zana. Nje ya geti hilo kulikuwa na gari aina ya Jaguar lenye rangi nyekundu. Akalitazama kwa harakaharaka na moyo wake ukaanza kumpiga harakaharaka. Hakufikiri mara mbili, aliliendea geti na kufungua kwani alikuwa na funguo ya akiba na kujitoma ndani. Hatua moja, mbili, tatu zikamfikisha mlango wa mbele wa nyumba hiyo, akatulia kusikiliza kama kuna atakachosikia, hakuna.

Akapachika funguo kwenye tundu la kitasa cha mlango huo. Moyo wake ukasita, akahisi mwili ukimsisimka, Gina akajishangaa kwa hali anayoihisi wakati huo, akahisi hatari. Akaicha funguo katika mlango na kuvuta pochi yake, humo akatoa bastola ndogo *Berreta* ambayo daima hupenda kutembea nayo, akaikunja katikati na kucheki ndani yake, risasi nane zipo tayari katika chemba zake. Akatikisa kichwa kuwa ameridhika, akaifunga na kuislide

kidogo, ikawa tayari kwa kazi kisha akakamata funguo na kuinyonga kufungua mlango.

Ni hapo aliponyonga funguo hiyo, aliposhuhudia mlango ukifumuliwa na risasi mfululizo kutoka ndani. Alipiga kelele za uchungu na kutupwa kando akaanguka kama mzigo huku nne kama si sita zikiwa zimeishi kifuani mwake.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Off Target… this one was not our

target!” sauti ya kukwaruza ya mwanaume ikasikika huku akifungua mlango wa lile Jaguar na kusimama mlangoni, akaipachika sigara yake na kupiga pafu kadhaa, “go and check if she is alive…” akawatuma vijana wake wakamwangalie Gina kama ni mzima. Wakatoka vijana wengine wawili, wakauendea mwili ule uliolala chini kwenye nyasi, safari hii ukiwa umelowa damu na nyingine nyingi ikiwa chini. Gina alikuwa kimya kabisa.

Mmoja wa vijana hawa, aliyebana nywele zake ndefu mgongoni akaichukua bastola ya Gina na kurudi nayo garini, yule mkubwa wake akampa kijimfuko cha plastiki akaitumbukiza.

"Tell me!"

"She is dead!" akajibu na ile gari ikayiwa moto na kuondoka kwa kasi ya hatari.

WINDHOEK

Uwanja wa ndege wa Hosea Kutako

Saa 7:21 Mchana

Kamanda Amata aliwasili katika Jiji la Windhoek kama alivyotakiwa, yaani saa saba mchana, baada ya safari ndefu na mapumziko ya saa kadhaa katika Jiji la Johanesburg. Daima hakupenda kuonesha ugeni mahali popote hata kama ni mara yake ya kwanza kufika kama ilivyo katika jiji hili. Katika muda

wake wote wa kazi hii ya kipelelezi hakuwahi kufaya kazi katika nchi hii hata kuja kutembea tu, hii ilikuwa ni mara yake ya kwanza.

Akiwa bado ameketi kwenye kiti cha ndege hiyo, huku abiri wengine wakiwa tayari wima wakitoa mizigo yao katika keria ya ndani, jicho lake bado lilikuwa likimtazama mwanamke yule yule aliyemwona tangu Dar es salaam. Kama ilivyo kwake, na

mwanamke huyo hakuwa kasimama bali aliendelea kutuli palepale kitini. Amata akendelea kumwangalia na mara hii tayari alikuwa ameweka wasiwasi kichwani mwake, na hivyo kujiandaa kisaikolojia kwa lolote litakalotokea. Watu walipokwishapungua ndani ya ndege hiyo, akasimama na kuuvuta mkoba wake kutoka kwenye kibebeo hicho, akaupachika begani, na suitcase yake ndogo akaishika kwa mkono

wake, akavuta hatua fupifupi kueleakea mlango wa kutoka nje. Kwa kutumia miwani yake aliweza kumwona mwanamke yule, naye akisimama na kuchukua mkoba wake mdogo na kuupachika begani.

"Thank you very much for your hospitality!" *asante sana kwa ukarimu wenu,* akamwambia mhudumu wa ndege hiyo aliyekuwa amesimama mlangoni akihakikisha kila mtu aliyeabiri

kwenye ndege hiyo ameshuka salama.

"You are welcome Sir!" *Karibu sana,* akamjibu huku akiachia tabasamu lake pana lililouacha moyo wa Kamanda ukidunda bila mpangilio. Baada ya kuvuta hatua kama nne hivi kuteremka ngazi za ndege hiyo, na kumwona mwanamke Yule akiwa nyuma yake kama ngazi mbili hivi akasimama ghafla na kugeuka kurudi tena juu.

“Any problem Sir?” *shida yoyote?* Yule mhudumu akamuuliza.

Kamanda Amata akapanda ngazi na kumpita yule mwanamke, akamfikia mhudumu na kusimama mbele yake.

“A little problem!” shida kidogo tu, akamjibu huku akiingiza mkono mfukoni na kuchomoa waleti, ndani yake akatoa kadikazi na kumpatia.

“Haitakuwa vyema mrembo kama wewe usinisalimie jioni ya leo,” akamwambia.

“Mmmmmh!” Yule mwanadada akaguna.

“Kuna tatizo lolote?” Amata akamgeuzia swali.

“Aaaanhh ok, let it be, see you!” *tuache iwe, tutaonana,* akajibu huku tayari akiingia ndani ya ndege ile kuendelea na kazi nyingine. Kamanda Amata akaanza tena kuteremka ngazi

zile, alipopiga macho mbele hakumwona yule mwanamke. TSA 1 hakuwa na lingine zaidi ya kutaka mwanamke yule atangulie mbele na yeye awe nyuma ili kuweza kujua hila za mtu huyo. Katika chumba cha ukaguzi, kulikuwa na foleni kama tatu hivi, hapa akamwona yule mwanamke akiwa katika foleni ya katikati, naye akajiunga foleni hiyohiyo na kuwa nyuma yake kwa takribani watu kumi hivi. Nusu saa baadae, akawa tayari nje

ya uwanja huo, akapepesa macho kumtafuta mwenyeji wake, haikuchukua muda kumwona.

Mwanamke kibonge, mfupi, mweusi aliyeujaza mwili wake ndani ya jinzi nyeusi na fulana yenye picha kubwa ya Madonna. Kamanda Amata, hakumpa nafasi ya kutazama naye, akapitiliza na kufuata viti vilivyowekwa maalumu kwa mapumziko, akaeti. Alichagua mahali hapa maalum kwa sababu

aliweza kumwona yule mwanamke wapi akaielekea. Akamsindikiza kwa macho mpaka alipoingia katika gari moja jeusi na kujifungia ndani yake. Lile gari halikuondoka maegeshoni, liliendelea kubaki palepale, Amata akaelewa mchezo huo, akatikisa kichwa juu chini. Akiwa bado katika hali hiyo, akahisi hayuko peke yake, alipozama pembeni akamwona yule mwanamke mwenyeji wake akiwa ameketi kando yake.

“Karibu Windhoek!” yule mwanamke akamkaribisha Amata.

Kwa karibisho hilo ndipobakagundua kuwa si umbo tub alia hata sauti ya mwenyeji wake ni nene na nzito kama ya kiume.

“Asante sana, nimekaibia,” Amata akajibu. Mwenyeji wake akachomoa waleti na kumpatia kipande cha ile noti aliyopewa na Madam S. akakipokea na

kuchukua cha kwake, akavilinganisha, vimeungana vyema kabisa, hata namba za pesa hiyo zilifanana, wakabadilishana.

"Naitwa Lolita…"

"Naitwa Johnson…" wakatambulishana.

"Gari lipo tayari twaweza kwenda," Lolita akamwambia Amata.

"Asante, ila subiri kidogo au tangulia tukutane hotelini…

nheeee, ni hoteli gani ya kufikia?" Amata akauliza.

"Hilton Windhoek Hotel," akamwambia huku akiwa tayari keshasimama.

"Ok, nakuja…"

"Hakikisha unafika, kuna maagizo yako!" Lolita akamwambia Amata wakati yeye akivuta hatua kuelekea yalipo maegesho. Baada ya kwenda kama hatua 200 hivi, Amata akanyanyuka na kuiweka miwani

yake vizuri, akinua mkoba wake na kuvuta ile *suitcase* akielekea kule alikoenda Lolita. Kwa makusudi mazima, akapita mbele ya lile gari ambalo alipanda yule mwanamke na kutupia jicho la wizi kwa kupitia kioo cha mbele, akaona watu kama watatu hivi ndani ya gari ile pamoja na yule mwanamke.

"Vipi?" Lolita akauliza.

"Let's go!" Amata akajibu. Gari likatiwa moto na kuondoka

kwa kasi kuelekea katikati ya mji. Kutoka Uwanja wa Ndege wa Hosea Kutako mpaka Hoteli ya Hilton ni kama kilomita arobaini na tatu hivi, kwa mwendo wa gari binafsi ni kadiri ya dakika thelathini na tatu. Mpaka nukta hii, Lolita hakujua lolote linaloendelea uwanjani hapo zaidi ya kumpokea mgeni wake tu. Wakati wakiwa njiani kuelekea hotelini, hakuna aliyekuwa anaongea ndani ya gari lile. Mara kwa mara Amata alikuwa

akigeuka nyuma kutazama kama jamaa wale wanakuja au la. Kutokana na mwendo wa mwanamke huyu, na ovateki alizokuwa akizifanya, ilimuwia vigumu kuona. Baada ya kuangalia vizuri akaliona lile gari likiwa kama nafasi ya nane hivi, yaani limeacha magari sita kati yao.

“Vipi?” lilikuwa neno la kwanza la Lolita kwa Amata

ndani ya gari hilo baada ya kimya kirefu.

“We have a company!” akajibu na kukaa sawa kitini huku akifunga vyema mkanda wake.

“Wepi?”

“Toyota Vox jeusi, nafasi ya saba nyuma…” Amata akamwambia. Lolita akapiga jicho kwenye kioo na kuliona gari hilo, akatikisa kichwa juu chini kama ishara kuwa ameliona.

“Sawa, ngoja nilitazame vizuri,” akamwambia Amata kisha akawasha taa ya kuonesha kuwa anaingia kulia. Alipopiga jicho upande ule, Amata akaona kuna kituo cha mafuta, akajua nini mwanamke huyo anataka kufanya, akamwacha. Lolita akaingiza gari kituoni hapo na kusimama katika moja ya pampu za mafuta. Kule barabarani wakaliona lile gari likipita kwa mwendo wa wastani na kuendelea mbele. Lolita

akaondoa gari na kuliegesha katika maegesho ya kituo hicho, akateremka na kusogea karibu na barabara kuu, akapiga jicho na kuliona lile gari limeegeshwa upande wa kulia wa barabara umbali kama wa mita mia mbili hivi.

"So! Tunafanyaje?" Lolita akamuuliza Amata.

"Simple! Twende kwa taksi," akatoa ushauri, wakachukua mizigo na kukodi taksi kisha

wakaondoka zao na kuliacha gari palepale.

* * *

Jesca Jefferson, mwanamke mwenye mwili mwembamba kiasi lakini uliokaa kimazoezi, alfungua mlango wa gari hilo na kutoka nje, akaiweka miwani yake vyema na kuvuta hatua kadhaa, akasimama na kutazama walipotoka. Kama ungefanikiwa kumwona mwanamke huyu, ungeweza kusema ni Mrangi

kutokana na rangi ya ngozi yake, lakini sivyo, alikuwa Mzungu mwenye asili ya nchi za Scandinavia. Mwanamke huyu alikuwa ni mmoja kati ya waajiriwa wachache wa siri katika mtandao wa WP. WP yaani White Protect, ni mtandao hatari sana ambao umejiwekeza katika kulinda maslahi ya mtu mweupe katika nchi mbalimbali Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Katika nchi ambazo mtandao huu ulikuwa umekita

mizizi yake ni pamoja na Tanzania, na hii ni kwa sababu walijua umuhimu wa nchi hiyo katika ukanda huu. Zaidi ya hapo walijua nguvu ya kiintelijensia ya nchi hii, hawakuambiwa na mtu bali walikuwa wanajua jinsi walivyoangushwa katika tawala mbalimbali ambazo kwazo waikuwa wakizikoloni.

Jesca akafunga mlango wa gari baada ya kuingia ndani na kuwatazama wenzake wawili.

“Itakuwa wametupiga chenga…” akawaambia.

“Turudi palepale tukahakikishe,” kijana mwingine akasema.

“No! hiyo si idea nzuri hata kidogo, cha muhimu ni kujua wapi mtu huyu anafikia basi, hatutakiwi kufanya kashkash yoyote, ndiyo maana nimemfuatilia tangu Tanzania mpaka hapa,” Jesca akawaambia.

“Kwa hiyo tufanyeje?”

“Tusubiri hapa hapa mpaka watakapopita,” akamjibu na wote wakatulia kusubiri wapite ili waendelee kuwafuatilia. Baada ya kukaa mahali hapo kwa takribani dakika arobaini na tano, Jesca akaamuru kurudi pale kituo cha mafuta kujiridhisha kama windo lake lipo au halipo. Walipofika ndipo wakakuta gari tupu, si Amata wala mwenyeji wake, wote hawakuwepo.

“Mxcioooouuu!!!” Jesca akasonya kwa hasira.

Amenizidi akili! Akawaza, kisha akamwendea dereva taksi mwingine aliyeegesha gari yake hapo hapo akamwuliza kuhusu ni wapi wenye gari hiyo wameelekea. Yule dereva akamueleza Jesca kila kitu.

Nitamsubiri hapahapa! Akafikiri na kisha akaingia ndani ya gari lake na kuwakuta wenzake wakiwa wanamsubiri.

“Vipi?” Mmoja akauliza.

“Wameacha gari lao na kukodi taksi, nafikiri tuisubiri tumuulize dereva ni wapi kawapeleka, tukishajua, mimi nitaendelea na kazi yangu…” akamjibu.

* * *

Hoteli ya Hilton Windhoek

“Hapa tumefika!” dereva taksi akawaambia wateja wake.

“Asante sana,” Lolita akajibu huku akifungua mlango na

kutoka nje, Kamanda Amata akabaki ndani kwa sekunde kadhaa.

“Sikia, mtu yeyote akikuuiza ni wapi umetuleta usimjibu na wala usimwelekeze, sanasana mdanganye mahala ulipotushusha, sawa?” akamwambia Yule dereva kwa msisitizo.

“Sawa!” akajibu huku akipokea Dola za Zimbabwe 3500 kama malipo ya safari hiyo. Kisha

Amata akachukua kadikazi ya dereva huyo kwa minajiri ya kumtafuta kama atahitaji huduma ya usafiri.

* * *

Kamanda Amata na mwenyeji wake walifika katika mlango mkuu wa kuingilia mapokezi ya hoteli hiyo. Kabla hawajaingia kabisa, Lolita akamtaka Amata kusimama, naye akafanya hivyo.

“Johnson! Una kazi ya kufanya…” akaanza kwa kumwambia.

“Enhe…”

“Kunahitajika ulinzi kwa ajili ya tume ya upatanishi kutoka Tanzania, hii ni tume ya siri ambayo mpaka sasa hakuna anayejua wajumbe wake, ila wameshafika na wapo sehemu tofauti tofauti… kesho saa mbili asubuhi watatakiwa kuwa barabarani kuelekea katika

ukumbi wa mkutano wa Hoteli Safari, kutokana na mrejeleo wa tukio la mwaka 1985, serikali ya Namibia iliomba ulinzi madhubuti, na nafikiri Tanzania imekuamini wewe," Lolita akamwambia Kamanda.

"Labda!" Amata akajibu kwa upole, "sawa, nimekusoma!" akamalizia.

"Kazi yangu inaishia hapa, karibu sana Namibia, karibu Windhoek…" akamwambia.

“Hah! Mi nilijua bado tupo pamoja…”

“No! ninaishia hapa,” akamjibu.

“Sawa, asante sana, nafikiri tutaonana wakati mwingine,” Amata akamwambia huku akimpa mkono mwanadada huyo kibushuti. Baada ya hapo kila mmoja akashika hamsini zake. Mbele ya meza ya mapokezi, Amata alikutana uso kwa uso na kijana mwororo, mwenye

tabasamu la makaribisho. Baada ya kumsoma kwa sekunde kama nne tano hivi akaona wazi kuwa ni kijana asiye na mawaa tofauti na hoteli nyingine ambazo hukutana na vijana valuvalu, wenye ma-deal na magenge ya kihalifu.

"Johnson Chilewa," akajitambulisha huku akiweka pasipoti yake juu ya kaunta hiyo

"Karibu sana Mr. John Chilewa…" baada ya kuisoma ile

pasiplti haraka haraka akamtzama mgeni wake usoni, “wanasemaje Zambia?”

“Zambia wazima kabisa, siku moja moja si mbaya kutembelea miji mikubwa kama hii katika Afrika yetu,” akamwambia yule kijana.

“Ghorofa ya nne chumba namba ishirini na sita,” akamwambia huku akimpa funguo maalum kwa kufungua mlango huo.

“Sawa, asante sana,” akamjibu kisha akaweka kibegi chake tayari na kuchukua lifti kupanda mpaka ghorofa aliyoambiwa.

Chumba cha wastani, kitanda kikubwa kilichotandikwa shuka safi jeupe, chini, pembeni mwa kitanda hicho kulikuwa na mitalawanda ya kutumia wakati wa kuoga. Jokofu dogo, kabati la nguo na meza ya kusomea pamoja na kochi la mtu mmoja lililotengenezwa kwa vono safi.

Akavuta hatua na kuurudisha mlango nyuma yake, akashika saa yake na kuizungusha pete ya juu kisha akasubiri kwa sekunde kadhaa.

"Twip-Twip" saa ile ikatoa sauti, Amata akainua mkono akaisoma, ilijiandika kwenye kioo 'Clear'. Akatupia mkoba wake kitandani na kuingia bafuni, mbele ya kioo kikubwa akasimama na kujitazama.

Nimeanza kuzeeka, yaani mvi zinaanzia kidevuni! Akajishangaa moyoni mwake. Alipogeuka nyuma kutaka kujisaidia, ndipo macho yake yakagongana na kitu ambacho hakukitarajia, bahasha moja ya nyeupe iliyoonekana kuwekwa kitu kikubwakubwa hivi ndani yake. Juu ilikuwa imeandikwa 'Johnson Chilewa', akainyakuwa mara moja na kuichana. Ndani yake hakukuwa na kingine zaidi ya bastoan 'Berreta Pico', akatikisa kichwa

nuiweka mahala pazuri. Ndani ya bahasha hiyo kulikuwa na karatasi nyeupe pia, akaivuta nje na kusoma kwa umakini wote. Karatasi ile ilikuwa ni ramani kubwa ya Jiji la Windhoek ambayo kwayo barabara kama nne hivi ambazo zinaweza kumfikisha katika ukumbi wa mkutano, yaani Hoteli ya Safari. Chini kabisa ya karatasi hiyo kuliandikwa umbali kwa kila barabara kutoka Hilton mpaka katika ukumbi huo.

'Saa nne kamili kikao kitafunguliwa na Waziri wa Uraia wa Namibia.

Usalama wa watu wetu ndiyo muhimu kuliko kingine chochote, hakikisha hilo. Hatutaki kusikia yale yaliyotokea Harare katika nchi ya Rhodesia.

All the best!'

Ujumbe uliondikwa chini ya karatasi ile ulisomeka namna hiyo. Hakuwa na haja ya kujua mwandiko ule ni wa nani, akili

yake iliwaza kile anachotakiwa kukifanya tu, kuilinda tume ya upatanishi.

Serikali ishakanyaga nyoka, sasa ikiona unyasi tu inashtuka! Akawaza huku akiitazama ile bastola mpya kabisa iliyolala juu ya sinki la kunawia mikono.

SURA YA 6

NJE YA JIJI LA WINDHOEK

Kama kawaida, kikao ambacho wao wanakiita cha siri kilikuwa

kikiendelea katika moja ya nyumba ndogo, kando kando ya Mtaa wa Moses Galoeb, ndani ya wigo mkubwa wa kiwanda cha Ramatex Garment. Hiki kilikuwa kiwanda chenye maghala kama sita hivi na nyumba kadhaa za wafanyakazi na wageni lakini vyote vilijengwa ndani ya wigo mmoja. Kiwanda hiki mali ya urithi ya Mr. Rolenzo Frankfurt mzaliwa wa Ireland kilijengwa nje kidogo wa jiji hilo, na kimekuwa hapo kwa miongo kadhaa. Baada

yam zee huyo kufariki ndipo urithi ukaangukia mikononi mwa kijana wake wa pekee, kijana mpendwa Raustarin Rolenzo ambaye alikiendesha kwa mafanikio makubwa sana. Kadiri miaka ilivvyozidi kwenda kijana huyu alifanay makutano ya siri ya watu wa WP kama ikitokea wana kazi za kufanya katika jiji hilo. Raustarin alijiunga na watu hawa alipokuwa masomoni huko Afrika ya Kusini katika Chuo Kikuu cha Pretoria.

Baada ya mikutano kadhaa kufanyika kati ya Makaburu na watu kutoka Serikali ya Tanzania na kutofikia muafaka wa makubaliano kati ya pande zote mbili, mara hii kikao hiki kiliitishwa baada ya miaka kama mitatu au mine kupita. Madai ya pande zote mbili yaliziingiza katika mgogoro mkubwa serikali ya Tanzania na kikundi hicho cha weupe ambao hapo mwanzo walikuwa ndiyo haswa walioshika dola ya mtu mweuei huko Kusini

mwa Afrika kabla ya kuangushwa na Madiba. Mpango wao ulikuwa ni kuidhoofisha Tanzania katika harakati zake za kuijenga kiujamaa Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara bado ulikuwapo na waliamini kuwa watautekeleza hata kama watakuwa nje ya Power. Na serikali kubwa kama Uingereza, Ireland, Wales na nyingine nyingine ziliunga mkono juhudi hizi.

Wakati wa vita vuguvugu za kuikomboa Afrika, makundi mengi ya wapigania uhuru yaliitumia Tanzania kama kambi ya mafunzo ya kijeshi, kiutawala na kisiasa. Na kila kitu kiliendeshwa na wakufunzi mahiri kutoka nchini. Serikali ya mkaburu haikupenda wala kufurahia hivyo ilikuwa ikituma majasusi wake mara kwa mara kuja kufanya uchunguzi na kupeleka taarifa kwao ya nini kinaendelea. Majasusi hao

walijificha kwa vifuniko mbalimbali lakini wapelelezi mashuhuri wenye intelijensia ya hali ya juu kutoka Tanzania waliwagundua. Wapo waliouawa wakiwa hawataki kabisa kutiwa mikononi mwa mtu mweusi, wapo waliotoroka nchi na wengine wakakamatwa na kutiwa magerezani bila hukumu yoyote. Mtandao huu wa WP ulikuwa unataka watu wao waachiliwe huru kutoka katika magereza ya Tanzania, wakati huo wao

wenyewe wakiwa wameswashikilia wapelelezi kadhaa wa kitanzania na nchi nyingine za Afrika huku wakikataa katakata kuwa hawana watu hao. Hapa ndipo mvutano mkubwa ulipokuwepo. Serikali ya Tanzania ilisema ipo tayari kuwaachia huru makaburu hao endapo nayo itakabidhiwa watu wake na wengine wa Afrika. Kama hiyo haitoshi makaburu hao waliitaka Tanzania kulipa fidia ya uharibifu mbalimbali

ambao walidai kuwa umesababishwa na wapelelezi wapiganaji kutoka nchini humo jambo ambalo Tanzania ililikataa katakata, na hapa ndipo ambapo palisababisha kuvunjika kwa hii mikutano kila wakati.

"Msimamo wetu ni ule ule!" Mwanamama Margaritha Kasbarai akawaambia wajumbe wa mkutano huo wa siri. Mwanamama huyu ambaye alikuwa katika tume hii miaka

mingi nyuma alikuwa kama mshauri wa hawa wapya ambao ni wao wenyewe waliwaunda katika kupigania hili.

“Tanzania ina watu wetu kama kumi na tano hivi, hao watu ni sawa na batalioni moja ya jeshi kwa uwezo wao katika medani ya kivita,” akadakiza Sterwart Mc Cain aliyekuwa waziri katik serikali ya kikoloni ya De Klerk. Kati ya watu walioukuwepo katika vikao vya nyuma sana

wengine walishakufa kwa magonjwa mbalimbali lakini watatu walibaki nao ni Sterwat McCain, Margaritha Kasbarai na The Cobra ambaye huyu tayari alikuwa akiishi Tanzania kwa siri bila kugundulika na mtu yoyote na kazi yake kubwa huko ilikuwa ni kufuatilia ili kujua watu wao wamehifadhiwa wapi katika magereza gani.

McCain na mwanamama Margaritha wao kama

wanadiplomasia wa enzi na enzi na wanaoju vyema mgogoro huu waliendelea kuwa washauri wa mamb ya kiusalama na kimikakati katika mtandao huo wa WP.

"Safari hii watakubali tu, maana tumeshawishi serikali kubwa kama Uingereza na Irelanda kusitisha misaada kwa taifa hilo ikiwa ni shinikizo la kuwaachia watu wetu," Mr. Owen Smith akawaeleza. Huyu jamaa alikubalika sana katika

maswala ya ushawishi wa kimataifa, safari hii alikuwa ndani ya tume hiyo.

“Nakuamini sana, na naamini tutashinda, watu wetu wataachiwa huru na fidia tutalipwa tu, hawawezi kutusumbua vichwa,” akadakiza kijana mwingine.

“Sasa sikilizeni, kikao kitakuwa kesho saa nne asubuhi katika ukumbi wa Hoteli ya Safari, hakikisheni vijana wanafika usiku

huu kama inawezekana, wafanye kama tulivyopanga…” Margaritha akawaambia watu wake.

“Sawasawa, na mfanye kwa makini, kumbukeni Tanzania si taifa jinga sana kama mengine, mauaji ya 1984 bado yapo vichwani mwao na sasa watakuwa wajanja sana,” Mc Cain akaongeza.

“Aaaa wapi, sahau hicho kitu, watu wetu wako kule na

wametuambia kuwa hakuna mtu mwenye uwezo wa kutugundua wala kutuzidi katika maarifa. Alikuwa yuleyule aliyewasumbua vichwa naye tumeshamaliza kazi miaka ile, sasa hakuna kitu cha kutusumbua, mtu wetu The Cobra yupo pale na anaisi maisha ya kawaida tu na hawajaweza kumgundua, mpaka keshatuhakikishia kuwa anakaribi kujua ni wapi hasa watu wetu wamewekwa, hii ina maana kuna udhaifu mkubwa san aktika nchi

ile. Kama The Cobra anaishi tu na hajagunduliwa je ni watu hatari wangapi kutoka nje ya nchi yao wanaishi bila kugunduliwa?" Raustarin Lorenzo akaliambia jopo na wote wakatikisa vichwa.

"Lazima tusimamie haki na tufanye kila kitu kwa maslahi ya watu weupe… nawategemea sana. Sasa kila mtu akafanya mwjukumu yake na tukutane hapahapa kesho saa nane mchana baada ya kikao…" Margaritha

aliwaambia na kufunga mkutano huo majira kama ya saa kumi na moja hivi.

* * *

Jesca Jefferson aliingia katika jumba la kifahari lenye walinzi kadha wa kadha kuanzia getini mpaka ndani kabisa. Jumba hili mali ya Margaritha Kasbarai lilijengwa pembeni kidogo mwa Barabara ya Monte Cristo katika kitongoji cha Big Bend. Kitongoji hiki kilikuwa kikikaliwa

na watu wenye pesa sana wengi wao wakiwa wazungu na Waafrika wachache wenye uwezo wa kipesa waliweza kujipenyeza katika eneo hilo.

Katika bwawa kubwa la kuogelea, mwanabibi huyu alikuwa katikati ya maji akiwa katika vazi la kuogelea *'bikini'* huku kandoni mwake, nje ya bwawa kulikuwa na walinzi wa kike kama wane hivi wakihakikisha usalama. Pamoja

na utajiri wake mwanamama huyu hakuwahi kuolewa wala kuufuarahia utamu wa mume, badala yake alikuwa mtu *kumgawia* huyu na yule hasa wanasiasa na viongozi wakubwa waliokuwa wakitoka Ulaya na kuja kwa ziara za kikazi, yeye aikuwa ndiyo keki yao. Na wapo waliodiriki hata kumtumia ndege ya kukodi imchukue kutoka Afrika kwenda Ulaya kwa ajili ya wao kuburudika juu ya mwili wake.

"*Yes My daughter!*" akamtamkia Jesca ambaye tayari alikuwa katika vazi la kuogelea ndani ya bwawa hilo kwa ajili ya kikao cha taarifa kutoka Tanzania alikomtuma. Huyu alikuwa ni mmoja wa walinzi wake ambao yeye hupenda kuwaita *'Daughters'*.

"Wote wamefika, na huyu wa mwisho nimekuja naye ndege moja ijapokuwa anaonekana mjanja kidogo kwani nahisi

kanigundua kuwa nipo naye…” Jesca akaeleza.

“Kivipi?” Margaritha akmuuliza.

“Kwa sababu, tangu tukiwa kwenye ndege ameonekana kutafuta mbinu ya kunitoroka…”

“Amefanikiwa kufanya hivyo?” Margaritha akamkatisha.

“Yes Mom!” Jesca akajibu, na ni nukta hiyo hiyo akajikuta akipokea kofi moja la shavuni ‘Paaaaah!”

“Stupid! Stupid girl… nilikufundisha nini jinsi ya kumchunga mtu? Na inakuwaje anakupotea?” akamuuliza.

Kimya!

“Sasa nataka uniletee taarifa ya wapi mtu huyo yupo na *profile* yake yote kabla ya saa mbili usiku, ukishindwa… *you are in trouble with me! Get out from here…*” akamkaripia na kumfukuza. Jesca akatoka ndani ya bwawa lile, akawapida walinzi wenzake

ambao waliendelea kusimama kama minara bila kujitikisa kila mmoja akiwa anatazama kona yake. Hakuna aliyempa pole wala kumhurumia kwa kofi lile kwani hakukuwa na kanuni hiyo katika kazi. Jesca akapotelea ndani ya jengo hilo la kifahari na kumwacha mwanamama huyo akiyaacha maji na kujilaza kwenye kitanda chake nje ya bwawa hilo huku wahudumu wakisaidia kumkausha na kumletea kinywaji akipendacho.

* * *

Ndani ya chumba cha hoteli ile, Kamanda Amata alimaliza kuoga na kusimama mbele ya kioo kikubwa akijikausha mwili kwa taulo. Katika meza iliyobeba kioo hicho, aliiweka bastola yake ambayo tayari ilikuwana risasi nane kama mtaji wa kazi yake. Akili yake bado ilikuwa ikizunguka, ikijaribu kuipanga kazi hiyo jinsi ya kuifanya, ianzie wapi na imalizie wapi. Mpaka

dakika hiyo hakujua kabisa ni wapi watu hao wanaohusika na tume ya upatanishi wamefikia kama timu au mmoja mmoja. Jambo ambalo kwake lilikuwa la msingi wakati huo ni kwenda ukumbi wa chakula kupata mlo wa jioni na kisha kinywaji kitakachousisimua mwili wake, kisha aingie kwenye kazi za usiku.

Akiwa anamalizia kufunga vishikizo vya shati lake, akasikia mlio wa simu ya mezani

ukimwashiria kuwa kuna simu inaingia wakati huo.

Nani anayenijua huku hata anipigie simu? Akajiuliza, kisha akaipuuzia na kuendelea kufunga shati lake, simu ile ikaita tena mara ya pili, akaifuata na kuinyakuwa, akaiweka sikioni pasi na kusema lolote.

“Karibu sana Widhoek Mr. Johnson Chilewa!” sauti ya upande wa pili ikaanza kwa kumwambia, lakini yeye hakujibu

na badala yake aliendelea kubaki kimya.

"Utakapofika katika ukumbi wa chakula, usisite pia kuingia katika ukumbi wa recreation, mwanamuziki kutoka Afrika ya Kusini, Tu Nokwe atatumbuiza leo, wewe kama mgeni wetu, kiingilio ni bure kabisa…" ile sauti ikamkaribisha namna hiyo na mara simu ile ikakatika.

Hii si simu mbaya kwa mtu kama wewe, lakini kwa Kamanda Amata akili yake ya kikachero

ilifanya kazi mara mia tano zaidi, kwake haikuwa simu ya heri vilevile. Maswali mawili makubwa yaliyomfanya aichukulie simu hiyo kuwa si ya heri ni; mtu huyo amejuaje kuwa ana wazo la kwenda ukumbi wa chakula? Na kwa nini amkaribishe kwenye *Recreation Hall*, yeye ni nani? Daima kwenye hoteli kubwa kama hizi, ufikapo tu mapokezi basi utakuta matangazo yote kama kuna dansi, sarakasi, mazingaombwe na

burudani yoyote ile, utakuta hapo. Na swala la kubaki bila kujibu chochote nalo lilikuwa la kimsingi vilevile katika usalama wake, hakupenda mtu huyo aijue sauti yake kwani angeweza kuitumia atakavyo na kuharibu kazi, lakini pia ilikuwa ni wakati mgumu sana kwa mp[iga simu kutokuisikia sauti ya mpigiwa.

Amata akaichukua bastola yake, akaiweka sawa na kuipachika katika mkanda

maalumu aliouvaa mwilini mwake, kisha silaha flani flani ndogo ndogo kukiwemo visu vitatu vya kukunja, sindano ndogo zenye dawa ya usingizi na vikorokoro ambavyo havina uzito mwilini mwake ila vina madhara makubwa mwilini mwa mwanadamu. Juu ya shati hilo, akavalia koti nadhifu kabisa. Katika kifungo cha kati cha koti hilo, akapachika kamera ndogo yenye uwezo wa kunasa picha na sauti. Ukitazama utajua kuwa ni

kifungo lakini ni kifaa chenye kazi maalumu, akajitazama kwenye kioo, akageuka huku na huko, swadakta! Akauende mlango na kutoka nje huku akiufunga nyuma yake.

* * *

Katika ukumbi wa chakula, hapakuwa na watu wengi sana kiasi kwamba aliweza kupata meza ya peke yake na kuketi. Baada ya kuikagua menu, kaagiza chakula alichokipenda huku

akisindikiza subira kwa kinywaji laini. Akiwa katikati ya mlo alishtushwa na sauti ya kijana mwingine mhudumu wa hoteli hiyo.

"Mr. Johnson!"

Akainua uso na kumtazama kijana huyo.

"Samahani kwa kukusumbua, samahani sana, hapo nje kuna mtu anakuhitaji haraka sana, anasema ana ujumbe wako

muhimu na wa haraka," akamwambia.

Kamanda Amata akafikiri kwa sekunde tatu tu, kisha akasukuma ile sahani pembeni na kuingiza mkono wake ndani ya koti kama anataka kuto kitu vile, kisha akasimama na kumfuata kijana huyo. Walipokaribia mlango mkubwa, Amata akamzuia kijana huyo kisha yeye akatangulia mbele. Kabla hata hajauliza mgeni huyo ni nani, moyo wake

ukapiga kite kwa kuiona taksi ile iliyomleta mchana wa siku hiyo ikiwa imeegeshwa si mbali na mlango huo. Akavuta hatua haraka kuiendea, akagonga kioo cha upande wa abiria kama mara tatu hivi lakini hakijibiwa chochote, akazunguka upande wa dereva na ndipo akamwona kijana yuleyule aliyemleta siku hiyo akiwa kalaliza kichwa chake kwenye usukani. Akajaribu kumtikisa, akaangukia kiti cha pili, marehemu.

Alitaka kunambia nini? Akajiuliza.

Imekuwaje? Maswali lukuki yapanga foleni katika kichwa chake yasipate majibu, akampekua hapa na pale, hakuona chochote cha maana kwa mtu huyo. Akamvuta na kumweka sawa kwenye usukuani, akamfumbua mcho, tayari hayana nguvu.

Wamemuua! Akawaza na kumwacha palepale, akatoa simu

yake na kupiga picha gari ile na Yule mtu kisha akareje ndani ya hoteli ile na kumtafuta yule kijana, hakumwona, akajaribu kuulizia, wakasema hawajamwona na wala hawana mfanyakazi mwenye wajihi kama huo. Akatafakuri kwa jozi la sekunde kisha akapata jibu.

Nahitaji kumpata yule kijana! Akawaza huku akienda mara upande huu na mara upande

mwingine, kama mtu aliyechanganyikiwa.

“Mr. Johnson vipi?” sauti ya mwanadada wa mapokezi ikamwuliza. Akashtuka na kumtazama mwanamke huyo kwa jicho la kichunguzi.

Kajuaje kama mi ndo Johnson? Akajiuliza na hapo kengele za hatari zikalia kichwani mwake.

“Kuna mtu ninamtafuta, mfanyakazi mwenzako, sasa

sielewi mnaponambia kuwa hamna mhudumu mwenye wajihi kama huo…" akamjibu.

"Kweli kabisa hatuna!" akamwambia tena.

Amata akaona isiwe taabu, akaingia katika ukumbi wa chakula na kukuta kila kitu chake kimeondolewa, akashuka ngazi na kuelekea kwenye recreatiaon hall ambako kulikuwa na muziki mtamu wa mwanamama Tu Nokwe. Kulikuwa na watu

wengi, wengine wakicheza kamali, wengine wapiga kinywaji, wengine wakicheza muziki na wengine wakiuza miili yao. Yote hayo kwake hayakuwa na maana sana.

Macho yake makali yalikiangaza chumba kile kikubwa na kuweza kuziona sura karibu zote, kama haitshi akachukua miwani yake na kuipachika usoni. Miwani hii iliweza kuonesha vitu vyote

vyenye asili ya chuma ambavyo mwanadamu kavihifadhi mwilini mwake. Akamjua mwenye silaha ya moto, akamtambua mwenye kisu na amekiweka upande gani. Katika wengi waliokuwa ndani ya ukumbi ule, wanawake waliongoza kuwa na silaha za moto kuliko wanaume. Akaivua ie miwani na kuiweka katika mfuko wa koti lake kisha akavuta hatua kuelekea kaunta ambapo watu walikuwa wakipata vinywaji.

“Hey puppy!” akakaribishwa na sauti nyororo ya mwanamke, akageuka kumtazama, sura yake ikawa ikiingia na kutoka.

Duniani wawili wawili! Akajisemea. Mwanamke yule *‘blonde’,* alikuwa na nywele ndefu ambazo zilifika karibu na makalio, alikuwa amevaa mikufu ya gharama sana na pete zisizotajika bei yake. Akajipachika katika ya Amata na wanaume wengine kaunta hapo.

“Nikusaidie nini kaka?” mhudumu wa kaunta akamuuiza Amata.

“*Couvosier* tafadhali,” akachagua pombe ya kifaransa na kumiminiwa kwenye bilauri yake. Mhudumu yule alipotaka kuirudisha akamshika mkono na kumwambia ampatie na mwanamke huyo, akafanya hivyo.

“Thank you very much! Hakuna mwanaume

aiyeninunulia pombe leo, umekuwa wa kwanza… na kwangu utakuwa wa kwanza leo bila malipo yoyote," yule mwanamke akamwambia Amata huku akimpapasa kwa mkono wake katika sehemu nyeti.

"Drink and go!" akamwambia akimaanisha anywe na aondoke.

"Mmmmmh! Puppy, wewe ni mgeni hapa ee? Hujui hapa ndani kuwa mimi ndiye wa bei mbaya? Na nimeamua kukuofa wewe

kwa free leo," akaitua bilauri yake kauntani na kumtazama Amata usoni, macho yao yakagongana. Hapo ndipo Amata akagundua kuwa mwanamke huyu ana macho kama paka, macho ya buluu yenye vitu kama leya za kioo ndani yake, macho adimu.

"Umeiona gharama yangu, macho kama haya umewahi kuyaona wapi?" akamwambia huku akiyalegeza. Amata akajikohoza huku tayari mwili

ukimsisimka, akainua bilauri yake na kupiga funda moja kubwa, akaishusha na kuweka mezani dola hamsini ya Kimarekani, akavuta hatua kuuelekea mlango mkubwa.

"I will visit you tonight," mwanamke yule akamwambia Amata.

Alipofika mlangoni hakutoka nje, akatulia akitazama ndani ya ukumbi ule, akawaona watu wawili walioshiba wakizungumza

na Yule mwanamke na kuonekana kama wakimpa maagizo fulani. Mara mmoja wa watu wale akatoa simu na kuiweka sikioni, kisha akatazama juu kidogo. Upande ule wa juu kulikuwa na mwanamke mwingine ambaye alikuwa akiongea na simu na mwanamume huyu. Moyo wa Amata ukapiga chogo chemba, akamtambua mwanamke yule mara moja, Jesca Jefferson. Akachukua miwani yake na

kuivaa, akamtazama Jesca, akamwona vyema, ndani ya koti lake jeusi kapachika *Shortgun* ambayo ukiichokoza, madhara yake ni makubwa. Kwa kumuona Jesca, Amata akajua sasa kazi imeanza kuiva, akajua wazi kuwa usiku huo ni usiku wa kazi, akaunganisha matukio na kupata picha kuwa kwa vyovyote mwanamke huyu katekeleza mauaji ya yule dereva taksi.

* * *

Jesca Jefferson alijikuta na kibarua kizito mara baada ya kuambiwa na bosi wake Margaritha kuwa ahakikishe anampata Amata na hata profile yake. Alielewa nini maana ya tumo lile. Kwa kofi alilozabwa, alijua kuwa ni uzembe mkubwa kafanya. Akatafakari na kuamua kuanzia pale alipoishia. Nje ya jumba la Margaritha akawapigia simu vijana wake waliompokea pale uwanja wa ndege, na moja kwa moja wakarudi mpaka katika

kile kituo cha mafuta na kuikuta taksi iliyomchukua Amata ikiwa hapo. Wanaume wale wakagawana, mmoja akashuka na kuifuata ile taksi, akaingia ndani kama mteja huku nyuma yake yule mwanamke naye akiungana naye kama mpenzi wake. Yule kijana akajua ni wateja tu wa kawaida, hakuwa na chembe ya shaka moyoni mwake. Akawasha gari huku akiwa tayari keshaambiwa wapi pa kwenda.

Iliwachukua mwendo wa kama dakika kumi na tano hivi walipoamuru gari ile isimame.

“Mbona hapa ni porini na hapasai kusimama?” dreva akawauliza.

“Jamani kama mteja kabanwa je!”Jesca akasema kwa mshangao. Yule kijana akaiweka gari upande wa kulia wa barabara. Akageuka kuwatazama wateja wake. Ni sekunde hii alipjikuta

akitazamana na domo la bastola, akaanza kuetetemeka.

“M-m-mni-sa-mehe, ka-ka-ma gari chu-ku-eni jamani,” akaongea kwa kitetemeshi.

“Atuhitaji gari, tunayo mengi ya kifahari kuliko hili,” jesca akamwambia huku akiwa kaishindilia bastola ile katika shingo ya kijana yule.

“Mchana wa leo kama saa tisa hivi, kituoni kwako uiwabeba wateja wawili, nyani weusi kama

wewe, mwanamke na mwanaume, uliwapeleka wapi?" Jesca akauliza.

"Uhhhhh!!!!! Mimi na-be-ba wengi…"

"Sawa, unabeba wengi mi nataka nijue hao tu," akasisitiza kwa kuikata kauli ya kijana huyo ambaye sasa alikuwa chapachapa kwa jasho.

"Sikia, mtu yeyote akikuuiza ni wapi umetuleta usimjibu na wala

usimwelekeze, sanasana mdanganye mahala ulipotushusha, sawa?"

Maneno haya ya Amata yakamrudia yule dereva kichwani mwake, akabaki njia panda.

Nisipowaambia wataniua, nikiwaambia sijui yule atanifanya nini! Yule dereva akabaki kimya akitetemeka tu.

"Mpige sachi," Jesca akamwambia Yule mwenzake naye akafanya hivyo, akatoa pesa mifukoni mwa dereva huyo na

waleti iliyojaa vitu kama vitambulisho, kadi za bima, na katika hivi wakaipata ile kadi kazi ambayo Amata amempatia dreva huyo. Yule mwanamume akampa Jescha ile kadi.

"Hii ni yake?" akamuuliza na yule dreva akabaki katumbua macho. Jesca akampiga kwa kitako cha ile bastola katika paji la uso.

"Ndiiiyo!" akajibu huku akijibamiza kwenye dashboard ya

gari lake. Jesca akatoka nje na kuisoma vizuri.

“Johnson Chilewa!” akatamka lile jina, “mlete nje!” akamwambia yule mwenzake, naye akamtoa nje kijana huyo, wakaanza kumsulubu.

“Kama husemi tunakuua kifo cha kiungwana!” Jesca akamwambia kisha wakamkamata miguu na mikono na kuanza kumchekechachakecha. Dakika kama nne hivi yule kijana alikuwa

hoi, tayari katika tumbo lake kila kitu kilikuwa kimevurugika.

“Sema!”

“Hiilt-ton!”

Wakamtia garini nyuma ya usukani, wakamwamuru aendeshe hata kama anajisikia vibaya. Dakika kama kumi baadae wakawasili katika hoteli hiyo. Jesca akashuka na yule kijana akafuatia, wote wakaingia ndani ya hoteli ile huku wakimwacha yule dereva akiwa

hoi. Yule kijana waliyemwavha kwenye gari, alikuwa akijua wazi ni wapi wanaelekea baada ya kuendelea kunasa mazungumzo yao kupitia chombo maalumu kwenye gari yake. Hivyo alikuwa wa kwanza kufika katika hoteli hiyo. Akawashuhudia wenzi wake wakiingia na lile gari, mpaka wakatokomea hotelini, mara katika simu yake kukaingia ujumbe.

Fikisha ujumbe tafadhali,

Akaelewa ni nini maana yake, akafungua buti la gari lake na kutoa nguo zilizofanana kabisa na za wafanyakazi za hoteli ile, akazivaa na moja kwa moja akafika kaunta ambako tayari mtu wao alikuwa kazini, akaelekezwa Johnson alipo akamwendea na kumpa ujumbe. Wakati wanatoka na yeye kuamriwa abaki ndani, akatoroka kwa kupitia mlango mwingine na kumwacha Amata, *Johnson wa bandia* akikutana na maiti yule ya dereva.

* * *

Kamanda Amata alikifikia chumba chake, na alipotazama mlango tu, akajua kuwa kuna mtu alikwishaingia au ameingia, akachomoa bastola yake na kuiweka tayari huku akiifunga chombo cha kuzuia sauti. Akashika kitasa na kukinyonga, mlango umefungwa. Akachukua funguo na kuufungua, kisha akausukuma taratibu, utulivu ulibaki kuwa uleule. Kupitia

swichi karibu na mlango akataka akawasha taa na kuingia taratibu, hakuna mtu. Macho yake yaipepesa huku na kule, akagundua kuwa kulikuwa na mtu au watu waliopekua chumba hicho kitaalam sana. Kama hauna macho ya kiuchunguzi, huwezi kujua kama kimepekuliwa. Akaingia bafuni kutazama, hakuna mtu. Akarudi na kuliondoa shuka kitandani kisha akatengeneza mfano wa mtu aliyelala, akafunika na blanketi

kisha akaliendea jokofu, akatoa pombe kali na kuketi kwenye moja ya kona ya chumba hicho, akaketi na bastola yake akaiweka juu ya meza ndogo mbele yake, akazima taa na kutulia huku akisubiri, maana alijua tu kuwa wageni wake watarudi na aliikumbuka ahadi ya yule mwanamke *macho ya paka*.

"You are welcome," akasema kwa sauti ndogo na kutulia huku

akipiga funda moja moja la kinywaji kusubiri.

Haikupita muda, wakati akiperuziperuzi simu yake akaona kitasa kikinyongwa, akaifunga simu hiyo na kuiweka pembeni, akachukua bastola yake na kuikamata sawia kwa mkono wake wa kuume. Mlango ukasukumwa taratibu na mwili wa mwanamke ukajitoma ndani. Amata akatulia kimya na kumtazama mwanamke huyo

ambaye bado hakuwa amemwona mwenyeji wake. Jicho la mwanamke huyo lilitua kitandani, akili yake ikajua wazi kuwa kuna mtu kalala hapo kumbe la. Kwa kutumia miwani yake Amata alimwona vyema mwanamke huyo, ana bastola katika paja lake la kushoto, na kisu kiunoni mwake.

Taa ikawaka, mwanamke Yule akashtuka na kusimama hima.

“Karibu sana kwenye nyumba ya shetani,” Amata akamwambia huku akisimama kutoka pale alipoketi. Akamfuata mwanamke huyu ambaye alimkumbuka kwa maana walikutana katika ukumbi wa burudani na akamzawadia bilauri moja ya kinywaji kikali na kitamu.

“Kama nilivyokwambia, nimekuja kulipa fadhila…”

“Fadhila za nini? Sihitaji fadhila zako, kwani ni heri kutoa

kuliko kupokea," Amata akamwambia huku akiwa tayari kamfikia mwanamke Yule ambaye baada ya kurudi nyuma kwa hatua kadhaa sasa alikuwa amekwama ukutani. Kamanda akamfikia na mwanamke Yule akamnyang'anya bastol na kuitupia kitandani huku akimnyenga kwa kumnyonya ulimi. Johnson wa bandia alikuwa bado na akili zake.

“Umetumwa kuja kuiniua siyo?” swali hilo likamshtua mwanamke huyo, Amata akamkamata vizuri na kutumia nguvu zake akamnyanyua na kumtupia kitandani, alipotua tu tayari kamanda alishafika na kuichomoa bastola kutoka kwenye paja la mwanamke Yule.

“Ya nini hii?” akamuuliza.

“Oh! ah! Siyo kwa ajili ya kukuua wewe, hapa Windhoek kuna wanaume makatili na wenye

dhulum, hivyo sisi wenye biashara ya ngono huwa tunakuwa na silaha za kujilinda," akajieleza huku akilegeza macho lakini Amata alikuwa ngangari.

"Nipe na hicho kisu!"

"Kisu?" akashtuka na kuuliza.

"Ndiyo, una kishu kiunoni mwako…" akamwambia.

Yule mwanamke akabaki katoa macho akishangaa mwanaume huyu kajuaje kama ana kisu na bastola kwa haraka namna hiyo.

“Inuka!” akamwamuru na hapo ndipo alipofanya kosa, yule mwanamke aliinuka kwa haraka huku tayari mkononi akiwa na bastola ile ya Amata iliyotupiwa kitandani. Akaiondoa usalama na ku kufyatua, haina kitu. Akiwa bado katika kushangaa kuwa bastola hiyo haina risasi ndani, Amata akahisi kama mlango unafunguliwa nyuma yake, kwa haraka akamvamia Yule mwanamke na kumgeuzia upande wa mlangoni. Akili yake

haikuwa imekosea, risasi nne zikatua kwtika mwili wa mwanamke huyo, na wakati huo tayari, Amata alikwishachomoa kisu chake na kukirusha kwa ustadi, kikatua katika koromeo la jamaa yule. Wakati anapigania uhai wake, mlangoni pale akaibuka mwanamke, huyu naye hakuwa mgeni kwa Amata, Jesca Jefferson, akiwa na silaha hatari mkononi mwake, Shortgun. Sekunde kadhaa kabla risasi kumiminwa, Amata akamsukuma

kwa nguvu Yule mwanamke aliyemshika na kusababisha Jesca kukutana uso kwa uso na mwili huo, ni nukta hiyo Amata alipopiga hatua moja na kuruka huku akikunja goti lake. Risasi za bunduki ile zikaishia tena kwenye mwili wa yulle mwanamke. Amata akatua na goti usoni mwa Jesca. Jesca akajibamisa kisogo mlangoni na wakati huo huo, Amata alitua sakafuni kisha akampa pigo moja la karate lililotua mbavuni, Jesca akajikuta

anazidiwa kwa mapigo hayo ya harakaharaka, alipotaka kujitetea, akakutana na pigo jingine lililotua nyuma ya shingo yake. Amata akamzungusha mwanamke huyo kwa ufundi sana na kumtandika futi la uti wa mgongo na kumbwaga sakafuni hoi. Shughuli hiyo ilichukua kama sekunde arobaini na tano hivi kukamilika. Akamwendea pale chini na kwa kutumia tai yake, mara baada ya kuivua akamkaba nayo shingoni

na kumfanya ashindwe kupata hewa.

“Nani kakutuma? Naniiii?” akamwuliza, lakini Jesca hakua na jingine zaidi ya kupigapiga mikono chini. Amata akalegeza kidogo kitanzi kile, na Jesca akaanza kukohoa.

“Unamfanyia nani kazi, nani bosi wako? Ukileta ujeuri sishindwi kukuua…” Amata akamwambia kwa gadhabu. Jesca

hakujibu kitu, alitulia kimya pale chini.

“Napenda sana warembo jeuri kama wewe…!” Amata akasema na kujiweka tayari kumshughulikia. Jesca akatumia upenyo huo kuonesha makeke yake, alijigeuza haraka na kwa ufundi wa hali ya juu, aliinasa mikono ya kamanda na kuindoa ile tai, miguu yake akaikunja kwa ustadi na kuinasa shingo ya kijana huyo. Amata hakuelewa nini

kinatokea, akiwa katika kutafakari cha kufanya, alijikuta akivutwa nyuma kwa nguvu na kujigonga vibaya ukutani. Alipoinua macho akamkuta mwanamke Yule mrefu kasimama wima akimtazama.

"Koh! Koh! Koh!" Jesca akakohoa, "usifikiri kila mwanamke wa kumdharau, paka ndushu wewe! Na leo ndo utajua WP ni kitu gani!" akaongeza kusema. Kamanda amata akajipapasa kwenye paji la uso na

kujikuta ana nundu, mara hii zile nyota nyota zilikwishaanza kutulia na nuru hafifu ya taa ikampa matumaini ya kuishi tena.

"Simama juu! Nakukata shingo yako kisha naipeleka kwa bosi wako huko huko aliko," Jesca akaendelea kusema. Akarudi nyuma na kuiruka maiti ya Yule mwanamke, akainama kwa haraka na kuchomoa kisu kutoka katika ubavu wa maiti ile. Aliposimama kabla hajajiweka

sawa, alimshuhudia Amata akija kama umeme, Jesca akarudi nyuma hatua kama mbili hivi, akarusha mkono wenye kisu, Amata akaruka nyuma lakini ncha ya kisu kile ikachana shati kiasi. Jesca akapeleka pigo lingine la mguu, Amata akaudaka na kumtupia upande wa pili. Mwanamke yule akatua kitandani na kujibingirisha mpaka upande wa pili. Aliposimama tu, Amata tayari alikuwa amelichukua shuka kitandani na kumrushia, akajaribu

kulidaka na kuliondoa lakini ikawa ngumu. Ni sekunde hiyo hiyo alipojikuta akikutana na pigo moja takatifu. Akajibamiza ukutani, bado lile shuka lilikuwa limefunika kichwa chake, Amata akalikamata na kumzungusha, likamkaba. Jesca, kwa nguvu zote akasukuma kisu kuelekea tumboni mwa adui yake lakini Amata akaliona pigo hilo, akaepa na kuachia mkono mmoja kisha akaudaka ule wenye kisu, akatumia nguvu zote

kuuzungusha ule wa mwanamke huyo. Mkono wa Jesca ulikuwa na nguvu kana kwamba ilikuwa ngumu kwa Kamanda kutimiza azma yake, akampiga kichwa kimoja na kumfanya mwanamke huyo kupoteza lengo kwa nafasi hiyo, akamshindilia kisu kile tumboni. Jesca akato macho huku chukka likimtoka usoni na kubaki uso kwa uso na Amata.

"Upumzike kwa amani, mwanamke hayawani wewe!"

akamwambia na kumsukuma chini, Jesca akaanguka kama mzigo. Kamanda Amata akampekua kwenye koti na ndani ya mfuko mmoja, akatoa funguo na mwingine akatoa simu, zaidi ya hapo hakukuwa na kitu kingine. Akaachana naye na kwenda bafuni haraka akanawa mikono yake kisha akachukua simu ya mezani na kupiga mapokezi kutoa taarifa ya uvamizi huo.

Dar es salaam

Usiku huo huo…

Ni vipi kama leo nisingekumbuka kuvaa bullet proof? Gina akajiuliza mara baada ya kuinuka kutoka pale chini. Akiwa barazanai mwa nyuma ya Amata, akavua blauzi yake, akatoa ile vest ya kuzuia risasi ikiwa imetoboka toboka huku imelowa kimininika kizito kama damu ambacho

kimetengenezewa ndani yake ili kumuaminisha adui kuwa aliyempiga kajeruhiwa. Akainua simu yake na kubofya tarakimu kadhaa kisha akaweka sikioni.

"Yes Madam, kama unaweza fika nyumba namba 1 haraka," akasema kisha akatulia kusubiri jibu.

"On my way!"

"Copy!"

Akafanya vivyo hivyo kwa Scoba, haikupita dakika kumi na

tano, Madam S akaingia na Scoba, wakaegesha gari nje ya geti na kuteremka. Wakamkuta Gina palepale barazani amekaa kwa kujikunyata huku mbele yake kaweka lile dubwasha la kuzuia risasi.

"Gina! Vipi?" Madam akauliza.

Msichana huyo akainua uso na kumtazama bosi wake.

"Nimekufa madam!" akajibu huku machozi yakimtoka.

“Kivipi?” Madam akauliza na Gina akamwonesha kile kilicho mbele yake. Scoba akawa wa kwanza kutupa jicho na kuona ile vesti, akaiinua na kuitazama.

“Shiiiiit!” akang’aka na kumpa Madam S huku yeye akichuchumaa kumtazama Gina vizuri.

“Pole!”

“Ilikuwa yangu hiyo, laity nisingelikuwa na hilo dude, hata

sijui nani angewapigia simu mfike," akaeleza.

"Gina!" Madam S akaita huku akimgeukia na kuliweka kando lile dubwana.

"Yes Madam!" akaitikia.

Madam S akatikisa kichwa, "nini kimetokea?" akauliza.

"Baada ya Kamanda Amata kutoka afisini akiniaga anakwenda kupata lunch, moyo wangu haukutulia kabisa na wala sikuona haja ya mimi kubaki

afisini peke yangu. Nikaamua kumfuata angalau kuhakikisha usalama wake, moja kwa moja nikaja nyumbani kwake baada ya kuhisi anaweza kuwa amekuja huku, nikafika hapa, maadam nimepazoea na funguo ninazo nikafungua mlango, hapo ndipo nikajikuta nikikumbana na risasi zote zilizolenga kifuani na tumboni," akaeleza kisha akaanza kulia.

“Sasa unalia nini na wakati umepona?” Madam akamuuliza.

“Najaribu kufikiri vile ambavyo ningekuwa marehemu, au kama Amata sasa angekuwa marehemu, na sijui yuko wapi mpaka sasa, simu yake siipati,” Gina akaeleza, Scoba akamuinua kutoka pale chini akiwa amebaki na blauzi nyepesi ya ndani, akamkokota na kumpeleka garini kisha yeye akarudi.

“Madam S, hii ni mbaya, hebu tuingie huko ndani,” Scoba akamwambia bosi wake.

“Scoba inaonekana huko ndani kuna bunduki iliyotegwa automatic, vipi kama risasi hazijaisha?” akauliza.

Kwa sekunde kadhaa, Scoba akatafakari kitu, kisha akamwambia Madam S asimame kando, mbali na mlango huo, akarudi nyuma hatua kama tatu na kuja kwa kasi, akaruka hewani

na kuupia double kick ule mlango. Madam S hakuwa amekosea, risasi mbili zikafyatuka kutoka ndani kisha ukimya ukatawala wakati Scoba akitua sebuleni na macho yake kujikuta yakitazama bunduki kubwa yenye nguvu iliyounganishwa kwa usatdi sana na waya na kufungwa kwenye kitu kama stuli au kiti hivi na domo lake kutazama mlango mkubwa.

Madam S akajitoma ndani na kuona mashine ile jinsi ilivyofungwa kwa ustadi wa hali ya juu. Ilionesha wazi kuwa mfungaji wa bunduki hiyo anaijua kazi yake ipasavyo na mzoefu wa miaka mingi.

“Cheki usalama wa vyumba kabla sijawaita wahusika,” akamwambia Scoba naye akaanza kupita chumba kimoja baada ya kingine kwa tahadhari ya hali ya

juu. Alipomaliza akarudi kwa bosi wake na kumpa ripoti.

"Ok, mwondoshe Gina, niwakute ofisi ndogo usiku huu, mpe taarifa Jasmini pia kuwa afike pale immediately!" akampa oda na Scoba akaondoka eneo hilo. Madam S akatikisa kichwa, akili yake ikaonekana kutokumkaa sawa kidogo, maana hakuamini nini kimetokea, kwake yeye hii lilikuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu kama mtu

mpaka anafanikiwa kuingia ndani ya nyumba salama kama hiyo na kufanikiwa kutege huo mbunduki basi wote wapo hatarini, ina maana mtu huyo hashindwi kwenda kwa Jasmini, au Scoba au hata yeye mwenyewe. Akachukua simu yake na kumwita Inspekta Simbeye na vijana wake. Dakika kama kumi na tano hivi akawasili, kisha nyuma yake, *defender* jeupe likawasili.

“Inspekta, huu ni uvamizi, kama Tanzania tunafikia hapa, kutegeana mabunduki ndani ya nyuma basi tuko hatarini na hakuna wa kumwamini,” akasema.

Wakati anasema hayo, Simbeya alikuwa keshaitegua bunduki ile na kuikagua huku mikono yake ikiwa ndani ya gloves kuzuia alama za mikono yake zisibakie.

“Remington model 1100 semiauto,” Simbeye akatamka baada ya kuitambua vyema bunduki hiyo, “pole sana Selina, sasa hili tuachie sisi tutalifanyia kazi, na tutahakikisha ujambazi huu unakomeshwa,” akasema huku akiiweka bunduki ile katika hali salama.

“Sawa, nitakutafuta baadae,” Madam S akamwambia huku akimkabidhi na risasi ambazo alizit kwenye lile *bullet proof*,

pamoja na maganda yake. Inspekta Simbeye na vijana wake baada ya kukagua hapa na pale, ndani na nje ya nyumba hiyo, wakaagana na mwanamama huyo na kutokomea zao. Huku nyuma, madam S akatazama saa kubwa ya ukutani iliyotundikwa sebuleni kwa Amata, ikamwonesha ni karibu saa tatu usiku. Akaiacha nyumba hiyo na kuondoka zake huku kichwani akiwa na wazo moja tu.

* * *

Katika Ofisi Ndogo, Madam S aliwakuta Daktari Jasmini, Scoba na Gina wakiwa wameketi huku wakibadiishana mawazo, naye alipoingia tu wote wakamwachia uwanja wa kuzungumza. Huku wakiendelea kuburudika na vinywaji, kikao nacho kilikuwa kikiendelea.

“Ninachowataka sasa, ni wote kuhamia Shamba mpaka nitakapowaruhusu kurudi mjini.

Mtakuwa mnakuja mjini kwa kazi zenu za kila siku na mkimaliza mvuke bahari mrudi kwa siri kama kawaida," akawaambia.

"Kama leo wamemtegea Amata mtego ule wa kifo, kesho watamtegea nani, hakuna ajuaye, au usiku huu nyumba ya nani imetegwa, hatujui. Hivyo basi kwa usalama, nyote mtakaa hapa, tukio la leo kwenye nyumba namba moja limenitesa akili yangu…"

“Kwani Madam, nini kinaendelea kwa sasa katika afisi yetu mpaka kuwindwa kunakuwa kwa hatari namna hii?” Jasmine akadakiza kwa swali.

“Hakuna kitu, lakini unafikiri unavyowavurugia mipango yao nao wanafurahi? Lazima wakuwinde ili wakutie adabu, ndiyo maana nawaambia siku zote muwe katika hadhari kubwa kuanzia mavazi yenu, maeneo muendayo, watu wanaowafuata.

Kama mlivyofundwa katika mafunzo yenu, hakikisheni hamuizowei kazi hii, hii si kazi ya kuzoeleka, kila siku ona kama umeajiriwa jana, yaani ifanye kwa umakini na hadhari," akawaasa.

"Sawa Madam…" Scoba akajibu.

"Au mmeoa na kuolewa? Maana nana mna wasiwasi. Hata wenzi wenu hawatakiwi kujua ni nini mnafanya, kama mmewaacha nyumbani

muwadanganye muendako ndiyo utaratibu wetu, nimemaliza…” Madam S akamaliza kuzungumza na vijana wake wahafikiana kwa kile alichowaambia. Baada ya kusema hayo, akainuka na kila mmoja akaingia kwenye kona yake ndani ya jengo hilo kubwa.

Dakika chache baadae, Scoba alitakiwa kufika katika afisi ya siri ya Madam S ndani ya jengo hilo, naye akawasili kusikiliza nini ameitiwa na bosi wao huyo.

“Scoba!”

“Ndiyo mama…” akaitika.

“Tukio la leo si la kawaida, ina maana tuna adui anayefuatilia maisha yetu, sasa kabla haijawa kama ile ya Kitisho, naomba uwe na ziara kwenye nyumba zetu zote uone kama kuna mzengeo, kisha nipe taarifa kwa njia yetu ile ile,” akampa maagizo.

“Sawa Madam!” akajibu na kuinuka.

“Eeee… sikia… hakikisha unafanya kazi kwa uangalifu wa hali ya juu, sitaki kupoteza mtu kwa kipindi hiki, hasa mtu kama wewe ambaye umuhimu wako mwenyewe unaujua,” akampa tahadhari kabla hajatoka katika afisi ile. Baada ya kijana huyo kuondoka, Madam S alibaki ndani ya afisi ile akijaribu kupanga na kupangua makabrasha ya kichwa chake. Ni yeye tu mpaka dakika hiyo aliyekuwa anajua ni wapi Amata

na Chiba walipo. Sakata lililoibuka la mazungumzo ya upatanaishi kati ya serikali ya Tanzania na ile ya zamani ya makaburu lilikuwa swala la siri sana katika idara ya usalama wa taifa. Lilifanywa na kupangwa kwa siri sana ili kuhakikisha siri haivuji hata tone moja. Hata Amata kutumwa Namibia, ni Madam S na Rais wa nchi tu waliokuwa wanajua. Tume yenyewe ikiwa huko haikuwa inajua kama kuna mtu

aliyetumwa kuwalinda na kuwachunguza.

* * *

Windhoek

Margaritha Kasbarai hakuamini kabisa kile anachokisikia, aliwatazama vijana wale wawili waliosimama mbele yake kisha akatikisa kichwa kwa masikitiko. Akainuka kutoka pale alipoketi na kusogea karibu kabisa na dirisha kubwa ambalo lilimfanya aweze kuona mandhari

jiji la Windhoek kwa mbali bondeni. Ijapokuwa alisimama dirishani hapo, hakuona chochote mbele yake maana kichwa chake kilikuwa kimevurugwa na taarifa hiyo. Akameza funda la mate kisha akageuka na kuwatazama tena vijana wale.

"Mmeuona mwili wake?" akawauliza.

“Ndiyo, na umekwishachukuliwa na polisi…”

“Shit!” akang’aka na kugonganisha viganja vyake, akaiendea simu na kuinyakuwa. Kwa mkono wake wa kulia akabfya tarakimu kadhaa na kusubiri ipokelewe.

“Yes hello!” sauti ya upande wa pili ikaita.

“Cobra! Ni nani huyu aliyekuja kutoka Tanzania leo hii?” akamtupia swali.

“No one, zaidi ni mjumbe mmoja wa tume, na kwa kuondoka kwake ina maana timu yote imekamilika huko…”

“No! kuna mtu mwingine tena inaonekana ni mtu hatari sana…”

“Kwa nini?”

“Amemuua Jesca jioni hii katika hoteli ya Hilton Windhoek…”

“What?!” sauti ya mshangao ikasikika kutoka upande wa pili wa simu hiyo.

“Nilikwambia, hakikisha kila anayekuja huku hata kama ni mwandishi wa habari nijue na ninjue kwa undani wake, ila nina wasiwasi hapa kuna makosa umefanya,” Margaritha akamwambia Cobra.

“Shabash!”

“Kwani ni nani ambaye ulimtuma Jesca amfuatilie?” akauliza.

‘Nilimtuma Jesca amfuatilie mtu mmoja anaitwa Chilubi Nchai, huyu ni afisa mawasiliano katika Wizara ya Mambo ya nje…”

“Nahisi kama si wewe basi Jesca kafanya makosa katika nani wa kumfatilia, huyu bwana anaitwa Johnson Chilewa ndiye ambaye Jesca kanipa habari zake

tangu wanatoka Dar es salaam mpaka wanafika Windhoek…"

"Oh! Jesca amemfuatilia mtu mwingine…"

"Siyo Jesca! Ni wewe umefanya makosa katika kumwelekeza…" Margaritha akang'aka kwa hasira, "and now Jesca is dead, imagine… she was the one among my best daughters!" akaongeza kusema kisha ukimya wa jozi la sekunde ukafuatia. Kwa ujumla

mwanamama huyu alichanganyikiwa kwa taarifa hiyo, vifo vya watu watatu kwa saa chache ndani ya chumba kimoja. Akarudi pale alipowaacha wale watu na kuwapa maagizo.

"Sikilizeni kwa makini, naitaka roho ya huyo mtu kabla ya jua kuchomoza… you can go!"

Wale jamaa wakatazamana na kisha wakarudisha macho kwa mwanamama huyo.

“Umesema kabla ya jua kuchomoza au nimesikia vibaya?” mmoja akauliza.

“Sina haja ya kurudia…”

“Ila anaonekana ni mtu hatari sana!” kijana mwingine akadakiza.

“Hilo mimi sijui, naitaka roho yake. Huyu si mtu wa kubaki hai, mkipata nafasi tu ninyi mummalize!” akwaambia.

“Sawa!!” wakaitikia na kuondoka zao.

Margaritha akajitupa kitini na mara hiyo akaletewa kinywaji na mjakazi wake, akakipokea na kuweka pembeni.

“Niitie Parrot!” akamwamgiza mjukuu huyo.

Zilipita kama dakika mbili hivi, akaingia sebuleni hapo mwanamke mwingine mrefu mithili ya Jesca, huyu hakuwa mwembamba ila alikuwa na umbo linaloonekana kushiba mazoezi. Fulana yake ya mikono

mirefu yenye rangi nyeupe na kupambwa na maadishi ‘Formula 1’ ilimkaa vyema kabisa na kuonesha wazi mwili wake jinsi ulivyokatika, kifua chake kilijaa matiti mawili yaliyokaa kwa jinsi ya kupendeza. Suruali ya jinzi yenye kuvutika ilimkaa vyema na kuruhusu bisto zake zionekane dhihiri shahiri kwa kila amtazamaye. Nywele zake ndefu alizozibana kisogoni zilichangia kumtambulisha kuwa yeye ni mwanmke tena Mzungu.

“Parrot!”

“Yes Mom!”

“Dada yako Jesca ameuawa ndani ya Windhoek Hilton Hotel, pamoja na watu wengine wawili. Sijajua na wala sijapata wasifu wa mtu aliyetekeleza hayo ijapokuwa jina nililolipata ni Johnson Chilewa… Sasa nakuagiza kamchunguze huyu mtu kwa kina sana, usimdhuru, ila niletee habari zake kabl ya jua

kuchomoza, sawa?" Margaritha akampa maagizo.

"Sawa!" Parrot akajibu na kuondoka sebuleni hapo.

* * *

Ndani ya Hoteli ya Safari, Kamanda Amata aliwasili usiku wa saa nane na kupewa chumba katika ghorofa ya pili. Hoteli hii kubwa ya nyota nne ndiyo iliyoandaliwa mkutano ule kufanyika asubuhi ya siku hiyo. TSA 1 alikuja kupanga mahali

hapa makusudi kabisa ili ajue nini haswa kinaendelea. Hii ilikuwa mara tu baada ya kuiacha hoteli ya Hilton kama Johnson Chilewa na kuingia hoteli ya Safari kwa jina la Mr. Spark.

Hii kazi nzito na hakika imeanza! Akawaza wakati anajitupa kitandani kuketi akiwa na mkoba wake begani huku begi lingine likiwa bado katika hoteli ile ya kwanza. Kutoka katika mkoba wake huo akachukua

bahasha moja ambayo alipewa na yule babu kule Dar es salaam, nje tu ya Ofisi Ndogo. Akaweka begi chini na kujilaza kitandani huku akiifungua ile bahasha, lakini kabla ya kuitoa karatasi iliyo ndani ya bahasha ile, zikadondoka picha zenye ukubwa wa pasipoti kama saba hivi. Akaziokota na kuziweka pamoja kisha akaanza kuiangalia moja baada ya nyingine na kugundua kuwa kwa nyuma kulikuwa na majina ya wenye picha hizo.

Picha zote hizo zilikuwa ‘Black and White’ ikiwa na maana kuwa ni za zamani.

Akazitazama tena na tena na kusoma majina yao, ni jina moja tu kati ya hayo alilitambua, Peter Simbaulanga. Mara nyingi alimsikia Madam S akimtaja mtu huyu kuwa ndiye haswa aliyekuwa mkufunzi wa mafunzo yao wakiwa kambini miaka ya 1983 huko, zaidi aiwahi kumwambia tu kuwa aliondoka

ghafla na hakuwahi kujua ni wapi alikwenda. Hawa sita wengine hakuwahi kabisa kuwasikia wala kuona picha zao kabla. Hakujali, aliitoa ile karatasi na kuifungua, ndani yake kulikuwa na nyingine kama tatu hivi zikiwa na maandishi na moja haikuwa na maandishi yoyote isipokuwa kulikuwa na picha nyingine saba na majina ya kila mwenye picha chini yake. Katika hizi nazo aliigundua moja tu ya aliyewahi kuwa Waziri katika serikali ya

awamu ya kwanza. Na alizijua habari zake japo kidogo tu kuwa aliuawa katika tukio la kigaidi huko Rhodesia ambalo lilichukua roho saba za Watanzania tena memba wa Tume ya Upatanishi kama hii ambayo amekuja kuipa ulinzi. Katika karatasi hiyo hiyo kulikuwa na picha nyingine sita za wazungu tupu, na kati ya wazungu hao mwanamke alikuwa mmoja tu, na wao majina yao yalikuwa chini ya kila picha.

'Usishtuke, bahasha hii imekuwako kwa miaka mingi sana ikimsubiri mtu kama wewe. Najua jukumu ambalo umekabidhiwa ni gumu sana, tena nakuomba usilichukulie kama kazi ya mzaa kwani unaweza kupoteza maisha yako muda wowote.

Elewa kwamba unapambana na kundi hatari sana ambalo sisi sote tumepambana nalo wapo walioshinda kwa nafasi yao na wapo walioshindwa

lakini zaidi ya hapo wapo waliopotea hata hatujui ni wapi walipo.

Mwaka 1984, watu saba akiwemo waziri ambao serikali ya awamu ya kwanza iliwapoteza katika shambulio baya kabisa la kigaidi ndani ya Jiji la Harare ndiyo chanzo haswa cha kazi hii uliyopewa sasa.

Katika vita ya ukombozi wan chi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, nchi yetu ilikuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo ya kijeshi, kiutawala na hata kisiasa ikiwa na lengo la

kuhakikisha kuwa Kaburu anaondoka kabisa Afrika. Katika moja ya kuendesha vita hii kulikuwa na majasusi wengi wa Kizungu hapa kwetu na wa kwetu kule kwao, kila mmoja akiwa anamchunguza mwenzake. Kumbuka kwamba hakuna aliyekuwa mjinga katika hili, wao walimwogopa Nyerere kutokana na ukali wa maneno na mbinu zake aghali za kimapambano, nay eye aliwaogopa kwa teknolojia na uwezo wao wa kiuchumi.

Habari hii ni ndefu sana ila kwa kifupi ni kuwa, picha hizo za kwanza ni majasusi wetu ambao walipelekwa huko Afrika ya Kusini na wengine Zimbabwe, Namibia, Botswana hata Msumbiji ili watafute habari za adui, walitekwa, wakawekwa vizuizini, wapo waliouawa, wapo waliorudi wakiwa na hali mbaya na wapo ambao mpaka sasa haijulikani, ila kuna uhakika kuwa wapo hai na wanashikiliwa katika magereza ya makaburu huko Afrika ya Kusini. Serikali ya Tanzania inawataka watu

wake kwa gharama yoyote, ndiyo maana umetumwa hata kama hujaambiwa.

Lakini makaburu hao tangu enzi walikuwa na hamu ya kuitawala Afrika hasa Kusini mwa Shara, hawakuweza, walikuwa na mtandao wao mkubwa na wenye nguvu uliojulikana kama WP yaani White Power ambao ni Willy Gamba aliusambaratisha kule Zaire. Zaidi ya hapo mipango yao mingi ilivurugwa na Joram Kiango, Mteko Vano na

wengine wachache, hawa walishinda kwa nafasi zao. Lakini tuna watu wetu kule, unaweza usiambiwe au ukaambiwa na si vizuri upigane bila kujua damu yako inapigania nini.

Hao makaburu baada ya kuangushwa mwaka 1994 hawakukubali, nao pia wanataka watu wao ambao tuliwakamata na kuwafunga katika magereza yetu. Serikai ya Tanzania iko tayari muda mrefu kubadilishana wafungwa, watupe, tuwape lakini wao wanadai

zaidi, wanataka fidia ya yote tuliyowaharibia, tumegoma. Na hapa sasa ndipo penye shida, hawataki, hatutaki…

Uwe mwangalifu sana katika jukumu hili, mtandao wa wazungu hao unaitwa WP, si tena White Power, sasa ni White Protect, unaongozwa na mwanamama Margaritha Kasbarai na Stewart McCain ila wana vibaraka wao sehemu nyingi hata Dar es salaam.

Nina mengi ya kukwambia, nitafute katika makaburi ya mission nikujuze mengi na ya siri zaidi'

Karatasi zile zikaishia hapo, Kamanda Amata akatazama zile picha kwa umakini sana ni hapo ndipo alipofunguka kichwa kuwa kuna mgogoro mzito kati ya serikalia yake na ile ya makaburu iliyoshindwa.

Wanataka watu wao! Akawaza.

Ndiyo, tunao, najua na nimeshapata historia zao… lakini

kumbe pia wana watu wetu, hawa ni baba zetu! Akazama katika fikra na mawazo.

Patachimbika! Akamaliza na kusimama, kisha akatazama tena zile picha za wale wazungu akajaribu kuziweka kichwani mwake huku akiwastadi ili kuwajua vyema japo kwa udogo tu. Kati yao hakukuwa na kijana, wote watatu walikuwa watu wazima sana ambao Amata angekutana nao kiheshima lazima

awasalimie. Majina yao hakupata kuyasikia wala kuyaona mahala kabla. Akazitazama zile za Watanzania wenzake, ambao wanasadikiwa kuwa wametekwa na kuhifadhiwa na Wazungu hao.

Kama walitekwa mwaka 1984 au ’83, leo watakuwaje? Bila shaka watakuwa hata wamekata tamaa ya maisha kama kuna tumaini tena! Akawaza na kujikuta anapata uchungu mkubwa moyoni mwake. Chozi

la uchungu likamdondoka, akafikiria je ni wangapi watakuwa hai na wangapi watakuwa tayari marehermu, na hawa wailio hai ni mateso kiasi gani wameyapata kwa kipindi chote hicho. Jambo hili likampa wakati mgumu sana Amata, akaeti kitandani na kuzikusanya zile picha akaziweka pamoja.

Nitapambana kwa ajili yenu! Na Yule mzee aliyenipa hii bahasha ni nani? Anajuaje yote

haya? Akawaza na kuzitia mkobani kisha akajilaza kitandani bila hata ya kuvua viatu.

Saa yake ikamshtua katikati ya usiku, kama saa nane hivi, akakurupuka na kuketi, kwake haikuwa bahati mbaya bali aliitega imshtue wakati huo makusudi kabisa. Akavuta mkoba wake na kutoa kidubwasha kidogo ukubwa wa Big G, akakitia mfukoni, bastola yake akaibana kiunoni, akachukua

mzula mweusi na kuuvaa kichwani mwake kisha akatoka chumbani humo na kusimama koridoni. Ukimya wa eneo hilo ukmwashiria kuwa wageni wote wamelala, kwa mwendo wa kipaka akavuta hatua ndefundefu mpaka kwenye ngazi, akashuka mpaka chini kabisa, akatupa jicho mapokezi, akamwona mhudumu wa eneo hilo akiwa ameegemeza kichwa chake mezani *kachapa* usingizi. Zaidi yake hakukuwa na mtu mwingine, akapita

nyatunyatu na kuingia upande wa pili wa afisi hiyo, kisha akaanza kusoma milango iliyojipanga eneo hilo mpaka akaupata ule anaoutaka.

'Conference Room'. Maandishi hayo yakamkaribisha, akatazama huku na kule, yuko peke yake, hakukuwa na hata kamera za usalama eneo hilo, wamebugi! Akachukua funguo yake na kuipachika, hakupata tabu mzungusho mmoja tu, mlango

umeachia, akaingia ndani na kuufunga nyuma yake.

Chumba hiki kilikuwa kikubwa chenye viti vilivyopangwa kwa mtindo wa kutazamana yaa mstatili vikitanguliwa na meza kubwa ya mtindo huo huo. Ndani humu kulikuwa kumepambwa tayari kwa wageni hao, mezani kulikuwa na bendera ndogo za Tanzania na upande mwingine za Afrika Kusini lakini haikuwa hii ya kisasa bali ile ya

zamani ya utawala wa Kaburu. Hii ilimpa picha Amata kuwa huu ni mkutano kati ya Watanzania na nchi isiyojulikana. Kwa kuwa halikumleta hilo, akafnya lile alilolijia, akachukua kile kidubwasha chake na kukichomoa antenna ndogo, akakipachika chini ya meza mojawapo mahala ambapo atahakikisha ananasa sauti zote pasi na shida. Alipohakikisha kipo sawa, akakiwasha. Hakuwa na wasiwasi, kwani kidubwasha

hiki kina uwezo wa kukaa *hewani* kwa masaa sabini na mbili kabla betri haijatoa ishara ya kwisha.

Akajivuta mlangoni, akauvuta tayari kutoka, alipotoa sura tu, akaona kuna mtu anakuja upande huo, akarudi na kutulia ndani, kimya. Bila kutarajia, mtu yule naye akaingia chumba hicho hicho kwa kujihami sana, kwakuwa alikuta taa zimezimwa, basi hata yeye hakuziwasha. Kamanda Amata akabaki katuli

kimya kabisa, pembeni ya mashine kubwa ya kupooza hewa. Akamtazama mtu yule anachokifanya.

Mara baada ya kuingia ndani na kuhakikisha usalama wake, akavuta hatua mpaka kwenye mipaza sauti kimoja kilicho mbele kabisa ambacho kilionekana wazi kuwa ndiyo nafasi ya msemaji mkuu wa upande wa Tanzania ambapo akikaa atakuwa anatzamana na

yule wa upande usiojulikana. Yule mtu akachomo kutoka kwenye begi lake la mgongoni, boksi dogo, akafungua ndani na kuchomo kipaaza sauti kingine, akaondo kile na kukiweka cha kwake ambacho kimefanana sana na vile vingine. Alipohakikisha kafunga vyema kabisa, akatoka taratibu katika chumba kile. Kamanda Amata, mara hii ndipo akagundua kuwa yule mtu ni mwanamke, hakumfanyia makeke, akasubiri atoke. Mara

baada ya kuhakikisha kuwa ameshatoka, akakiendea kile kipaza sauti na kukifungua vizuri kisha akaenda kwenye kile kiti cha msemaji wa upande wa makaburu, akafungua kile kipaza sauti na kubadilisha yaani cha huku kule na cha kule huku. Naye akatoka taratibi ndani ya chumba kile. Cha kushangaza hakusikia muungurumo wa gari wala nini, hii ikamfanya ahisi kuwa mtu huyo katokea ndani ya jengo hilihili kama yeye, kazi ipo.

* * *

Parrot alirudi kwenye kasri la Margaritha kama saa tisa usiku hivi, akamkuta mwanamke huyo akiwa bado sebuleni akimsubiri.

“Welcome my daughter!” akamkaribisha na mwanamke huyo akachukua nafasi na kuketi, “nipe taarifa tafadhali,” akamwambia huku akipiga funda la pombe yake.

“Nimekwenda Hilton na kuonana na watu wetu,

wamenipa jina ambalo ndilo wewe unalo, yaani Johnson Chilewa, Mtanzania, mfanyabishara. Zaidi ya hapo wanasema mtu huyo ametoweka hotelini na ndani ya chumba chake ambapo kulifanyika mauaji, kumebaki suitcase ndogo, hivyo inaonekana atarudi…”

“Wait!” Margaritha akamsubirisha Parrot, “ametoweka kivipi, hajapita

mlangoni? Na kamera za ulinzi hazijamuonesha?" akamuuliza.

"Hakuna taswira yake iliyonaswa na kamera zaidi ya ile alipokuwa anawasili," Parrot akajibu na kumpatia picha tatu tafauti ambazo zimemwonesha huyo Johnson Chilewa. Mwanamama huyo akaziangalia mara kadhaa, picha hizo zilizopigwa kwa tofauti ya muda, moja wakati anafika, nyingine wakati akiwa chakulani na ya

mwisho alipokuwa katika ukumbi wa muziki.

“Siwezi kuamini kama huyu ni mfanyabisahara, ama la anafaya biashara ya kuua watu,” Margarita akamwambia Parrot, kisha akainuka na picha hizo nakuingia katika chumba kingine na kumwacha msichana wake akiwa sebuleni anasubiri.

Dakika kumi na tano zilimchukua ndani ya chumba hicho, alizichukua picha zile na

kuziskani kisha akazituma kwa watu wake ili wamletee majibu kuwa ni nani huyo anayeonekana katika picha hizo. Akarudi sebuleni na kuendelea na mazungumzo na mjumbe wake.

"Kaa tayari na wadogo zako, kesho kunaweza kuwa na kazi ngumu sana. Vipi ile kitu nimekupa umeweka?"

"Yes Mom!"

"Hah! Hah! Hah! Hah! Safari hii tutaua mmoja mmoja,

tukianza na kiongozi wao wa msafara, atafia kwao baada ya siku tatu hivi…" Margaritha akamwambia binti huyo, "Parrot, Jesca amekufa, ninakuagiza tena kuwa, nahitaji aliyemuua Jesca auawe!" akamwambia. Wakati huo huo nukushi ndani ya chumba kile alichoingia muda mchache uliopita ikapiga keleel kwamba kuna ujumbe umewasili. Akamtaka Parrot kusubiri kwa mara nyingine, akaenda ndani ya chumba kile na kujifungia

mlango. Dakika kama saba baadae akatoka mpaka pale sebuleni.

"Ok nenda kapumzike, nilijua wameshamtambua mtu huyo lakini wamesema wameshindwa kumtambua ila wanaendelea na uchunguzi juu yake. Nakukumbusha tena, kaeni tayari kesho kwa lolote," Margaritha akamwambia Parrot wakaagana.

07

Jua changa la asubuhi hiyo liliipendezesha Windhoek, baridi la wastani lilikisumbua chumba cha Amata na sauti za magari zikamfanya ashtuke na kujikuta ndani ya siku nyingine.

“Kumekucha!” akasema kwa sauti ndogo ya kujisikia mwenyewe. Akainuka na kuliendea dirisha, akavuta pazia na kutazama jiji hilo jinsi linavyopendezeshwa kwa miale ya rangi ya dhahabu. Baada ya

kujiridhisha na uzuri wa jiji hilo akaingia maliwato na kusafisha mwili wake, kisha akaeti mbele ya kioo na kuanza kujigeuza sura yake hapa na pale. Alipofika katika hoteli ya Hilton alijiweka vingine ndiyo maana hata watu wa Margaritha wameshindwa kumtambua, na mara hii ndani ya hoteli hii ya Safari, hakujigeuza sana zaidi ni mboni za macho za bandia alizojipachika machoni mwake.

Sasa siwezi kuwa katika mtazamo huu! Akawaza. Akavaa jinzi na fulana ya kisasa ambazo vijana hupendelea kuvaa. Amguuni akavaa raba ya gharama sana kisha akachukua kitu kama simu ambacho kina mawasiliano ya moja kwa moja na kile alichokipachika ndani ya ule ukumbi, masikioni mwake akapachika earphone na kuiunganisha na kifaa kile ambacho ukikiona kwa harakaharaka utasema ni simu ya

kisasa. Aliporidhika na mwonekano huu mpya akajiweka tayari kutoka nje ya hoteli hiyo, bastola yake ndogo na mpya akaipachika kwa ndani ya fulana hiyo, akachukua heleni moja ya kubana na kujibana sikio la kushoto. Kama ungefanikiwa kumwona basi ungejua kuwa ni kijana kutoka Marekani.

Nje ya hoteli hiyo, shughuli ziliendelea kama kawaida, maduka yalifunguliwa na

migahawa ikafanya kazi. Kamanda Amata katika mwonekano wa ki-sharobaro akaingia ndani ya mgahawa mmoja wa kisasa kabisa uliokuwa ukitazamana na hoteli ile, akachagua kiti ambacho kwacho angeweza kuona kila kinachoendelea katika lango kuu la hoteli ile. Akaagiza kifungua kinywa na huku kifaa chake kikimletea mazungumzo ya wafanya kazi waliokuwa tayari wakiweka mambo sawa katika

ukumbia mikutano. Nje ya hoteli ile kuliandaliwa vijana nadhifu wenye suti za gharama, tayari kuwapokea wageni wa kikao kile.

Muda ulipowadia, magari ya kifahari yaliingia katika hoteli hiyo na watu wenye heshima zao waliteremka na kupokelewa. Kamanda Amata, kutoka pale alipoketi aliweza kupaa picha ya kila anayewasili kwa kutumia kamera yake ndogo. Walipowasili Watanzania aliwatambua bila

kificho mpaka majina yao ijapokuwa mwanzoni hakujua ni nani na nani wamefika. Walipoingia tayari kwa kikao, yeye akanyanyuka na kulipa anachodaiwa kisha akatafuta sehemu nyingine ya kuketi ili asikie nini hasa kinachoendelea katika mkutano huo.

Katika barabaraya ya Mandume upande wa pili, ng'ambo ya hoteli hiyo kulikuwa na maduka ya bidhaa mbalimbali.

Amata alichukua muda huo kufanya window shopping lakini hakuwa na lengo la kununua chochote isipokuwa kufuatilia nini kinazungumzwa ndani ya mkutano huo na azma yake ikafanikiwa. Kilichomshtua zaidi ni malumbano makali ya pande hizo mbili huku makaburu wale wakitaka kupewa watu wao na kulipwa fidia na Tanzania ikigoma kulipa fidia ikidai kuwa wao ndiyo wanastahili kulipa fidia kubwa zaidi kwa Afrika.

'Ipo sheria ya kimataifa ya kubadilishana wafungwa, mtupatie watu wetu tuwape watu wenu,'

'Hapana, sisi hatuna watu wao hawa…'

'Nani alikwambia, sisi tunajua na tuna uhakika kuwa watu wetu wapo kwenu, hapa mpango nipe nikupe,'

Kamanda Amata alisikiliza mabishano hayo huku akifanya hiki na kile hakuna aliyemtilia shaka, zaidi walimwona tu kama kijana check bob.

'Sisi tupo tayari, lakini si kuwapa bali kubadilishana,'

'Tubadilishane nini, sisi hatuna watu wenu, na ninasema hivi, kama hamkubaliani nahili tutajua sisi nini tutafanya'.

'Tamko la mwisho, kwa upande wetu sisi, hatuna mfungwa yeyote kutoka Tanzania katika maeneo yetu wala nchi yoyote ya Afrika, tunaiomba Tanzania ikubali kutupatia watu wetu kabla hatujaishitaki katika Mahakama ya Kimaifa. Mbali na

hayo, tunaitaka serikali ya Tanzania kutulipa fidia ya uharibifu wa miundo mbinu yote katika nchi ya Afrika ya Kusini ambayo ilikuwa ni mali yetu kwa wakati huo. Na hili tunataka litekelezeke ndani ya siku saba'.

Kikao kile kikavunjika tena bila maelewano yoyote, upande wa weupe wakitoa madai hayo na kuyakataa ya Watanzania na huku Watanzania wakipinga kulipa fidia na wakisema kwa uhakika kuwa ndugu zao wapo huko.

Kamanda Amata akasogea barabarani kabisa na kushuhudia wageni wale wakiondoka katika hoteli hiyo. Akasubiri zaidi kujua nini mwisho wake, bado alikuwa hajatoa kifaa chake masikioni, ndipo akasikia habari yenye utata kiasi, mbinu chafu ambazo nyuma yake zilikuwa zikizungumzwa na weupe hao.

The daughters? Amata akajiuliza baada ya kusikia wakitajwatajwa. Dakika chache

baadae alimwona Waziri wa Mambo ya Nje akiondoka na gari ya ubalozi huku akitanguliwa na wale wanatume wenzake. Bila kuchelewa akakodi taksi na kulifuata gari hilo mpaka lilipoingia katika hoteli moja kubwa yenye hadhi ya nyota tano iliyojengwa ndani ya shamba kubwa la Maxwell. Yule waziri akateremka na kuelekea ndani ya jengo hilo. Kamanda Amata naye akateremka kwenye taksi hiyo na kushika njia kuingia ndani ya

hoteli hiyo, moja kwa moja akaifikia kaunta ya vinywaji na kuagiza bia baridi na kunywa taratibu. Baada kama ya dakika kumi hivi, akaiacha ile kaunta na kuelekea mapokezi hapo akapata habari za mgeni huyo baada ya kufanya ubembe mwingi kwa mhudumu wake.

Ngazi kma sita hivi zikamfikisha katika chumba namba 307, kabla hajagonga akasikia maji yakimwagika ndani,

alipojiridhisha kuwa ndani kuna usalama, akapachika funguo yake kwa nje na kuisukuma ile ya ndani, kisha akaingia na kuufunga mlango.

Ndani ya chumba hicho hakukuwa na mtu mwingine zaidi ya mheshimiwa huyo ambaye alisikika akipiga mruzi bafuni kwa kuwa mlango haukuwa umefungwa.

“Anha! Umefika ee, nakuja mrembo nisubiri kitini!” sauti ya

Mheshimiwa ikasikika na Amata akacheka kimoyomoyo. Dakika chache baadae, mlango ukafunguliwa kwani Amata hakuwa ameufunga. Mwanamke mrefu wa wastani, mwenye mwili wenye nyama kiasi alijitoma ndani akiwa na chano kubwa yenye vifaa anuai kwa ajili ya huduma ya masaji. Mwanamke huyu, Mzungu mwenye nywele ndefu aliushtua mwili wa Amata kwani mtindo huo wa nywele ulimkumbusha kitu. Akavuta

kumbukumbu na kumkumbuka Jesca, mwanamke huyo naye alikuwa kama huyu, urefu, mwili, na msuko wa nywele mbaya zaidi akamkumbuka hata yule aliyemwona usiku ule katika kile chumba, naye alikuwa na mwili kama huu na msuko wa nywele huo huo. Kengele za hatari zikalia kichwani mwake.

Akaendelea kumtazama, akiweka chano ile juu ya meza ndogo, na wakati huo huo

mheshimiwa akatoka maliwato akiwa na taulo tu. Yule mwanamke akasimama na kumshika mkono mteja wake akimtaka kulala kitandani, nukta hiyo ndipo alipokutana macho kwa macho na kamanda Amata, akasita na kutulia bila kufanya chochote, aliwahiwa maana tayari domo la Berreta Pico lilikuwa likimtazama 'perpendicular'.

Mheshimiwa alipoona hakuna kinachoendelea, akageuka

kumtazama mwanamke huyo, naye akakutana na kitu kilekile.

“Wote ketini chini kama mlivyo!” akawaambia, nao wakataka kuketi kitandani.

“Nooop! Ketini chini, sakafuni!” akawaamuru huku akivuta nusu hatu kuwasogelea.

Mheshimiwa Waziri na yule mwanamke wakaketi chini, macho ya mwanamke Yule yalikuwa yakipepesa huku na

huku, Amata tayari alishamnoti kwa hilo.

“Saa sabini na mbili utakuwa umekufa mheshimiwa! Kwani microphone uliyokuwa umetumia pale ukumbini imewekwa sumu ambayo itakuua taratibu,” Amata akamwambia. Mtu mzima baada ya kusikia maneno hayo macho yakamtoka, “andika urithi, nitampatia mkeo!” akazidi kumchanganya.

“Kwa kukusaidia tu, aliyekuwekea sumu hiyo si mwingine ni huyu mwanamke uliyekaa naye, na wala si huyu ambaye alitakiwa akufanyie masaji, ila kafanya hila tu kukufikia, kuna kitu anachokitaka na sasa amekipata!” Amata akasema huku tayari dole lake la shahada likiwa limeshaibana *trigger* ya bastola hiyo ndogo. Kijasho chembamba kikamtiririka mheshimiwa, akamtazama yule mwanamke na

nukta hiyohiyo akajikuta amepigwa kipepsi kimoja matata sana ubavuni, akajipinda kwa maumivu maana mambo hayo hajayazowea. Amata akajua tayari mambo yameharibika na mwanamke huyo.

"No time to waste!" akatamka na kufyatua bastola ile, risasi moja ikamtandika mwanamke huyo gotini na kuvunja mguu.

"Aaaaaaiiiggggghhh *fuck you*!"

"*And you too!*" akamjibu na kumtazama mwanamke yule akijaribu kuinuka lakini wapi.

"Wewe ni nani kwanza?" mheshimiwa akauliza.

"Mimi ni malaika mlinzi, nimetumwa kukuokoa… haya inuka haraka!" akamwambia mheshimiwa naye akainuka lakini kabla hajawa sawa, yule mwanamke akamtia ngwala kisha yeye akainuka haraka pamoja na maumivu yote. Kamanda Amata,

akafyatua risasi, ikakmkosa na kufumua kioo cha dirisha, Parrot akapata upenyo na kuruka sarakasi ya kiufundi akapenya dirishani na kuangukia nje. Risasi nyingine mbili za Amata zikamkosa huku mheshimiwa akiwa chini kajikunyata. Amata akawahi dirishani na kushuhudia vijana watatu wakimbeba mwanamke huyo na kumtia garini kisha wakaondoka kwa kasi.

Akamtazama mheshimiwa, akamwona bado anajizoazoa kuinuka.

“Hapa hakuna usalama tena, tuondoke haraka, waambie na wengine wote tukutane uwanja wa ndege haraka sana, yaani hivi ninavyosema, tuanze safari,” akamwambia. Mheshimiwa Waziri akitetemeka akachukua simu na kupiga nambe ya mkuu wa msafara na kumpa ujumbe huo. Kisha akisaidiana na Amata,

wakafunga mabegi haraka na kutoka nje.

“….kwani wewe ni nani? Isije kuwa unataka ku-kuniteka!” mheshimwa akaonesha mashaka.

“Kama unataka kubaki we baki, ila hujue hawatakuacha hai hawa jamaa!” Amata akamwambia huku tayari wakiwa mlango wa dharula, akaupiga teke moja nao ukafunguka, wakateremka kupitia ngazi za nje mpaka kwenye maegesho ya

magari ya wageni upande huo. Kwa mbali akaona Land Cruiser moja ya watalii imeegeshwa ikiwa haina mtu ndani, akaiendea, akapiga ngumi kioo kikavunjika, akaingiza mkono kwa ndani na kufyatua loki

“Ingia huko, weka mizigo haraka!” akamwambia naye akatiii. Amata akavuta hapa na pale, na katika droo ya dashboard hiyo akatoa bisibisi, akang’oa sehemu ya swichi na kuunganisha

nyaya, injini ikawaka, hakuna kusubiri, akatia gia na kuondoka kwa kasi.

“Wenzako wako wapi?” akamuuliza.

“Si tumewaambia tukutane nao uwanja wa ndege!” mheshimiwa akajibu.

“Ndiyo, ila uwanja wa ndege si salama, inabidi tubadili mpango, usipige simu ila nambie walipo,” akamsisitiza.

“Wapo Girrafe Hotel, Barabara ya Sam Nujoma,” Amheshimiwa akamwelekeza. Bahati nzuri ndani ya gari ile kulikuwa na GPS Locator kwa sababu ya safari za kitalii. Akaiseti huku akiendesha impe uelekeo wa hoteli hiyo.

“Yes!” Amata akakubali baada ya mashine hiyo kumuuliza kuwa ana uhakika kuwa anabadilisha uelekeo wa safari.

Hoteli Giraffe ilikuwa imejengwa nje kidogo ya jiji hilo, kilomita takribani ishirini na tano hivi, watu wengi waliipenda kwa upekee wake mahali ilipo na utulivu uliyoizunguka. Kamanda Amata akaegesha gari nje tu ya hoteli hiyo, akamwamuru mheshimiwa kushuka na kuchukua mizigo yake.

“Sasa mbona tunashusha mabegi?” akauliza.

“We tulia utajua kwanini baadae!” Amata akajibu na kuchukua simu nyingine mfukoni mwake, tayari namba ya mmoja wao wa wale wanatume alikuwa nayo kichwani baada ya kupewa na waziri huyo. Akaipiga ikapokelewa, wakatoa jibu kuwa tayari wameondoka na wapo kilomita kadhaa kuelekea uwanja wa ndege, akawaamuru kurudi mara moja nao wakafanya hivyo. Dakika kama kumi hivi wakawasili na gari nyingine ya

kutosha kuwabeba wote. Amata akamwambia mheshimiwa aungane nao, wakapanda ndani.

“Vipi mheshimiwa mbona namna hii?” mmoja wa wanatume akauliza.

“Acha tu tutayaweka sawa baadae!” Waziri akajibu huku akipishwa kiti akae; akaketi na kufuta jasho. Kamanda Amata akamto aliyeketi kiti cha mbele na kuingia yeye.

“Ok, dreva, nisikilize mimi nitakachokwambia na si vinginevyo …”

“Sawa!” akajibu dreva.

“Safari yetu itaishia Gobabis, mafuta unayo?” Amata akauliza.

Kwa kitetemeshi dereva Yule akajibu kuwa mafuta yapo.

“Usiogope, hakuna kibaya hapa, washa gari twende!” akamwamuru na dereva Yule akawasha gari na kuingiza barabarani. Dakika chache tu

akawa tayari kwenye Barabar kuu ya kwenda Gobabis. Kamanda Amata akawageukia watu wake.

“Wote mpo?”

“Tupo!”

“Kwani we ni nan? Jambazi au?” mmoja wao akadakia.

“We tulia, msikilize!” mheshimiwa akamkemea mjumbe wake.

“Haya naombeni simu zenu zote!” akawaambia na wao

wakazikusanya wakampatia, alichofanya Amata ni kuzifumua fumua, betri kwake na mashine huko akawaachia sim card tu na mashine hizo akazitupa nje kwa umbali tafauti, baadaye akachukua ya dereva na kuifanya vivyo hivyo, akavunja GPS iliyofungwa ndani ya gari hiyo na kuitupa nje. Yote haya ilikuwa ni kuitenganisha safari hiyo na mawasiliano yoyote ya kidijitali.

“Usihofu dereva, hujatekwa, mimi ni mwema tu na utarudi kazini kwako ila tufikishe Gobabis,” Amata akamtoa hofu na kumwona kijana huyo akitweta taratibu tafauti na mwanzo. Gobabis ni mji mwingine katika nchi ya Namibia, kilomita 212 na ukiendesha bila kusimama basi utatumia saa mbili na robo hivi kufika. Mji huu mdogo upo katika barabara kuu ya kwenda Botswana Kusini Mashariki mwa

Namibia. Majira ya saa nne usiku hivi wakawasili katika mji huo na kumwamuru dereva awashushe katika Mtaa wa Cuito Cuanavare. Amata akatoa burungutu la noti za Kimarekani na kumpatia kadhaa dereva yule.

"Tunailipia safari yako, kanunue simu mpya, na nyingine ya kwako…" Amata akamwambia.

"Thank you! Thank you sir!" Yule kijana hakuamini,

akashukuru mpaka anataka kupiga magoti lakini tayari Kamanda alikwishavuta hatua kuingia upande mwingine huku akifuatiwa na wageni wake.

* * *

Katika Jiji la Windhoek, hekaheka zilichukua nafasi, mara baada ya kuitishwa kikao cha dharula baada ya mkutano wa upatanishi wa pili kuvunjika bila mafanikio hali ya Mc ikaanza kuleta shida. Mara kwa mara

akajikuta akikohoa sana na kuanza kuishiwa nguvu. Wazungu wenzake katika kikao hicho akiwamo Margaritha wakaona ni vema kumwita daktrai wao mapema zaidi. Na haikuchukua muda akawasili kwa kutumia helikopta maalumu yenye chapa ya 'Flying Doctors'. Naye alipomwona akawaambia jamaa hao kuwa zaidi ya huduma ya kwanza mgonjwa huyo alitakiwa kufikishwa katika hospitali kubwa kwani tayari

alihisi kuwa amevuta hewa ya sumu.

Hekaheka hiyo haikuwa ndogo, mwanamama Margaritha na wenzake watatu waliokuwamo kwenye kikao hicho wakajikuta sasa wamesahau kuwafuatilia adui zao na badala yake kuanza kutafuta tiba ya kumganga mwenzao. Tayari, Kamanda Amata alikwishabadili upepo wa kila kitu.

“Who done these mother fu*ker?” Margaritha akafoka baada ya dege lile kuondoka nay eye akitakiwa ubaki Windhoek ili kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa na akitakiwa kujua haraka ni mchezo gani umefanyika. Muda wote alikuwa akiizunguka sebule yake kama aliyeshikwa na wazimu.

This is Parrot! Akawaza.

Why she turned on us? Akajiuliza kiwa kafumbata

mikono yake na macho yake yakiwa kwenye dirisha kubwa sana la nyumba hiyo ambayo usiku huo ilitakiwa kufanyika kikao cha maamuzi ya mwisho cha WP. Bahati mbaya Amata lifanikisha kile alichokifikiri, kwa kitendo hicho aliweza kusogeza mbele mambo mengi ambayo jamaa hao walifikiri kufanya.

Akiwa katika mawazo hayo, akashuhudia gari ya vijana wake ikiingia kwa kasi sana katika

egesho la mbele ya nyumba yake, haraka akatoka maana alijua nini amewatuma na hapo alikuwa akisubiri majibu tu.

"Amevunjwa mguu, na ameumia sana!" mmoja wa vijana wale akamwambia Margaritha kabla hata hajafika katika gari ile.

"Nani?"

"Parott!"

"Oh! Come on! Why all this happen?" akang'aka kwa uchungu na kurudi ndani, lakini

kabla hajafikia mlango akasimama na kuwatazama wale vijana.

“Mpelekeni katika hospitali yetu, mumchunge, akipata nafuu na kuweza kuongea mniite nije kumwona ana maswali ya kujibu!” akaingia ndani na kubamiza mlango.

Ndani ya nyumba yake akakaribishwa na mlio wa simu, moja kwa moja akajua kuwa kuna nukushi imeingia, akawahi ndani

ya chumba chake kidogo na kuiruhusu nukushi hiyo kuingia. Dakika moja baadae ikakamilika.

'Real Name: Amata Ric

'Status: Tanzania Secret Agent 01

'Height: 1.75 m

'Code of Status: 005 – Intelligent and unstoppable human being

'Martial Arts Rank: Unknown

Chini ya maandishi haya machache kulikuwa na picha ya mtu huyo anayeelezewa kuwa ni

mtu hatari kuliko hatari yenyewe. Ni vitu vichache tu ambavyo vilielezwa vingi vilijazwa kuwa ni *'unknown'* yaani havijulikani. Margaritha akajikuta akivuja jasho jembamba kwa maana picha ile ilikuwa imefanana sana na ile aliyoituma mara ya kwanza.

Huyu ndiye niliyetaka The Cobra amshughulikie kule Dar, I know the man. Ina maana alikuwa hapa Windhoek?

Margaritha akajiuliza na kubaki kimya.

Siamini sana, labda wamefanana tu, nitajua! Akajipa moyo na kuikunja ile karatasi huku akishusha umzi ndefu sana. Kama kuna usiku ambao mwanamke huyu alihisi dunia imegeuka ndani nje – nje ndani, basi ni huu, hakuelewa nini kinaendelea, kumpoteza Jesca kulimpa wakati mgumu, hali mbaya ya McCain,

ilimnyong'onyesha, kipigo alichokipata Parrot kikammaliza kabisa; akabaki teeeeh!

Akiwa kamezwa katika lindi la mawazo, sauti kali ya simu ikamshtua, akainyakua haraka na kutazama kwenye kioo.

'Alfa'

Ilijiandika. Moyo ukaanza kumwenda mbio kama saa mbovu, akajua tayari, kumekucha, kwa maana kawaida inaweza kuchukua hadi miezi sita

jina hili kuonekana kwenye kioo cha simu ya mmoja wao au wote kabisa. Margaritha kwa mikono ya kitetemeshi akaiweka karibu na sikio kisha akafumba macho na kubofya kitufe cha kijani kuruhusu mawasiliano yashike hatamu.

"Alfa!" akaitikia kwa namna hiyo.

"E.M will take place at Prague wthin twenty four hours from now, over and out!" mwito huo ulimpa

taarifa mwanamke huyu ya kuwa E.M yaani kikao cha dharura ‘Emergency Meeting’ kitafanyika Prague ndani ya saa ishirini na nne.

“Copy!” Margaritha akajibu na simu ile ikakatika.

“Mh!” akaguna na kuinuka mara moja, aijua nini maana ya wito huo, hakutakiwa kupoteza muda bali kufika mara moja huko anakotakiwa. Chumbani kwake, akafungua saraka iliyojengwa

vizuri katika ukuta wa nyumba hiyo, kama si mdukuzi wa mambo hayo huwezi kujua kama mahali hapo pana hazina kubwa ya kutisha. Akafungua kijimlango na kutoa kijisanduku kingine kidogo cha chuma, ndani yake akachukua hati yake ya safari, pesa taslimu za Kimarekani na kadi ya benki 'Visa' inayomwezesha kulipia chochote mahali popote. Hakuhitaji viza ya safari kwani katika mtandao wao wa WP walitambulika kwa hati za

kidiplomasia hivyo nchi yoyote ya Ulaya huingia huru.

* * *

Katika kiwanja hiki kidogo cha Gobabis huko Namibia, Kamanda Amata aliweza kukodi ndege ndogo ambayo ingewasogeza mpaka Botwsana na huko wangeweza kupata ndege ya kutoka Afrika Kusini kuelekea Tanzania siku hiyo hiyo. Wakiwa bado katika uwanja huo, wakati itifaki za mambo ya anga

zikiwekwa sawa tayari kwa ndege hiyo kuruka na kuvuka mpaka, Kamanda Amata alikuwa ndani ya chumba maalumu na watu wake.

“Mnisamehe kwa hichi nilichowafanyia, lakini ni kwa ajili ya usalama wenu, kama si hivi basi ninyi nanyi mngeangamia kama wale wa mwaka 1984,” akawaambia, na kutoka katika macho yao Amata akaona wazi

woga na mshtuko uliowapata watu hao.

Punde si punde wakatakiwa kuingia ndegeni kwani chombo hicho kilikuwa tayari kikiwasubiri kwa safari ya kuelekea Botswana. Dakika kumi ziliwachukua kuwa tayari kila mmoja katika siti yake. Ndege hii ndogo aina ya Sessina haikuwa na utenganisho kati ya abiria na rubani hivyo Amata aliweza kumwona na kusikia vyema juu ya nni anchoongea.

Alikuwa mwanamke wa makamo kati ya miaka arobaini na hamsini hivi. Hakuwa na wasiwasi katika eneo hili, sasa aliamini kuwa kazi ambayo alikabidhiwa amefanya vyema.

Kwanini, kwanini watufanye hivi? Lazima nipate uhakika juu ya watu wetu kama kweli wanao au wanachosema ni sahihi! Akawaza akiwa kafunga mkanda vyema katika kiti cha ndege hiyo

wakati ikinyanyuka na kuiacha ardhi ya Namibia.

Nikirudi Tanzania hii ni kazi ya kwanza, lakini nitaanzia wapi? Akazidi kujiuliza, kisha akaamua kutulia tu. Kwenye viti vingine wenzake walionekana kuanza kusinzia na baada ya dakika kama thelathini hivi angani tayari wote waikuwa wamemezwa na usingizi. Katika kiti cha mbele yaani pembeni ya rubani hakukuwa na mtu aliyeketi,

akainuka kutoka pale alipoketi na kuchukua nafasi hiyo. Yule mwanamke rubani, alimtazama mara moja na kurudisha macho yake mbele.

“Itatuchukua muda gani kufika?” akmuuliza.

“Saa kama nne hivi, kwa kuwa ndege hii haina kasi sana,” akajibiwa.

“Inaonekana mzowefu wa kazi hii?” Amata akaanza kudodosa.

“Hah! Hah! Hah!” Yule mwanamke akacheka na hakujibu kitu.

“Unanicheka?”

“Hapana, sikucheki ila umenifurahisha,huwezi kurusha chombo hiki kwa mwendo mrefu kama si mzowefu…”

“Ok! Nimekupata”.

Amata akajiweka sawa kitini na kufunga mikanda ya kiti hicho baada ya kusikia kengele iliyomtaka kufanya hivyo.

“Thank you!” Yule rubani akajibu.

“Unajua wanawake wengi huogopa kazi kama hizi, vipi kuhusu wewe?”

“Mi siogopi na nilikuwa napenda kurusha ndege tangu utoto wangu, nilipoingia jeshini ndipo azma yangu ilitimilika…”

“Ina maana wewe ni mwanajeshi?” Amata akatupa swali.

“Ndiyo, ni mwanajeshi wa Kikosi cha Anga cha Namibia, naitwa Captain Jojina Mamedelo!” akajieleza. Katika safari hiyo mambo mengi sana yalizungumzwa kati ya watu hawa wawili ambao urafiki wao ulianzia hapo.

Kama alivyosema, saa nne baadae, ndege ile ilikanyaga ardhi ya Jiji la Gaborone, lakini mwandada huyu hakuwashusha

katika uwanja wa ndege za kawaida bali uwanja wa jeshi.

“Nimekosa njia kwenye Uwanja wa Ndege wa Gaborone, hivyo nitawashusha jeshini na kuna mtu atawapeleka mtakako,” akamwambia Amata.

“Sawa maamuzi yako ni ya msingi Captain Jojina Mamedelo,”

“Umeshanikariri?”

“Aaa sana, na ungekuwa unabaki hapa nafikiri tungemaliza

usiku pamoja!” Amata akaanza machombezo.

“Mmmmh si umesema mnachukua ndege ya alfajiri ninyi au?” Jojina akauliza.

“Ni kweli lakini, bado tuna saa kama tatu au nne, kwani haiwezekani?”

“Chukua business card yangu ukija tena unitafute, labda utabahatisha!” mwanamke Yule akamwambia Amata wakati tayari ndege imeshakanyaga ardhi na

inelekea mahala pake pa maegesho katika uwanja huo wa jeshi.

08

Dar es salaam

Madam S akashusha kikombe cha kahawa na kukiweka mezani kwa madaha kabisa, macho yake yalikuwa yakimtazama mtu aliyekuwa wameketi katika kiti cha mbele yake na kutenganishwa na meza tu kati

yao. Kamanda Amata kwa utulivu mkubwa alikuwa ameketi katika kiti hicho dakika kumi tu tangu awasili kutoka Botswana.

“Umefanya vizuri kwa kuwarudisha salama!” Madam S akamwambia huku akijiegemeza kitini.

“Ni kazi uliyonituma, hivyo sikuwa na budi kuitimiza, madam, hili swala si dogo kama wewe unavyonambia tu

nikahakikishe usalama wa hii tume…”

“Ndiyo, ila mimi nawewe tunatekeleza amri ya Rais,” Madam akamwambia.

“Ni kweli, lakini kama tume hii inang’ang’ania kuwa hawa Makaburu wana watu wetu, ina maana ni kweli kuna watu upande ule, je tutaidhihirisia vipi dunia kuwa hawa jamaa wanatukandamiza katika haki

yetu ya msingi?" Amata akaongea kwa jazba.

"Kiukweli mi sijui kwa undani juu ya hili, ila nitalifanyia uchunguzi na nitakwambia ukweli wote," Madam akajibu.

Ijapokuwa alikuwa akiuliza au kusema hayo, Amata tayari alikuwa na ile bahasha mkononi ambayo hakutakiwa kumwonesha mtu yeyote kwa kuwa iliandikwa *'for your eyes only'*, na huwezi kujua kwa nini imeandikwa hivyo. Kwa

maswali haya, alichokitaka yeye ni uhakika tu, lakini aliona wazi kuwa inawezekana hata bosi wake hajui upande wa pili wa jambo hili.

"Madam S, yakubidi ujue kuwa hawa jamaa wana tawi lao hapa, maana inaonekana nimekuwa nikifuatiliwa tangu nikiwa huku, wananifahamu…"

"Wanakufahamu?"

"Ndiyo! Nimekuwa nikufuatiliwa tangu nipo kwenye

ndege na mwanamke wa kizungu ambaye sasa ni marehemu kwa sababu ya ujinga wake…" Amata akamwambia bosi wake

Madam S akashusha pumzi na kujiegemeza kitini, akamtazama kijana wake kwa makini sana, kisha akamwambia, "Sikia Amata, sasa umenipa jibu ambalo limeunganisha matukio…"

"Kivipi?"

“Unajua kilichompata Gina?” Madam akauliza, Amata akajikuta anashtuka kwa swali hilo.

“Nini tena?”

“Kama si kuheshimu mawazo yake, angekufa badala yako…”

“Sikuelewi!”

“Huwezi kunielewa, ni kweli, siku ulipoondoka, ndani ya nyumba yako kulitegwa bunduki ambayo ingekufumua pindi tu ungenyonga kitasa,” Madam S akamwambia Amata. Paji la uso

la kijana huyo likaanza kupata makwinyanzi ghafla, alikuwa ameegama kwenye kiti lakini sasa aliketi wima kitini.

"Unasema?!" akauliza kwa mshangao.

"Ndo hivo! Lakini bahati nzuri alikuwa amevaa fulana ya usalama mwilini mwake. Risasi tano … tano, mwilini mwake…*(akamtazama Amata)*… hizi hapa!" akavuta droo na kumpatia risasi hizo ambazo

zilikwama ndani ya fulana ile. Madam S akaendelea kusema wakati Amata midomo ilikuwa ikimcheza kwa hasira, “sasa inaonekana hawa jamaa walidhamiria kukuua! Ina maana walijua kuwa umeingia kwenye misheni hii?

“Sijui! Poleni sana, maana labda ningekuwa marehemu mara hii… kwangu swala hili si la ufumbia macho… nitahakikisha nalishikia kidedea, na nitawatia

mkononi," Amata akamwambia Madam huku akipigapiga ngumi mezani.

"Sawa, nenda kapumzike, na nashukuru kwa kuwasaidia hawa jamaa kusika salama," Madam S akamwambia huku tayari akiwa amesimama na kupeana mikono na Amata.

* * *

Makaburi ya misheni…

Kamanda Amata aliegesha gari lake kando tu ya makaburi ya

misheni ya Anglikana Mikocheni. Akateremka na kuweka vyema koti lake, akapachika miwani yake vizuri na kuvuta hatua kuingia ndani ya uwanja huo. Mkono wake wa kuume alikuwa kashika ua na mkono wa kushoto ulikuwa ameshika moja ya vifungo vya koti lake kana kwamba anafunga vizuri. Uwanja mzima ulikuwa kimya kabisa, ni sauti za ndege tu zilisikika, huku na kule kulikuwa na mabomba ya maji yaliyokuwa yakimwagilia

eneo hilo. Hakukuwa na mtu aliyeonekana hata kufanya usafi tu ijapokuwa eneo lote lilikuwa safi kabisa. Kijana huyu mtanashati alivuta hatua huku akijua ni wapi kaelekezwa kufika.

'Dassen Keputo'

Msalaba wa kaburi hilo ulisomeka hivyo.

Dassen Keputo! Akalirudia jina hilo, akainama kidogo na kuweka ua lile karibu kabisa na msalaba kisha akarudi nyuma na

kusimama. Ni wakati huo alipogundua kuwa hakuwa peke yake, nyuma yake kulikuwa na mtu mwingine ambaye naye alikuwa kashika ua kama la kwake, akavuta hatua na kuliweka juu ya kaburi lile, kisha akarudi nyuma na kusimama sambamba na Amata. Alikuwa mwanaume, mtu wa makamo, umri wake ulionekana kuwa umeenda, Amata akamtazama kwa sekunde chache asiitambua sura ile.

“Unamjua Dassen Keputo?” Yule mtu wa makamo akamuuliza Amata bila hata kumtazama.

“Simjui … wewe unamjua?” Amata akajibu na kurudisha swali.

“Simjui ila namwelewa, amekufa mwaka 1984, alifia Rhodesia katika shambulio la kigaidi lililofanywa na watu wasiojulikana,” yule mtu akamwambia Amata.

“Asee, Mungu amrehemu!” Amata akajibu.

“Huyu Dassen, ana ndugu zake, na hawa ndugu wapo ndani yake, ina maana amezikwa nao, ila nina uhakika kuwa wapo hai…”

Amata akageuka mzima mzima kumtazama mtu huyo, lakini Yule mtu hakumtazama Amata kabisa ila machoye yalikuwa katika msalaba ule.

“Mbona unaongea maneno magumu sana halafu hayaeleweki!” Amata akamwambia.

“Si magumu, utayaelewa tutakapoonana tena!” akamwambia na kuanza kuondoka, Amata hakuwa na jingine zaidi ya kumtazama tu mtu Yule akipotelea kwenye miti miukubwa ya maua iliyotenga makaburi hayo na kanisa. Amata

naye akavuta hatua kurudi garini kwake.

Dassen Keputo! Akawaza huku akifungua mlango wa gari lake, kabla hajaketi kitini, akaona kijikaratasi kidogo juu ya kiti cha gari, akakiinua na kukisoma. Upande mmoja kiliandikwa jina la kike *'Stella Bandauani'*. Upande wa pili kiliandikwa, *'Mtaa wa Ngomati – Keko, namba 287 K'*.

Akatia moto injini na kuendesha kwa kasi. Saa moja

baadae akawasili Keko, akautafuta Mtaa wa Ngomati, akaupata, ikawa kazi kutafuta nyumba yenye namba ile. Bahati nzuri akagundua kuwa ninyumba za NHC hivyo hazikumsumbua kuipata. Akaegesha gari na kuteremka, akaiendea nyumba aliyoihisi haswa. Mbele ya nyumba hiyo yaani kwenye kibaraza kulikuwa na wanawake wawili wakisukana.

"Hodi!" akabisha.

“Karibu! Karibu baba!”

mmoja wale wanawake akamkaribisha huku akinyanyuka na kuingia ndani huku akimwacha shoga yake nje. Ilikuwa nyumba ndogo, kama unavyojua nyumba za kota za enzi hizo. Ndani ya nyumba hii kulijazwa na samani za kawaida sana zilizopangiliwa vyema. Upande wa juu, ukutani kulining’inizwa picha nyingi za *black and white*, yaani zilikuwa zinaashiria kuwa ni za zamani.

Akashusha macho na kumtazama mwanamke huyo kibonge ambaye umri pia ulikuwa ni changamoto kwake.

“Shikamoo!” Amata akamwamkia.

“Marahaba karibu baba!” akaitika.

“Samahani, bila shaka hapa ni Keko, Mtaa wa Ngomati, namba 287 kwa Bi. Stella Bandauani…”

“Yaani umefika baba, na huyo Stella ndo mimi…” akajibu kwa

kumkatisha, “nikusaidie nini baba?” akauliza.

Amata alishangazwa na ukarimu wa hali ya juu sana wa mwanamke huyu, maswali kadhaa yalikuwa yakipita kichwani mwake bila kupata majibu, macho yake yakarudi kwenye picha moja ambayo ilimwonesha msichana mrembo aliyevalia gauni la mtindo wa *Zembwela*, na nywele zake zilikuwa zimesukwa mabutu ya

uzi. Upande mwingine wa picha hiyo kuikuwa na kijana mtanashati, aliyevali shati matata sana la *Juliana* na suruali ya *Dengriz*, kiatu cha *Rise On* au raizoni kilim-*rise* kwelikweli, nywele zilizochanwa kwa mtindo wa *Afro* ziliudhihirisha utanashati wa kijana huyu. Katikati yao kulikuwa na gari aina ya *Peugeot 504* ambayo wao wawili waliiegemea kila mtu kwa upande wake.

“Mbona watazama sana picha yangu?” Stella akauliza.

“Nimeipenda hiyo old school!” akajibu Amata.

“Enzi za ujana wangu hizo, hii tulipiga mwaka 1984 miezi miwili kabla ya huyu bwana kufariki…”

“Amefariki?”

“Ndiyo kwenye ajali mbaya ya gari huko Chamwino, Dodoma,” Stella akaeleza huku akiitungua ile picha na kuishusha mezani.

“Alikuwa nani yako?” Amata akahoji huku akiitazama picha ile kwa karibu zaidi.

“Alikuwa bwana ‘angu huyo… alikuwa ana pesa sana, kila weekend sisi ni kutoka tu, mara Tazara Club, mara Ruvuma mpaka Maputo, siku nyingine DDC Kariakoo yaani weh! Enzi zile nimekula sana maisha…” Stella akaeleza.

“Alikuwa anaitwa nani?”

“Kiukweli, na nikikwambia utanicheka, tumekuwa wapenzi kwa zaidi ya miaka mitatu lakini sikuwahi kumju jina lake, hata kazi yake sikuijua, yeye mara kaenda huku, mara kule ye ni kusafiri tu, na jina tulilokuwa tunatumia sana ni Chamellione!” Stella hakuwa mchoyo wa majibu, akamweleza Amata.

Chamelleone! Akajaribu kuvuta kumbukumbu ya jina hilo, akatikisa kichwa juu chini.

“Unamjua? Aaa hata hivyo ulikuwa mdogo sana au…”

“Simjui, na nisingeweza kumjua, ok tuache hilo, nimekuja kwako nina shida…”

“Sema baba!”

“Unamjua mtu anaitwa Dassen Keputo?” akauliza.

“Dassen, Dassen, Dassen… mh! We mbona jina geni sana? Ni mtu au?”

“Ndiyo ni mtu, ameshakufa na amezikwa Mikocheni…” Amata akamwambia.

Stella akatulia kimya kwa sekunde kadhaa akijaribu kuvuta kumbukumbu.

* *

‘Yaani mi hata sijui walinitekaje, watakuwa na dawa wale, yaani wamenichukua kama kondoo’.

‘Poe tumeshaokoka mpenzi wangu ila wao lazima huko nyuma wakipate

cha mtema kuni. Lile jumba mi nalijua, ni jumba la Dassen'.

'Huyo Dassen ndiyo nani? Niambie Chamelleon…"

'Dassen, sio mtu mama, ni eneo, nimewasikia wakizungumza hayo…'

* *

Stella akainua uso na kumtazama Amata, "Dassen siyo mtu!" akamwambia.

"Nini?" Amata akauliza.

"Dassen siyo mtu!"

“Siyo mtu?” Amata akauliza kisha ukimya ukambeba.

Sekunde kadhaa, akarudi katika hali yake ya kawaida, akamtupia jicho Stella, akagundua kuwa yupo kwenye lindi la mawazo.

“Umesema si mtu?” akamuuliza.

“Ndiyo si mtu, ni eneo…”

“Si mtu ni eneo!” akarudia kauli ya mwanamama yule. Kamanda Amata alijikuta

anaingia katika mtego mwingine ambao hana budi kuutegua. Labda akiutegua huu ataweza kupiga hatua ya tatu au nne mbele, sijui. Mawazo na akili yake vikaanza kuchekecha mambo, mambo mazito, akamkumbuka yule kichaa aliyempa bahasha, akakumbuka alivyomsisitizia kuwa ni ujumbe wake.

Yule kichaa ni nani? Akajiuliza. Ana uhusiano gani na jambo hili?

Akazidi kujitwika maswali ambayo hakupata majibu yake. Kila alipofikiri uzito wa ujumbe ndani ya bahasha ile alijikuta akidundwa moyo kama saa iliyopoteza mwelekeo. Mawazo yake akasafiri mpaka makaburini alipokuta kaburi la Dassen Keputo, na Yule babu aliyekuja kuweka shada baada yake na kumuuliza maswali kadhaa, akamuunganisha katika mawazo yayohayo.

Naye ni nani? Ni yuleyule kichaa au? Akaendelea kujilundikia maswali yasiyo majibu. Akavuta kumbukumbu aliporudi kwenye gari na kukuta kile kijikaratasi ambacho kwacho ndo sasa yupo katika nyumba hii, akizungumza na Stella, mwanamke wa makamo, mwenye mwili uliojaa nyama, hakuwa msichana wala mzee bali mtu wa makamo. Mara hii alikuwa tipwatipwa, ukimtazama

mwonekano ule wa mwaka 1984 na huu wa sasa, tafauti.

Rudi 1984…

Baa ya Lango la Jiji

Stella alibaki peke yake kitini baada ya Chamelleon ‘mtu mzima’ kumwacha kwa sekunde kadhaa huku akimtaka kuendelea na kinywaji kwa kuwa yeye angerudi baada ya sekunde au dakika chache.

“Unaenda ‘api?” Stella akauliza.

“Msalani, naja sasa hivi!” Mzee huyo akajibu huku hatua zikianza kupeleka huko asemako. Hakuna linguine alilolifanya Stella zaidi ya kumsindikiza kwa macho na kumshuhudia akimezwa katika wingi wa watu waliokuwa wakiburudika na muziki wa taarabu kutoka JKT. Alipoletewa bia yake ya Pilsner hakufanikiwa hata kupiga funda moja, akasikia

sauti ya kiume ikimjulia hali, akashtuka na kumtazama mtu huyo asiyemjua. Alikuwa mwanaume, mzungu si mzungu, mwafrika si Mwafrika, yaani yupo yupo tu, tumwite chotara, hili litamfaa zaidi.

"Usiniharibie starehe yangu!" Stella akamwambia kijana yule.

"Sasa kama ni starehe, nataka nikakupe leo," Yule kijana akamwambia Stella na kumwonesha ndani ya koti lake

jisu kubwa linalong'aa japo kwa mwanga hafifu wa taa, "na ukileta ubishi nakutumbua hayo macho yako," akaongeza. Msichana huyu, akapiga macho harakaharaka kumtazama bwana wake asimwone.

"Hah! Hah! Hah! Usijisumbue kabisa, hata kuja haji," Yule kijana akaongea kwa sauti ya kukwaruza na kuogofya, akamwamuru Stella kusimama na kuondoka naye, hakupinga,

alikiogopa kisu kile kikubwa.
Kwa macho yake ya nyama zaidi
ya kisu cha jikoni hakuwahi
kuona aina hii ya kisu au tuite jisu
sanasana aliona kwenye filamu
ambako bwana huyu,
Chamelleon pia alipenda
kumpeleka kama sehemu
mojawapo ya starehe, mara
Odeon, wakati mwingine New
Chox, ila Stella alipapenda
Avalone, na hakupapenda kabisa
Drive In. hakuwa na budi
kusimama, hakuwa mbishi,

akafuata amri na kutolewa nje huku hajui wapi apelekwapo. Nje ya ukumbi huo, kulikuwa na watu wengi kama kawaida, mara hii walikuwa wengi kuliko wa mwanzo, hakuna aliyejali, kila aliyemtazama akisukwasukwa na mwanaume huyo alisonya na kutupa neno la kejeli, 'keshakunywa za watu, wacha akalipe…'

Akasukumiwa ndani ya gari na kufungwa kinywa chake chake

kwa gundi pana la nailoni,
mlango wa gari ukafungwa huku
mwanamke huyo akijikuta
kwenye sakafu ya gari hilo lisilo
na viti.

Rejea Sasa…

Mtaa wa Ngomati, Keko

"Nakumbuka waliniteka, lakini hatukufika mbali, tukapata ajali, nakumbuka nilijikuta ndani ya ghala nikiwa peke yangu nimefungwa kamba miguu na

mikono huku watu hao wakinipa vitisho vya kuniua," Stella akaeleza.

"Walikuteka! Akina nani?" Amata akauliza kwa shauku maana sasa alihisi anakaribia kujua kitu kingine zaidi.

"Siwajui …"

"Walitaka kukuua?"

"Hapana, nafikiri walikuwa wakimtaka bwana'angu, maana kama kuniua si wangeniua tu!" akaeleza.

“Kwa nini walimtaka bwana’ako?” Amata akazidi kuhoji.

“Hapo mi sifahamu, unajua Yule bwana naye hata alikuwa haeleweki, sijui alikuwa jambazi yaani sijui tu, siku moja keshakuja na bunduki chumbani kwangu, siku nyingine kaja mikono ina damu mpaka nikawa naogopa,” akazidi kueleza na Amata akatega sikio akisikiliza.

“Sasa baada ya kujikuta ndani ya ghala hilo ukatokaje au walikuua?” Amata akamuuliza.

“Aaaaa hah! hah! hah! We kaka jamani, hivi mtu ukifa utakuwa hapa tena loh!” Stella akacheka na kwa swali lile akaonekana hata kubadilisha aina ya mkao, “kwanza we ni nani, hujanambia isije nikawa naongea na askari hapa, mi nabwabwaja tu…”

“Usihofu, mimi ni mtoto wa Chameleon!” Amata akaanza

mbwembwe zake wakati hata sura tu ya mtu huyo haijui. Jibu hili liliufanya moyo wa Stella kupaa kwa hofu. Akaonekana kama kukosa cha kusema zaidi ya kumwemwesa midomo yake.

"Umepajuaje hapa?" Stella akauliza.

"Baba yangu kabla hajafa aliniandikia kijikaratasi hiki…" akampa ile karatasi aliyoikuta ndani ya gari.

“Ina maana umekitunza mpaka leo tangu mwaka ‘85? Naona hata kalamu hii ni *Simba* au *Laska*,” Stella akaongeza maneno katika jibu hilo, akaigeuzageuza kile kikaratasi.

“Dah! Mwandiko huu ni wa mpenzi wangu kabisaaaa, ngoja nikuoneshe basu za mapenzi alizokuwa ananiandikia,” Stella akasema na kuinuka, akaingia chumbani na kutoka na kimkoba cha ngozi, akafungua na

kumwaga bahasha kadhaa mezani, akaifungua moja na kumwonesha hati za mpenziwe huyo kwa kuifananisha na ile ya kwenye kijikaratasi. Kweli ilifanana kabisa, Amata alitikisa kichwa kukabali.

"Alinambia nikija kwako wewe utamjua Dassen Keputo ni nani, na alisisitiza nimwone. Ni miaka mingi imepita mama, nilikuwa nasoma shule ya msingi, ila sikuwa nimesahau juu ya hili…"

“Ndiyo, nakumbuka, baba yako alikuwa na marafiki wengi sana, ila sikuwahi kumwona huyu Dassen, nitakachofanya labda kukuonesha eneo ambalo jumba lile lilikuwepo, na sijuia hata kama nitapakumbuka sawasawa,” Stella akajibu na kumwambia Amata.

“Nafikiri utapakumbuka kabisa, tunaenda sasa au vipi?”

“Hata kama ni sasa ni sawa! Ila siku ile kila kitu kililipuka, baba

yako alilipua kwa bomu jengo lote. Sijawahi kupita tena kwa sasa, ila si mbaya, labda wamejenga tena. Mimi ninampenda sana baba yako, marehemu Chamelleon. Naye alinipenda sana nini nataka alinipa, ila jambo moja tu alilokuwa ananikuna ni kuwa hakuwahi kumdharau mama yenu…"

Laiti angejua kuwa anayeongea naye hata hamjui huyo

Chameleon sijui ingekuwaje, lakini aliaminishwa na maneno ya kijana huyo kumbe hakujua kamani muintelijensia mwenye uwezo wa kucheza na akili ya mtu na kumgeuza atakavyo. Kichwani mwa Amata tayari alikwishajua kuwa kwa hatua hiyo amefika mahala pakubwa sana, anamkaribia zaidi Dassen hata kama kaburi lake aliliona kule mikocheni.

Kuna siri iliyojificha! Akawaza

Na siri hii ni Dassen Keputo! Akajijibu na kuridhika na jibu hilo. Dakika hiyohiyo simu yake ikaita, akatazama kwenye kioo na kujua mpigaji mara moja, Gina. Hakuipokea zaidi ya kuifunga sauti isipige kelele. Dakika kumi baadae, safari ilianza, yeye na Stella ndani ya gari. Hakukuwa na mazungumzo zaidi ya maelekezo tu. Ijapokuwa ni miaka mingi ilikuwa imepita, Stella bado alikuwa akikumbuka ingawa alibabaika kidogo. Baada ya

muda walifika Kinondoni Moscow, mitaa kadhaa wakafika mtaa maarufu wa 'Maandazi Street'.

"Nakumbuka, hapa kulikuwa na soko kubwa sana…" Stella akasema.

"Ina maana hayo yote uliyaona usiku huo huo?" Amata akauliza.

"Hapana, siku nyingine tulikuja kuangalia, tukagundua kuwa lile jengo halikuteketea lote… yes, nafikiri ni hapa!

Ndiyo ni hili jumba kubwa nyuma kulikuwa na sijui banda sikumbuki, hii imekarabatiwa au imejengwa upya, lakini ni hapa, nakumbuka duka lileee, na huu mtaro gari yetu ilipata ajali mbaya hapa tukijaribu kutoroka," Stella akauliza.

"Kwa hiyo bila shaka Dassen anaishi humu?" Amata akauliza.

" 'Dassen siyo mtu', Chamelleon alinambia. Lakini

waweza kushuka kwenda kuuliza..”

“Haina haja kwa sasa, inatakiwa nije kwa muda muafaka maada umenionesha nakushukuru,” Amata akajibu na kuanza kutafuta njia ya kurudi barabara kubwa. Nusu saa baadae akaegesha gari tena katika nyumba ya Stella na kumshukuru. Kutoka kwenye pochi yake akampatia shilingi elfu kumi na tano.

“Yaani we una moyo mwema kama baba yako… asante sana!” Stella akajibu na kuteremka kwenye gari na Kamanda Amata akashika nji na kuondoka zake. Njiani alikuwa na mawazo mezngi sana, zaidi ni kuhusu huyu Dassen, iweje awe si mtu, na aliyezikwa kule ni nani? Akazidi kujiuliza na hakupata jibu.

Hapa kuna kazi kubwa, kumpata au kufumbua fumbo la

Dassen Keputo! Akawaza huku akikunja kona kuiacha Barabara ya Kawawa na kukamata ile ya Nyerere, akakanyaga mafuta na kuelekea mjini. Akaiacha Barabara ya Nyerere na kuchukua ile ya Nkurumah, akazunguka mzunguko wa Mnara wa Saa na kukamata Barabara ya Samora mpaka akalifikia jengo la JM Mall.

Ndani ya afisi ya AGI Investment, Kamanda Amata

alifungua mlango na kuukuta uko wazi, akausukuma na kuchungulia ndani. Jicho lake likagongana na lile *tamu* la Gina. Mwanamke huyo hakuamini kama anayemwona mbele yake ni Yule ampendaye sana. Akainuka haraka kitini na kumkumbatia kwa nguvu huku akibubujikwa machozi.

"Aaaamat jamani, umenitesa mwenzio, ulikuwa wapi wewe?"

akauliza huku akimpigapiga vijingumi vya kimahaba kifuani.

“Basi Gina, pole, najua sikukuaga, ila sikutakiwa kukuaga pia, ila pole kwa yaliyokukuta…” Amata akambembeleza.

“Ningekufa kwa ajili yako, wivu wangu ungeniponza mimi,” akaanza kulia tena na kijana huyo akawa akimbembeleza kwa maneno matamu huku bado wakiwa wamesimama katikati ya

afisi hiyo, “hivi Kamanda, nikuulize?”

“Ndiyo niulize mpenzi, nyonda wangu!” Amata akaitikia.

“Unanipenda? Unanipenda Amata?”

* * *

09

Old Town Prague

Jopo la watu kama watano hivi lilikutana katika jengo la Liben pembezoni kidogo mwa mji wa

Prague panapojulikana kama Old Town Prague. Jopo hili lilikuwa ni watu watano tu, wawili upande huu na wawili upande mwingine na mmoja aliketi mbele ya wote. Huyu wa mbele alikuwa akiongoza kikao hicho kifupi kinachojuikana kama E.M. Mara nyingi vikao hivi huwa ni kujadili maendeleo ya pale au kubadilisha tawala hii na ile, lakini leo haikuwa hivi kwani kila mjumbe alifika akiwa hajui hata agenda ya kikao hicho.

“Ninasikitika na hali inayoendelea huko Kusini mwa Afrika, nahitaji ripoti kamili kutoka kwa Margaritha, ni nini kimetokea Namibia? Taifa kama Tanzania linawasumbua nini?” sauti ya Alfa ilisikika.

Macho yote sita yakamtazama mwanamama huyo pekee katika kikao hicho, aliyekuja kumwakilisha McCain ambaye hali yake ilikuwa tete katika moja ya hospitali kubwa huko Afrika

ya Kusini. Margaritha alilieleza jopo hilo kile kinachoendelea kati yao na Serikali ya Tanzania, akaeleza juu ya vikao vya upatanishi viwili vya mwisho ambavyo vimeleta matatizo makubwa kati yao.

“Ina maana Serikali ya Tanzania inataka kumuua McCain?” akauliza Alfa.

“Siwezi kukupa jibu kuwa ni ndiyo au siyo, kwa sababu sisi ndiyo tulipanga kufanya hivyo

kwa upande wao, ila nashangaa mambo yakageuka kwetu….”

“Na ni nani huyu anayeitikisa ngome yangu?” Sauti ya Alfa ikapaa kati ya jopo hilo.

“Tunafanya uchunguzi kumjua mtu huyu, tayari nimepata baadhi ya information kuhusu yeye,” Margaritha akaeleza.

“Tuambie hiyo information…” Alfa akaunguruma huku ule mwanga wa taa unaopiga kutoka nyuma

yake ukimficha sura asijulikane. Ukumbi huo mdogo, ndani ya jengo la Liben, ulikuwa kimya kabisa, ni sauti mbili tu moja ya ukali, ya kiume na nyingine ya woga, ya kike zilikuwa zikisikika.

"Jina ni Amata Ric, *Status* ni *Tanzania Secret Agent 01*, *Code of Status: 005* – ikimaanisha *Intelligent and unstoppable human being"* Margaritha akaeleza na wajumbe wale wakaandika taarifa hiyo kwa kifupi.

"Who is that cockroach?" Alfa akauliza na kuuacha ukimya utawale kwa sekunde kadhaa, "Ok, sasa najua cha kufanya, nitaongea na Rais wa Umoja wa Ulaya, Tanzania, itawekewa vikwazo vya kiuchumi mpaka itakapotupatia watu wetu, na itawatoa tu. Na sasa naweka saini katika hii hati ya kuhakikisha huyu mdudu aliyefanya haya, huko Namibia, shughulikiwe hii ni *Licence to Kill*," akasaini karatasi moja na kuiacha hapo mezani.

Zile taa zikazimika, na zilipowaka, Alfa hakuwepo katika kiti chake, maagizo na maazimio tayari yalikuwa kwenye karatasi ile.

Waliobaki katika kikao hicho wakamtumbulia macho Margaritha, mwanamke pekee aliyetumwa kumwakilisha McCain ambaye hali ya kiafya ilikuwa tete. Mwanamke huyu alifura kwa hasira, alijua ni nini maana zaidi ya manneno ya Alfa

katika kauli zake. Mpaka yeye, Alfa aamue kwenda kuzungumza na mtu mkubwa kama Rais wa EU, maana yake ni kwamba wao wa chini wameshindwa kazi; alijua nini kitakachofuata kwa yeye na wenzake katika ukanda wan chi hizo za Kusini mwa Afrika. Akili yake yote ikamfikiria Parrot, mwanamke alipewa kazi ya kutekeleza kifo cha taratibu kwa mtu mmoja wa Tanzania kama shinikizo kuwa ‘tunataka watu wetu’, lakini badala yake ni

bosi wake ambaye anakumbana na kadhia hiyo. Maswali mwengi akajiuliza, ina maana daughter huyu amewageuka au ni vipi? Hakuelewa. Iweje awageuke, maana kama ni pesa ni nyingin analipwa, nani anaweza kumrubuni akaacha njia sahihi? Akajiuliza huku akili yake ikiwa inazunguka kwa mawazo.

“Kikao kimesitishwa, kila mmoja arudi katika jimbo lake isipokuwa gavana wa Jimbo la

Afrika ya Kusini na Afrika ya Mashariki watafuata maelekezo watakayopewa hivi punde, asanteni," sauti ilisikika kutoka katika vifaa vyao walivyovaa masikioni. Wajumbe wakasimama na kila mmoja akashika nji yake.

* * *

Kliniki ya mifupa ya Oasis – Namibia

Parrot alikuwa kimya kitandani, miguu yake ilikuwa

imefungwa plasta ya Paris (P.O.P), madaktari walimpa tiba hiyo baada ya kufanikiwa kuiweka sawa mifupa yake iliyovunjwa vibaya kwa risasi na kitendo cha kujirusha kutoka ghorofani.

Ndani ya chumba hicho hakukuwa na mtu mwingine zaidi ya yeye na muuguzi aliyekuwa anakuja mara kwa mara kumwangalia. Hiki kilikuwa chumba cha siri sana ambacho

mtu wa kawaida hakuwekwa ndani yake, ni hawa WP tu walikuwa wanakilipia na kuhifadhi watu wao pindi wanapohitaji matibabu. Akiwa kalala kimya, na macho yake yakitazama runinga ndogo iliyofungwa juu yake kwa mbele, mlango ukafunguliwa, wanaume wawili walioshiba wakingia na kusimama huyu upande huu na mwingine upande ule wa mlango. Nyuma yao akaingia mtu mwingine mtanashati, aliyevalia

suti nadhifu sana. Hakupata shida kumtambua, alikuwa ni mmiliki wa Hoteli ya Safari, mahali ambapo mkutano ule ulifanyika siku iliyotangulia.

Wote watatu hawa walikuwa Wazungu pyua, hata kama ungewaona ungewatambua kwa rangi ya ngozi yao ijapokuwa mabaunsa hawa walikuwa wamenyoa upara vichwani mwao. Bwana huyu, mmiliki wa hoteli naye alikuwa ni

mwanamtandao wa WP ambaye kazi yake kubwa ni kujua wageni wote hatarishi wanaoingia katika hoteli yake ni nyinginewe.

"What have you done, woman?" akauliza bila hata salamu. Parrot akabaki kumwangalia tu, hakujibu neno, *"you have killed a big man daughter,"* akaongeza kusema akilaumu kuwa mwanamke huyo amemuua mtu mkubwa sana.

“Si mi-mi!” Parrot akajibu kwa taabu sana, “muuaji aliingia katika shamba la Maxwell, ndani ya hoteli yake, wakati wa jioni, tafuteni hiyo picha mtamjua tu, ila si mimi!” Parrot akaeleza japo kwa sauti ya chini sana. Yule bwana na vijana wake wakatazamana, maana walikuwa wanaijua vyema kabisa hoteli ile, nayo pia ilikuwa ya mtu wao, Lord Maxwell ambaye makazi yake yapo Pretoria, Afrika ya Kusini.

“Mim nilifanya kama nilivyoagizwa, lakini nashangaa nini kimetokea, ina maana kuna mtu aliyegeuza microphone, nani mwenye mamlaka hayo kama si vijana wako, wahudumu wa hoteli? Maana hakuna mtu mwenye uwezo wa kuingia ndani ya chumba kile…” Parrot akaeleza huku akibubujikwa kwa machozi.

“Nitalifanyia kazi ndani ya saa hizi’…! mbili, ikibainika maelezo

yako si kweli, basi hiki ndicho kitakuwa kitanda chako cha mwisho hapa duniani… *Let's go!*" akamwambia Parrot na kuwaamuru vijana wake kutoka katika chumba kile. Parrot akabaki tena peke yake baada ya milango kujifunga na kumtenganisha na watu hao. Mwanamke huyo alijua nini kitafuata kama watu hao wasingepata uthibitisho kwa hilo alilowaambia, alijua, adhabu ya

msaliti katika WP ni kunyongwa kwa siri mpaka kufa.

* * *

Katika chumba kidogo ndani ya jengo la kizamani katika Jiji la Prague, Margaritha na watu wengine wane walikuwa wameketi kwa kuizunguka meza ndogo ambayo kioo chake ni skirini kubwa ya kompyuta inayoweza kuwaonesha mambo mbalimbali.

“Hii napa ndiyo picha yake?” mmoja wa watu hao aliyevalia nadhifu sana akaliambia jopo hilo.

“Kama *crossmatch* imekubali basi huyo ndiye…” Margaritha akajibu.

“Bila shaka, huyu ndiye kwa sababu kila kitu kimekaa sawa, kuanzia nywele, macho, kidevu na vingine… anhaaaa yes, ni yeye…”

“Cheki status zake…” mwingine akasema.

“Tanzania Secret Agency 01…”

“Jina…”

“Really name ni Amata Ric na jina la kificho ni Kamanda Amata…”

“Yes!” Margaritha akaafiki, “anatakiwa kuuawa,” akaongeza.

“Atakufa tu, ni kazi ndogo tu, kama tulimuua Dal Baboz kule

Peru tutamshindwa mjinga huyu?" mmoja wa wale waliokuwa katika ile meza wakizidi kumchimba mbaya wao alisema.

"Nina hasira sana na huyu mtu, kwanza kamuua Jesca, pili kamvunja miguu Parrot, sasa naanza kuhisi kuwa ndiye aliyefanya mchezo wa kummaliza McCain…" Margaritha akawaambia wale wengine.

“Kuwaumiza au kuua hao wawili isitufanye tumuhofie, Alfa keshatoa Licence to Kill…” mwingine akadakia.

“Hey! Hey! Hey! Hey….”

“Nini wewe?”

“Amata Ric au Kamanda Amata, wakati mwingine hutumia jina Mr. Spark…” alipotamka maneno hayo wote wakamgeukia kijana huyo na kutazama pale anapoangalia katika ile skirini kubwa juu ya meza.

“Ndiye aliyeangusha kampuni ya uchimbaji madini ya Robinson Quebec…” akawaambia.

“What?” mwingine akashangaa.

“Shiiiiitttttttt!!!!!!!” akang’aka.

“We nini, una pepo?” Margaritha akauliza.

“Ni mtu hatari, hatari sana, hapa imeandikwa kwa kutumia kodi za kiitelijensia duniani…” akaeleza.

“Enhe yeye ni ngapi?” Margaritha akauliza.

“Code 005, cheki kwenye listi ya CIA code hiyo maana yake nini?” Yule kijana akawaambia na mwingine akabofya hapa na pale akafanikiwa kupata maana ya kodi hizo katika maswala ya kiintelijensia.

“Intelligency code 005 ni ‘Intelligent and unstoppable human being’…”

“Mather fuck*r … unstoppable what?” mwingine akang’aka kwa dharau, “mpelekeeni ujumbe wangu, ni nani alikuwa ameshindikana kama Batross, Benitez, Almandro na wengine, wote hawa nimeua kwa mkono huu, seuse yeye! Nikitua tu Uwanja wa ndege tayari yeye anazimia kabla sijamgusa,” akasema.

“Utampataje? Maana The Cobra mwenyewe kaingizwa

mjini na huyo huyo mtu, mpaka sasa hana sura yake…. Kiukweli hatukutegemea kama Tanzania kuna watu wa hatari namna hii kama enzi zile za kina Gamba na Kiango, walitusumbua sana washenzi wale, ila sasa watakuwa wazee… na kama mnakumbuka mwaka ’84 alikuwapo mwingine anaitwa kwa kificho Chamelleon, huyu tulishammaliza kwa ajali ya lori kule Dodoma, sasa huyu nani?” Margaritha aliongea kwa jazba.

“Mwambie The Cobra atulie, mwanaume naingia kazini, nitamuua kama ninavyoua mbu!” yule jamaa akajisifu. Akachukua moja ya picha zake ya nakala ngumu na kuikata X kwa kalamu yake nyekundu. Jamaa huyu alizoeleka kwa tabia yake hii, akishaikata picha mtu kwa X nyekundu basi mtu huyo mpe siku zisizozidi tatu, tayari hatokuwa na roho.

* * *

Katika eneo la stendi ya Mkwajuni, Kamanda Amata alikunja kona kushoto na kuifuata gari moja ndogo nyeupe ambayo aliiona tangu ikiwa inatoka katika jengo lile alilopelekwa na Stela mchana wa siku hiyo. Mara hii alikuja tena peke yake ili tu kuona nini kinachoendelea na ndipo alipoiona gari hiyo ikitoka.

Wakashusha bonde la Mwongozo na kuibukia

Magomeni, lile gari likakunja kushoto na kukamata Barabara ya Morogoro mpaka Faya, likapita moja kwa moja mpaka baharini na kuegeshwa karibu kabisa na Hoteli ya Five Star. Pale akashuhudia tu akishushwa mwanamke na ile gari ikaondoka kuelekea Kurasini, akaachana na yule mwanamke na kulifuata lile gari huko liendako, kituo cha mwisho kilikuwa Kurasini, Mtaa wa Chakarani, mbali na barabara kuu ya Shimo la Udongo na

jumba hilo kubwa na zuri lilijengwa kando tu ya Bahari ya Hindi. Lile gari likaingia ndani ya wigo na kusimama mbele tu ya mlango mkubwa. Kutoka katika gari hilo akateremka mzungu mmoja mrefu lakini mwenye mwili ulioshiba akapotelea ndani yake, hakuna mwingine aliyeshuka. Kamanda Amata akasogeza gari lake mbali kidogo na lile geti, katika mtaa huu nyumba zote zilikuwa kimya yaani zenye wigo mkubwa na

mageti ya kutisha, hakuna kumwomba chumvi jirani yako. Akatafuta mahala pazuri pa kuegesha gari lake. Baada ya kupita kama nyumba tatu nne hivi, akakuta kuna ujia unaoingia kwenda baharini. Ujia ule ulitosha kabisa kuweza kuliegesha gari lake na linguine likaweza kupita bila shida, akafanya hivyo. Akaitazama saa yake, ikamwonesha kuwa bado ni mapema sana, saa mbili ya usiku inakimbilia tatu, akashuka na

kuufunga mlango, kisha akarudi kwa kupiti njia ileile ambayo alijia kwa gari.

Taa ndani ya jumba lile ziliendelea kuwaka, Amata akatzama vyema kupitia geti kama kuna chochote ambacho kinaweza kuwa hatari kwake, hakuona. Kitendo cha sekunde tatu tu tayari alitua ndani bila kufanya ukulele wowote. Akataulia kama sekunde kumi na tano hivi kusubiri nini kitatokea,

hakuna, akavuta hatua za kipaka mpaka kwenye kiambaza cha nyuma hiyo, akiwa kaweka mgongo upande wa ukuta huku mikono yake ikisambaa vyema ukutani humo, akatembea kiubapababapa mpaka karibu na dirisha kubwa la sebule hiyo, macho yake yakapenya katikati ya mapazia mawili makubwa, sebule pana, yenye samani za thamani ikayalaki. Akatoka eneo hilo na kuzunguka upande wa pili ambako huku sasa aligundua

kuwa ni vyumbani. Kutoka katika moja ya madirisha madogo alisikia maji yakiflashi chooni.

Yuko toi! Akawaza na kusubiri mahala hapo. Baada ya maji yale kutulia, akasikia mluzi kwa mbali jamaa akijiburudisha, hili lilimfanya Amata atabasamu. Akawahi kusogea dirishani ili kumwona mtu huyo. Ewaaaaa! Akamwona wazi kabisa, Mzungu, mwenye ndevu za kiasi, nywele ndefu mpaka shingoni, mwili

wake hasa mikono ilikuwa na vinyweleo vya kutosha. Akamtazama nyendo zake ndani ya chumba kile. Yule jamaa alipotoka tu chooni akaliendea kabati kubwa la ukutani, akavua shati alilovaa na vesti akaziweka kando, hapa Amata akashuhudia mchoro mkubwa wa Cobra uliochorwa mgongoni mwa jamaa huyo. Na chini ya mchoro huo kulikuwa na maandishi yaliyoandikwa kwa nakshi safi, kwa Amata haikuwa ngumu

kuyasoma, *'The Cobra'*, yalisomeka.

Jamaa Yule akabadilisha nguo alizovaa, yote haya aliyafanya pasi na kujua kuwa nje kuna mtu, alipomaliza kwenye viwalo, akaelekea upande mwingine wa chumba, ukutani, akabofya katikati ya picha fulani, ikafunguka kama mlango wa *tabernacle* na kisha akabofya kwa ndani mara kadhaa, Amata akajua kwa vyovyote ndani hapo kuna

keypad yenye tarakimu fungushi. Yule bwana akatoa bastola moja kubwa hivi, Amata kwa kuiona tu akaijua, *Winchester*, akaisweka kiunoni na kurudishia ule mlango kisha akatoka nje na kuzima taa ya chumbani. Kamanda Amata akatulia kimya akaimtazama kijana huyo mpaka kaondoka na kupotelea nje, kisha yeye akatafuta dirisha la sebuleni na kuingia kupitia hilo.

Kwa kutumia macho yake makali ya kikachero yenye mafunzo ya hali ya juu katika kuangalia, Amata akatazama kwa nukta kadhaa sebule ile, haikuwa na kitu cha kumkwamisha misheni yake, akachukua miwani yake na kuipachika usoni tayari kwa kazi. Miwani hii ilimwezesha kuona hata kati ya giza nene, hivyo aliweza kutazama kila kitu kwa ufasaha kabisa. Akavuta hatua na kufika kweye korido inayompeleka chumbani hasa

kule anakotaka, akatembea harakaharaka mpaka katika ule mlango, akainua mkono wake na kuuingiza ndani ya fulana kisha akashika kitasa na kukikunja, akautikisa, umefungwa, akachomoa funguo zake zishizoshindwa kitasa, kwa kutumia mkono uleule, akapachika ufunguo na kuutikisa mara tatu tu, chumba kikawa wazi. Akaingia taratibu kabisa na moja kwa moja akafika palepale kwenye ile picha maana alijua

kwa vyovyote vile hapo ndipo penye kila kitu cha siri cha mzungu huyu. Akapapasa picha ile na kugundua ile nobu ilipo, akabofya, kile kimlango kikafunguka taratibu na kubaki wazi. Baada ya huo mlango akaona kamlango kengine kenye padi ya namba fungushi kama alivyofikiri. Daima anajua jinsi ya kufungua vitu hivyo kama ambavyo Chiba alimfundisha namba jinsi ya kupanga namba ambazo zingefungua padi yoyote.

Akabofya hizo namba mara ya kwanza zikakataaa, ya pili zikakataa ya tatu, nayo ikakataa. Amata akasukuti kwa nukta kadhaa, akachukua waleti yake na kutoa kitu kama chipio chenye mchongoko kwa mbele, katika padi hiyo, kati ya namba tano na nane palikuwa na tundu dogo, akaipachika na kuhakikisha imekaa vizuri, kisha akabofya namba nyingine, bila taabu, ule mlango ukafunguka.

Naam, kilikuwa kijisanduku kidogo chenye citu vichache, pesa taslimu dolari za Kimarekani na Euro za Ulaya, nyingi za kutosha zilizobanwa katika rababendi maburungutuburungutu. Kamanda hakutaka hayo, akasogeza pembeni na kuvuta bahasha iliyotunatuna, akaitoa nje.

T.S. ilisomeka namna hiyo juu kwa maandishi ya kuchapwa kwa

mashine. Kamanda Amata akaanza kufikiri nini maana ya TS, hakuona kama ni jambo lenye uzito sana, akaigeuzageuza na kugundua hata haikufungwa.

Asante sana! Akashukuru moyoni na kutoa vilivyo ndani, makabrasha machache lakini yalikuwa yamefungwa vizuri sana.

For your eyes only!

Mojawapo liliandikwa hivyo, moyo wa Kamanda ukaruka tik tak kwa sentenso hiyo,

akakumbuka bahasha aliyopewa na yule kichaa, akaduwaa kwa sekunde chache akifikiri uhusiano wa bahasha hizo mbili, utata. Amata, mara hii hakuja rasmi kwa kazi hii, akajikuta anashindwa afanyeje, kawaida kabrasha kama hiyo, huatoa kivuli na kuacha ile orijino ili mwenye nayo asihofu kuwa imedukuliwa. Sasa hakuwa na mashine hkwa kazi hiyo.

Opportunity never come twice! Akawaza. Kisha akaifutika bahasha ile ndani ya shati lake.

Akiikosa ndo' atajua kuwa Tanzania si mtu ya nchi ya mchezo, atawapa taarifa wenzake na mtandao mzima utatikisika! Akajisemea moyoni kisha akendelea kupekua ndani ya kijisanduku hicho. Mara ghafla akabutwaika kwa kuikuta picha yake ndani ya kikabati hicho.

“Shiiit!” akang’aka. Moyo wake ukapiga kwa nguvu. Juu ya picha ile paliandikwa *‘Terminate Immediatelly’*, yaani mwenye picha hiyo aondolewe haraka kwa lugha nyepesi ni *auawe*.

Kamanda Amata akaitazama ile picha na kugundua ni wapi imepigwa, Windhoek saa chache kabla ya kumvunja miguu Parrot. Aliikumbuka fulana hiyo, akaikunja ile picha na kuitia mfukoni, akapepesa macho huku

na kule na kuikuta ukutani picha ya The Cobra, akaichukua na kutafuta maka peni, alipoipata akaipiga X ile picha na kuiandika *'You are terminated'*, kisha akaondoka zake.

* * *

Saa nne usiku katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, dege kubwa la KLM liliikanyaga ardhi ya Tanzania. Mvua ya wastani ilikuwa ikinyesha na barabara za

kupita ndege hiyo zilikuwa zimejaa maji, hivyo ikalazimika ndege hiyo kutumia barabara ya dharula na kuegeshwa mahala pake. Kati ya watu walioshuka katika ndege hiyo alikuwamo mtu hatari sana, mzungu kutoka Urusi, huko nyuma aliwahi kuwa jasusi wa KGB kabla shirika hilo kusambaratika. Daniel Kremikov, pande la mwanaume, tungeita jitu la miraba minne liliruhusiwa kuingia nchini bila mtu wa

uhamiaji kujua dhamira haswa ya mtu huyo ni nini.

Nje ya uwanja huo alilakiwa na The Cobra na kukaribishwa katika gari ya kifahari sana, Jaguar, na safari yao iliishi katika Hoteli ya Double Tree. Chumba namba 430 kiliandaliwa kwa ajili yake.

“Karibu sana, utapenda siku ya leo kiburudisho cha aina gani? Muziki, pombe au mwanamke wa

Kiafrika?" The Cobra akamuuliza mgeni wake.

"Asee nimekuja kuua tu, kwa hiyo kwanza ni kumsaka mbwa huyu, nimmalize, ns hiyo ndo itakuwa starehe yangu, nikishamvunja shingo naondoka zangu, siwezi kukaa nchi za kimasikini kama hizi, hewa ya kuvuta imejaa vumbi, hakuna hata pa kukanyaga!" Kremikov akaongea kwa dharau ya hali ya juu sana akimwambia mwenyeji

wake huku begi lake akilitupia kitandani. The Cobra alikuwa akimya kando ya dirisha akitazama yanayojiri nje ya hoteli hiyo.

“Hivi mnaishije na mnafanyje kazi zenu katika nchi hizi za dunia ya tatu?” akamtupia swali mwenyeji wake.

“Usijali, utajua tu ni jinsi gani tunaishi na tunafanyaje kazi…”

“Kwanza we umeshindwaje kumuua huyo mbwa mpaka mi

nije kupoteza muda wangu? Hauna bunduki kubwa ya kummaliza, maana hutakiwi kumgusa, utachafuka," Kremikov akamwambia Cobra huku akitoa henga na kuning'iniza shati lake.

"Sikumjua mtu ninayepambana naye!" Cobra akajibu. Kaui hii ikamfanya Kremikov kumwangalia mwenyeji wake juu hadi chini.

"Kivipi?" akamuuliza. The Cobra kutoka pale aliposimama,

akageuka na kumtazama mgeni wake, “nilidhamiria kumuua, lakini kilichotokea nilimuua labda mpenzi wake au mke wake, sijui, kwani kila kitu kilikuwa sawa isipokuwa tu siku hii aibadili ratiba yake,” akamjibu.

“Ina maana unapajua mpaka anapoishi?”

“Hakika!”

“Basi kazi hiyo inaisha muda si mrefu. Mpango ukoje?” akazidi kuteremsha maswali.

“Twende kwanza nyumbani tukayaweke sawa, huko ndiko kuna kila kitu,” Cobra akamwambia mgeniwe, Kremikov akachukua fulana yake na kuivaa, mbele iliandikwa *‘Kill ‘em all’*, wakaondka zao kuelekea Kurasini.

* * *

Usiku huu Kamanda Amata aliegesha gari lake nje ya kliniki ya Daktari Jasmin ambako daima hufanyia kazi zake huko.

Huduma za usiku zilikuwa zikiendelea, ijapokuwa yeye mwenyewe hakuwepo muda huo, wahudumu wa afya na daktari mwingine wa zamu walikuwapo kama kawaida.

"Karibu!" akakaribishwa na muuguzi wa zamu.

"Asante sana," akajibu na kuketi kwenye viti vya kusubiria, "naomba mpe taarifa Dkt. Jasmin mwambie mgonjwa wake amekuja…"

“Amekwishaondoka yupo tu daktari wa zamu…” yule muuguzi akajibu.

“Najua, ila daima huwa ananiattend yeye, na alishasema nikija kama ye hayupo aitwe…”

“Ok nimwambie nani jina?”

“Mwambie Spark! Tena msisitizie kuwa najisikia vibaya,” akasisitiza. Kamanda Amata akabaki kitini akiwa amejiinamia huku mikono yake ameifumbata tumboni. Dakika chache baadae,

Yule muuguzi akaja na daktari mwingine, wakamchukua Amata mpaka chumba maalum, VIP, akapewa kitanda cha kulala na kutakiwa kumsubiri daktari husika. Nusu saa baadae, Jasmin akafika, moja kwa moja akaingia wodini na kumkuta Amata akiwa kapitiwa na usingizi mzito.

“We mwanaume!” akamwamsha. Amata akaamka na kuketi.

“Asee nimechoka sana, unajua tangu nimerudi sijapumzika kabisa…” akamwambia.

“Pole, nikuchome Varium ulale?” Jasmin akamuuliza.

“No! kuna kazi ngumu mbele yangu ambayo sitakiwi hata kufumba jicho…”

“Sure?” jasmine akauliza.

“Sure!”

“Usijali, hapa upo mahali salama kabisa, mpaka sasa ni

mimi tu ninayejua ulipo," Jasmin akasema.

"Na kwa sasa sihitaji mtu ajue nilipo, mpaka nitakapokwambia, nipe dakika sitini za kupumzika, nitakuita," Amata akamwambia Jasmine.

"Umezipata!" Jasmine akajibu na kutoka nje ya chumba hicho na kuingia afisini kwake. Kamanda Amata akatoa ile bahasha na kuiweka mezani.

T.S! akaisoma na mara moja akapata maana ya herufi zile, *'Top Secret'*, kutoka ndani ya bahasha ile akachukua kabrasha la *'For your eyes only'* na kulifungua ndani, kurasa ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne, hazikutofautiana sana na zile za kwenye ile aliyopewa na yule kichaa, isipokuwa tu jinsi ya kuandika, huyu aliandika kama taarifa na yule akaandika simulizi.

Ina maana yule kichaa aliliona kabrasha hili? Akajiuliza. Mbele

ya kurasa hizo zilifuata nyingine tatu, moja ilikuwa imeeleza mkakati mzima wa kuhakikisha Afrika haiwapati watu wake, na nyingine iliandikwa wapi wamefichwa na ramani ya kufika sehemu hiyo ilitaarifiwa kuwa imeambatanishwa na kabrasha hilo. Amata akachakura haraka kurasa ya mbele kwa minajiri ya kuiona ramani ile maana alijikuta anashikwa na shauku, haipo. Kurasa hiyo ilieleza kuwa hali

halisi ya watu hao na taarifa zao zimezikwa Dassen Keputo.

Dassen Keputo again! Akawaza. Kutokana na uandishi huu akathibitisha kauli ya Stella kuwa Dassen Keputo si mtu, bali ni eneo. Hata hivyo hakutaka kukubaliana moja kwa moja na jambo hilo.

Ina maana Dassen Keputo anajua kila kitu, na ameshakufa, amekufa nazo kwenye ubongo wake au amekufa nazo moyoni

mwake? Akajiuliza, shaka. Hapa Kamanda Amata akahamisha uthibitisho wake kutoka ile kauli ya Stella kuwa Dassen Keputo si mtu na kile alichokiona yaani kaburi la Dassen Keputo. Akili yake ikazunguka na kubingirikabingirika lakini hakupata jibu la moja kwa moja. Akafunga kabrasha lile na kuliweka kando, akachukua lingine, hili halikuwa na halikuandikwa chochote, pia ndani yake kulikuwa na kurasa

tatu tu, ya kwanza kabisa ilikuwa picha yake, yaani ya Kamanda Amata, ya pili ilikuwa picha ya Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye alikuwa akiongoza tume ya upatanishi iliyokuwa na kikao huko Windhoek. Maelezo machache yalifuatia.

Maelezo ya kwanza yalikuwa ni jinsi ya kumuua Amata siku moja kabla ya kikao cha Windhoek kwani walipewa taarifa na mtu wao ambaye alikuwa na ukaribu

sana na serikali. Maelezo hayo yalieleza jinsi gani ya kumuua pia yalisisitiza kuwa huyo ni mtu hatari, hivyo ni *shoot and kill*.

Maelezo ya pili yakaeleza jinsi ya kumuua huyo waziri na sababu ni kwamba mtu huyo anachokochoko nyingi sana katika swala hili, endapo watamwacha hai anaweza kuleta madhara. Wakaandika pia jinsi ya kumuua, kwa sumu ndani ya kikao huko Windhoek lakini afie

kwao baada ya saa sabini na mbili. Kabrasha hilo likaishia hapo, halikuendelea mbele, Amata akacheka kwa cheko la moyoni.

Kabrasha la tatu ambalo yeye hakuona kama lina umuhimu sana kutokana na wepesi wake, kiukweli halikuwa na hata karatasi moja, lilikuwa jalada tupu, akalirudishia ndani ya bahasha hiyo na kutulia kimya.

“Kama ilikuwa ni mipango yenu, basi sasa mtajuta, badala waziri atakufa mkubwa wenu muda si mrefu, na badala yangu, atakufa huyo nyoka wenu!” akajisemea kwa sauti ya chini. Hili kabrasha la pili lilimpa faraja kwa sababu aligundua mpango umeshafeli, kwa kuwa tayari huyo waziri alikwishamwokoa na yuko Tanzania, salama salimini, anaendelea na majukumu yake. Na yeye mwenye ndiye huyu anasoma kabrasha hilo.

Sikutegemea kama mna mbinu za kitoto hizi! akawaza na kujibwaga tena kitandani. Mara mlango ukagongwa hodi, akaruhusu mtu huyo kuingia maana alijua aina hiyo ya mbisho kuwa ni Jasmine. Katika TSA kila mmoja alikuwa na jinsi yake ya kugonga mlango au kengele ya mlango anapokwenda kwa mwingine, hivyo mwenyeji alijua ni nani agongaye. Endapo mbisho utakuwa tafauti basi

angechukua tahadahari kabla ya kwenda kufungua.

Jasmine alijitoma ndani na kufunga mlango nyuma yake, akamtazam Amata aliyejilaza kitani huku ile bahasha ikiwa mchagoni kiasi kwamba asingeweza kuiona.

“Unatafutwa!” akamwambia.

“Na nani?” Amata akauliza.

“Bibi yako,”

“Aaaah! Atulie kwanza, kuna jambo naliweka sawa kichwani likishajiseti, nitamtafuta, kwa sasa aniache, nimezima simu zote hapa, sitaki usumbufu na mtu. Au ushmwambia nilipo?” Amata akamwambia Jasmine.

“No! nimemwambia kuwa kwa leo hatujawasiliana kabisa…”

“…good! Nipe muda zaidi,” akamwambia, Jasmine akatoka na kuondoka zake.

* * *

Usiku huo huo, kama saa saba au nane hivi, The Cobra na mgeni wake walikuwa tayari Kurasini kwa mipango yao ya siku inayofuata. Moja kwa moja, jamaa huyo akaingia chumbani kwake na kuiende saraka yake ya siri kwa minajiri ya kuchukua ile bahasha na kumpa mgeni wake picha halisi ya kile wanachokipigania.

Baada ya kuingiza mkono ndani ya saraka hiyo hakukuta

bahasha zaidi ya maburungutu ya pesa.

“Shiiiit!” akang’aka na kutazama vizuri, hakuna bahasha.

Impossible, it was here! Akawaza kwa kiingereza, hakuamini kama ni kweli bahasha hiyo haipo, akatzama na kutoa mapesa yote akayamwaga chini, hakuna bahasha.

“Dannnyyyy!!!!” akaita. Na sekunde tu, Kremikov akawa pale.

“Vipi?” akauliza.

“Hakuna bahasha!”

“What?”

“Hakuna bahasha, na mimi niliiweka hapa, na siku zote hakuna anayejua hii saraka wala tarakimu fungushi zaidi ya mimi tu,” akajibu.

Daniel Kremikov akatulia kimya na kujishika kiuno huku akimtazama mwenyeji wake aliyeonekana wazi kuchanganyikiwa.

“Una uhakika ulivyoweka hapo hakuna aliyekuona?” Daniel akauliza.

“Hakuna, hata kama kungekuwa na gari inanifuata ningejua tu, lakini hakuna…”

“Sasa kama hakuna limeenda wapi? Kama si wewe umeliuza basi kuna mtu alikuwa nyuma yako akikufuata…” Daniel akaeleza na kumfanya The Cobra kuzidi kuchanganyikiwa, “nini kilikuwa ndani?” akaongeza

swali. The Cobra akaeleza kila kitu kilichokuwa ndani ya bahasha hiyo, Kremikov akatikisa kichwa.

"Yaani hata wewe mwenyewe bado hukujua nini kipo ndani, kwa maana hiyo kama wameiba basi ujue wazi kuwa hawawezi kujua nini kipo zaidi ya kusoma watakayoyaona kwa maandishi tu. Taarifa zilizosomeka na wewe na aliyeiba si Top Secret, zile ni

Confidencial tu, hazina madhara sana…”

“Kwa nini hazina madhara?” akauliza.

“Kaa chini nikwambie”.

The Cobra akaketi juu ya kitanda na Kremikov katika kiti ndani ya chumba hicho, “sikia, taarifa moja imeeksipaya kwa sababu mpango umefeli, haina maana tena. Taarifa ya pili, haijakamilika ipo kwenye mafumbo sana, ili uielewe wazi

lazima upate taarifa ya tatu nah ii ya tatu ndiyo Top Secret ambayo hata wewe huijui," akamwambia huku akiendele kuvuta sigara yake aliyoiwasha punde tu. Mara macho yake yakatazama maburungutu yale ya pesa pale chini, zaidi ya hizo akaona kitu kingine, "nini hicho?" akauliza na kumwonesha kwa kidole, picha. The Cobra akainama na kuiokota picha yake ambayo sasa imepigwa X na kubebwa na maandishi 'You are terminated',

mwili wote ukamfa ganzi, akampa picha ile Kremikov kisha yeye akatzama ukutana akagundua kuwa imetunguliwa humo humo.

"Tunatakiwa kumaiza hii kazi mapema zaidi ya mpango ulivyo… sasa nimeelewa. Hii nyumba imetembelewa baada tu ya wewe kutoka, na huyu mtu atakuwa alikufuatilia kwa muda mrefu. Kama hukugundua kuwa unafuatiliwa basi ujue kuwa mtu

huyu ni hatari sana, kama unasema hiyo kodi ya kufungulia ni wewe tu unaijua nay eye kafankiwa kufungua basi juwa huyu mtu ni zaidi ya mjuvi wa mambo," Kremikov akazungumza huku kijasho kikilowesha kichwa chake kwa mbali.

Kama alifikiri kuwa kaja kuua inzi, mara hii akaanza kuona akili ya ziada ya mtu anayemtaka.

Code 005, Intelligent and unstoppable human being! Akawaza na kujifuta jasho. Baada ya sekunde kadhaa za kufikiri, akajikuta akipiga ngumi juu ya meza ndogo ya kioo nayo ikatawanyika vipande vitatu.

“Lets go and find the bastard!” akamwambia The Cobra kuwa waondoke wakamsake mwanaharamu. Akaingia mkono ndani ya koti lake na kutoa bastola, akaiweka sawa na

kuhakikisha imejaa vyema, akatazama na kila anachohitaji kwa kazi yake, kipo sawa.

SEHEMU YA 21

10

ASUBUHI YA SIKU iliyofuata ilimkuta Madam S bize afisi ndogo, kabrasha kadhaa zilitapakaa mezani pake. Zile

ambazo zilizowezekana zikafanyiwa kazi, na zilizoshindikana zikawekwa kando, ikiwa na maana kuwa kuna ambao watakuja kuzifanyia kazi. Akiwa anaendelea na kazi hizo mlango wa ofisini kwake ukagongwa kwa mtindo ambao anaufahamu. Kutoka katika meza yake akaufungua kwa kubonyeza nobu fulani chini ya meza yake.

Kamanda Amata akaingia ndani ya afisi hiyo na

kujikaribisha kitini bila kungoja. Akiwa hapo akamwekea mezani katasi tatu, moja yenye picha yake na nyingine ya picha ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

"Za nini?" Madam akauliza.

"Soma…" Amata akamwambia. Madam akapekuwa zile karatasi na kusoma maelezo yote katika kurasa ya mwisho, alipomaliza, akaziweka kando na kumtazama Amata.

“You are dead!” akamwambia, wote wakaanza kucheka kwa sauti na kugonganisha viganja vya mikono yao.

“Mpango wao huu umefeli, kama waziri nimeshamwokoa na mimi ndimi mimi hapa, mzimaaaaaaa wa afya. Madam, sasa kazi inaanza na kazi hii si ndogo…”

“Kwanini unasema hivyo?”

“Jana najua ulinitafuta, nilizima simu makusudi kwa

sababu najua kama hawa jamaa wameshindwa kuniua kama walivyopanga, basi wananisaka, tena mara hii wana hasira kali kuliko mwanzo…”

“Kuliko mwanzo?” Madam akauliza.

“Ndiyo, kuliko mwanzo kwa sababu, jua kabisa kuwa kuna mtu yupo karibu sana na serikali anawapa information zote kuhusu kinachoendelea kati yetu na adui zetu…” Amata akamjibu.

“Umejuaje?”

“Hilo siyo swali kama unajua kuwa mimi ni mpelelezi… sikia Madam, wamenikosa, kifo change kikakutana na Gina, kifo cha Waziri wetu kimekutana na Mc Cain, kwa maana hiyo adui sasa ana hasira na mimi kuliko mama yake aliyemzaa,” akasisitiza. Madam S akatikisa kichwa kama mtu mwenye mdudu masikioni. Tangu Amata akutane na bosi wake siku

iliyotangulia, hakuweza kuzungumza naye mengi sana katika sakata la Windhoek, siku hii ndipo alipomwambia kuhusu mkasa mzima wa Parrot na Mc Cain.

“Nimewacheza shere! Wana hasira, wakinikamata watanitafuna na maganda, hakika nakwambia,” akamwambia bosi wake. Madam S akabaki kimya hakuwa na jibu lolote katika hilo.

“Najua kuwa upo mbele zaidi yangu katika hili, nijuze zaidi…” akamwambia Amata.

“Watu wetu wapo mikononi mwa Makaburu, akili yangu haiwezi kutulia mpaka nijue wapi hasa walipo…”

“Ukijua….”

“Nitaitangazia dunia udhalimu wa mtu mweupe, sitawaacha, nitawaaibisha mbele ya vyombo vya habari vya dunia, na nina

uhakika watajiona wajinga…” Amata akasema.

“Una uhakika wana watu wetu?” madam akauliza.

“Nina uhakika kwa asilimia hamsini na moja…”

“Na hizo arobaini na tisa, je?” Madam akauliza.

“Ndo nazifanyia kazi,” Amata akajibu.

“safi, ndo maana nakupenda we mwanaume, ningekuwa kijana

ningekuzalia mtoto ila nimeshazeeka na mayai yamekufa. Sasa sikia, tena nisikilize kwa makini, kuanzia sasa, nakupa kazi hii rasmi, uishughulikie kwa makini na tupate jibu la uhakika, kama utagundua kuwa kuna watu wetu kule nipe taarifa, tutapeleka hata kama ni makomandoo tukawaokoe…"

"Hilo ndilo haswaaa nilikuwa nalisubiri… asante sana,"

akasimama na kupiga saluti ya heshima. Madam S akavuta mtoto wameza na kutoa kabrasha linguine akampatia.

"Ndani ya kabrasha hili, kuna taarifa zote za kamati ya upatanishi tangu mwaka 1984 mpaka hii ya juzi," akamkabidhi. Amata akalipokea na kulishika vyema.

"Key point ni moja tu, nikiitegua tu tumemaliza kazi," akamwambia.

“Ipi hiyo?”

“Lazima nimpate au nipate Daseen Keputo,” akajibu.

“Dassen Keputo?”

“Yes!”

“Ok, fanyia kazi, kama kuna uhitaji wa msaada nimabie!” Madam S akamwambia na kuagana naye. Baada ya Amata kufunga mlango na kumwacha Madam S peke yake, mwanamama huyu akabaki akijisemea peka yake.

“Sijajua mpaka sasa kijana huyu ana matatizo gani? Hapendi mtoto au Gina hana uzazi?” akajiuliza lakini hakupata jibu.

* * *

“Jana hajarudi, ndo maana mpaka sasa hatujapata signal yoyote, camera ziko blank!” kermikov akamwambia The Cobra.

“Huyu jamaa baada ya kumuua mkewe nahisi amegundua mbinu

yetu…” The Cobra akamwambia mgeni wake.

“Mauaji ya kuvizia mi sijazoea, nataka nijue ni wapi anapatikana nimmalize,” Kermikov akamwambia Cobra.

“Unajua hata vijana wangu wote hawajamwona jana katika vijiwe vyake…”

“Kajificha,” Kermikov akamwambia swahiba wake.

“Sina uhakika, sasa hivi naanza kumfahamu mtu huyu taratibu,

ila nitamtia mkononi tu, mbinu pekee ya kufanya sasa, tuachane naye, twende tukastarehe, kwa vyovyote yeye anakusaka wewe, akikuona atakufuatilia na hapo ndipo tutamwonesha kazi," Daniel Kermikov akamwambia Cobra.

"Copy!" Cobra akajibu.

Kama kawaida ya Jiji la Dar es salaam, jioni huwezi kujua kuwa leo ni jumatatu au jumatano, starehe kwenye makazino na

mabaa hupamba moto. Na ni sehemu hizi ambazo Amata hupenda kutembelea nyakati kama hizi. Kwa sababu The Cobra alikuwa akijua nyendo zote za Kamanda haikuwa shida kujua ni wapi wanaweza kumtega zaidi ya nyumbani kwake.

"Popote hata kama ni kanisani tunamwanzishia msinambe, no time to waste!" Daniel akamwambia Cobra.

Wakati wao wakizungumza na kupanga hayo, Kamanda Amata alirudi katika maficho yake kwa siri, akaingia chumba kilekile na kuendelea kuwa chini ya uangalizi wa Dkt Jasmini kama mgonjwa mwenye shida maalumu.

“Vipi?” Jasmine akamuuliza pindi tu alivyopanda kitandani.

“Naumwa sana, naomba nipumzike!” Amata akamwambia.

“Nikikwambi mikupatie dawa unaringa, sasa nikusaidiaje?”

“Dawa yangu ni kulala tu kwa sasa, hivyo naomba nipe siku nyingine ya kulala nikiamka nitajua nianzie wapi,” akamwambia Jasmine.

“Sijakuelewa tangu jana, maana hii ni mbinu mpya nafikiri,” Jasmine akazidi kuchokonoa.

“Nikipona nitakwambia,” akamjibu na kuvuta shuka, akajifunika gubigubi.

Queen Elizabeth Memorial Hospital – Cape Town

Mc Cain aliruhusiwa kutoka hospitali baada ya kuonekan kuwa hali yake imetengemaa. Wataalam wa afya katika hospitali hiyo, walifanya kazi kubwa kuhakikisha wanasafisha sumu yote ndani ya mwili wa mtu huyo, wakafanikiwa.

Mzee huyu alitoka hospitali akiwa na nguvu zake kama zamani, na ndani ya kichwa chake alijenga vitu viwili tu; kumuua Parrot kwa sababu alisaliti na kutaka kummaliza kwa sumu, kumsaka mtu ambaye anajaribu kuitikisa ngome ya WP katika Kusini mwa Afrika.

Saa moja baadaye akawa tayari katika jumba lake kubwa la kifahari huko nje ya Cape Town, juu ya kilima ambacho ukitazama

chini hakuna unachokiona zaidi ya bahari tu. Zaidi ya bilauri yake mkononi, mzee huyu alikuwa akizungukazunguka huku na kule akipanga na kupangua mambo. Mara akashtuliwa na kijana wake aliyemtaka sebuleni kwa kuwa kulikuwa na wageni. Akaitazama saa yake akajua ni mgeni gani ambaye yupo muda huo. Aakavuta hatua na kuingia ndani ya kasri lake, kama alivyofikiri, Margaritha asbarai alikuwa amejaa katika sebule hiyo

kukutana na mzee huyu. Akampa ishara kuwa amfuate, naye akafanya hivyo.

Ndani ya chumba kidogo, waliketi watu wawili tu yaani Mc Cain na Margaritha, huu ulikuwa mkutano wa siri kati yao. Haikutakiwa mtu yeyote kujua nini kinaongelewa.

“Im so sorry Comrade!” Margaritha akaanza kwa kumpa paole kisha akampa taarifa ya kila

kitu kilichotukia siku ile ya mkutano.

“Kwa hiyo Parrot alitusaliti?” Mc Cain akauliza.

“Hapana, taarifa niliyoipata baada ya uchunguzi, si Parrot, bali kuna mtu alikuja kwa siri kutoka Tanzania, na huyu mtu ndye aliyemuua Jesca na kumvunja miguu Parrot, kisha akaharibu mipango yetu yote katika utekelezaji,” akaeleza.

Mc Cain akanyamaza kwa nukta kadhaa na kisha akainua kichwa kumtazama mwanamke huyo, “nini mmefanya baada ya hilo?” akauliza. Kwa swali hili, mwanamama huyu akamweleza kuhusu mkutano mzima wa wajumbe wa juu pamoja na Alfa kule Prague.

“Alfa amejua hili?” akauliza.

“Yes!”

Kisha akampa taarifa yote ya kikao cha Prague na maadhimio

yaliyoazimiwa, Mc Cain akakubaliana na mpango mzima ambao Alfa aliufikiria.

“Wakipata vikwazo vya kiuchumi, watatupatia watu wetu, na hii ndiyo dawa yao, kataifa kadogo kanataka kutusumbua? Margaritha, nahitaji kuona maiti ya huyu mtu na nitaichoma moto kwa kiberiti change,” akamwambia.

“Bila shaka, Daniel Kermikov, yupo Tanzania kwa kazi hiyo,” mwanamama huyo akasema.

“Kermikov?” akauliza.

“Yes, Kermikov!” Margaritha akajibu.

“Good, kazi imeisha, kama Kermikov yupo huko kazi imekwisha. Mimi nitaondoka hapa kesho kuelekea Prague kuonana na Alfa, nitakuachia utawala kwa siku kama nne hivi…” akamwambia.

“Sawa!”

Margaritha akamaliza kumpa mrejesho wote wa kikao hicho, na baada ya hapo wakaagana na mwanamama huyo kurudi Namibia kwa ndege ya kukodi.

* * *

Daniel Kermikov alijikuta anapoteza siku ya pili bila matumaini ya kuliona windo lake.

“Kila kona hayupo,” Cobra akamwambia Daniel.

“Twende afisini kwake, tutakayemkuta tunamteka, hapo lazima ajitokeze tu popote alipojificha,” Daniel akasema. Gari likawashwa kutoka Hotel ya Double Tree kuelekea Barabara ya Samora, katika afisi za Agi Investment.

Ndani ya afisi hizo, Gina alikuwa ametingwa na makabrasha mbalimbali, akchambua habari na kuziweka sawa, na kutazama yale ya msingi

zaidi kwa kazi zao hususani zile alizoachiwa na bosi wake ambaye mpaka dakika hiyo hata hakujua ni wapi alipo. Akiwa katika kujisahau na kazi hiyo, akashtushwa na kengele ya mlango.

SEHEMU YA 22

Ugongaji huo wa kengele ukamfanya Gina kuwa makini kwa sababu alikuwa akijua aina zote za ugongaji wa wenzi wake. Akajiweka tayari, na kuuelekea

mlango, akazungusha kitasa na kuufungua kidogo, macho yake yakagongana na ya Wazungu wawili asiowajua. Kabla yeye hajafungua vizuri, tayari Daniel Kermikov aliusukuma mlango ule kwa guu lake la kulia wakati huo tayari The Cobra alikwishakamata bastola yake barabara mikononi. Gina akasukumwa nyuma na ule mlango hata hivyo akauepa ukabamiza ukuta. Kermikov akaingia ndani na kufuatiwa na

Cobra, mlango ukafungwa nyuma yake. Gina hakukubali mambo yaende kipumbavu, hakupenda kushikwa na Mzungu huyo aiyejichorachora tatuu za kutisha mwilini mwake. Kermikov akamdharau mwanamke huyo kwa kuwa alijua ni skretari tu hana lolote, akamfuata kumkamata kizembe, lakini kabla hajamfikia akajikuta akipewa pigo moja tata, kwa maana aliliona akaepa upande wa kushoto kumbe mwanamke huyo

alimcheza shere, pigo lile likatua sawasawa mbavuni mwa Mrusia huyo, akaguna.

Wakati Gina anajiandaa kupeleka pigo linguine, akakamatwa mkono na jamaa huyo akaunyonga vibaya lakini Gina akawa mjanja, akaruka hewani na kujizungusha huku mguu wake mmoja ukimtandika The Cobra mikononi na kumpoka bastola yake kabla haijaleta madhara. Konde moja

zito kutoka kwa Kermikov likatua tumboni kwa Gina, kabla hajakaa sawa akajikuta akipokea teke moja kali lililomsukuma mpaka kwenye mlango wa kioo unaotenganisha afisi ya Gina na Amata. Gina alitua kimgongomgongo na kuuvunja mlango huo, akaangukia ndani ya afisi ya bosi wake. Ilikuwa ni vurugu mechi ndani ndani ya afisi hiyo, lakini watu wan je hakuna aliyejua nini kinaendelea. Kermikov akajitoma mzima

mzima ndani ya afisi ile na kumuwahi Gina kabla hajainuka na kumtandika teke linguine lililompeleka mpaka kwenye meza ya bosi wake. Gina akatambaa akivujwa damu mpaka uvungu wa hiyo meza na kuwahi kubofya kitufe cha siri ambacho humpa ishara Amata kuwa kuna hatari.

"Shiiiiit!" Cobra akang'aka kwa kitendo kile cha Gina, akaokota

bastola yake na kuiweka tayari kufyatua.

“Noooooo! Do not shoot her!” Kermikov akamzuia, “simhitaji huyu mwanamke, ila kwa kumchukua huyu nitampata ninayemtaka, son of bitch!” akaongeza kusema. Huku akimwendea Gina pale chini.

“Bosi wako yuko wapi?” Kermikov akamuuliza.

“Si -si –si -na boss!!!” akajibu kwa kwikwi huku damu zimchurizika usoni.

“Nitaondoka na wewe na ukileta ujinga wako nakuua,” Kermikov akamwambia Gina kwa kiingereza.

“Kabla hujani-u-a utakuwa ta-yari umekufa!” Gina akamjibu kwa tabu kidogo. Daniel Kermikov akamtazama The Cobra, akamwona kama hayuko sawa hivi.

“Vipi?” akamuuliza.

“Huyu ndiye mwanamke ambaye tulimuua nyumbani kule nilikokwambia!” akajibu.

“Hukumuua ndiyo maana hata sasa yupo hai, Cobra, uwe na uhakika na unachokifanya, naona siku hizi unaanza kuzeek au umeweka starehe mbele, inakuwaje unashindwa kutofautisha kati ya marehemu na aliye hai?” Kermikov akamuuliza.

“Come on!” The Cobra akajikuta akiwakwa na hasira juu ya Gina. Wakamwinua na kumfuta damu usoni.

“Unaondoka na sisi, hatutakuacha mpaka utukutanishe na bosi wako,” Cobra akasema kisha wakatoka mle afisini taratibu, mbele alitangulia The Cobra, katikati Gina na nyuma Kermikov ambaye alishika koti la suti la Gina ambalo alilitumia kufunikia

bastola ambayo tayari ilikuwa na risasi chemba na ingefanya kazi endapo tu mwanamke huyo angeleta makeke. Gina hakuleta shida, aliongozwa, akaongozeka mpaka kwenye gari ya hao jamaa wakamwingiza ndani na kuondoka kwa kasi.

* * *

Kamanda Amata akagutuka ghafla kitandani baada ya saa yake kubwa ya mkononi kumfinya kwa nguvu sana.

Mfinyo ule alijua ni nini maana yake, akainuka na kuketi kitandani.

“Gina! Gina!” akajikuta akizungumza peke yake, akachukua viatu haraka na kuvivaa, akakusanya simu zake na kuinuka. Alipofika tu mlangoni akakutana na Jasmini naye anaingia ndani ya chumba hicho.

“Vipi Kamanda?” Jasmine akauliza.

“AGI Investment imeshika moto…”

“Moto?” Jasmine akauliza.

“Ndiyo, imeshika moto, hakuna kusubiri,” akamwambia Jasmin huku akiwa tayari keshampita anakimbilia katika gari yake, akaingia na kupiga stata, alipotaka kuliondoa tu akagundu mlango wa nyuma uko wazi, akageuka na kumkuta Jasmine akmalizia kufunga. Hakuuliza akaondoka kwa

mwendo wa hatari na kukamata barabara kubwa kuelekea mjini.

“Sijakuelewa Amata!” Jasmine akamwambia.

“Gina yupo kwenye hatari sasa,” akamjibu huku akikata kona moja mbaya ambayo ilisababisha kelele kwenye gurudumu za nyuma, ikakaa sawa na kuendelea na kasi ileile.

“Jasmine, sikukwambia, kuna ishu moja nzito sana mbele yetu kwa sasa mimi nimeanza nayo ila

najua muda si mrefu mtaingizwa kazini kama ilivyo ada!”

“Ishu gani Kamanda?”

“Atakwambia bosi wako wakati wako ukifika, ndiyo maana unaona nakuja kujificha pale kliniki kwako, nawindwa, na ninajua kuwa nawindwa. Tatizo ni kwamba, ningekuwa namju anayeniwinda nisingeteseka na kujificha, sasa simjui, na nafahamu kuwa kafanya hivi makusudi akitaka kuwa

nijitokeze…. Sasa namwambia hata kama hanisikii, nimejitokeza na nitahakikisha namvunja shingo. Kumteka au kumtesa mmoja wa TSA nikiwa hai ni kunichezea pumb* zangu,” Amata akaongea kwa hasira huku nakiingiza gari maegeshoni na kuteremka. Hakutaka hata kutembea, mwendo wake ulikuwa ni mwa kukimbia tu huku akifuatiwa na Jasmine nyumaye.

Sekunde kadhaa baadae, tayari wakajikuta mbele ya mlango wa afisi yake, “Jas, chunga mkia wangu,” akamwambia Jasmin huku yeye akikamata kitasa kufungua mlango. Alimwambia maneno hayo kwa kuwa hakujau kama adui yake katoka au bado yuko ndani ya afisi hiyo. Dkt Jasmini akachomoa bastola na kuikama sawia kwa mikono yake miwili huku tayari akiwa keshaondoa usalama. Kamanda Amata akafungua mlango na

kuusukuma kwa nguvu kisha akasubiri sekunde kadhaa, kimya.

“Hakuna mtu!” Amata akasema, Jasmin akashusha bastola yake kisha wote wawili wakingia ndani kama mita moja tu na kusimama kuangalia jinsi vitu vilivyoanguka anguka huku na kule, mlango wake wa kioo ulivyovunjwa vibaya. Amata akamtazama Jasmin, na daktarin huyu akaona wazi hasira za Kamanda katika paji la uso na

macho yake. Akainua simu yake na kupiga kitengo cha usalama cha jengo hilo na dakika tatu tu wakawazili watu wa usalama wanaoongzwa na kampuni binafsi ya ulinzi. Kamanda Amata akachukua nafasi hiyo kuwaonesha uharibifu wote uliofanyika nao wakaushuhudia kwa macho yao.

"Je kuna chochote ambacho umegundua kimeibwa?" Yule jamaa wa usalama akauliza.

“Ndiyo!”

“Ni nini na thamani yake ni sh ngapi kwa kukisia?”

Amata alilisikia swali hili, lakini likamkera tangu moyoni, hakujisikia kujibu ila ikabidi ajibu.

“Nitakwambia, ila nahisi kipo kilichoibwa!” akamwambia kisha akaingia ndani kabisa na kuketi juu ya kiti chake, mbele ya kompyuta yake kubwa. Wale jamaa wa usalama wakaangalia na

kupiga picha uharibifu wote kisha wakaondoka zao.

“Vipi?” Jasmin akauliza.

“Lazima nimpate Gina usiku haraka iwezekanavyo, ama zao ama zangu!” akamjibu Jasmini kisha akawasha kompyuta yake na kuingiza nywila akawasha window ya siri ambayo ni yeye tu anayeijua jisni ya kuifikia. Window hii ya kompyuta ilikuwa imeunganishwa na kamera maalum za siri sana ndani ya ofisi

hii, hata Gina mwenyewe hajui kama kuna hizo kamera siku zote. Ni siri ya Amata tu, peke yake. Kutoka katika kompyuta hiyo, akaona tukio zaima, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, hakumwambia Jasmin nini anachoangalia, ila alifanya screen shot za sura za watu hao wawili na kuruhusu printa yake iweze kuzitengeneza picha hizo katika karatasi.

Alipotaka tu kunyanyuka, Madam S aliingia bila hodi katika ofisi hiyo akifuatiwa na Inspekta Simbeye pamoja na vijana wawili wenye bunduki nzito lakini wamevalia kiraia kabisa na vichwa cyao vikwa na upara unaong'aa kwa mafuta ya nazi.

"Pole Amata!" Madam akamsalimu.

"Asante, majambazi yamevamia afisi Inspekta…"

“Walinzi hawakuwagundua?” Simbeye akamuuliza.

“Mzee Simbeye, hawa ni majambazi wa kimataifa, wameingia na wametoka bila kugundulika na mtu yoyote,” akamjibu. Inspekta Simbeye akatazama tazama jinsi uharibifu ule ulivyofanyika kisha akateta na Madam S falagha na baada ya dakika kama mbili hivi, Simbeye akaondokana na vijana wake na

kumwacha Madam S na vijana wake.

“Gina ametekwa!” Amata akamwambia Madam S.

“So…?”

“Kufa na kupona lazima apatikane tu, Madam, Chiba anatia timu lini? Hii kazi inamhitaji mpaka ilipofikia…”

“Hivi tunavyoongea nafikiri yupo JNIA!” Amadam akamjibu.

“Yessss!!!!”

“Unamtaka?”

“Yaani akiwepo Chiba, kwa hapa tulipo, kazi hii imeisha kabisa, ila leo nakwambia HOT, Dar itatikisika kwa mizinga ya kijeshi, siwapi nafasi ya kupumua,” Amata akazungumza kwa hasira. Simu ya Madam S ikapata uhai katika dakika hiyoyo, akaichomoa katika suti yake na kuitazma kiooni, akatabasamu.

“Yes my son!” akaitikia namna hiyo.

"Mom, I am in…" sauti ya pili ikajibu.

"Unakaribishwa sana, fika AGI mara moja, kaka yako ana shida na wewe," Madam akampa ujumbe.

"Copy!"

Madam S akakata simu na kuirudisha mahala pake, akamtazama Amata, kisha akatabasamu kwa mara nyingine.

"Tulia hapa, anakuja, usisahau kutoa taarifa… namchukua

Jasmine, kwa heri," Madam S akaagana na Amata na kutoka ndani ya afisi ile akifuatwa na Jasmine, wakamwacha Kamanda Amata peke yake.

* * *

Ni mchana huo huo, nukushi ya Ikulu ilipata uhai nakuingiza ujumbe mrefu uliosainiwa na viongozi wakubwa duniani. Katibu wa Ikulu, akainyakua ile karatasi na kuiweka vizuri kisha

akaifikisha panapohusika yaani kwa Mkuu wa Nchi.

“Imeingia sasa hivi Mheshimiwa….” Akamwambia.

Rais akaipokea na kuisoma, ilikuwa ni waraka mrefuy kutoka Jumuia ya Ulaya ulioandikwa kwa msisitizo wa hali ya juu sana, uliomfanya Mkuu wan chi huyu kuchanganyikiwa, akautupia kando ya meza yake na kushusha pumzi ndefu na kujiegemeza

kitini huku uso wake ukibaki umesawajika.

SEHEMU YA 23

Dakika chache baadae, akawasiliana na makamu wake, naye hakuchukua muda akafika afisini hapo kusikiliza mwito huo. Mara baada ya kusalimiana na mkuu wake, akasogezewa ile karatasi ambayo ilifika kwa nukushi saa kama moja iliyopita. Naye akachukua muda kuisoma na kuirudia, akatazama chini ya

ujumbe huo na kukuta saini ya mtu mzito duniani ikisainiwa kwa niaa ya watu wa G8.

"Wanasitisha misaada?" Makamu wa Rais akauliza.

"Siyo misaada tu, wanaweka na vikwazo wa kiuchumia kabisa, ina maana hatutaweza kuuza wala kununua kutoka kwao kuanzia sasa," akajibiwa.

"Kisa!"

"Kama ulivyokisoma katika barua hiyo… kwa kifupi Umoja

wan chi za Ulaya unatushinikiza kuwaachia huru makaburu tunaowashikilia kwenye magereza yetu, kwa kuwa wameona kuwa njia ya kidiplomasia hatuitaki, wameamua kutumia mabavu," akamfafanulia Makamu wake. Yule Makamu wa Rais akabaki kimya kabisa akitafakuri kitu, hakujua nini hasa cha kufanya ili kujikwamua na kongwa hilo la mtu mweupe. Baada ya dakika kadhaa za ukimya akajikohoza kwa kusafisha koo na kumgutua

mkuu wake kutoka katika lindi la mawazo.

“Hivi hatuwezi kuendesha nchi bila misaada yao? Maana daima hawa watu wakitaka kukushinikiza utimize matakwa yao lazima wafanye hivi,” Yule makamu akauliza.

“Unajua mifumo ya utwala katika nchi zetu haikujengwa imara katika kufikiri na kuamua nini clha kufanya kama sisi. Kwa ujumla tulitawaliwa kimwili,

tukaleta ujeuri kuwatimu lakini wenzetu wakawa wajanaja sana wakatutawala kiakili na kutugawanya," Rais akazungumza.

Makamu wake akabaki kimya akimsikiliza na kutafakuri maneno hayo mespesi kinywani lakini yenye nguvu ya kupindua dunia.

"Tunafanyaje? Na wao si wana watu wetu, kwa nini tusifanye kubadilishana wafungwa kwa

kuwa sheria za kimataifa zinaruhusu hilo," Yule amakamu akazidi kutaka kujua maamuzi hasa ya mkuu wake.

"Yote unayosema tumejaribu kuzungumza kwenye vikao vya upatanishi lakini havikukubaliwa nao. Wao wanasema sisi ndiyo tuna watu wao na wanajua ni wapi walipo lakini wanakana kabisa kuwa sisi tuna watu wetu mikononi mwao," akamjuza. Ukimya ukajidai tena kati yao,

wawili hawa wakajikuta hawana maamuzi ya kufanya juu ya taifa lao.

“Nafikiri kuitisha kikao cha dharula juu ya kujadili hili….”

“Hapana mkuu, hebu tulijadili sisi kama sisi kwanza na kuona jambo la kufanya kisha tuite wengine,” akashauri.

“Ni kweli usemacho, lakini nilitaka kuuliza kwao maswali kadhaa yenye utata, nikipata majibu yake ndo nitajua tufanye

nini," Rais akazungumza kwa uchungu.

"Umasikini wetu umekuwa fimbo ya kutuchapia!"

"Bila shaka!" akamjibu makamu wake kwa kifupi, "nataka nijue na niwe na uhakika kama tuna watu wetu kule, isiwe kuwa tunang'ang'ania kumbe ni kweli hatuna," akaongeza kusema.

"Sawa, nimekuelewa vyema kabisa, kwa hilo ni kweli kabla

hatujaamua inabidi tuwe na uhakika na tunachokitetea. Hawa jamaa wametupa saa ishirini na nne tu za kukubali au kukataa…”

“Sijui lini Afrika tutajitawala!” akamaliza kusema na kuvuta simu yake ya mezani, akabofya namba fulani na kuitega sikioni.

11

Alasiri ya siku hiyo hiyo, Chiba aliwasili ofisini kwa Amata kama alivyotakiwa kufanya. Baada ya

kusalimiana na kutazama uharibifu huo akarudisha macho kwa TSA1. Kamanda Amata akamruhusu kuketi.

“Sasa leo dada ako wa kukutengenezea kahawa hayupo, umefika na yakupasa kuanza kazi mara moja!” Amata akamwambia.

Chiba akabaki kimya kwa jozi la sekunde akitazama huku na kule. Ndani ofisi hii ndogo dakika na sekunde hii kulikuwa

na watu hatari sana katika maswala ya kijasusi ndani ya idara nyeti ya Tanzania Secret Agency, na wawili hawa ambao kila mmoja kabobe katika Nyanja yake walipenda sana kukutana kikazi hasa inapobidi kutegua vitendawili vigumu kama hicho. Chiba, mtaalamu wa Tehama, daima hakukubali kushindwa katika kutatua vifungo vya siri kabisa vya kimtandao na muda wote alikuwa akifanya ujasusi wake kwa njia ya mtandao.

Baadhi ya mashirika makubwa ya kijasusi duniani yalimtambua kijana huyu kama Cyber Spy na mara kadhaa walimtumia katika kazi zao zenye utata mkubwa. Siku hii alikuwa akitoka New Delhi, India kufuatilia mauaji ya vijana wa Kitanzania yaliyotekelezwa ka siri sana ndani ya jiji hilo.

“Pole braza, kama unavyojau sisi daima tupo kazini! Nipe mpya tusipoteze muda,”

akamwambia Amata. Kamanda hakujibu kitu zaidi ya kumpa zile picha mbili tatu alizofanya kwa screen shot kwenye kompyuta kwa msaada wa kamera zake za siri. Katika picha hizo kulikuwa na watu wawili, Wazungu wakiwa katika mionekano tafauti, ijapokuwa mmoja alikuwa akimfahamu kwani alimwona siku moja tu ilopita, alitaka kujiridhisha zaidi kumjuua nasaba zake na kila kitu. Chiba akatazama zile picha kwa

umakini sana, tena kwa macho makali ya kikachero yanayojua kutazama kitu, kisha akachukua kitu kama simu, ambacho mtu kama wewe hata ungepewa usingejua kazi yake zaidi ya kujipiga *selfie* kwa kuwa kila kitu ilikuwa ni simu. Akakiwasha na kilipokuwa tayari kimewaka, akaondoa ile *widget* ya simu na kufungua kurasa hasa ya kazi ya kidubwasha hicho. Akawassha scanner na kuziskani picha hizo na zote zikawa katika kifaa hicho,

kisha akaziingiza katika mfumo wa utambuzi ambao umeunganisha na taarifa za nchi mbalimbali za kiutambuzi. Juu ya *screen* ya kifaa hicho zikapita picha nyingi kwa kuzunguka kutoka juu kuja chini huku zikijiandika kwa tarakimu zilizokuwa zikibadilisha na kwa kasi hiyo hiyo.

Dakika kama tatu hivi, kikasimama, na juu ya kioo kulionesha picha inayoshahabiana kabisa na ya

yule jamaa wa kwenye picha za Amata. Chini ya picha hiyo kulikuwa na maandishi yanayosomeka 'WANTED', na huku pembeni kulikuwa na maelezo kadhaa ya nasaba na wajihi wa mzungu huyo.

"Jina halisi ni Stephen Antonov, amewahi kuwa mwanajeshi katika jeshi la Chechinya wakati ikiwa bado katika Umoja wa Kisovieti na ndiye aliyeongoza vita baridi kati

ya Moscow na jimbo la Cosovo mwaka ule wa mgogoro. Amewahi kuendesha operesheni za kijeshi kama jasusi wa jeshi yani MI wa Urusi katika nchi kama Uingereza na Marekani, kutokana na umahiri wa kazi yake akajiunga na KGB kabla ya kusambarayika kwake. Kwa sasa code zake hazisomi isipokuwa kuna maelezo hapa chini kuwa ni mtu hatari na akamatwe popote duniani atakapoonekana…”

“Wameelezwa uhatari wake nini?” Kamanda akamkatisha Chiba kwa swali.

“Wamesema tu kuwa ni *Professional Killer*, anayekodiwa na makundi mbalimbali ya kiharifu na mitandao mikubwa duniani inayotaka kutekeleza vifo vyenye utata,” Chiba akajibu na kumeza mate, “anatafutwa na FBI na Interpool Police, na daima ukiona kuna watu hawa wanakutafuta ujue basin a CIA

hawako mbali," akaongeza kusema.

"Good, sasa atakutana na TSA, kama wao wamemshindwa huko hapa hachomoki," Kamanda Amata akasema. Baada ya mazungumzo na kuliweka sawa swala hilo, yeye pamoja na Chiba wakatoka ofsisini na kuondoka zao mpaka kwa HOT, ambaye alikuwa ofisini akisubiri taarifa yoyote kutoka kwa Amata.

Ofisi Ndogo

“Tuna mtu hatari sana ndani ya nchi yetu!” Kamanda Amata akamweleza Madam S huku akimwekea picha na maelezo ya mtu huyo mezani. Madam S akazichukua na kuangalia vizuri kisha akasoma yale maelezo na kujiridhisha, akamtazama Amata usoni kisha Chiba, halafu akarudisha macho kwenye zile karatasi, akatikisa kichwa na kuziweka kando.

“Mwambieni tunamkaribisha! Taarifa hapa zinasema atakapoonekana popote duniani, wataarifiwe FBI au Interpool…”

“Hataarifiwi mtu, hapa ni kukimbiza mwizi kimyakimya, huyu jamaa kamteka Gina, hivi tunavyozidi kuzungumza huwezi kujua amefika naye wapi…”

“Ni kweli usemacho,” Mada akahafiki na kukivuta kiti chake mpaka katika meza ndogo yenye kompyuta na simu yake kazi

ambayo imeunganishwa hapo hapo, akainyakuwa na kuweka sikioni, akabofya namba fulani na kuzungumza na watu wapande wa pili.

"Kuna picha naituma sasa hivi, naomba watu wetu wote wawe macho, kumbe huyu hasitoke nje ya mpaka wa nchi kwa njia yoyote ile, iwe anga, maji au barabara…"

"Copy that! Work in progress…"

“Ok, waiting for process,” akajibu na kukata simu. Baada ya simu hiyo, dakika kumi zilikuwa nyingi, mipaka yote ya nchi ika[ata taarifa hiyo na picha ikawekwa kwa siri kabisa, wataalam wa kukariri picha za watu wakatawanywa na kufanya kazi sambasamaba na wafanyakazi wa kawadia katika sehemu hizo, wengine wakaungana na polisi wa mipakani, wengine wakaingia idara ya uhamiaji, wengine

wakaingia kwenye wakaguzi wa mizigo kwenye viwanja vya ndege na kadhalika lakini wote hawa walikuwa vijana wa TISS au tuwaite Smart Guys, vijana wasiotaka mchezo hata kidogo katika kazi.

“Ok, sasa sina budi kukuruhusu uingie kazini, Chiba atakusaidia, naomba msimhusidhe Jasmini isipokuwa tu kama mtahitaji msaada wa tiba na mnipe taarifa kwanza,

nimemaliza. Aaaannhh hakikisheni mchakato unakwenda kimya kimya na huyu bedui namhitaji akiwa hai, namhitaji shamba ila ninyi mnajua jinsi ya kumleta, ila kama akileta ubishi basi hamna budi kufanya linalowezekana, nimemaliza. Mi nimeitwa Ikulu kuna kikao cha dharula kama kinatuhusu nitawaambia," akawapa kazi vijana wake na kuwatakia heri. Akawatazama wakiondoka mpaka wakapaotelea mlangoni.

Wamekutana, sasa sipati picha hili jiji litakavyokuwa kwenye mbilinge usiku huu! Akawaza na kucheka peke yake moyoni.

* * *

Mara baada ya kuchukuliwa ofisini pale Gina alifikishwa katika maficho ya siri ambayo hakuweza kutambua ni wapi baada ya kuzungushwa zungushwa huku akiwa kafungwa kitambaa cheusi ndani ya gari hiyo. Baada ya kumshusha katika

maficho hayo ambayo yalikuwa kamaghala au tuite stoo, The Cobra akampa kipigo ksicho cha kawaida na kumwacha hoi kabisa. Gina hakuwa na uwezo wa kujitetea kutokana na kuwa alifungwa mikono na miguu hivyo alipokea kipigo hicho na kubaki akiwa hoi, uzuri na urembo wote vilikwisha.

“Yaani wewe wa kunidanganya mimi kuwa umekufa, mshenzi

wewe, sasa nakuua kweli," Cobra akaunguruma kwa hasira.

Gina hakujibu kitu, akamtemea mate yakampata usoni, kitendo hicho kikamfanya kijana huyu awe mbogo. Akarusha teke pale chini, Gina aliliona akatumia uwezo alio nao na kulizuia kwa mikono yake iliyofungwa, akausukuma ule mguu kwa nguvu, jamaa akakosa stamina. Giana akatumia nafasi hiyo na kujizungusha kwa nguvu

na kwa miguu yake miwili akmtia ngwala maridadi kabisa, The Cobra akatua sakafuni kama mzigo, puuuuuh! Vumbi kutoka kwenye sakafu chafu likatimka. Dakika hiyo hiyo, mlango ukafunguliwa na Kermikov akaingia kwa kasi, na kumrukia Gina guu la uso, akaanguka na kupiga kisogo chini, akalala kimya.

“Bastard!” Kermikov akatamka kisha akamwangalia

The Cobra, “sikukwambia umpige, nimekwambia utumie njia ya nguvu, akwambie ni wapi bosi wake tutamwona, basi…” akamwambia huku akitoka ndani ya jengo lile na kufuatiwa na huyo jamaa yake.

“Kazi iliyonileta ni kumtia mkononi huyu mwanaharamu na kumvunja shingo, Alfa anaihitaji roho yake,” Kermikov akamwambia Cobra.

“Haina shaka, vijana wametawanyika na nina uhakika leo lazima atajitokeza hawezi kumwacha huyu mwanamke wake jeuri ateseke, lazima atajitokeza…”

“Vijana wakimwona tu wasifanye lolote, walete taarifa, nitakwenda mwenye katika hilo eneo na nitammalizia hapo hapo,” akasema. Kermikov alimwambi swahiba wake kwa maana yeye alijua anasakwa kila

kona ya dunia hivyo hakutaka kabisa kujitokeza ovyo hadharani, yeye alitaka kujitokeza tu na kufanya tukio basi. Na sehemu zote alizotekeelza mauaji alionekana si zaidi ya sekunde kumi hadharani, na katika sekunde hizo tayari aliondoa uhai wa mtu.

SEHEMU YA 24

* * *

Katikati ya Jiji la Dar es salaam

Kamanda Amata aliegesha gari nje ya uwanja wa makaburi Mikocheni, akafungua mlango na kushuka huku akifuatiwa na Chiba upande wa pili.

“Vipi kaka makaburini usiku huu?” Chiba aliuliza.

“Kuna kaburi moja hapa nataka ulione, nafikiri ni msaada sana kwa kazi yetu hii,” Amata akajbu huku tayari amekwishaingia ndani uwanja huo.

“Hapa!” Amata akamwonesha Chiba.

“Mbona hunipi maelezo ya kutosha juu ya hili?” Chiba akamuuliza Amata.

“Soma huo msalaba!”

“Dassen Keputo,” akasoma.

“Good, lets go now and find Gina,” Amata akamwambia Chiba wakatoka na kuliendea gari lao, wakaingia na kuketi.

“Kamanda sikuelewi!”

“Huwezi kunielewa kaka, ila utaelewa baadae….” Akamjibu huku akiitekenya injini na kuondoka zake kuelekea katikati ya jiji.

“Hujapumzika Chiba, nikupeleke nyumbani? Na nimpigie shemenga aje akukandekande,” Amata akamtania huku safari ya kuingi katikati ya jiji ikiendelea.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Ukweli nimechoka lakini nahitaji

kukusaidia kazi ya usiku huu," Chiba akajibu.

"Hii, hii wewe niachie, ila nitakupa nyingine ambayo nataka unisaidia na kesho asubuhi unipatie majibu yaliyojitosheleza," akamwambia.

"Sawa braza, nipeleke home, ila kwa lolote nipigie nije nikupe tafu…"

"Usijali we nicheki kwenye locator," Amata akamwambia swahiba wake Chiba na

kumshusha posta mpya huku akimkabidhi bahasha moja ya kaki. Baada ya kuachana wawili hao, Kamanda Amata akaondoka kwa gari hiyo mpaka mgahawa wa Salamander kujipatia japo sharubati. Alipoegesha gari lake nje ya mgahawa huo, gari jingine aina ya Toyota Harrier jeusi lilipita na kuegeshwa kama sehemu ya tatu hivi kutoka pale. Kamanda Amata machale yakamcheza, hisia zake zikamwambia hatari imemkaribia,

hakujali, akafunga mlango wa gari hilo na kuzikwea ngazi kuingia ndani mgahawa. Kiti alichokaa aihakikisha analiona lile gari vizuri kabisa na kujua kila kinachoendelea.

Mpaka dakika hiyo, hakuna mtu aliyeshuka katika gari hilo. Amata akaagaiza sharubati ya embe na kuendelea kunywa taratibu huku jicho lake likiwa kwenye gari lile. Baada ya dakika kama kumi hivi, akamaliza haraka

ile sharubati na kuondka ghafla kwenye ile meza, na kupotelea upande wa pili.

Huko alikoibukia akaingia kwenye BMW jeusi ambalo daima huegeshwa hapo, kwa kitendo hicho tayari alijua amekwishawapoteza watu hao.

Ndani ya lile gari, yaani Harrier, kulikuwa na vijana watatu, wawili Wazungu na mmoja chotara. Vijana hawa walipewa kazi ya kumsaka

Kamanda Amata popote alipo ndani ya jiji hilo. Baada ya bosi wao kumteka Gina ndipo wakaliona windo lao pale Posta mpya wakati akaimshusha Chiba. Kabla hawajatoa taarifa kwa mkubwa wao kama walivyoagizwa, wakaamua kumfuatilia kwanza kujua ni wapi hasa anaelekea. Ndipo wakafika hapo Mgahawa wa Salamander.

“Anaelekea wapi kule?” mmja wao aliyekuwa nyuma ya usukani akauliza.

“Sijui, labda chooni!”

“Mfuatilie, haraka asije kutupotea, mi nachunga kama atarudi garini kwake,” akawapa maagizo na wale vijana wawili wakateremka haraka na kugawana njia, mmoja akapita upande huu kwa kuuzunguka ule mgahawa na mwingine akapita upande alipoegesha gari na

kuzikwea ngazi zilezile kuingia ndani ili kutokea upande wa pili. Ndani ya gari kuibakia yule dereva akfuatilia mtafutano huo kwa ukaribu. Hawa vijana kiukweli walikuwa hawajui wanacheza na mtu wa namna gani. Yule dereva ndani ya gari akainua simu na kutoa taarifa kuwa ni wapi Amata ameonekana na yupo, hivyo akawaomba akina Kermikov kufika haraka sana eneo la tukio.

Kamanda Amata alitulia kimya ndani ya gari akiwaangalia vijana wale kila mmoja upande wake, akatazama yupi anakaribia eneo hilo na akapanga kabisa aina ya shambulizi tuli atakalompa kiasi kwamba mwenzake hatotambua kuwa kuna hatari eneo lile.

Lazima nifanye kama kinyonga anavyokamata mdudu! Akawaza. Upande ule lilikokuwa gari lile alimoketi Amata kulikuwa na maua marefu hivyo kufanya

vivuli hapa na pale. Mmoja wa wale vijana alikaribia kabisa gari alimo Amata, akapita mbele ya gari lile, akasimama kidogo, na kisha akachukua simu yake na kupiga namba fulani.

"Simuoni upande huu…. Vipi huko?" Amata akasikia kwa mbali nini kijana huyo anasema, akajiandaa na kumlia timing, kijana yule akatakiwa kurudi mara moja upande alikotoka, ni kukta hiyo akapita karibu na mlango

aliyoketi Kamanda. Ghafla akaufungua mlango na kumbamiza nao eneo la tumboni, Yule kijana akasukumwa nyuma na wakati huo tayari Amata alikuwa nje, akamuwahi kijana huyo kabla hajafanya makeke, akampa konde moja zito likatua kwenye mwamba wa pua na damu zikaanza kumvuja. Kabla hajafanya chochote akamkamata na kumsindika bichwa lenye kilo nyingi yule kijana akaishiwa

nguvu, Amata akavuta ndani ya gari na kujifungia naye akiwa hoi.

“Nani amekutuma kwangu?” akmuuliza huku wakiwa wamemlaza kiti cha nyuma na goti lake kumkandamiza mbavuni.

“Usitake kujua!” yule jamaa akajibu kwa dharau, hakika alikuwa hajui ni nani anayemjibu. Kamanda Amata akashusha pigo moja zito ubavuni na kuvunja mbavu moja.

“You want to kill me mother fucker!” Yule jamaa akapiga kelele ambazo hazikufika popote, kama mtu angepita nje labda angeona tu mtikisiko wa gari na asingejuaka kuna mtu anapata kichapo badala yake angejua ni ile michezo ya vijana ya jig jigg.

“Kufa tu! Mmempeleka wapi mke wangu?” Amata akamuuliza kabla hajajibu akamshushia pigo jingine na kutengua ubavu mwingine, kabla hajamweka sawa

akamtandika pigo jingine zito na kumzimisha, kimya.

“Shenzi kabisa sitaki ujinga saa mbaya hii!!!” Amata akaongea na kufungua mlango akimwacha kijana yule nusu mfu na hana fahamu.

Katika gari ya wale jamaa, kijana mmoja Yule chotara alirudi na kuketi kitini.

“Mwenzio yuko wapi?” akamuuliza.

“Anakuja!” akamjibu huku wakisubiri, dakika zikapita, jamaa hajarudi. Kidogo simu ya dereva yule ikaita, akainyakua na kuiweka sikioni.

“Bado mnamchunga huyo bwege?” sauti ya upande wa pili ikauliza.

“Ndiyo! Bado tupo hapa Salamander,” akajibu.

“Ok nipo njiani,” akajibiwa.

Yule dereva akamtazama kijana wake kwa mara nyingine, “we mwenzio vipi? Mpigie

simu!” akamsisitizia. Yule jamaa chotara akainua simu yake na kuipiga namba ya swahiba wake, ikaita pasi na majibu.

“Hapokei!”

“Kishapata machangudoa, najua tu yaani jamaa Yule ni mgnjwa wa wanawake sijapata kuona si ajabu kapata vodafasta, anamchezea Cobra huyu! Nenda kamcheki” akatoa maagizo. Yule kijana akashuka tena na kuzunguka upande uleule wa

mwanzo, akasimama mahala na kuangaza angaza huku na huko asimwone.

Kamanda Amata, akamwona Yule kijana akibofya simu yake, akajua kwa vyovyote anamtafuta mwenziwe. Haraka akachukua simu ya yule mwingine na ilivyoita tu, akaipunga hewani. Yule kijana chotara akaona tendo hilo, akajua mwenzie anamwita upande huo.

“Jamaa unatuyeyusha braza, eneo hatari hili, twen’zetu jamaa anakuja kufunga kazi,” akalalama Yule chotara huku akimkaribia Amata bila kujua kutokana na vivuli vya miti ile ya maua. Amata akamssubiri mpaka alivyomkaribia, akamtandika karate moja ya paji la uso, jamaa akaenda chini mzima mzima kama mzigo. Kamanda Amata akamwahi na kumburuza mpaka nyuma ya gari yake, akawahi kufungua buti na kumtupia ndani

yake, akamtoa na Yule wa ndani na kufanya vivyo hivyo. Vitendo vyote hivyo vilifanyika kimya kimya, hakuna aliyetilia shaka na kwa wakati huo watu walikuwa wachache tu upande huo. Akaingia garini na kuwasha, akapiga rivasi na kuingia barabarani, akazunguka upande ule alioegesha gari lake na kuliona lile Harrier likiwa pale pale.

“No time to waste!” akajisemea na kuchukua Shot Gun, akashusha kioo na bila huruma akamwaga njugu kutokea dirishani. Risasi zile zikafumua vioo vyote vya ile gari, Kamanda Amata alikuwa anajua nini anafanya, akapandisha kioo na kuondoka kwa kasi huku akiacha mayowe na kelele za watu waliokuwa ndani ya mgahawa ule. Amata akaondoka kwa kasi na kuacha varangati nyuma yake, akakata mtaa wa kwanza, wa pili

na wa tatu akaingia gari katika maegesho ya jengo la Haidari Plaza. Akateremka na kuchukua kutoka katika dahaboard pleti namba nyingine, kitendo cha haraka, akazifyatua na kuziondoa zilizopo na kupachika hizo. Kisha akachukua simu yake na kubofya namba fulani, akaiweka sikioni.

“Mzee! Hapa Haidery Plza kuna gari namba TZH 025K kwenye buti kuna mizigo

naomba uichukue nitakuja kuiona afisini kwako," akaongea na Inspekta Simbeye akimtaka kuja kuchukua wale watu butini.

"Sawa, vijana watafika sasa hivi," akajibiwa.

Akakata simu na kuwahi kuchukua taksi, "nipeleke Salamander tafadhali," akamwambia na Yule dereva akawash gari na kuelekea kule mteja anakotaka.

* * *

Daniel Kermikov alifikishwa eneo la tukio, akiwa ndani ya gari alijiweka tayari kwa kazi, bastola yake kiunoni ikiwa na risasi nane, visu vyake vidogo vya kukunja akavipachika mahala pake. The Cobra akaendesha gari lile kwa mwendo wa taratibu hukua kipiga simu kwa mtu wao waliyemtuma eneo hilo. Badala ya kukuta utulivu katika eneo hilo, Cobra akakutana na umati wa watu pamoja na askari polisi wakiwa wametanda na kuweka

utepe wa njano kuizunguka ile gari.

“Shiiiiit!” Cobra akang’aka.

“Vipi?” Kermikov akauliza.

“Hapa hapako salama, tafadhali abort mission!” akamwambia Daniel huku akiendesha taratibu na kufuata maelekezo ya askari wa usalama barabarani kuwa asikaribie eneo lile.

“That is our car!” Cobra akasema na kutaka kushuka mara

baada ya kuegesha kama mita ishirini hivi.

“Subiri, usalama kwanza! Una uhakika ni letu?”

“Yes!”

“Kwa hiyo vijana wameshambuliwa?”

“Nahisi!” Cobra akajibu. Daniel akashikwa na hasira na kupiga ngumi kwenye dashboard.

“Bastard, son of bitch! Atakuwa amewawahi vijana, dah,

mshenzi huyu anazidi kuniumiza kichwa…" Kermikov akalalamika. Akatulia kimya kwa sekunde kadhaa kisha akafungua mlango na kuteremka, "twende tukajiridhishe!" akamwambia Cobra. Wakateremka wote na kuelekea eneo la tukio.

Upande mwingine Kamanda Amata alikwisharudi katika eneo lile kuhakikisha nini kinaendelea. Umati wa watu ulikuwa hapo, vimulimuli vya polisi

vilitengeneza maua mzuri kabisa. Akiwa katika kusogeasogea ndipo akapitwa na gari aina ya Subaru Salon ambayo ikaongozwa na kuegeshwa mbali kidogo. Kabla hajavuka barabara kuna jambo likamshtua, mtu aliyetermka kwenye gari, moyo wake ukapiga kite, akasimama na kushusha pumzi.

Wamefika! Akawaza, akajaribu kusogea kujiridhisha na watu hao, ndiyo wenyewe, alimtambua

vyema The Cobra kutokana na picha ile iliyonaswa kule afisini, akamtambua Kermikov kwa mtindo huo huo. Akachukua simu yake yenye uwezo mkubwa sana wa kupiga picha gizani, akapiga picha kama kumi hivi za watu hao na kisha akazima simu hiyo na nyingine alizo nazo mfukoni.

Wakati The Cobra na Daniel wakiwa katika kuihakikishia kuwa vijana wao wameuawa au vipi,

Amata aikuwa akitekenya loki ya buti la gari hiyo, akafungua na kuingia ndani yake, kisha akatuia kimya kabisa akisubiri safari….

SEHEMU YA 25

Kamanda Amata alitulia kimya ndani buti lile, huku akiwa ameacha uwazi kidogo kwa ajaili ya kupata hewa. Dakika kama kumi na tano hivi tangu aingie, akasikia sauti za watu waongeao wakisogelea gari lile na baadae

wakingia ndani na kuketi bila kuongea.

"He is dead! Where are the other two?" Kermikov akauliza. Cobra hakuwa na cha kuzungumza, kutoka ndani ya buti la gari lile, Amata aliweza kufuatilia mazungumzo yale kwa uzuri kabisa.

"Huyu jamaa anasumbua kichwa yangu!" Kermikov akamwambia Cobra.

"Kwa nini?"

“Kwa kanuni zetu za kikachero, yaani hapa adui yangu yuko mbele hatua mbili, kwanza anajua nini nataka kufanya, kisha anaharibu na kutia uharibifu, sasa kamuua Dereck, sijui na wale wawili kawaua au kawapeleka wapi!” Kermikov akasema.

“Daniel! Huyu jamaa nilifanya mbinu zote kummaliza nimefeli, nilivyoambiwa unakuja nikasema afadhali…”

"…Nitampata tu, jua la kesho halitachomoza, nitakuwa na roho yake mkononi!" Kermikov akaongea kwa jazba.

"Tunafanyaje?" Cobra akauliza.

"Ninamsaka, usiku huu ama zake ama zangu!" Kermikov akamjibu Cobra huku akiwasha gari tayari kwa safari.

Ndani ya buti Amata aliendelea kusikiliza yote yaliyokuwa yakizungumzwa, yeye kazi yake ilikuwa ni kusikiliza na

kupembua, lipi linamfaa na lipi hapana.

"Twende kwa Yule mwanamke, nitambana mpaka atanambia sehemu zote ambazo bwana wake anapatikana!" Kermikov akamwambia Cobra huku akibaki hoi bin taabani. Kamanda Amata alikuwa akihesabu kona na kutazama nje kwa jico pembe ili mradi tu ajue ni wapi alipo.

Kinondoni! Akawaza baada ya kugundua kuwa wamekunja kulia

na kuiacha Barabara ya Morogoro na kuchukua ile ya Kawawa. Huku ndani ya buti Amata aliwatumia taarifa watu wachache tu na kuwataka kuwa standby kwa taarifa yoyote. Baada ya kuimaliza barabar hiyo wakakunja kulia na kuingia Kinondoni Moscow. Ni jumba lile lile ambalo Amata alikuja na Stella siku moja nyuma, na ni jumba hili hili ambalo Chamellen na Stella walifanya uharibifu mwaka 1984. Liliteketea kwa

moto mara baada ya Chameleon kufanya yake katika harakati za kumwokoa mpenziwe, Stella. Ni kitu kama kilekile ambacho sasa kinataka kutukia, katika eneo na jumba lile mara hii Amata anataka kumwokoa Gina, historia imejirudia.

Kama wao walichoma kidogo sasa mimi naangusha panakuwa uwanja wa mpira! Amata akawaza huku hasira ikizidi kumpanda.

"Yaani nikimpata huyu jamaa sijui nitampa kifo gani," Kermikov akazungumza.

Laiti mngejua kuwa tupo pamoja, msingeongea hayo! Amata akawaza hukuakiendelea kustarehe kwenye buti la gari hilo. Baada ya kuhisi kuwa gari lile linaacha barabara ya lami, akafungua buti kiasi ili aweze kuona nje, kutokana na giza la nje hakuweza kutambua eneo hilo haraka lakini baada ya dakika

moja hivi, akajua kuwa walikuwa eneo la Mkwajuni, Kinondoni.

"Tunafika nyumbani, Cobra toa taarifa ya kimaandishi kuhusu mauaji na upotevu wa watu wetu, mimi nahitaji kuchukua silaha nyingine ili kumsaka mwanaharamu huyu usiku huu…" Kermikov akampa Cobra mpango kazi.

"Yaani nashindwa kujua taarifa hii itapokelewaje!"

"Kwani hapa Tanzania huwa mnafanya reference kwa nani?" akauliza Kermikov.

"Sisi pamoja na Zambia na Malawi tupo chini ya Zimbabwe kwa Sir. Bernad Logarton," Cobra akajibu huku akiendelea kuendesha gari kwa kasi na kumfanya Amata ndani ya buti kujigonga huku na kule. Gari lile likasimama na kupiga honi kali, Amata akahisi geti likifunguliwa, akajiweka tayari na bastola yake

mkononi, gari lile lilipoingia tu getini, kama mita tano hivi, akafungua buti kwa ustadi na kujirusha nje akabiringita na kujificha kwenye kichaka cha maua kimya. Lile gari likasimama na jamaa wakashuka na kuingia ndani mkuku mkuku, Amata akatazama usalama kwanza kabla hajaanza makeke yake.

Katika uwanja ule kulikuwa na mataa kama manne hivi yenye kuangaza eneo kubwa tu, miti

kadhaa ya maua ilifanya vivuli ambavyo kama wewe ni mjuzi wa kujificha basi unaweza kujificha hata mwezi mzima wasikuone. Zaidi ya miti na maua, kulikuwa na mlinzi mmoja wa Kimasai ambae mara tu baada ya kufungua geti aliendelea kuzungukazunguka jengo hilo kubwa ambalo nyuma yake kulikuwa na banda kubwa lililojengwa kwa matofali upande wa chini na nondo kubwa upande wa juu.

Yule mmasai akapita palepale ambapo Amata amejificha na asimwone, akamtazama ni wapi anaelekea, akamwona akizunguka nupande wa nyuma wa jengo lile.

Sasa naliamsha dude, watasoma namba! Akawaza na kuchomoka pale alipo, akavuta hatua na kuikimbilia nguzo kubwa ya taa akikatisha karibu kabisa na geti, mara king'ora kikali kikalia. Amata akajua mambo yashaharibika na kile

anachotaka kufanya akaona kama hakitafanikiwa. Sarakasi moja ikamfikisha kwenye ile nguzo, nyuma yake kuikuwa na mfuniko wazi wa sakiti ya umeme.

Nilijua tu, nguzo hizi nyingi huwa hazina vifuniko, watakoma! Akawaza huku akitazama zile nyaya jinsi zilivyojipanga kwenye ile chemba.

“Rafikiiiiii! Nini huko?” sauti ya Cobra ikasikika, kamanda akajua kumekucha, akavuta waya

mwekundu, ukachomoka kwenye konekta yake kisha akaupachika kwenye waya mweusi.

Puuuuuuhhhh!!!! Shoti ya umeme ikatokea, taa zote mpaka ndani ya nyumba zikazimika. Amata akaiweka sawa bastola yake, akajitokeza barabarani na mtu wa kwanza kukutana naye ni Yule mmasai. Konde moja la maana likampeleka chini, Mmasai akainuka na kuvurusha rungu lake, alipolichia Amata akaepa

likapita. Mmasai akachomoa sime refu, akaanza kuruka akipiga kelele, mori.

Kutoka ndani Kermikov akachukua bastola yake na kuiweka tayari, kelele za mmasai zikamfanya ajue huko si salama. Wakati haya yakiendelea, The Cobra alikuwa upande wa nyuma kaenda kuwasha jenereta. Kermikov alipotoka nje alimkuta mmasai akiruka na kutua huku

akipiga yowe la hatari lakini hakuona mtu mwingine eneo lile.

“Heyyyyy stoooppppp!!!” akamzuia yule mmasai. Alipotulia, akaangaza huku na huko asione mtu zaidi ya mmasai tu.

“Nini shida?” akmuuliza.

“Eee this way!” Mmasai akajitahidi kujibu kwa kiingereza huku akimwonesha Kermikov njia ambayo Amata amepita na kutoweka eneo hilo. Kwa

tahadhari kubwa sana, Kermikov alipita kwenye ujia huo kuelekea upande wa pili, huku nyuma yake mmasai naye alikuwa akinyata kwa kumuiga mzungu huyo anachofanya.

Kamanda Amata baada ya kukwepa rungu la mmasai Yule na kushuhudia jamaa akichomoa sime, aliondoka kiaina na kuelekea kule upande wa nyuma wa jumba hilo. Bahati mbaya au nzuri katika moja ya upenyo

akamwona Cobra akiwa na tochi ake kubwa akifungua mlango wa banda la jenereta tayari kuwasha.

"You are late!" Amata akamwambia na kumfanya mzungu huyo ashtuke na kuangalia nyuma, uso kwa uso akakutana na TSA 1.

"Anhaaa umekuja mwenyewe!!!!" Cobra akamwambia huku akimrushia ile tochi, Amata akaigundua mbinu hiyo mapema sana, akaiepa na

nukta hiyo hiyo akamwona
Cobra hewani akija kwa
shambulizi la hatari.
Hakumsubiri, na wala hakupenda
kutumia bastola kwani nafasi
ilikuwa ndogo sana, akamsubiri
kidogo alivyomkaribia akampa
pigo moja zito na kisha akahamia
upande wa pili na kumwacha
Cobra akijibwaga chini huku
akitoa yowe la uchungu na
mikono yake akiwa ameibana
katika eneo nyeti.

Kutoka ndani ya banda lile, Gina akashtushwa na vishindo hivyo, akinuka kutoka alipoketi, mwili ukiwa unamuuma kwa kipigo. Hakuweza kuona kinachoendelea kutokana na urefu wa jengo hilo. Akaliendea geti na kuanza kulipiga kwa nguvu. Kelele zile zikamshtua Amata, akamsahau Cobra pale chini na kuuendea mlango huo, akatikisa kufuri, limefungwa, akatoa bastola yake na kufyatua risasi moja tu, likaachia.

Akafungua haraka lakini kabla hajamalizia, akjikuta akibamizwa kwa nguvu katika lile lango na kupita nalo mpaka ndani, akaanguka chini bila kipingamizi. Alipojaribu kuinuka, akachelewa, Kermikov akatua kwa futi na kumtandika vibaya kwenye uti wa mgongo, Amata akajipigiza tena chini, na kujikuta akikosa hewa na mbavu zikimbana.

"Noooooooooooh!"Gina akapiga ukulele na kumvamia

Kermikov lakini akajikuta akipokea konde lenye kilo nyingi shavuni na kubwagwa upande wa pili akiwa hoi. Naye akajitahidi kuinuka lakini guu moja lenye nguvu likaufumua uso wake na kumwangushia kando. Amata akapiga ngumi chini kwa hasira, pigo lile hakuwahi kukutana nalo tangu aanze kazi hii.

"Yes, you are in my hands now!!!" Kermikov akamwambia Amata, "come to me

boy!”akaongeza kusema huku akimwita kwa mikono yake ambayo alikuwa amevalia gloves zenye vyuma vyenye ncha kali. Amata akajitahidi kuinuka na kujifanya mnyonge sana, akakumbuka ‘Art of War’ inayosema ‘jifanye mnyonge unapokuwa una nguvu na jifanye una nguvu unapokuwa mnyonge’, akainuka kwa taabu na kabla hajasimama sawa, Kermikov akampelekea mapigo ya kifo, karate za maana

zilizopelekwa kwa ustadi wa hali ya juu. Mapigo yote yakamwishia Amata na kumwacha chini hoi.

“Hah hah hah aaaaa!!!!” Kermikov akacheka kwa dharau huku akichezesha miguu yake kama bondia anayetaka kumshambulia adui yake. Gina akainuka na kujaribu kumtetea bosi wake katika hilo, Kermikov akampelekea pigo moja, Gina akaepa kwa umahiri, pigo la pili, akaepa tena, la tatu, akaepa na

kumtisha kama anamvamia, jamaa akatishika na nukta hiyo hiyo Gina akamzabua pigo moja lililotua shavuni na kumchana kwa pete yake ya uchumba ambayo kabla aliigeuza na kuweka ua la pete hiyo upande wa ndani ya kidole chake.

Huko nje, Cobra akasaidiwa na mmasai kuinuka, aliposimama akamsukuma kando mmasai Yule na kuingia ndani, mkononi mwake akiwa na kipande cha

ubao alichokiokota nje tu. Alipoingia ndani akakuta Amata amelala chini hoi, shati lake likiwa na damu kutokana na mapigo ya mikono ya Kermikov.

"Cobra, hawa wanatakiwa wafe taratibu, tutawatia kwenye surphuric acid, watapotea kabisa duniani kana kwamba hawajahi kuzaliwa," akamwambia Cobra.

"Never happen!" Amata akasema, maneno hayo yakamfikia Kermikov sambamba

na Cobra. Kitendo cha haraka, Ama atakachomo bastola kutoka kwenye soksi yake na kuirusha kwa Gina. Mwanamke huyo akajirusha kutoka pale chini na kuidaka huku akindoa usalama na kufyatua risasi mbili za haraka.

“Cobraaaaa!!!!” Kermikov akapiga kelele huku akirukia upande wa pili kuikwepa risasi ya Gina, lakini Cobra akachelewa na kupokea moja ya bega, ikambwaga chini. Tayari Amata

alikuwa wima sakafuni, Kermikov akamjia haraka na mapigo ya karate ya kiwango cha juu, kati ya mapigo ishirini akashangaa yote yamepanguliwa kwa ustadi sana. Akajipanga upya akitazama Amata usoni. Kamanda hakutikisika, misuli yake ya mwili ilidinda kama samba anayetaka kushambulia, macho yake hayakupepeseka, mwanaga hafifu wa ndani ya banda lile uliwanya kuonana kila

mmoja kwa uwezo wake, kazi imeanza.

Mara mngurumo wa jenereta ukasikika na taa zikawaka ila si zote, Kermikov akatumia hapohapo kupeleka mapigo mengine mengi ya haraka haraka. Kamanda Amata alishuhudia kama mikono zaidi ya mia ikizunguka hewani na kumshambulia kwa hasira huku kelele za hamasa zikisikika, nay eye aliitumia mikono yake kwa

kasi ile ile kupangua mapigo hayo kwa umakini. Akiwa ameshamsoma adui yake, akajua ni wapi ataishia, na alipojua kuwa sasa anamaliza, hapo hapo, Amata akpiga pigo la kwanza zito likatua kifuani na kumsukuma nyuma Kermikov, hakuanguka, akasimama lakini kabla akili haijkaa sawa, akapokea pigo linguine na linguine kisha akapata ngwala ya magoti akajikuta chini. Kamanda hakujali, akaenda hewani na kushuka na futi la

mgongo kisha akajirusha kando na kumwacha mzungu huyo hoi kwa mtindo ule ule.

Gina alimwende Cobra na kumnyooshea domo la Berreta Pico “nakukumbuka sana! Ulitaka kuniua, sasa zamu yak….”. hakumaliza, Cobra alijirusha na kuipiga teke bastol ikamtoka Gina na kwenda hewani, akaruka juu na kuidaka kwa minajiri ya kushambulia, lakini kabla hajatua, tayari Amata

alitumia kiatu chake na kufyatua kitu chenye ncha kali kilichotua mbavuni mwake, akarudi chini na kukutana na mapigo kutoka kwa Gina. Mwanamke huyu akaiwahi tena bastola na kumtandika gotini, akamvunja mguu.

Upande wa pili Amata aliendelea kupambana na Kermikov, pambano gumu lisilo na refarii. Kila mmoja aishambulia na kujilinda. Makonde mazito mazito yalikuwa

yakirushwa aidha yampate mlengwa au yamkose. Kermikov baada ya kuchoka kutumia ngumi na karate sasa akachukua visu kutoka kwenye mkanda wa suruali yake. Kwa kasi akaanza kumshambulia Amata, naye akajitahidi kukwepa lakini kisu kimoja kikapita kwenye nyama ya mbavu na kuchaana kama robo sentimeta. Mauamivu hayo hayakumfanya apoteze sahababa, akasimama na kumsogelea mzungu huyo, akampa konde

moja, naye akarusha mkono wenye kisu, akaudaka na kuzunguka nao akaupachika begani na kuuvunjilia mbali. Akamwinua na kumbwaga chini kwa nguvu, Kerimikov akatoa yoe la uchungu, pigo la mwisho la Amata likatua katikati ya paji la uso na kumzimisha mzungu huyo akimwacha akiung'ata ulimi wake. Akasubiri akimtazama kwanza, lakini akaona hana dalili ya kuamka.

“Vipi, umemvunja roho?” Gina akauliza.

“Sijamvunja, nimemtengua tu, vipi huyo?”

“Huyu hali mbaya sijui hata kama atanyanyuka hapa!” Gina akajibu.

“Yule mmasai kaenda wapi? Atatuletea shida,” Amata akamwambia Gina.

“Ni kweli sasa hawa tunafanyaje?”

“Tunaondoka nao! Piga simu kwa babu yako, mi namsaka huyu masai!” Kamanda Akamwambia Gina na kumpa simu, yeye akatoka nje na kuangaza angaza asimwone mmasai Yule. Akaamua kuachana naye na kuingia ndani ya jumba lile, hakutaka kingine zaidi ya kompyuta ya mezani aina ya apple, akaondoa nyaya zake na kuinyanyua, akatoka nayo nje na kuitia kwenye gari ile ile ambayo walitumia kuja.

* * *

Inspekta Simbeye aliwasili navijana wake, kama kawaida yao wakaizingira nyumba hiyo kwa nje na wachache wakaingia ndani.

"Kuna watu wawili humo bandani hakikisheni mmewatia kwenye defender, ila muwe waangalifu, ni viumbe hatari sana," akawaambia vijana wa polisi na kisha yeye akaingia katika ile gari pamoja na Gina, alipokuwa akitoka tu nje ya geti

akakutana na Madam S naye akiwa anaingia mahala hapo. Akasimamisha gari lake na kuteremka huku upande mwingine akishuka Jasmini.

“Upo sawa?” akamuuliza Amata kupitia dirishani.

“Mwili una maumivu na nina jeraha la kisu,” Amata akajibu huku mkono wake mmoja ukiwa umezuia mchano ule wa kisu. Madam S akamwambia jasmine awachukue haraka kwa kutumia

gari yao na kuwakimbiza Shamba kwa matibabu.

Jumba lile likawa chini ya ulinzi, askari wenye silaha wakaizunguka, hakuruhusiwa mtu yeyote kuingia ndani ya jumba hilo bila kibali maalumu..

* * *

SEHEMU YA 26 –bonus-

KIKAO KIZITO…

Siku iliyofuata kulikuwa na kikao kizito katika moja ya kumbi

ndogo za mikutano ndani ya Ikulu ya Magogoni. Rais na watu wake wa juu kabisa katika maswala ya kidiplomasia na usalama walikutana katika kujadili nukushi iliyoingia siku iliyotangulia kutoka umoja wa Ulaya 'EU'. Ujumbe mkubwa katika nukushi hiyo ulikuwa ni shinikizo la umoja huo kwa Tanzania kuwaachia huru Makaburu inayowashikilia katika magereza yao tangu miaka ya themanini mpaka sasa. Zaidi ya

hilo, ujumbe huo ukasisitiza kuwa kama nchi hiyo haitawaachia huru basi itawekewa vikwazo vya kiuchumi pamoja na kusitisha misaada yote ambayo umoja huo ulikuwa ukiifadhili.

“Mnaona! Sasa umasikini wetu unageuka kuwa fimbo ya kutuchapia,” mmoja wa wajumbe akazungumza kwa jazba.

“Hawa tayari wametuzunguka, si wenzao ndo maana!” mwingine akadakiza.

Katika ukumbi huo mabishano yakachukua nafasi kiasi kwamba wakasau kuwa wapo na mheshimiwa ndani humo.

“Waheshimiwa, hebu tujadili jambo hili kisomi zaidi na si kuropoka tu,” Makamu wa Rais akatoa rai.

“Kiukweli hapa tulipofikia ni pagumu, hawa jamaa wamegundua kuwa sisi tunajua kuwa hata wao wana watu wetu, na ni wazi kabisa kuwa

wanakataa ile sheria ya kimataifa ya kubadilishana wafungwa, wao wanataka watu wao kwa nini sisi wale kule nyani? Sio watu wale?" Waziri wa mambo ya nje akazungumza, "kumbukeni kuwa mwaka 1984, tume nzima ya upatanishi katika sakata hili waliuawa akiwemo waziri mwenye dhamana na wajumbe wake. Tukasitisha mazungumzo mpaka na Mwalimu akatutaka kuikomboa Afrika kidiplomasia, tukapambana sana mpaka

Mandela akaachiwa huru, baada ya serikali dhalimu ya kikaburu kuangushwa na kuona wazi kuwa wameshindwa mbele ya mtu mweusi, wakaanza mikakati ya kudai watu wao, mikutano kama mine au mitano imekosa muafaka. Tukipanga hapa hawaji wanataka twende kwao, tukienda wanataka kutudhuru, tufanyeje sasa?" akaongeza kusema kwa uchungu na ukumbi ule ukawa kimya kabisa.

“Mheshimiwa uko sahihi kabisa, lakini swali la msingi ni kwamba, je tuna uhakika kuwa kuna watu wetu kule? Kwa sababu wao wamesema kuwa kama tunajua walipo tuseme wazi, maana kama ni Kisiwa cha Roden lie gereza lilikwishafungwa kabisa…. Je tuna uhakika na tunachokitaka? Isije tukang’ang’ana na jambo hewa huku wananchi wetu wanakufa njaa, unafikiri wakiweka vikwazo vya kiuchumi

na kufunga misaada tutafanyaje wakati bajeti yetu tu asilimia karibu hamsini wanachangia wao… tuliangalie kwa makini," Mheshimiwa mwingine akazungumza.

Baada ya wajumbe wengi kuzungumza, mheshimiwa Rais akachukua nafasi kutoa ya moyoni, "wajumbe mmesema mengi sana, lakini nimenasa mambo mawili ya msingi ambayo nitahitaji yafanyiwe kazi: Kwanza

ni je; kuna watu wetu kule? Nahitaji kupata uhakika wa hili kwa taarifa za kiuchunguzi, pili nataka iundwe tume nyingine itakayofikia muafaka katika hili," akasema. Ukimya wa nukta kadhaa ukachukua nafasi na kisha Mkuu wa majeshi akaomba nafasi ya kuzungumza.

"Inaweza kuwa ni kweli kuna watu wetu au si kweli, mi nafikiri kwanza tujue uhakika wa hili kama alivyosema mkuu wan chi,

mimi kwa niaba ya JW nipo tayari kushirikiana na serikali katika hili…" akapigiwa makofi ya pongezi kwa uamuzi wake huo.

"Aaaa ni vizuri umesema, lakini hili la kujua ukweli kuhusu watu wetu huko South Afrika, niachieni mimi najua ni jinsi gani nitafanya, ila muwe tayari kwa lolote itakapobidi," Rais akamwambia Mkuu wa majeshi na wengine wote wakaafikiana na

hilo kuwa operesheni hiyo lazima iwe ya siri.

“Na kuhusu kuwajibu hawa jamaa tunafanyaje mheshimiwa?” mjumbe mwingine akauliza.

“Iundwe tume makini ya upatanishi, nyingine kabisa, hawa jamaa tutawajibu kuwa Serikali ya Tanzania imekubali kuwaachia huru watu wao ili kudumisha uhusiano wa kidiplomasia uliopo kati yetu na wao. Lakini kuwepo tukio la kusainiana kama

maridhiano na mapatano kati yetu…" akamaliza kusema na kusimama tayari kuondoka. Wajumbe wote nao wakasimama kuonesha heshima kwa Mkuu wa Nchi naye alipotoka wao wakaketi tena kufanya mambo ya mwisho katika hili.

* * *

Baada ya siku mbili kupita tangu Kamanda Amata kuwa katika mapambano mazito na Kermikov, hali yake ilanza kurudi

vyema, mwili ukapata nguvu na mazoezi madogo madogo yakaanza kuchukua nafasi mwilini mwake. Katika kliniki ya Daktari Jasmini ndipo alipewa mapumziko na kupatiwa matibabu stahiki yeye pamoja na Gina. Ni chumba chake kilekile ambacho siku tatu au nne zilizopita alipumzika. Akiwa kakodoa macho kutazama runinga iliyopo mbele yake, akagutushwa na hodi iliyogongwa chumbani mwake. Hakuishangaa,

bali alijua ni nani anayegonga. Akachuku kifaa maalumu kilichounganishwa na waya mpaka kwenye mlango huo na kuufungua kwa kubofya tu. Hakuwa mwingine bali Chiba wa Chiba, akaingia na kuketi kitini mara tu baada ya kufungwa mlango ule.

"Usalama upo?" Kamanda akauliza.

"Upo kwa asilimia nyingi, jiji limetulia lakini hekaheka za nje

ya nyumba inaonekana zimekuwa kubwa zaidi. Taarifa mpya ambazo ninazo ni kuwa mama anajipanga upya kumaliza tatizo hili baada ya kupata vitisho kutoka kwa mwenye nyumba," Chiba akatoa taarifa kwa kifupi kwa lugha ambayo Amata aliielewa vyema kabisa.

"Upuuzi, upuuzi kabisa Chiba… tutawanyenyekea hawa watu mpaka lini? Tuyaache hayo, kazi yangu vipi?" akamuuliza.

“Kazi imekamilika…”

“Umewang’amua wote?”

“Bila shaka kaka, nitakwambia juu ya mmoja baada ya mwingine,” Chiba akamwambia na Amata akajiweka tayari kupata taarifa hiyo ya kiuchunguzi ambayo mtaalamu huyu wa kimtandao alikwishaifanyia kazi stahiki.

“Kwanza kabisa, hawa watu watano ni viongozi au wenyewe hujiita magavana wa WP. WP ni

mtandao mkubwa sana unaofanya kazi sehemu nyingi duniani hasa Afrika na Asia ukiwa na lengo moja tu la kumlinda mtu mweupe dhidi ya mweusi. Na mweupe huyu ni Mzungu tu, yaani Yule anayetoka Ulaya, lakini jua kwamba Ulaya si wote wazungu. Wanaokuwa chini ya mtandao huu ni wale kutoka United Kingdom na nchi chache chache za jirani na hapo…”

“….enhe naona umeingia ndani zaidi,”

“Yes! Sasa hawa kwa ujumla wametokana na uzao wa makaburu yaani wazungu waliovamia Afrika ya Kusini na kulowea katika nchi hiyo kama isemavyo historia. Na katika harakati za kutaka kuitawala Afrika hasa hii ya kusini mwa Jangwa la Sahara ndipo ulipozaliwa mtandao huu hatari sana wa WP ambao uliweka

mizizi yake Rhodesia, Mozambique, Namibia, Botswana, Afrika Kusini yenyewe ndiyo makao makuu na wengine walijiweka huko Congo na hapa kwetu Tanzania. Taarifa zinasema kuwa mtandao huu zamani ulikuwa unaitwa White Power lakini katika vita ya ukombozi iliyoongozwa na Mwalimu Nyerere, ulisambaratishwa chini ya timu hatari ya upelelezi iliyoundwa

kama Kikosi cha Kisasi kule Congo," Chiba akaeleza vyema.

"Haswaaaa mpaka hapo najua vyema…" Amata akaunga mkono.

"Sasa baada ya kusambaratika wakajipanga upya na kuendeleza mapambano, mara hii wakajiita WP lakini si White Power sasa ni White Protects na kiongozi wao mkubwa kwa sasa anaitwa Mc Cain ambaye katika serikali ya De Klerk alikuwa waziri wa juu sana.

Msaidizi wake anaitwa Margaritha Casbarai huyu ni mwanamama hatari sana kutoka Ireland ambaye makao yake ni Namibia Windhoek. Zaidi ya hapo huyu mama anafuga wasichana ambao wana mafunzo makali sana ya kijeshi na upiganaji wa bila silaha, anawaita '*Daughters*'. Hawa huwatumia sana katika kupeleleza mtu wenye shaka naye hasa wanaume, hujitoa kimwii kwako na kisha

hupata kila kitu," akazidi kuchambua.

Hapa Amata akamkumbuka mwanamke Yule ambaye alimfuatilia tangu Dar es salaam mpaka Windhoek na akafanikiwa umdhulumu roho yake, pia akambuka Yule mwingine Parrot ambaye alimvunja miguu kikatili kabisa pale hotelini.

Daughters! Akawaza.

“Umechimba sana, umepataje yote haya kaka?” Amata akamwuliza Chiba.

“Ndiyo kazi yangu, nimevunja codes nyingi sana za usalama mpaka kuufikia huu mtandao, lakini kabla sijamaliza nafikiri wakagundua kuwa kuna sehemu siri zao zinavuja, wakawahi kufunga tena, lakini nilishapata za kutosha,” akamwambia.

“Enhe!”

“Sasa hawa jamaa mpango wao wa sasa baada ya mtu mweusi kuwazidi maarifa wameamua kuitawala Afrika kiimla kutokana na umasikini wetu. Kwa hiyo hawa WP wanafanya kazi zao kwa siri sana na wakati mwingine hata kuua viongozi wagumu wa bara hili ili kuweka wa kwao…”

“Kwa hiyo tuna vibaraka wengi sana…”

“Of course… sasa Amata kuna kitu cha siri sana ambacho wewe hukukigundua na usingeweza kukigundua kaka, lakini kwa akili nyepesi ungejiuliza kwa nini bahasha ile ilifungiwa ndani ya safety box kwa Yule jamaa kule Kurasini ilhali haina kitu ndani…”

“Enheeeee hapa hapo sasa, nilijiuliza kuhusu hilo sikupata jibu…”

“Sasa jibu ni hili, ile bahasha ule utepe wake ambao wewe ungeubandua na kuutupa ili uweze kuifunga bahasha, haukuwa utepe wa gundi kama tulivyozoea…. Ile ni Data Belt, kwa hiyo ile bahasha ilihifandhi Data Belt ambayo mtu wa kawaida angeitupa tu lakini imebeba nini ndani, ndiyo haya yoooote niliyokwambia na nitakayokwambia, mfumo mzima wa WP Afrika na nje ya Afrika upo humo, mikakati mibaya kwa

mizuri, nani anatakiwa kuuawa na anatakiwa kuishi, mikakati juu ya mikakati. Na siri zao wamezificha sehemu mbalimbali kwa namna ya pekee sana ambayo mtu huwezi kujua kirahisi…" Chiba akaeleza kinagaubaga.

"Hapa Tanzania wapo tangu lini hawa WP?" Amata akauliza.

"Wapo tangu Mjerumani alipoachia koloni kwa Mwingereza, mwaka 1961 wakati wakikabidhi uhuru kwa Mwalimu

Nyerere tayari walikuwa wameshajiwekea mikakati ya jinsi gani ya kutawala kwa namna isiyoonekana, hawakuondoka, wapo mpaka sasa, akifa huyu anakuja Yule bila sisi kujua na wengine wanazidi kuja kwa uwekezaji na misaada mbalimbali…”

Maelezo haya yakampa Amata fikra nyingi sana, akawaza na kuwazua, akaiona kazi ngumu amabayo sasa inalikabiri taifa

lake. Ni juzi tu amesambaratisha kama si nyumba basi ni afisi ya watu hawa labda, na hakika mpaka dakika hiyo watakuwa wameshaju ni nini kimeendelea Tanzania. Nini watafanya? Lilikuwa ni swali ambalo liliupeleka mbio moyo wake na kuufanya mwili kuwa baridi na moto kwa wakati mmoja. Chiba akaeleza mengi sana kiasi kwamba mengine ni ya kushtusha ambayo yanaweza kumfanya mtu kuanguka na kufa kabisa.

“Umeprinti?” akamuuliza.

“Kila kitu kipo secured katika boksi letu,” Chiba akamjibu Amata.

“Nini kingine umegundua?” akamuuliza.

“Dassen Keputo!”

Amata aliposikia jina hili, akainuka na kuketi kitako juu ya kitanda hicho, “enhe! Nambie”.

“Nimekuta taarifa kidogo juu ya Dassen Keputo, siku ya kufa

na kusikwa kwake, katika taarifa hii Dassen ameandikwa kama Gate to Heaven, na inaonekana kuna siri kubwa sana ndani kaburi hili, sasa nina wasiwasi kuwa hakuzikwa mtu mle ndani," Chiba akaeleza.

'Dassen Keputo siyo mtu!' maneno ya Stella yakamrudia Amata.

Amata akainuka na kuchukua shati lake akavaa, na kutwaa vifaa vyake vichache akavipachika

mahali fulanifulani mwilini mwake.

"Vipi?" Chiba akauliza.

"Tunaondoka tunaelekea *shimoni*, peleka taarifa HOT tukutane huko…" Kamanda Amata akasema na Chiba akatii na kufanya alivyotakiwa kufanya. Dakika kumi baadae walikuwa barabarani kuelekea kituo kikuu cha polisi cha Jiji la Dar es salaam.

DAR ES SALAAM

KITUO CHA POLISI KATI –

Inspekta Simbeye alikuwa kimya kabisa kitini pake akifuatilia habari kwenye gazeti la siku hiyo iliyokuwa ikizungumzai tukio la siku mbili zilizopita huko kinondoni. Alijaribu kumtazam mwandishi huyo aliyeandika habari hiyo kwa jazba pasi na kufanya uchunguzi. Akiwa kazama kabisa kwenye gazeti hilo akagutushwa na hodi na

kufuatiwa mlango kufunguka kabla hata hajakaribisha. Mbele yake wakasimama watu watatu, mmoja mwanamama mtu mzima ambaye kichwa chake tayari kilipoteza hadhi ya nywele na kukaribisha mvi. Pembeni yake kuikuwa na vijana shupavu, wakakamavu wenye sura zinazoonesha uzalendo kwa nchi yao. Hawakuwa wengine zaidi ya HOT, TSA 1 na TSA 2.

“Karibuni sana,” akawakaribisha, na wao wakaketi, “ndo mmekuja?” akauliza swali.

“Ndiyo, tumekuja kuwacheki watu wetu, maana tutahitaji kuwahamisha muda si mrefu, wanaendeleaje?” Madam S akajibu na kuanzisha mazungumzo hayo.

“Madam Sellina, hapa kuna kazi ngumu kidogo kuhusu hawa watu, wale vijana wawili tuliowachukua pale Salamander

wako ok, na wale wa juzi wa Kinondoni mmoja amefariki na mwingine hali yake mbaya," Inspekta Simbeye akaeleza, taarifa hii ikamshtua kidogo Madam S, Amata hakushtuka kwa maana alijua hali ambayo alikuwa nayo Cobra ila alikuwa na uhakika kabisa kuwa Kermikov ataamka na atakuwa salama tu.

"Tunahitaji kuwachukua leo hii, kwa mahojiano zaidi…"

“Aaaa Madam S, ni leo tu nimepata barua hii, (akampa bahasha) nilipoisoma nikafikiri kukuita lakini nimefurahi kwa kuwa umekuja mwenyewe. Oda tuliyoipata kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ambayo pia imepitia afisi zote muhimu, inatutaka kuwaachia huru watu hawa haraka iwezekanavyo na kuondoa ulinzi kwenye ile nyumba pale Kinondoni,” akawaambia.

Taarifa hii ilikuwa mpya, kwa wote hawa, wakashtuka na kutazamana, Madam S akaifungua ile barua na kuisoma kisha akampatia Amata naye akaisoma na kuirudisha mezani.

“Haya ndiyo mi nisiyoyataka, watu kama hawa waachiwe huru iweje? Hawa ni wahalifu kama wahalifu wengine tu…”

“Bora ningeua tu ijulikane moja,” Amata akamkatisha

Madam S huku tayari amekwishasimama wima.

“Nataka kuwaona!” Madam S akaomba na muda mfupi baadae, wakapelekwa shimoni na kuwakuta watu hao. Vijana wawili walikuwa wameketi kwenye chumba kilichotengwa kwa nondo katikati. Chumba kingine alikuwepo Kermikov kitandani akiwa hajitambui na mashine ya kupima mwendo wa moyo ilionesha wazi kuwa bado

yu hai. Chumba cha nne alikuwako The Cobra, kimya juu ya kitanda huku shuka jeupe likiwa limemfunika gubigubi.

"Action moja tu ya Gina imekuondoa uhai, nyama wewe!" Amata akasema. Madam S akamtazama kijana huyo kana kwamba hajamwelewa nini amesema.

"Umesemaje?"

"Kazi ya mrembo Gina hiyo…"

Baada ya kuwatazama watu hao, wakarudi tena afisini lakini kabla ya kuingia afisini humo walikutana na ugeni katika korido ya kituo hicho. Si Madam S wala Amata aliyeshangaa kuhusu watu hao. Kwa mavazi yao tu ilijulikana kuwa ni maafisa ubalozi, na wanajeshi kadhaa kutoka nje. Wao wakiwa nyuma, mbele alitangulia RPC wa mkoa wa Dar na maafisa wengine kadhaa. Dakika kama kumi baadae, watuhumiwa wale

waliondolewa na kuingizwa kwenye gari tatu maalum kabisa.

"Thank you very much for everything!" Mzungu mmoja aliyevalia suti nadhifu alitamka hayo huku akimshika begani Amata kisha wakaondoka zao. Kamanda Amata akatoka eneo hilo na kukodi taksi akifuatiwa na Chiba huku nyuma wakimwacha Madam S akirudi afisini kwa Inpekta Simbeye. Si kwamba

waliingia kimakosa katika taksi hiyo bali kwa makusudi mazima.

“Fuata huo msafara!” Amata akamwambia dereva ambaye alimjua vema kwa kazi yake, Scoba. Akaliondosha lile gari na kuufuata ule msafara ambao ulikuwa ukiongozwa na pikipiki ya polisi kuelekea Uwanja wa Ndege.

“Wanasafirshwa!” Scoba akasema.

“Ndiyo nataka nijue kila kitu, twende mpaka airport…”

SEHEMU YA 27

Scoba aliendesha gari lake kama asiye na malengo na msafara huo, nah ii yote aliifanya ili wasimjue kuwa anawafuata. Msafara ule ulipofika katika barabara ya kuingia uwanja wa ndege Terminal II haukukunja bali ukapitiliza na kuelekea Terminal I.

“So?” Scoba akauliza.

“Ingia Terminal II najua cha kufanya,” Amata akasema. Scoba akakunja kushoto na kuingia katika uwanja huo mpaka maegeshoni. Kamanda Amata akashuka na kumtaka Scoba kusubiri, Chiba naye akateremka na kumfuata wakaingia ndani. Kwa vitambulisho vyao wakafanikiwa kupita vizuizi mpaka upande wa ndani wa uwanja huo. Wakafika katika

eneo ambalo kampuni ya Swissport huegesha magari yake ya kuvutia mizigo. Hakuna kuuliza, Amata akadanda katika moja ya magari hayo madogo kwa umbo na Chiba akakaa nyuma yake, wakaondoka na kuelekea uwanja wa jeshi ambao jamaa wale walielekea na msafara wao. Chiba akamgusa Amata mgongoni na kumpatia koti l akung'aa ili avae na yeye akavaa jingine.

Katika uwanja wa jeshi, kulikuwa na dege kubwa la jeshi limeegeshwa na lango lake la nyuma likiwa wazi. Kamanda Amata hakutaka kufika kule, akatafuta mahali ambako akiegesha gari hiyo haitakuwa rahisi kugundulika hila zake na yeye pia ataweza kuna vyema kinachoendelea. Kwa kutazama haraka haraka akagundua kuwa ndege ile ni ya jeshi la Afrika ya Kusini lakini alichoshangaa ni kuwa wanajeshi aliowaona

walikuwa wazungu tu.
Akashuhudia watu wake wakipakiwa huku vitanda viwili vikifuatia akajua tu kuwa ni cha Cobra marehemu na Kermikov mahututi. Baada ya dakika kama kumi hivi mwanajeshi mmoja wa kike akatoka na begi lake la kijeshi akasimama nje ya lile lango. Akawapa saluti wenzake na lango likafungwa. Muda wote huu, Amata hakugeuka nyuma kumtazama Chiba, baada ya kuona ile ndege ikiondoka ndipo

akageuka na kumkuta Chiba akiwa katingwa na simu yake kubwa huku mbele akiwa kaifunga kitu fulani kama zoom lakini ni ndogo.

"Vipi?" Amata akauliza.

"Safi nimepata yote," Chiba akajibu.

Amata akawasha lile gari na kugeuza haraka kurudi uwanja mpya, "kuna mwanamke amebaki yabidi kumfuatilia, yale yote niliyotaka kwahoji washenzi

wale, atajibu yeye," akamwambia Chiba wakati akiegesha lile gari mahala pake. Wakateremka na kutoka nje ya uwanja, Scoba hayupo.

Kamanda Amata daima alikuwa akimpenda Scoba kutokana na akili ya ajabu aliyoumbwa nayo, nah ii ndiyo siri kubwa ya mwanaintelijensia. Kwa kutomwona pale, hakushangaa wala kuogopa kwa sababu kwanza kama ni kutekwa,

kwao ni jambo la kawaida maana hata wakati mwingine yabidi kujifanya mjinga ili utekwe na kuingia kirahisi kwenye ngome ya adui. Hakuwa na wasiwasi alijuwa tu kuna mja kati ya hayo yametukia.

Kumbe mara baada ya jamaa hao kumwacha Scoba pale maegeshoni, yeye akaona hapana, kama ni kujua kuhusu hao jamaa kuna upande ambao utakuwa na *back door* ya kufanya wanayotaka.

Akawasha gari na kuelekea uwanja wa zamani yaani Terminal II. Alipofika moja kwa moja akaegesha gari lake na kufanya kama anasafisha hapa na pale na kuliweka gari hilo katika hali nzuri. Dakika kama ishirini baadae akashuhudia ule mdege ukiwa hewani unatokomea. Hakushtushwa na hilo, akaendelea kusafisha gari lake huku akipiga mruzi kufuatisha wimbo wa Labamba.

‘Para baila labamba…”

Scoba akasikia sauti ya kike nyuma yake ikiimba wimbo huo huo, akashtuka na kusimama wima huku akivuta shati lake chini kidogo maana mgongo ulikuwa wazi. Macho yake yakagongana nay a mwanamke wa kizungu aliyebana nywele zake za blonde kisogoni, usoni mwake alivalia miwani ya jua na suti yake nyeusi ilimpendeszesha kama mhudumu wa ndege.

Mkononi mwake alikuwa na kijibegi cheusi kidogo chenye magurudumu.

“Mh! You have nice voice enh!” Scoba akamchoza kwa kumsifu kuwa ana sauti nzuri.

“Yeah, Im musician… by the way can I use your tax?” Yule mwanamke akamjibu na kumwambia kuwa yeye ni mwanamuziki, zaidi ya hapo akamwomba huduma ya taksi.

“Bila shaka!” Scoba akajibu na kumfungulia mlango mwanamke huyo.

“Wapi destination yako?” akamuuliza.

“Double Tree Hotel,” Yule mwanamke akajibu huku akijiweka vizuri kwenye kiti cha nyuma. Mara simu ya Scoba ikaita, aiakainyakuwa na kuiweka sikioni.

“Nina mteja, nitafute baadae!” akakata simu na kuondoa gari kuelekea mjini.

Kamanda Amata akamtazama Chiba, “ana mteja!” akamwambia.

“Mteja?”

“Nimemwelewa, kuna ishu, hebu mcheki …” Amata akamwambia Chiba, naye akachukua kifaa chake mfano wa simu, akalitafuta gari la Scoba na kuingiza kodi maalumu za

utambuzi. Sekunde chache tu kile kifaa kikaonesha kuwa Scoba yupo eneo la Kipawa akielekea mjini.

"Anaenda mjini," akajibu.

"Ok". Amata na Chiba wakavuka egesho la kwanza na kufika la pili, hapa wakaingia kwenye gari moja aina ya BMW jeusi. Haya ni magari maalumu ambayo TSA wameyaweka katika maeneo maalumu kwa ajili ya usafiri wa haraka au wa kujificha

inapobidi. Amata akakaa nyuma ya usukani na mkono wake wa kushoto akaketi Chiba, safari ikaanza. Baada ya mwendo mkali na ovateki za maana sana katika Barabara ya Nyerere, wakalifikia gari la Scoba na kulipita. Hawakuwa na haja ya kulifuata bali kumpa ishara tu ambayo yeye angejua maana yake nini. Kamanda Amata akalipita gari la Scoba na kuingia mbele yake huku akipiga honi kali. Scoba akaelewa maana alilijua gari hilo,

akashika kioo cha dereva cha ndani na kukiweka vizuri kikimtazama mwanamke yule.

Ndani ya gari alilokuwamo Chiba na Amata, wakapata ishara maalumu, Chiba akawasha runinga ndogo iliyo katika dashboard ya gari hilo na moja kwa moja ikaonesha picha mubashara ya mgeni Yule aliye ndani ya gari la Scoba. Katika kioo cha ndani katika magari haya yanayotumiwa na TSA

kulifungwa kamera ndogo sana ambazo huwezi kuziona kirahisi. Na hizi zilizweza kupeleka picha katika gari nyingine ndani ya mita mia moja tu.

“Umemng’amua?” Amata akauliza.

“Bila shaka! Huyu ni yule mwanajeshi aliyebaki,” Chiba akajibu.

“Fanya crossmatch ya picha uliyopiga uwanja wa ndege na hii ya sasa tujue kama ni yeye na ni

nani zaidi kisha tujue kwa nini amebaki wakati wenzake wameondoka," Amata akamwambia Chiba.

"Halafu Chiba, usiku wa leo tuna kazi ngumu…"

"Kazi ngumu?" Chiba akauliza.

"Ndiyo lazima twende mpaka kwenye *door of heaven*…"

"Kivipi?"

“Chiba, ushasahau nini umenambia mchana huu… Dassen Keputo, yaani huyu leo lazima ajulikane, tunaenda kufukua lile kaburi tuone nini kipo ndani…”

“Kamanda kufukua makaburi ya watu tunahitaji vibali…” Chiba akasema.

“Ah! No, tupo kwenye uchunguzi, tutachukua kibali cha haraka, Madam S anajua atafanya nini, ila usiku huu lazima

tukachimbe tupate kuwa kuna nini kimezikwa hapo," Amata akaeleza wakati Chiba akiegesha gari nje ya afisi ya Madam S, *Ofisi Ndogo*.

* * *

CAPE TOWN

Margaritha Casbarai, alijikuta hana la kusema, kama kuna mwaka ambao kwake ulikuwa mgumu ni huu, kama kuna mtu ambaye aliwahi kukiumiza kichwa chake ni huyu wa sasa, na

alimjua kwa jina, Amata Ric. Akainua uso wake na kuwatazama watu waliokuwa mbele yake, wanaume watano walioshiba kimazoezi, wote walikuwa ndani ya suti nyeusi.

"Mpo tayari?"

"Yes Madam!" wakaitikia.

"Mkapokee mwili wa The Cobra na mfanye utaratibu wetu ule ule wa kuzika, Mc Cain keshasema tuendelee na taratibu zetu kule kisiwani lakini

amesisitiza kuwa ulinzi wa kisiwa uimarishwe mara mia hata sisimizi asiingie," akawaambia.

"Umesomeka Madam!"

Vijana wale wakaondoka na kumwacha mwanamama huyo katika lindi la mawazo, saa kwake hazikuwa zikienda kabisa. Juu ya meza iliyo mbele yake kulikuwa na picha mbili za Kamanda Amata. Alikuwa akitamani kuzichana na kuzitupia kwenye

moto, lakini haikusaidia kuwa ndiyo kamuua kiumbe huyo.

Who is this? Lilikuwa ni swali ambalo alitamani sana kupata jibu lake lakini hakufanikiwa, akabaki kinywa wazi kwa mbutwao. Sekunde kadhaa simu yake ikaita, akainyakuwa na kuiweka sikioni.

“Mmefika? … sawa, moja kwa moja kisiwani,” akaijibu simu hiyo na kuikata. Kisha akabofya

namba fulani na kuirejesha tena sikioni.

"Vipi? Umeshamweka kwenye target?" akauliza.

"Bado, ndo namsaka lakini haitachukua muda nitamtia mkononi…" sauti ya upande wa pili ikajibu.

"Ok, Bih! Hakikisha unatumia mbinu ile ile niliyokwambia, na ukifanikiwa tu usipoteze tone la sekunde," akamsisitizia.

"Yes Mom!" akajibu na ile simu ikakatwa.

"Aaaaaaaiiiiiggggghhhhhhhhhhhh !!!!!!" Margaritha akapiga unyende wa hasira huku akiuma meno na kujitupa kitini. Mikono yake ikachakurachakura nywele zake nyeupe na kuziacha timtim. Dakika hiyo hiyo mlango ukafunguliwa na vijana wawili wakaingia haraka na kusimama mbele ya huyo mama wakiwa

tayari na bunduki mikononi mwao.

“Vipi mama?” wakauliza kwa pamoja.

“Oh! Endeleeni na kazi hakuna chochote hapa!” akawajibu, nao wakatoka na kuelekea nje kuendelea na ulinzi wa jumba hilo.

* * *

Mwanzo wa usiku wa siku hiyo ulimkuta Kamanda Amata pamoja na Chiba afisini kwa

Madam S, jirani kabisa na jengo la hazina, jijini Dar es salaam. Kikao cha mpango mkakati kilikuwa kikiendelea ndani ya afisi hii.

"Sasa, kwa mara nyingine Rais anataka kuunda tume mpya ambayo itakaa mezani na wale jamaa kufikia muafaka. Inaonekana kuna mgogoro mkubwa ambao umepelekea EU kuiwekea vikwazo vya kiuchumi Tanzania ikiwemo kukata

misaada yote na miradi inafadhili kuisitisha…" Madam S akawaambia vijana wake.

"Kila siku tunaunda tume tu…."

"Ndiyo, ila kwa sasa mzee amechanganyikiwa kabisa, ameamua tu kuwaachia hao majasusi ili amani irudi, hakuna jinsi…" Madam akaeleza.

"Wewe unaafikiana na hilo?" Chiba akauliza.

“Nitafanyaje sasa? Kila mtu imebidi atulie atii kauli ya Rais, kwa hiyo atatangaza muda si mrefu nani na nani wapo katika timu hiyo kisha mkutano utaandaliwa. Mara hii kutakuwa na mpatanishi kutoka EU ambaye ana uzoefu wa hali ya juu katika kutatua migogoro kama hii…”

“… Madam S, unamfahamu Peter Simbaulanga?” Amata akampiga swali Madam S.

Badala ya kujibu, Madam S akabaki amkimtolea macho kijana wake, “we umemjulia wapi?” akamuuliza.

“Nijibu!”

“Ninamjua, huyu ndiye alikuwa mkufunzi wa maswala ya kiupelelezi, huyu bwana alitumwa na Mwl. Nyerere kwenda Afrika ya Kusini kama sijasahau mwaka 1982 na mnamo ’83 tukapata taarifa kuwa amefariki…” Madam S akaeleza.

“…mmemzika wapi?”

“Mbona maswali mengi sana Kamanda?” HOT akajibu kwa swali.

“Madam S, Mzee Simbaulanga, hajafa!” Kamanda akasema.

“What?!!!”

“Kati ya wanausalama wa Tanzania ambao walipambana vikali katika vita vya ukombozi, na makaburu wakawaaminisha kuwa wamekufa, huyu ni mmoja

wapo… lakini Madam amini usiamini, watu hawa wapo hai akiwemo Simbaulanga!" Kamanda akaeleza.

Ukimya ukatwaa nafasi kati ya watatu hao, Madam S akaendelea kuwatazama vijana hao kwa zamu.

"Kwa hiyo mnataka kusemaje?" akawauliza.

"Tunataka tukawarudushe ama wakiwa hai au masanduku yao!" Amata akajibu, "na hii ndiyo

itadhihirisha uongo wa makaburu hawa, wanao watu wetu, na watu wenyewe ndiyo hawa!" Akaweka picha mezani. Zilikuwa picha ndogo ndogo saba, kwa kuzitazama tu Madam S akawatambua watu hao kasoro wawili, akasogeza kando picha hizo tano na mbili akaziacha mezani.

"Mbona umezitenga?" akauliza.

“Hizi tano, ninazitambua, na hawa watu ninawajua vyema, nakumbuka bado nilikuwa mchanga katika mambo haya nilipokutana mara kadhaa na sura hizi kwenye maofisi tofauti ya serikali. Ila hawa wawili siwajui kabisa yaani…” akaeleza.

“Sawa, sasa wakati kaburu anatushinikiza kuwapa watu wake na sisi tunadai watu wetu, na ndiyo hawa, wanao na wamewaweka chini ya ulinzi wao,

hatujui wanalishwa nini au wanaishije…. We need them!" Amata akamwambia Madam S.

Kamanda Amata akahamisha macho yake kutoka kwa Amata kwenda kwa Chiba, "na wewe unasemaje?" akamuuliza.

"Kuna siri moja tu ambayo imebaki, tukiitangua tu… tunaenda kuwarudisha nyumbani…" Chiba akasema.

"Siri. Siri gani?"

“Dassen Keputo!!” Chiba akajibu.

“Dassen Keputo? Mbona vijana mnanipeleka puta namna hii ina maana mlikuwa mnafanya kazi kimya kimya?” Madam akapiga swali.

“Niliona nisikwambie kwanza, ili nipate uhakika na kile nilichopata, hata hapa tumekwambia muda ulikuwa bado ila tu kuna jambo lazima

tukuhusishe ndo maana tumekuja!" Amata akasema.

"Lipi?"

"Usiku huu kuna kaburi lazima tukalifukue," Chiba akajibu.

"Kaburi? 'nyi tangu lini mmeanza kufukua makaburi?" Madam S akauliza kwa shauku.

"Ndiyo hii leo tunataka kwenda kuanza…"

"Sasa mnahitaji nini kwangu?" akawauliza.

“Tunahitaji kibali…”

SEHEMU YA 28

“Sawa, tutakwenda wote, habari hii imenivutia sana lazima nishuhudie nini kilizikwa kama mnavyodai ninyi,” akawaambia, “haya tukutane saa ngapi na wapi?”

“Saa sita usiku, Mikocheni B pale stendi, kisha tuingie kule makaburini,” Amata akasema.

“Sawa, sikuwahi kujua kama nyuma ya hili kuna habari nzito

namna hii… basi watapata tabu kama walijua hili ni shamba la bibi," Madam S akawaambia vijana wake. Dakika hiyo hiyo kengele ya mlango ikalia.

"Gina!" akasema, na aliporuhusu mlango ule ufunguke, hakuwa amekosea, mrembo huyo akaingia ndani na kukaribishwa, "umepona sasa?"

"Yes Mom!"

"Good! Kaa tayari, muda wowote kazi…" Madam

akamwambia Gina naye akaitika kwa kichwa. Amata na Chiba wakanyanyuka tayari kuondoka, bosi wao akawaruhusu na kubaki na Gina pekee.

Nje ya afisi hiyo, Amata akamwambia Chiba, “tumtafute Scoba tujue kuhusu ule mzigo!”

“Yap, ni la maana sana,” Chiba akisema hayo simu yake ikaita, akaicheki.

“Duh!”

“Vipi?”

“Hakika ukimsema shetani utamwona mkia, Scoba anapiga…” akasema.

“Nenda hewani,” Amata akampa nafasi.

Chiba akaiweka simu yake sikioni huku akiwa keshaifyatua tayari kwa kusikiliza.

“Tuonane Club Santiago, Sinza kabla ya saa tatu usiku!” ile simu ikasema hayo na kukatika. Chiba akampa Amata ujumbe ule naye akaunga mkono safari ile. Amata

alipotazama saa yake ilikuwa inakimbilia saa moja usiku.

“Na sasa ile kazi tunaifanyaje?” Chiba akauliza.

“Ipi?”

“Si ya kuchimba kaburi…!”

“Unajua nilikuwa nafikria kitu hicho hicho, hatuwezi kukodi mtu, lazima tuchimbe wenyewe…” Amata akasema.

“Sawa, swali ni kuwa pale kuna nyumba ya mlinzi sijui

mchungaji, si watashangaa watu usiku tunachimba kaburi, watajua vigagula!" Chiba akatia shaka.

"Usemalo ni kweli … lakini *halothene* itahusika…"

"Oh yes! Nimekupata," Chiba akajibu huku akiwasha gari na kuliingiza barabarani kwa kasi.

12

KISIWA FULANI HUKO AFRIKA KUSINI

Moto uliendelea kuwaka kwa kasi ukiendelea kuteketeza mwili wa The Cobra na Jesca. Kando ya moto huo kulikuwa na watu kama ishirini hivi wakitazama tukio hilo la kusikitisha. Mtandao huu wa WP walijiwekea taratibu ya kuchoma miili ya watu wao ambao watakufa katika harakati za kumpigania mtu mweupe. Dakika thelathini baadae, moto ule ukatulia, na tayari hakukuwa na alama ya mtu huyo isipokuwa jivu tu.

“Hash to hash!” Margaritha akatamka na wote waliokuwa hapo wakatawanyika na kuingia ndani ya jengo fulani lililojengwa katika kisiwa hicho. Upande wa pili wa jengo hilo kulikuwa na shamba kubwa sana, lenye miti machaka ya hapa na pale na kwa mbali ungeweza kuona gofu la nyuma iliyobomolewa zamani kidogo.

Ndani ya jengo hilo zuri kulikuwa na samani za kawaida

kabisa, watu hao waliketi katika mtindo wa duara kana kwamba wana kikao fulani. Nje ya jengo hilo na kuzunguka kisiwa hicho kulikuwa na ulinzi mkali wa binadamu na mbwa waliopewa mafunzo maalumu.

"Taarifa nilizozipata ni kuwa Tanzania imesalenda," Margaritha akawaambia wale watu na wote wakapiga makofi kushangilia hatua hiyo, "kwa hiyo kaeni tayari kuwapokea

wapiganaji wetu ambao ni miaka mingi sana wameshikiliwa ndani ya nchi hiyo," akamalizia kusema.

"Hakuna mkate mgumu mbele yachai!" mwingine akadakia na wote wakacheka kwa sauti.

"Kwa hatua hii, mapambano na wao yamefika mwisho, tutaunda timu ambayo itakutana na ile ya Tanzania na mpatanishi atatumwa kutoka EU kwa ajili ya kusimmamia mazungumzo hayo," akawaambia, kisha

mazungumzo ya hapa na pale yakafuatia. Muda huo huo watu wawili wakaletwa; mmoja mwanaume na mwingine mwanamke, hawakuwa wengine bali Parrot na Kermikov.

“Hawa mnaowaona ndiyo watu hai ambao wamewahi kupambana na huyo jamaa wa Tanzania, sijajua uwezo wake lakini tutaujua kupitia hawa…” Margaritha akauambia mkutano. Wajumbe wote ndani ya chumba

hicho wakawakodolea macho watu hao.

“Unataka kutuambia nini?” mjumbe mmoja akauliza.

“Tumefanya kazi yetu ipasavyo, lakini safari hii kumetokea kikwazo, Jesca tumemchoma leo, yeye aipambana na mpelelezi kutoka Tanzania lakini hakufanikiwa kumshinda, The Cobra nyote mnamjua, mtu mzima huyu kaanza harakati hii miaka mingi

sana na aikuwa na ujuzi mkubwa sana wa kimapambano, lakini amefei mbele ya huyu shetani. Parrot kapambana naye lakini ndiyo kama mnavyomuona, miguu yake haina kazi. Kutoka makao makuu kule Prague wakatuletea mtu huyu, Kermikov, nyote mnamjua, lakini kajikuta akishindwa kufurukuta. Sasa hiki ni kikwazo, hata kama watatupatia watu wetu, lakini huyu shetani lazima aondoshwe…" mwanamama

huyo akawaambia huku akiweka picha ya Amata mezani. Kila mmoja katika jopo lile akaitazama, na ilipofika kwa mjumbe mmoja mtu mzima ambaye hata kichwa chake kilikuwa na nywele nyeupe za kuhesabika, akashtuka kidogo, akaitazama vyema picha ile kisha akatikisa kichwa na kumpatia wa kando yake.

"Mr. Frank, whats wrong…?" Margaritha akamuuliza mzee

huyo kuna shida gani, maana alimuona jinsi anavyoishangaa picha ile.

"I know the person! I know him…" *namjua huyu mtu! Namjua*…

"How?" *kivipi?* Margaritha akauliza huku wengine wte wakimkodolea macho.

"Huyu niye aliyesambaratisha mtandao wa Robbinson Quebec akamuua Don Angelo na Robbinson mwenyewe! Huyu

jamaa ndiye aliyesambaratisha harakati za siri za kuipindua Serikali Tanzania miaka ileeee ambayo bmtandao hatari wa Kireno uijikuwa ukiitumia Mozambique kama sehemu byake ya kupanga njama hizo…. Ni huyu! Sasa kama ameingia kwenye hii kazi yetu nawsema ukweli, Tanzania si wajinga kukubali kutugea hao watu, hapa kuna kitu te si kidogo…" Mzee huyo akaeleza kinagaubaga juu ya Amata.

“Na anaitwa nani?”

“Namtambua kwa jina la Mr. Spark na si vingine, ila sura yake haiwezi kunitoka kwa mambo aliyoyafanya ndani ya kasri la Don Angelo… ni mtu hatari sana, mwenye werevu wa hali ya juu, mwenye akili inayotambua jambo kabla halijatukia. Mtu kama huyu angekuwa CIA lakini yupo huko Tanzania, si ajabu tunaongea hapa kumbe yupo chumba cha pili…” akasema na

wote wakageuka upande wenye mlango wa kuingia hicho chumba cha pili, kitete.

"Code 005" Margaritha akanong'ona kisha akabaki kimya.

Mipango ya kazi ikapangwa, kila mmoja akitakiwa kuimarisha ulinzi na weledi wa kazi katika idara yake, kuhakikisha wananasa kila taarifa au simu zinazopigwa kwa namba ya Kamanda Amata, na kwa kuwa walikwishamwacha

mtu kwa kazi moja tu ya kumtupia jicho kijana huyo walisubiri tu kupata taarifa mara baada ya kuonekana.

"Mmefanya vizuri kutuma mwanamke, sasa mjue kuwa udhaifu mkubwa wa mtu huyu ni wanawake, anapenda sana wanawake na ndiyo ulemavu wake mkubwa, sasa inabidi kuutumia udhaifu wake kummaliza…" Mr. Frank akaeleza mkutano.

“Aaaaa ina maana unataka Bih amnase huyu mtu kimapenzi?” Margaritha akamwambia.

“Yes, hiyo ndiyo mbinu mahsusi, akishamtia mkononi kazi imeisha… hakuna mwanaume mjanja mbele ya umbo zuri la mwanamke hasa mwanamke huyo awe Bih!” Mr. Frank akasema na wengine wote wakacheka.

“Bado nahitaji kupambana naye!” Kermikov akatamka na jopo zima likamtazama.

“Sure?”

“Yes!” akajibu.

“Sawa, anza mazoezi makali na ndani ya siku hizi nne utarudi Tanzania,” Margaritha akamwambia.

“Nooo!” Mr. Frank akakana, “Siku nne ni nyingi sana Margaritha, huyu mtu si mjinga kusema kuwa saa hii amelala

anasubiri au anasema kamaliza kazi, la; huyu mtu yupo kazini, si ajabu Bih yupo Dar, nay eye yupo South Africa, si mtu wa mchezo, narudia tena, si mtu wa mchezo, kama Kermikov anasema atapambana naye, anatakiwa aondoke sasa, kuweka mwili fit atafanya huko huko!" Mr. Frank akaeleza kwa msisitizo huku wengine wakionekana kuunga mkono hoja hiyo.

Mkutano ukaendelea kama saa nyingintatu hivi na maazimio yakawekwa ikiwa ni mkutano wa tume za upatanishi utakaoongozwa na mpatanishi kutoka EU ufanyike Cape Town. Hii ilikuwa ni mbinu ya kumvuta Amata kwani walijua wazi kuwa mtu huyo lazima atakuja kwa siri, hivyo wakahakikisha wanaimarisha watu wao na kuwaweka mguu sawa, kuanzia viwanja vya ndege, bandarini, vituo vya treni na mabasi,

kwenye viwanja vya helikopta za kukodi, mahotelini na kila kona kwamba huyu jamaa yaani Amata, akionekana popote ashughulikiwe.

* * *

DAR ES SALAAM

7:20 Usiku

Kazi nzito ilikuwa ikiendelea katika makaburi ya Mikocheni, Chiba, Amata na Scoba walikuwa bize, mashati wametundika pembeni, majembe mikononi,

kaburi la Dassen Keputo lilikuwa taari limechimbuliwa futi nne na nusu. Kazi hiyo ilifanyika kimyakimya, hakuna aliyekuwa akiongea na mwingine. Madam S alikuwa ameketi ndani ya gari, nje ya uwanja huo, kazi yake kubwa ilikuwa ni kuangalia kama kuna hatari yoyote katika eneo hilo, ni yeye tu aliyekuwa akizungumza na vijana hao, na wao hawakutakiwa kujibu. Waliweza kumsikia mama huyo kupitia vinasa sauti maalum

walivyovipachika masikioni mwao. Utaratibu waliojiwekea ni kuwa Kamanda Amata atatoa taarifa btu pindi wakifika mwisho wa kazi hiyo.

Jirani na makaburi hayo, kulikuwa na kanisa, si kubwa sana, lakini lilikuwa halitumiki mara kwa mara. Wenyeji wa eneo hilo walithibitisha kwamba kanisa hilo hufunguliwa mara chache sana, na hata waumini wake si Waafrika, wengi ni Wazungu.

Pembeni ya kanisa hilo, kulikuwa na nyumba ambayo ilikaliwa na familia moja ya Kiafrika ijapokuwa wenyeji walithibitisha kuwa watu hao si Watanzania.

Majira ya saa nane hivi, walifanikiwa kufika pale wanapopataka, jeneza la mbao ngumu, lililala ardhini.

“Tumefika!” Amata akatamka, na neno hilo likafika kwa Madam S.

"Fungua hilo jeneza, unambie kuna nini ndani," akamwambia.

"Yes mom!" akamjibu na kazi a kufungua sanduku hilo ikaanza. Haikuwa kazi ndogo kuweza kuondoa mfuniko huo, lakini baadae wakafanikiwa. Kila mmoja alijikuta moyo ukimwenda mbio, kabla ya kuuondoa mfuniko huo.

"Moja, mbili, tat…." Wakauondoa mfuniko, kisha Scoba akawasha tochi kubwa

iliyoweza kuangaza vyema ndani shimo hilo. Walichokiona, hawakukitegemea na walichokitegemea hawakukiona. Ndani ya jeneza lile hakukuwa na mwili wa mwanadamu wala mnyama yoyote. Chini palikuwa na mbao safi ya mpingo iliyoonekana wazi na pembeni yake palionekana kitasa kama cha mlango.

“Mlango!” Amata akasema, kisha akawatazama wenzake.

"Mlango!" Madam akashangaa.

"Yes, kuna mlango," Amata akasema.

"Fungua, nakuja, lazima tujue nini mwisho wa yote!" Madam akajibu.

Mlango ule ulikuwa umefungwa barabara kabisa, kila ulipotikiswa haukutikisika. Mbinu zote zikatumika, wapi. Wanaume hawa watatu, walijikuta wakitota jasho na huku muda unaenda. Madam S, tayari alikuwa amefika

katika kaburi hilo, akabaki kinywa wazi. Amata akamtaka kuteremka ndani ya shimo hilo, akafanya hivyo.

"Inabidi tuvunje hii mbao," Amata akamwambia Madam.

"Kwanini?"

"Tumekosa mbinu ya kufungua, sasa tufanyeje?" Kamanda akauliza.

"Hebu sogea pemnei kidogo," Madam S akamwambia Amata kisha akainama pale kwenye lile

jeneza, “Mulika hapa hivi!” akamwambia Scoba naye akafanya hivyo, “mmmmmmmhhhhhhh!!!! Yes, here it is!” akatamka. Wote wakakusanyika na kutazamaa nini ambacho mwanamama huyu amekigundua. Madam S akakamta kile kitasa, akakikandamiza ndani na kukisukuma taratibu kwenda juu kisha akakivuta nje, kikafyatuka na ule mlango ukafunguka kwa kutumbukia ndani. Wote

wakatazamana, kisha wakamwangalia boss wao.

"Hili sio kaburi!" akawaambia.

SEHEMU YA 29

"Yes, tangu lini kaburi likawa na mlango…" Amata akaongeza.

"Muda unakwenda, tuingie ndani yake tuone kuna nini!" Madam S akawambia vijana wake. Amata, Chiba na Scoba wakajiweka sawa, bastola mkono mmoja, tochi mkono mwingine, Amata akatangulia, Chiba

akafuata, Scoba akamalizia huku wakimwacha Madam S pale pale shimoni. Ile ngazi iliteremka na kisha ikaanza kwenda tambalare. Watatu hawa walitembea katika sakafu safi ns kuufikis mlango mwingine tena, kana kwamba wabaingia ndani ya chumba kingine.

“Tumekuta mlango!” Amata akasema. Nje, Madam S akasikia ujumbe huo.

“Fungua na uingie ndani, hakikisheni hakuna kamera zinazowaona,” akawaambia.

“Yes mom!” Amata akajibu kisha wakauchezea mlango huo kwa namna wanayoijua, ukafunguka. Kwa ishara ya vidole, Kamanda akawapa ishara kuwa yeye anaingia, na Chiba amfuate, Scoba abaki hapo ahakikishe usalama wao. Wakaafikiana, wawili, wakaingia mpaka ndani, kilikua chumba

kidogo, chenye kabati moja lililojaa kabrasha anuai. Meza na viti vitatu vilikuwa hapo, juu ya meza hiyo kulikuwa na ramani kubwa ya Afrika Kusini, kisha eneo la Cape Town lilizungushiwa mduara mwekundu, na mstari mwingine ukatoka kwenye duara lile na kufika mpaka kwenye moja ya kisiwa, nacho kikazungushiwa duara kama lile, na pembeni kukachorwa alama ya jicho.

Amata akatazama kwa makini ramani ile, akamwita Chiba, naye akaitazama, kisha akatoa simu yake na kupiga picha pale kwenye lile jicho, akaingiza kwenye mtandao wake wa utambuzi na kusubiri kidogo. Ndani ya chumba hicho, hawakuwa wakiongea kwa sauti, ishara za mikono tu zilikuwa zikitumika. Chiba akaliendea kabati hilo, na alipshika kitasa cha mlango wake na kukinyonga, kabati zima likahama na kuacha uwazi

mkubwa tu. Kamanda Amata na Chiba wakabaki wameduwaa kwa kuona chumba kikubwa kabisa cha mikutano na masanduku kadhaa yakiwa yamejengewa ukutani.

"TSA 1!" Madam akaita.

"HOT, HOT," Amata akaitikia.

"Nipe ripoti!"

"Maktaba ndogo na ukumbi wa mikutano, pia ni kama treasury hapa, kuna masanduku

yamejengewa ukutani na sijui yana nini ndani," Amata akasema.

"Sawa, chukua vya muhimu tu, uje nje kisha tutafunga eneo hili kwa uangalizi zaidi," Madam S akatoa amri.

"Copy!" akajibu na kumpa ishara chiba. Aliprudi mahala ambapo amemwacha Chiba yaani kwenye mlango ule ambao kwa nyuma ni kabati, akamkuta kakamata kitabu kimoja chanye

jalada gumu jekundu juu kimeandikwa ‘DASSEN’.

Wakakusanya na ile ramani kisha wakatoka mpaka walipmwacha Scoba na kwa pamoka wakatoka nje mpaka shimoni kwa Madam S.

“Vipi?” Madam akauliza. Amata akaitazama saa yake na kumtazama Madam S.

“Evacuation time!” akajibu.

Haraka haraka wakafunga lile sanduku, na kutoka nje ya shimo.

Wakatazamana baada ya kugundua kuwa muda walio nao na kufukia havilingani.

“Tutumia saa moja na nusu kufukia, tutakapofikia tuache hapo,” Madam akawaambia na vijana hao wakaanza kazi mara moja. Kwa kasi waliokuwa wamakwenda, dakika tisini zilipokamilika, walikwishafukia robo tatu ya shimo.

“Stop!” akawaamuru, wakaacha, akawapa ishara

wakaingie garini, wakafanya hivyo. Muda kidogo naye akafuatiaAlipoketi kitini na kushusha pumzi ndefu akawatazama vijana wake waliokuwa na vumbi mpaka kwenye kope, akaanza kucheka.

“Unacheka nini?” Chiba akauliza.

“Mmefanana na vinyago,” aliposema hayo wote wakacheka tena. Saa ya kwenye gari ilionesha saa kumi na robo alfajiri.

“Sasa tupawekee ulinzi au?” Chiba akuliza.

“Hapana, tuache ii watu wakija asubuhi watajua ama majambazi yamechimba kuchukua vitu vya thamani au wachawi…”

“Dah! Asee Madam una akili za haraka sana, sikufikiri kabisa jibu kama hilo,” Amata akasema wakati huo tayari, Madam S keshaondoa gari na kuliacha eneo hilo pekee. Muda waliokuwa wakifanya kazi ile, ulikuwa

sambasamba kabisa na ule ambao kule Cape Town kulikuwa kukiendelea kikao kile kizito.

HOTELI YA DOUBLE TREE

Alfajiri ya saa kumi na moja simu ya Bih ikaita, akainyakua kivivu kutokana na usingizi uliombeba kitoto.

“Yes!” akaitika.

“Saa tatu asubuhi mpokee Daniel Kermikov mtafanya kazi naye pamoja

katika kutimiza jukumu lenu," simu ile ikamwambia.

"Copy!" akajibu na kuiweka kando, kisha akaendelea kuchapa usingizi kana kwamba kaja nchini kwa likizo ya utalii.

Bih aliamka saa kumi na mbili asubuhi na kujiweka tayari kwa mazoezi ya viungo, dakika chache baadae alikuwa barabarani akifanya jogging. Mwanamke huyu mwenye mwili wa kawaida sana yaani si mnene

wala si mwembaba, alikuwa fiti kimazoezi, mwanajeshi ambaye anafanya kazi karibu sana na 'The daughters' wanawake nhatari sana chini ya Mama Margaritha Casbarai. Mwanamke huyu alipewa majukumu kadhaa ya kutekeleza akiwa Tanzania na alipangiwa muda maalumu wa kumaliza kazi hiyo.

Upande wa pili wa barabara hiyo, umbali kama wa mita mia tatu hivi Gina alikuwa katika

baiskeli akiendesha taratibu kuelekea mkabala na mwanamke huyo. Miwani yake aliyoivaa ilikuwa na uwezo mkubwa wa kunasa picha. Walipopishana, ikamnasa mwanamke huyo vyema kabisa, lakini kila mmoja akaendelea na hamsini zake. Mwendo mfupi mbele akaegesha basikeli yake kando ya gari moja aina ya Mazda, pick up, akateremka na kuinua baiskeli yake aakitupia nyuma kisha yeye mwenyewe akingia ndani ya gari

hilo na kuketi nyuma ya usukani. Taratibu akingia barabarani na kuelekea upande ule ambao Bih alielekea. Kutokana na mwendo wa gari hilo, akampita Bih njiani nay eye kuendelea na safari mpaka katika hoteli hiyo ya Double Tree, akaingia katika maegesho na kuteremka haraka na kuingia kwenye gari nyingine aina ya Subaru yenye vioo vya tinted, akatulia ndani akifuatilia kila kitu.

Bih aliwasili hotelini na kuingia ndani, dakika kama thelathini baadae akatoka tena nje, mara hii akiwa vingine kabisa. Gauni jepesi lililotanguliwa na leya iliyozuia maungo yake kuonekana, lilimkaa vyema mwilini. Miwani ya giza ikayaficha macho yake, akatzama saa na kuingia ndani ya gari, kisha gari lile likaondoka kwa kasi. Gina akawasha gari lake na kuingia barabarani kumfuatilia mwanamke huyo.

* * *

Saa tatu asubuhi, Kermikov aliikanyaga tena ardhi ya Tanzania kwa mara ya pili. Safari hii sifanyi makosa! Akawaza huku akivuta hatua kuelekea eneo la kudikia wageni, akafanya taratibu zote za kiuhamiaji, maswali mawili matatu kutoka kwa afisa uhamiaji wa eneo hilo yakatosha kabisa kumfanya mgeni huyo kuingia nchini. Nje ya uwanja akalakiwa na Bih kwa

bashasha, hatua kwa hatua mpaka kwenye gari, wakaingia ndani.

Gina akashusha kamera yake baada ya kupata picha kadhaa za mgeni huyo, huku moyo ukimwenda mbio, akachukua simu yake na kupiga upande mwingine, kisha akasubiri kimya kujibiwa.

"Ground zero… nakusikiliza…" upande wa pili ukajibu. Gina

alielewa nini maana ya neno hilo, hakujali akaendelea.

"Terminal two, jamaa amerudi, narudia, jamaa amerudi!" akasema.

"Amerudi?"

"Yes! Amerudi, amepokelewa na huyu mwanamke," akazidi kueleza.

"Ok, abort mission, return to Ground Zero…" sauti ya upande wa pili ikajibu. Gina akazima simu na kuwasha gari akaondoka

na kuuacha, uwanja huo, akatekeleza lile aliloambiwa.

* * *

SHAMBA

Katika meza ya duara, Kamanda Amata akashusha simu yake na kuiweka mezani.

“Nani karudi?” Madam S akauliza.

“Daniel Kermikov!” akajibu.

“Siku mbili tu zimemtosha kupona?”

“Nafikiri…. Badi ninamkaribisha tena nchini, safari hii atazikwa Mwanayamala na dunia haitajua nini kimempata,” Amata akazungumza.

“Hapana, hatuna muda wa kuzika wafu, huyu tunamkamata mzima mzima yeye na huyo mwanamke kisha tunawatia ndani bila mtu kujua, watakufa taratibu,” Madam S aakamwambia, nukta hiyo hiyo, Chiba akaingia ndani ya chumba

hicho akiwa na makabrasha kadhaa, akaketi na kuyaweka mezani.

"Kitendawili kimeteguka!!!!" akawaambia huku akionekana mwenye furaha kupita kawaida. Maneno yake yakawatia shauku Amata na Madam S kusikia.

"Tunakutegemea, tupe jibu," Madam akamwambia.

"Dassen Keputo, nimeshamjua…" akawatazama wenzake.

“Sema sasa!!!!”

“Hili jina si la mtu, ni majina ya sehemu mbili tofauti zenye mahusiano ya karibu, na nahisi ni maeneo nyeti ya WP ndiyo maana wakayazungushia maduara kwenye hii ramani…”

“Enhe!”

“Hili eneo hapa (akaonesha kwenye ile ramani) ni kisiwa, hiki kisiwa kinaitwa Dassen, yaani Dassen Island kwa mujibu wa tafutishi zangu. Lakini kuna eneo

jingine tena nje ya Afrika linaitwa, Dassen, sasa hii Keputo ni kutofautisha maeneo haya. Dassen wanayoitaja hawa na ambayo imezungushiwa hili duara ipo Afrika Kusini…"

"Aaaaaahhhhhh Dassen Island, ya Afrika Kusini, Cape Town!!!" Kamanda Amata akadakiza kauli ya Chiba.

"Yes! Keputo ni kificho cha Cape Town… kwa hiyo ni Kisiwa cha Dassen katika Jiji la

Cape Town… TSA, kazi imeisha!" Chiba akamaliza na kuliendea jokofu akatoa Coka baridi na kujimiminia kinywani yote kabisa.

"Siri yote imezikwa Dassen keputo!" Kamanda Amata akasema.

"Kwa nini unasema hivyo?" Madam S akauliza.

"Ni ujumbe ambao nimewahi kuupata siku kadhaa nyuma, na ndiyo uliyonisukuma kufanya

ufukunyunyu mpaka kufikia hapa, serikali na vyombo vyetu vya usalama vilichukulia swala hili kwa wepesi sana, lakini mimi sikuchukulia hivyo, nililipa uzito mkubwa sana. Hii ni Cold War Madam, kumbuka watu wetu walishambuliwa mwaka 1984 huko Rhodesia, na mara kadha wa kadha tumeona shida ambazo wanazipata hawa wajumbe wa K.U. Kwa upande fulani nilifurahi kwa kunipa nafasi ya kufika Windhoek, nilifanya

nililopaswa kufanya, wao wanatamba kuwa walinyanyaswa na Joram Kiango, na hawatamsahau Willy Gamba, Mteko Vano na wale wa enzi zile. Madam S, TSA imewashtua, sasa wanahaha, na nasema watahaha sana, na ninajua kuwa watu wetu akiwemo Simbaulanga, watakuwa wamefichwa hapa, Dassen Island ndani ya Cape Town. Nahitaji kufika pale, na nitaudhihirishia ulimwengu kuwa hawa jamaa ni

waongo na wadhalimu, ninajua nini cha kufanya…”

“Amata!” Madam akamkatisha kwa kumwita na kumwoneshea mkono wake kuwa asubiri kwanza, “Unayoyasema ni mazito sana, mwaka 1984, nilikuwa katibu muhtasi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa… nakumbuka sana jinsi ambavyo tulipokea taarifa ile, nchi ilizizima, maana wapigania haki waliuawa kinyama.

Nakumbuka idara ilimtuma mwanausalama mashuhuri sana wakati ule ambaye alikuwa *Invinsible*, yaani wale watu hatari sana ambao daima huwa jirani na Rais na hata kazi zao hufanya chini yake, alikuwa akiitwa Chameleon, huyu jamaa alikuwa Rhodesia kama ulivyokwenda wewe, taarifa yake aaaaannnnhhh, ngoja niitafute nafikiri ninayo…" Madam akasema kisha akanyanayuka.

“Mom, tuambie tu nini kilikuwapo katika taarifa hiyo…” Amata akamuuliza.

“Naye aliripoti kuwa jamaa wameuawa kwa sababu anasema kuwa shambulio lile, halikuwa la kubahatisha, bali la kupangwa kabisa kabisa. Angekuwa hai, tungemuuliza mengi huyu bwana, angetujuza. Na hata hivyo walihakikisha wanamuua, na wakafanikiwa kumtengenezea ajali…” akasema.

“Anyway…” Kamanda Amata akasema huku akigonga meza kwa ngumi yake.

* * *

SEHEMU YA 30

13

HOTELI YA DOUBLE TREE

Daniel Kermikov na Bih waliketi ufukweni

wakibadilishana mawazo mawili matatu, wawili hawa hawakuwahi kukutana kabla, hii kwao ndo ilikuwa mara ya kwanza. Kama ungewaona, basi usingesita kujua kuwa wao ni wapenzi ambao wapo hapo kwa ajili ya starehe tu, kumbe la. Pumziko hilo lilikuwa na maana kamilia, kutokana na akili pevu walizonazo walijua wazi kuwa kujadiliana swala nyeti kama hilo ndani ingekuwa rahisi kudukuliwa. Lakini kumbe hapo ufukweni walipolala mchangani

isingekuwa rahisi kwa kuwa nani atajua kuwa mtaenda ufukweni ili atege vifaa vyake huko.

“Inabidi leo hii apatikane!” Bih akamwambia Kermikov.

“Sawa kabisa, lakini inabidi akili nyingi sana kumnasa, lazima utumie akili ya kike na si vinginevyo,” Kermikov akamwambia.

“Najua, na ndiyo maana niko hapa!”

“Sawa! Sehemu anazopenda kutembelea nazijua vyema, nitakuelekeza moja wapo,” Kermikov akasema huku akibadilsha pozi, badala ya kulala, akaketi mchangani.

“Huko mbali, najua mimi jinsi ya kumnasa, na wewe nitakupa taarifa tu kuwa niko wapi,” Bih akaeleza huku naye akisimama wima na kuanza kuvuta hatua kuelekea kwenye mabafu kujiswafi.

“Sawa!” Kermikov akaitikia.

* * *

Dakika thelathini baadae, Bih alikuwa barabarani na gari lake la kisasa aina ya *Mazda Sports*. Jua lilikuwa kali na joto halikuwa haba sana. Safari yake, hata yeye hakujua wapi inaishia ila alikuwa analifuata gari moja aina ya Ford Ranger lililokuwa mbele yake katika barabara ya kwenda Coco Beach. Alihakikisha alipotezi gari hilo na zaidi aliongeza kasi

kuliwahi. Bih alikuwa mjanja sana wa kumfuata mtu bila mfuatwa kujua. Tangu Mtaa wa Samora mpaka hapo alikuwa ana uhakika kuwa anayemfuata hajajua kama anafuatwa.

Ndani ya lile Ford, Kamanda Amata aliliona Mazda hilo likija kasi upande wa kulia kwake, hakutilia maanani sana na sekunde chache tu, lilikuwa ubavuni mwake. Akapiga jicho kulia, alichokishuhudia ni nywele

ndefu za mwanamke wa kizungu zikitimkia upande wake, akajua wazi kuwa mtu huyo alikuwa amegeukia upande wake. Amata hakutilia maanani gari hilo, likampita na kuwa mbele yake huku likiwa kasi sana, lilipokaribia mchepuko wa kuingia katika fukwe hiyo ya Coco likapunguza mwendo na Kamanda Amata akalipita na kuingia kulia mpaka kwenye maegesho, akaliweka gari lake hapo. Bih akatafuta mahali

pengine na kuegesha gari lake kisha akatembea taratibu kuelekea upande ambao kijana huyo alikuwepo.

Sijawahi kumwacha mwanaume salama! Akawaza pindi alipogundua kuwa windo lake liko ndani ya grosari moja matata sana katika eneo hilo. Katika kaunta, Amata aliagiza Safari bia, na kuinywa akiwa mchapulo. Mwili wake ulimsisimka na kugeuka nyuma.

Wala hakumaliza azma yake hiyo kwani macho yake yakagongana na mwanamke huyo aliyekuwa akivuta hatua za taratibu kuingia katika grosari hiyo. Kila mwanaume aliyekuwa hapo alijikuta anasahau ni nini hasa kilichomfanya kuwa hapo na kubakia kukodoa machokwa kiumbe hicho adimu.

“Mzungu wa wapi huyu mwenye shepu ya Kinyamwezi,

loh!” alisikika mlevi mmoja kutoka kwenye kona.

Bih akatua kauntani, sentimeta chache kutoka aliposimama Amata.

“Karibu bibie!” mhudumu wa kaunta akamkaribisha, naye akaitikia kwa kutikisa kichwa. Akageuka na kumtazama Kamanda Amata.

“Safari - Beer - please,” akatamka kwa kuvuta maneno.

Amata akamtazama juu mpaka chini, kweli, mwanamke huyu aliumbika, alikuwa na siha hasa ya kumvuta mwanaume rijali. Bia yake ilipofika, akamiminiwa katika bilauri.

“Hapa kwetu, mwanamke hunywa bia ya Kilimanjaro au Redds,” Amata akamwambia.

“Basi mi si mwanamke!”

“Ila…”

“Mwanaume kama wewe kasoro matiti tu,”

“Basi siyo mwanaume…”

“Hah! Hah! Hah!” wakacheka pamoja kisha wakagonga cheers.

Nishamkamata huyu! Bih akajiwazia huku akijimiminia kinywaji kinywani mwake na kushusha bilauri tupu. Baada tu ya kugonga bilauri zile, Amata hakunywa kwanza akasanifu kifua cha mwanamke huyo na kujikuta mwili ukisisima na kupata shida katika maeneo fulani.

Simwachi huyu, ila sura yake si ngeni sana! Amata akawaza huku akinywa taratibu.

“Mgeni wewe hapa?” Amata akauliza.

“Hapana, si mgeni kwa kuwa huwa ninakuja mara kwa mara…” Bih akajibu.

“Una shughuli gani zinazokufanya uwe unakuja mara kwa mara?”

“Aaaaaaaa … anyway, nina mpenzi wangu hapa, huwa

nakuja kumsalimu, anafanya kazi Tanzania Breweries…”

“Mtanzania?”

“Oh no! Ni kama mimi!” Bih akajibu.

“Sasa anakuachaje mwanamke mrembo kama wewe, utembee barabarani peke yako?” Amata akazidi kuchokonoa huku kila akimwangalia Bih, alikuwa akipata shida, “nyingine tafadhali, kwake na kwangu!” akaagiza. Bia

mbili zikatua na kila mmoja akamiminiwa bilaurini.

“Oh shit! You wanna kill me?” Bih akauliza.

“No! mwanaume huwa hamuui mwanamke kwa bia…”

“Bali…”

“Bali kwa mapenzi matamu yenye kukirimia kila atakalo…” Amata akajibu.

“Waoh… you are a man!” Bih naye akasindikiza jibu la Amata

huku akiweka bia yake kinywani na kujimiminia mafunda kadhaa.

“Sasa mpenziwo umemwacha na nani? Si ajabu anakuhitaji muda huu akupe mapenzi matamu,” Amata akachombeza.

“Loh! Mpenzi ni Yule anayenipa maneno matamu ya kunifurahisha moyo wangu… kama yako,” Bih akajibu huku tayari bia yake ikiwa imekwisha.

“Yaani huyo uzimwacjhe kabsaaa, nenda kafaidi maana du,

toto linanoga kwa macho tu je kwenye nanihii zi ndiyo blaaa….!” Sauti ya kilevi ilisikika kutoka kona ile ile, Amata akamtazama mtu huyo na kumbania jicho, “nipe moja basi na miye, maana msaada mpe mwanaume mwinziyo, mwanamke hakuziki kaka…”

Amata akabaki kucheka na kumwagizia mlevi Yule bia moja kisha akachukua simu yake na

waleti vilivyokuwa juu ya kaunta hiyo.

“Vipi?” Bih akauliza.

“Is time to go!” Amata akajibu akiwa tayari keshavuta hatua mbili mbele.

“Nilifurahia sana kampani yako, sasa unaniacha?” Bih akauliza huku akimtazama kijana huyo aliyeonekana kuwa makini na maamuzi yake.

Anaonekana mjuvi kweli! Bih akawaza kisha akaamua kutoka nje ya grosari hiyo.

“Kama unahitaji kampani yangu, twende!”

“Twende wapi?”

“Ninakoenda mimi,”

“Wapi?” Bih akahoji.

“Au we unataka wapi?” Amata akamuuliza.

“Hotelini kwangu…” Bih akajibu na kubakia akitazamana na kijana huyo.

* * *

IKULU – DAR ES SALAAM

Kikao nyeti kilikuwa kikiendelea, wajumbe wa juu kabisa wa Kamati ya Usalama chini ya rais mwenyewe walikutana alasiri hiyo. Lengo kuu katika kikao hicho ilikuwa ni kujipanga tayari kwa mkutano wa upatanishi ambao taarifa yake

ilifika siku moja iliyotangulia ikiwataka kukutana Cape Town wiki moja inayofuata. Mara baada ya kupata waraka huo kutoka katika afisi za kamisheni ya juu ya Umoja wa Ulaya ya hapa nchini, Rais hakuchelewa kuita kamati yake kwani tayari athari za kuwekewa vikwazo na watu hao zilikwishaonekana.

“Kwa hiyo nataka tuunde tume makini yenye watu waliobobea katika nyanja

tofauti," Rais akasema. Ujumbe wote ulikuwa ulikuwa kimya kabisa ukiendelea kumsikiliza, "tutawapa watu wao lakini pia tuwe makini na usalama wa watu wetu," akaendelea kusema.

"Na vipi kuhusu madai ya kusema kuwa na sisi tuna watu wetu kule?" mmoja wa wajumbe akahoji.

"Hatuna ushahidi sana juu ya hilo, na kwa hali ilivyo sasa basi,

tuwape watu wao…” Rais akajibu.

“Sawa mheshimiwa, lakini hapa naona wazi kuwa kongwa la mtu mweupe kwetu limekuwa zito… watu wao wana thamani kuliko wetu, kama EU wameshinikiza na hata kutuwekea vikwazo kwa nini AU isiingilie kati?” Waziri wa Mambo ya nje akauliza mara baada ya kupewa nafasi.

“Siwezi kulijibia hilo, naomba sasa tuweze kupanga tume tunayoihitaji kwani siku saba zijazo inabidi iwe kule. Waziri wa mambo ya nje ni mjumbe anayeingia bila kupingwa,” Rais akamaliza na kazi ya kupanga tume hiyo ikafanyika.

* * *

Jioni ya siku hiyo, majira ya saa kumi hivi, Madam S akaegesha gari lake katika uwanja wa Ikulu, akateremka na kuvuta hatua

kuelekea lango kuu la jengo hilo. Mlangoni akakaribishwa na mtu maalumu aliyekuwa akimsubiri, akaongozwa mpaka chumba maalumu, Kilimanjaro Square, ambamo ni mikutano ya watu wawili tu hufanyika kati ya Rais na mtu amtakaye. Mkutano ambao hautakiwi kuwa na mtu wa tatu.

“Karibu Selina!” Rais akamkaribisha mwanamama huyo.

“Asante, nimeitikia wito wako mheshimiwa,” Madam S akaitika huku akikaa kitini na kufungua kabrasha lake.

“Tumefikia muafaka, hii ndiyo tume mpya ya upatanishi tuliyoiundam unaweza kuitazama…” Rais akamwambia huku akimpa karatasi moja yenye majina saba. Madam S akaipokea na kuitazama.

Ilikuwa orodha ya watu saba, ambayo hata Madam S

mwenyewe alitikisa kichwa kuafiki.

“Safi, hapa wamepangwa watu makini, huyu Bi. Hindu Hassan Al Mahroon namkubalia sana kwa kujenga hoja za kidiplomasia…” Madam S akauunga mkono baada ya kupitia orodha nzima na kumchambua mtu mmoja mmoja.

“Tumeangalia watu makini ili kazi hii iende vizuri, sasa

nilichokuitia ni hiki kifuatacho. Tume hii itaondoka hapa kesho kutwa kuelekea Cape Town kwa kikao. Nahitaji mtu makini kama wakati ule kwa ajili ya usalama, Yule kijana wako alifanya vyema sana safari ile na sasa namhitaji tena…" Rais akazungumza akimtaja Kamanda Amata lakini hakuwa akijua jina sawasawa.

"Sawa, nakubaliana na wazo lako, lakini mheshimiwa sisi hatukuwa kimya katika kufanya

uchunguzi wa jambo hili kama nilivyokudokezea mwanzoni. Mpaka sasa tumepata uhakika wa asilimia themanini na tano kuwa tuna watu wetu kule, na kwa sasa tunafanyia uchunguzi kuju mahali walipo…”

“…unasema kweli? Hebu nipe habari hiyo…” Rais akadakiza kwa furaha.

“Vijana wanafanya kazi, hawajalala, ila tumeiweka siri, na iwe siri kwanza mpaka sisi

tutakapojiridhisha kuwepo kwao kwa hizo asilimia kumi na tano zilizobakia…" Madam S akaeleza.

"Sawa, naomba mfanye kazi, kwa lolote yaani msaada wowote mniambie na nitatoa mara moja… napenda sana tuwapate ili dunia ijue kuwa tunaonewa…"

"Usijali tupo kazini…" Madam akajibu.

"Sawa, sasa tunafanyaje kwa hili…"

“Hili lisikusumbue, kama umepanga kutupatia sisi we tupatie sisi, nitaipanga timu yangu na kazi yote itafanyika. Ila kuhusu safari za hawa wanatume naomba ofisi yako isiratibu, niachie mimi nitaziratibu na wataondoka tunavyotaka sisi, ili irahisishe kazi zetu,” Madam S akajibu.

“Ok Selina Head Of TSA, namshukuru aliyekuteua na kukupa kitengo hicho….”

“Ila hii ikiisha naomba kustahafu mheshimiwa!” Madam akachomekea.

“Hah! Hah! Hah! Utastahafu tu mama, kwanza tumalize haya matatizo. Sasa nakupa go ahead katika hili na wengine wote nasitisha wasifanye chochote juu ya safari hii ya KU…” Rais akasema.

“Sawa mheshimiwa,” Madam S akajibu.

Chizi kapewa rungu, sasa watakoma! Madam S akawaza huku akitoka katika chumba hicho na kuondoka zake.

SEHEMU YA 31 INAKUJIA JAMVINI SASA

* * *

SEHEMU YA 31

Akili ya kamanda Amata ikampa taarifa ya hatari mara tu baada ya kuingia katika gari la

Bih. Baada ya kuketi kitini, sekunde chache tu tayari macho yake yalikuwa yameshakagua gari hiyo, katika sehemu ndogo ya kuwekea vitu, kulikuwa na kadi yenye picha ya miti miwili na jengo kubwa pembeni yake. Picha hizi zikampa mara moja maana kamili, 'Double Tree Hotel', damu ikamsisimka, kwa ujanja wa haraka akampiga picha mwanadada huyo kwa kutumia saa yake ya mkononi. Picha ile

akaituma moja kwa moja kwa Chiba na kusubiri majibu.

Nimetekwa! Akawaza. Mara hiyo lile gari likaondolewa kwa kasi na kuingia barabarani. Mazungumzo ya kawaida tu yalikuwa yakiendelea katika gari hilo huku mkono wa Kamanda ukipapasa paja la mwanadada huyo aliyekuwa nyuma ya usukani. Simu yake ikaita kwa mlio hafifu, akaitoa mfukoni na

kutazama; sms toka kwa Chiba ilifika.

'Upo kwenye mdomo wa mamba,

Bih, mmoja wa wapiganaji wa Daughters

Mwanajeshi katika jeshi la South Afrika.'

Kamanda Amata akashusha pumzi na kuiweka simu ile mfukoni, dakika chache baadae gari likaegeshwa mbele ya hoteli ile. Kamanda Amata akachukua miwani yake na kuipachika usoni,

kwa haraka akatazama madirisha ya jengo hilo. Ni katika moja ya madirisha hayo alipoona kitu ambacho kiliushtua moyo wake. Daniel Kermikov, alijitokeza dirishani akichungulia chini, hii ikamfanya Amata kujua wazi kuwa ulikuwa mpango mahsusi way eye kuwekwa katika mikono ya watu hao.

Wametumia mwanamke anilaghai kimapenzi kuniteka, basi mimi na wao leo!

Akajisemea moyoni na kuchukua simu yake akaandika ujumbe wa haraka kwa watu wake.

'Rescue DTH'

Katika lile dirisha, Kermikov alikuwa tayari na bunduki matata sana ya kudungulia, safari hii hakutaka kabisa kupambana na adui wake ana kwa ana ila alifikiri kummaliza kwa stahili hiyo. Tayari kila kitu kiliwekwa sawa, mabegi yalikwishafungwa kwa safari. Ilibaki tu kutimiza azma ya

kumuua TSA 1 na wao kuondoka zao haraka kabla hawajagunduliwa. Wingi wa watu katika eneo hilo la maegesho, lilimpa wakati mgumu Kermikov kufanya shabaha yake. Na kwa kuwa Amata alikwishaona hilo, akawa anahamahama mara kwa mara huku akiwa kamkumbati kiunoni mwanamke huyo wa kizungu, ambaye naye alikuwa akimbembabemba mwanaume huyo kumpa nafasi Kermov kumaliza mchezo.

Dakika kama tano hivi zikapita, hakukutukia chochote, Bih akajua kuwa plan A imeshindikana na sasa hakuwa na budi kumwingiza ndani mwanaume huyo. Kama kuna kitu ambacho Amata alikuwa akikisubiri ni hicho, alijua wazi nini kitatukia huko ndani lakini akapiga moyo konde na kukokotana na mwanamke huyo mpaka kwenye lifti.

Ndani ya chumba cha Bih, Amata akamtupa mwanamke huyo kitandani na kwenda juu yake akimnyonya ulimi na kumminya hapa na pale kimahaba. Bih akamsukuma kando Amata nay eye akasimama wima kando ya kitanda akiwa tayari na moto wa kuingia mapenzini, kwa ufundi wa Amata ndani ya dakika chache ulimfanya mwanamke huyo kuona kuwa yuko pepo ingine, akasaula nguo moja moja na kubaki yeye tu

akionesha ubindamu wake ulivyokamilika kimaumbile. Kamanda Amata akameza mate ya uchu, akaondoa viwalo vyake na miwani akaiweka juu ya meza ndogo ikiwatazama wao. Miwani hiyo iliweza kuchukua picha za tukio hilo vizuri kabisa na kurusha kwa umbali wa mita 200 hivi, alifanya hivyo makusudi kwa maana alijua Chiba na kikosi kazi watawasili eneo hilo na hiyo ingemsaidia kujua nini kinaendelea.

Amata na Bih wakajitupa kitandani na kujifunika shuka kubwa juu yao, kilichofuata hapo ni miguno ya mahaba na mabembelezano ambavyo vilileta sauti za kupendeza. Amata alionesha ufundi wake na mwanamke huyo nye hakuwa nyuma kwani alihakikisha anamkoleza mtu wake huku akivuta muda kwa Kermikov kuwasili katika eneo hilo, hii ilikuwa plan B yao.

Muda wote huo Kermikov alikuwa kajificha bafuni ndani ya chumba hicho hicho cha Bih akisubiri watu hao wakaribie kilele cha tendo lao, ndipo ajitokeze kwani alijua katika nukta hiyo, mwanaume hawezi kufanya lolote kwani akili yake huwa haipo tena.

* * *

Chiba na Scoba wakawasili katika eneo hilo wakiwa ndani ya Land Cruiser lao lenye vioo vya

giza. Gari hili mara nyingi walikuwa wakilitumia kwa kazi maalum kama hizi. Walitakiwa kuwachukua watu hao wakiwa hai ili kuwaficha na ndugu zao wasijue ni wapi walipo. Mara tu baada ya kuegesha gari, akawasha kitu kama simu chenya skrini kubwa kiasi, kutoka katika chombo hicho akaweza kunasa picha zile ambazo miwani ya Amata ilikuwa inazichukua.

“TSA 1 on mission…” akasema.

“What?” Scoba akauliza na Chiba akampatia ile masine naye akatupia macho.

“Mmmm kama kawaida, haya ipachike hapo tuangalie muvi ya bure, itakuwa ameweka makusudi tu…”

“Of course, si kwamba kaweka bahati mbaya, ni makusudi mazima, inaonekana anajua kuwa hapo kitandani panaweza kutukia

jambo, ngoja tuone…” Chiba akamjibu Scoba huku akiipachika ile skirini katika dashboard ya gari wakisubiri kuona nini kitatokea na wao watatakiwa kufanya nini, hapo tayari bastola zao zilikuwa zimesheheni risasi za moto.

“Unajua hapa tuko mbali ee, nafikiri tupande na tusubiri jirani kabisa…”

“Kweli Scoba, let us go huko huko, wasije kumzidi nguvu na

tukampoteza namba moja wetu," wakateremka na kile kiskrini na kuelekea katika hoteli hiyo.

* * *

Daniel Kermikov, akiwa na bastola aina ya PPK iliyofungwa kizuia sauti, akajiweka tayari kufanya shambulizi hilo la ghafla. Hasira yake ilipanda mara mbili; kwa kushindwa kumdihibiti katika pambano lao la kwanza na mara hii kufanya mapenzi na Bih mbele yake. Kermikov

alimhusudu sana mwanamke huyu, lakini kila alipomtongoza alijibiwa tu ‘kazi kwanza, mapenzi baadae’. Kwake lilikuwa tusi kubwa na dharau kwa adui yake ambaye anatakiwa amuue akimwona kitandani na mwanamke yuleyule wa ‘kazi kwanza mapenzi baadae’.

Aliposikia miguno ile imeongezeka akajua tayari muda aliousubiri umefika, akajitokeza kwa ghafla huku bastola yake

ikiwa tayari imebanwa na kono lake la kulia. Kilikuwa ni kitendo cha sekunde kama mbili hivi, ya kwanza lijitokeza, na ya pili akafyatua risasi.
Alichokishuhudia ni shuka likivurugika na kuanza kutona damu huku mguno hafifu wa mauti ukisikika na nukta hiyo hiyo akajikuta anatazama na domo la Berreta Pico, lililotema risasi iliyomfikia begani na nyingine ikatua gotini, Kermikov akaenda chini bila pingamizi.

Chiba na Scoba nao wakavamia kwa kuupiga kiki la nguvu mlango na kutua nao ndani.

“Upo salama kaka?” Chiba akauliza.

“Kama kawaida ila nahisi huyu mwanamke amekufa…”

“Shiit! Tia pingu huyo mpumbavu!” Chiba akamwambia Scoba naye akafanya hivyo. Yeye akakiendea kitanda na kufunua shuka. Bih alikuwa chali

kitandani, uchi wa nyama, tundu la risasi likiwa katikati ya moyo wake upande wa mgongoni ila kwa mbele haikutokea maana yake risasi ile ilikuwa imekwama ndani.

“Hakuwa na shabaha?” Chiba akauliza.

“Ana shabaha nzuri sana, ndiyo maana kaua kwa risasi moja tu,” Amata akajibu akiwa anamalizia kuvaa nguo, maana burudani ilikatika ghafla.

* * *

Sekunde chache kabla ya Kermikov kufanya shambulizi hilo, Amata alihisi kila dalili ya hatari, kichwani mwake akajua wazi kabisa kuwa kama ni adui hakuna sehemu ya kutokea zaidi ya chooni kwaku hakukagua huko. Akiwa hajamaliza kufikiri, macho yake yakatazama mlango wa kioo wa chooni na ndipo akashuhudia mtu huyo akijitokeza. Hakupoteza nafasi

kwani yeye alikuwa juu na Bih alikuwa chini wakiendelea kuvunja amri ya sita. Amata akamgeuza haraka mwanamke yule na kumwelekeza mgongo upande wa mlango. Bih hakujua kabisa nini kinaendelea, zaidi alijua kuwa ni moja ya manjonjo ya mwanaume huyo kumbinuabinua. Baada ya kufanya hivyo, akavuta shuka juu na kujifunika na mwanamke huyo hii ikamchanganya Kermikov na akilini mwake

akabaki na taswira ya kwanza kuwa Amata yuko juu na Bih yuko chini. Kitend hicho hicho, Amata akashusha mkono wake mpaka kwenye sakafu na kuchukua bastola yake ndogo kutoka katika suruali yake upande wa ndani na kuurudisha mkono kwa kasi na kufyatua risasi ya kwanza iliyotua katika bega la adui yake na ya pili ikatua gotini.

Mwili wa Bih, ukafunikwa kwa shuka lile lile na Kermikov

akakokotwa kutokea mlango wa dharula huku damu zikiwa zimedhibitiwa kwa vipande vya nguo, akigugumia kwa maumivu. Akatiwa ndani ya gari na kufungiwa humo.

"Hautoonekana tena duniani," Amata akamwambia na kuufunga mlango.

Yote haya yakitukia ni watu wachache sana waliojua ambao tayari walitoa taarifa mapokezi kuwa kuna majambazi

yamevamia huko juu, nah ii ni baada ya kushuhudia Chiba na Scoba wakiingia kwa staili ile. Walinzi walipofika katika chumba kile, waliukuta mwili wa Bih pekee, taarifa ikafika polisi nao wakawasili. Lakini wakiwa hapo wakapewa taarifa wasiguse chochote mpaka watakapoambiwa vinginevyo ila wahakikishe ulinzi katika chumba hicho. Tayari Amata alikwishafanya yake.

* * *

CAPE TOWN – AFRIKA KUSINI

Saa mbili baadae ikagundulika kuwa mawasiliano kati ya Dar es salaam operesheni maalumu na Cape Town hayakupatikana. Mr. Dunkan akatoa taarifa ya anguko hilo kunakohusika. Bi. Margreth Casbarai aliipokea taarifa hiyo kwa hofu sana, haraka akafanya mawasiliano na ofisi ya siri ya Dar es salaam, na dakika chache

baadae akapata taarifa mbaya kabisa ambayo hakuwahi kufikiri kuipata kwa siku hizo.

"Amata Ric, once again!" Margaritha Casbarai akatamka huku mishipa ya hasira ikimtoka. Akamtazama Dunkan na kumtaka arudi kuendelea na kazi.

Kutokana na maandalizi ya mkutano wa kamati za upatanishi, tayari wajumbe wengi walikwishaanza kuingia katika Jiji la Cape Town hasa wale kutoka

EU na kwingineko. Katika siku nne hizi walitakiwa kukutana ili kuweka mambo yao sawa. McCain akiwa mzima wa afya alikuwa tayari katika jiji hilo, huku kiongozi wao mkuu, Alfa akiingia kwa siri katika jiji hilo pasi na mtu yoyote kujua.

Nitawakomesha, safari hii tutawafanya kama mwaka 1984, na hiki kitakuwa kisasi! Margaritha akawaza akiwa ameketi juu ya kiti kizuri sana

katika kasri hilo la bosi wake Mc Cain. Akiwa katika lindi la mawazo, mlango ukafunguliwa bila hodi, hakuwa mwingine, McCain aliingia akiwa kafuatana na vijana wengine wa kizungu kama watano hivi. Vijana hawa wakatawanyika ndani ya sebule hiyo kwa mtindo wa nusu duara na kumwacha *mdosi* huyo akichukua kiti mkabala na Bi. Casbarai.

“Im not happy at all!” ilikuwa sentensi ya kwanza ya McCain huku akiweka mtemba wake kibwetani.

“I know!” Margaritha akajibu.

“Kwa nini tunashindwa kumdhibiti huyu *cockroach*?” akauliza huku mishipa ya hasira ikiwa imemtoka.

“Tumefanya kila mbinu, lakini inaonekana katudhidi ujanja,”

“Acha kuongea upuuzi kama huo! Mtu mmoja aitikise WP

nzima, ulinzi wote na intelijensia tuliyonayo aishinde ujanja, haingii akilini!" akaongea kwa ukali na kushusha pumzi ndefu, akajiegemeza kitini.

Ukimya ukatawala kwa nukta kadhaa, *'shetani kapita'*, watoto wa zamani tungesema hivyo. Simu ya mezani ikaita kwa fujo, Mc Cain akaitazama na Margaritha pia, hakuna aliyeichukua, tswira ya TSA 1 ilikuwa ikiwanyanyasa akili zao. Kwa ishara ya macho,

Mc Cain akamtaka kijana mmoja kuipokea, akafanya hivyo.

“Yes!” akaitikia, kisha maelezo mafupi kutoka upande wa pili yakafuatia. Kijana Yule akabana kwa kiganja chake katika kidosho cha kuongelea.

“Madam! Is yours!” akasema na kumpatia Margaritha.

“Yes, hello!” akaita na kusikiliza. Kwa kumtazama tu sura yake, ungejua kuwa habari anayoipokea si nzuri. Baada ya

sekunde kama kumi hivi akaitua simu hiyo na kumpati Yule kijana naye akaiweka mahala pake.

"Bih, has been killed!" -*Bih ameuawa,*- akamwambia Mc Cain.

Akashusha pumzi kwa mara nyingine na kutoa kitambaa chake mfukoni, akajifuta jasho hata kama hakuwa nalo, "yuko wapi Kermikov?" akauliza.

"Utata!"

"Utata?"

“Ndiyo, utata, taarifa inasema, Bih ameuawa kwa risasi, uchunguzi unaonesha kuwa risasi ile ni ya Kermikov…”

“Ina maana Kermikov kamuua Bih, kwa nini?” McCain akamkatisha Margaritha kisha ukimya mwingine ukatawala, “hebu nipe idadi ya waliouawa na huyu jamaa…” akaongeza.

“Jesca, The Cobra, Bih, na vijana wengine wawili, pia alimwacha Parrot katika hali

mbaya pamoja na Kermikov mwenyewe…”

“Memba wawili wa The Daughters wamekufa, si ndiyo maana yake?”

“Ndiyo!”

“Nipe mkakati wako juu ya huyu jamaa, nafikiri inabidi kuifutilia mbali hiyo TSA, sijui kidudu gani sijui,” Mc Cain akataka kujua.

“Sasa sijui kama TSA ni idara au mtu mmoja…”

“Margaritha, kule Prague umeeleza wazi kuwa TSA ni idara na ni sahihi ni idara ya ujasusi ya Tanzania inayotekeleza mipango yote ya siri ya serikali hiyo. Kwa maana hiyo badala ya kupambana na mtu mmoja inabidi tuijue idara yenyewe kwanza…” McCain akaeleza.

“Ndiyo, sasa mkakati ni kuwa; kwanza najua wazi hawa wajumbe watakuja wakiwa na ulinzi wa siri kama ilivyokuwa

kule Windhoek, na tuna uhakika kuwa ulinzi utakaokuja ni TSA na si mtu mwingine yoyote. Hivyo tumepanga kuwahook wote tutakaowashuku na kuwachinjilia mbali," Margaritha akasema.

"Sawa, na habari ya Dassen Keputo inasemaje au mmeiwekaje?" McCain akauliza.

"Tuliketi kikao siku chache zilizopita, tukajadili hili kwa undani, tunajua kuwa hakuna wa kuweza kujua siri iliyopo katika

kaburi lile zaidi ya hawahawa TSA…”

“Kwa hiyo watakuwa wameshajua siri zetu, kwa maana hiyo tuna kazi kubwa sana ya kupambana na mtandao huu,” Mc Cain akazungumza kwa uchungu, “naona giza nene sana mbele yetu, *code 005*, lazima ifanyiwe kazi,” akasema na kusimama wima.

“Kwa hiyo tunafanyaje?”

“Katika siku hizi mbili kabla kikao hakijaanza, inabidi tuwe tumeleta watu makini katika maswala ya kiuchunguzi, ili wamng’amue kila atakayeingia ndani ya jiji hili. Halafu maswala mengine yote yanayotakiwa kutekelezwa kwa siri, nakupa *go ahead*,” Mc Cain akatoa maagiza na kutoka ndani ya sebule ile.

Margaritha Casbarai, akajikuta peke yake kama ilivyokuwa mwanzo. Baada ya kikao hicho,

mwanamama huyo akawasiliana na watu wake muhimu katika idara ya usalama, na kuhakikisha anaweka ulinzi mkali katika sehemu nyeti za kuingilia katika jiji hilo kuanzia uwanja wa ndege, bandarini, viwanja vyote vya kukodisha helikopta, magari, mahoteli yote yakawa chini ya uangalizi maalumu ili kung'amua wanausalama watakaoingia katika jiji hilo ama kutoka Tanzania au nchi yoyote ya Kiafrika.

* * *

SHAMBA – SAFE HOUSE

Daniel Kermikov alitupwa ndani ya chumba chenye giza nene ambalo huwezi kuona hata umbali wa milimita 3. Akiwa na pingu mikononi na mnyororo uliombana miguu sawia kabisa, akatua sakafuni kama mzigo akiwa na boksa tu.

“Kaa hapa kwa saa kadhaa, na ndani ya saa hizo tunataka utuambie nani kakutuma kwa

nini," Amata akamwambia kisha akafunga mlango na kuingia kwenye chumba kingine. Kutoka chumba hichi kingine kulikuwa na Amata, Chiba na Scoba ambao waliweza kumwona vizuri tu mzungu huyo.

"Unafikiri kwa njia hii atasema?" Scoba akauliza.

"Atasema tu!" Amata akajibu. Dakika chache baadae, Madam S akaingia na kufuatiwa na Jasmine na Gina, wote watano wakajikuta

ndani ya chumba hicho ambacho kilikuwa na kompyuta na vifaa vingine maalumu kwa kunasa sauti.

“Mtanitesa sana tu, lakini hamtoweza kupata chochote kutoka kwangu,” Kermikov akasema na TSA wakasiki kutoka chumba kile cha pili.

“Huwa hatutesi watu, bali tunawafanya watuambie tunachotaka!” Chiba akamjibu. Na baada ya kujibu hayo,

akabofya kidubwasha fulani kilichopo katika ukuta chenye rangi nyekundu na kimeandikwa namba 1. Kutoka pale kwenye kioo wakaona kijimlango kikifunguka na nge kama ishirini hivi wakatoka katika tundu lile wakiwa mikia juu kwa hasira. Nge wale walimvamia binadamu waliyemkuta humo na kumuuma kila kona ya mwili. Kermikov alijikuta aking'atwa mwilini lakini hakuweza kuwaona nge hao. Maumivu makali sana

yalimtapakaa mwilini, uvumilivu ukamshinda.

“Aaaaaaiiihgggggghhhh, come onnnn!!!! Nasema nasema…”akapiga kelele.

“Sema! Nataka useme….” Amata akaungurum kwa kiingereza safi.

“WP, nimetumwa na WP…”

“WP ndo nini?”

“Sijui, sijui kwa kweli…” akajibu huku bado aking’atwa na nge hao.

“Nataka unambie nani aliyekutuma, namaanisha mtu!” Amata akamwambia tena. Kermikov hakujibu akajaribu kuvumilia kumbe hakuwa anawajua vyema nge wa Afrika. Chiba akabofya kitufe kingine, kutoka kwenye kile kioo wakaona kijimlango kingine kikifunguka,

siafu wengi wasiohesabika wakatokamo.

“Mtumeee!!!!” Jasmine akang’aka na kutoka katika kile chumba. Wale siafu wakamvamia Kermikov, kelele alizozipiga hazikuwa za kitoto.

“Yaaaahhhh!!!!! oooooh!!!! Nasema!”

“Sema….!”

“Alfa, Alfa…”

“Alfa ndiyo nani?”

“Ndiye kiongozi wao mkuu…”

“Anaishi wapi?”

“Aaaaaiiiggghhhh!!! Aaaiiii!!!!! Prague, Prague!” akajibu.

Kamanda Amata akampa ishara Chiba, naye akabofya kidude kingine, moshi wenye dawa ukakijaza chumba hicho. Wale nge na siafu wakakimbi na kila mmoja akaingia kwenye tundu lake bila kukosea.

“Jasmine!” Amata akaita kwa sauti ya chini.

“Beh!” akaitika kutoka nje ya mlango.

“*Antivernon* tafadhali,” akamwambia, na mwanadada huyo akaondoka. Dakika kama mbili hivi, taa zikawaka katika kile chumba alimokuwamo Kermikov. Jasmine akaingia ndani akiwa na koti jeupe na gloves mikononi. Pamoja na vyote alikuwa na sindano iliyojaa

dawa ndani yake, ngozi ya Daniel ilikuwa imebadilika rangi kabisa, hakuweza kufumbua macho na aikuwa akipumua kwa shida. Akamfikia na kumdunga sindano hiyo kisha akamwacha na kutoka.

* * *

Katika meza ya duara, ndani ya jumba hilo, Madam S aliketi na vijana wake wote. Ukiachana na kazi anazowapa mmoja mmoja ambazo wakati mwingine hata wao hawajui nini anafanya nani

na nani anafanya nini, ni mara chache hasa kukiwa na kazi ngumu inayohitaji timu nzima, huwaita katika meza hii.

"Yatupasa kujipanga!" akawaambia, "keshokutwa mkutano huo wa upatanishi utafanyika Afrika Kusini, kama kawaida, Mkuu wa nchi katoa kazi kwetu kuhakikisha usalama wa watu hawa ambao wanaondoka muda si mrefu kwa makundi makundi kuingia katika

jiji hilo," akaweka ukimya kidogo, "Amata nipe mkakati unaoufikiri maana najua kuwa hii ni kazi ngumu kuliko maelezo," akamalizia kusema.

"Ndiyo, Madam S, nina uhakika kabisa kuwa kwa tukio la leo hii la kufa huyo Bih, watakuwa wamefyumu mpaka kupasuka… hawa jamaa wakimkamata hata mmoja wetu watamnyonya damu kwa kweli. Hoja ya ngu ni kwamba,

tunaingiaje Afrika Kusini? Nina uhakika watakuwa wanatuwinda kila kona na kila mlango wa kuingia katika jiji hilo," Amata akajibu kwa hoja hiyo.

"Upo sahihi!" Chiba akadakiza, "kama tunaingia kule lazima tutumie njia ya kificho sana, sijui tufanyeje, lakini lazima tuingie," akamaliza kusema.

"Ipo hivi, mimi na Chiba lazima tutue Kisiwa cha Dassen

kuhakikisha tunawapata watu wetu," Amata akasema.

"Enhe!" Madam akaunga mkono.

"Halafu, Scoba, Gina na Jasmine waingine Cape Town mjini kwa kazi hiyo ya kuweka ulinzi. Kwa hesabu ninazopiga mimi nataka tuwaokoe watu wetu wakati ninyi mnawapa wao…" Amata akaongeza kusema.

"Nimeelewa, mtaingiaje Dassen?" Madam akauliza.

“Hilo niachie mimi, najua tutafanya nini na tutafika Dassen, na tutakinukisha!” Amata akajibu.

“Mtahitaji msaada wa uvamizi?”

“Sidhani, sisi wawili tunaweza kutosha!”

“No, nitaweka wanajeshi watatu standby, kitengo *special force*, watakuwa sambamba na ninyi,” Madam akatoa maelekezo na Amata na Chiba wakaafiki kwa kichwa, “mimi nitaondoka

hapa kesho kuelekea Cape Town kwa maswala mengine kabisa," akawaambia.

"Ok, nimepata wazo…"

"La nini?" Madam akauliza.

"Jinsi ya Scoba kuingia Afrika Kusini…"

"Njia gani?"

"Ndege!"

"Ndege? Si tumeona hapa kuwa jamaa kwa asilimia kubwa wataweka macho viwanja vya

ndege na njia nyingine za kuingia katika jiji hilo! Au umesahau?" madam akamwambia Amata.

"Sivyo, kuna mpango wa siri, nitakwambia nafikiri kwa huo tutafanikiwa, na tutatumia ndege," Amata akasema. Kikao kikaendelea kwa kufanya uchunguzi hasa juu ya majibu ambayo Kermikov amewapatia. Kuhusu WP tayari walikuwa na habari nyingi sana kupitia tafutishi zao ambazo walizipata

kupitia data belt na kabui la Dassen Keputo, kutoka kwa mateka wao walipata kujua tu juu ya kiongozi mkuu wa kundi hilo, Alfa. Alfa ni nani? Ndo swali ambalo lilikaa kichwani mwao.

14

LUGALO BARRACKS

'Jua lileeee literemke mama!

Jua lieeee literemke mamaaa!!

Aiyaiyaaaaa iyaaa iyaaa mama….

Aiyaa iyaaaa iyaaa mama….!”

Kikosi cha wanajeshi kama thelathini hivi kilipita kikimbia mchakamchaka mbele ya lango kuu wakitoka upande wa Tangi Bovu na kuingia ndani ya kambi hiyo huku kiongozi wao akiwa kazuia magari kwa bendera yake

nyekundu. Miongoni mwa magari yaliyosimamishwa lilikuwapo BMW jeusi na ndani yake alikuwapo mwanamama mwenye umri wa kutosha. Kwa wenyewe wenye magai haya huwa wanajua kuwa gari hilo ni la nani lakini wengine huona gari kama gari jingine lolote.

Baada ya kikosi kile kuingia ndani, magari yakaruhusiwa kupita na kuendelea na safari. Lile BMW likawasha indiketa

kuwa linaingia upande wa kushoto na hapo ndipo penye lango kuu la kuingia katika kambi hiyo maarufu ya jeshi. Madam S akaegesha gari lake nje ya jengo lililosheheni ofisi mbali mbali. Afisi ya kwanza kufika ilikuwa mapokezi ambapo *bintijeshi* mmoja alimpokea na kumsikiliza shida yake, kisha wakatoka pamoja mpaka jengo jingine ambalo mbele yake kulikuwa na bendera mbili zikipepea.

“Asante sana!” akamshukuru Yule binti na kisha yeye kuingia ndani ya afisi hiyo.

“Karibu Madam!” akakaribishwa kwenye ofisi hiyo nadhifu yenye samani za thamani. Akakaribishwa kiti na kuketi mara tu baada ya kusalimiana na afisa huyo aliyesheheni vyeo na nishani nyingi kifuani mwake.

“Naitwa Brigedia Justus Sebanza!” akajitambulisha huku akijiweka vizuri kitini.

“Nashukuru kukufahamu, naitwa Selina,” naye akajitambulisha na kumpatia bahasha iliyo mkononi mwake. Afisa Yule mara baada ya kuipokea, ndita za paji la uso wake zikajifinyanga zikionesha umakini wa bahasha hiyo anayoipokea. Kwa mikono yenye kitetemeshi akaifungua na kuanza

kuisoma na alipomaliza akashusha pumzi ndefu.

"Sawa!"kaitikia na kuiweka kwenye faili, kisha akasimama na kuiweka suruali yake vizuri, akachukua *copstick* yake na kuvuta hatua mpaka mbele ya meza hiyo, "Madam, nikuoneshe mazingira kidogo!" akamwambia, kisha kwa kufuatana wakazunguka nyuma ya majengo ambako kulikuwa na uwanja mkubwa na vijana wa jeshi wengie walikuwa wakifanya

mazoezi ya hatari sana, wakasimama kwa sekunde kadhaa wakitazama kisha wakaenda upande wa pili. Huko kulikuwa na jengo lingine ambalo vijana wengine walikuwa wakilenga shabaha. Kati ya vijana hao, walipoanza kulenga shabaha, kijana mmoja alionesha uhodari wa hali ya juu kwa kupiga risasi zote thelathini na mbili katikati ya kibao.

“Hawa ni vijana wetu wa special force!” Yule afisa akamwambia Madam S.

“Hata mi naona, wako vizuri kwenye upiganaji na shabaha pia…” Madam S akajibu huku akitikisa kichwa juu chini. Kisha wakarudi afisini na kuketi, “kwa hiyo kwa maelezo ya barua hii nitakupatia vijana wawili ambao watawajibika kwa muda chini ya Ofisi ya Rais, mimi najisikia faraja kama Mkuu anajua kuwa

ana vijana wanaoweza kubeba jukumu kama hilo japokuwa silijui… by the way, wewe unafanya kazi wapi au gani?" akamuuliza Madam S.

"Aa mimi ni secretary katika moja ya afisi pale kwa Makamu wa Rais," Madam S akajibu kwa uwongo unakaribiana na ukweli. Yule afisa akainua simu ya mezani na kukoroga namba fulani kisha akaweka sikioni, na baada ya kuongea maneno

machache, akatoa maagizo kuitiwa vijana wawili kisha akakata simu.

Dakika tatu baadae, vijana wawili wakaingia wakiwa ndani ya combat safi za kijeshi, wakasimama kwa ukakamavu na kupiga saluti kwa mkuu wao.

“Mnaweza mkashangaa kwa nini nimewaita mimi! Sasa ni hivi, muwe tayari leo hii mtatakiwa kuondoka na kwenda kwenye operesheni maalumu, kwa hiyo

mkitoka hapa mkaandae vitu vyenu muhimu kwa kazi na maelezo mengine mtataarifiwa yakifika," akawaambia.

"Sawa Afande!!!" wakajibu huku bado wakiwa katika msimamo uleule.

"Madam S, huyu hapa ni John Mlolele, mahiri sana katika mapigano ya ana kwa ana bila silaha, huyu mwingine anaitwa Joseph Rutashobya au hapa tunamwita Joru, yeye pia ni

mpiganaji mzuri lakini zaidi ya hapo ana shabaha ya ajabu," akawatambulisa na baada ya mzungumzo na maagizo machache, vijana wale wakaondoka na Madam S akaagana na mwenyeji wake na kuondoka

* * *

WINDHOEK – NAMIBIA

Saa 12 jioni

Jioni hiyo ilimkuta Kamanda Amata katika Jiji la Windhoek

kwa mara ya pili, alikumbuka jinsi ambavyo aliwachachafya WP katika jiji hilo miezi kadhaa ilopita.

Sasa sijaja kuwachachafya tena! Akawaza huku akiingia ndani ya taksi tayari kwa safari.

"Goldbeg Hotel tafadhali," akamwambia dereva huku akijiweka vyema kitini na kijana yule akaikamata barabara kuelekea mjini. Ndani ya gari hilo hakuna aliyekuwa akiongea,

kichwani mwa amata mambo mengi yalikuwa yakipita. Kufumba na kufumbua, akajikuta akitakiwe kuteremka katika hoteli hiyo kubwa na ya kisasa.

“Dola ishirini na mbili tu,” yule kijana akamwambia, Amata akatoa waleti yake na kumpatia kisha wakaagana.

Hatua kama mia hivi zikamfikisha mapokezi ya hoteli hiyo, “Mr. Spark, kutoka Angola!” akajitambulisha kwa

jina bandia na kufuatia itifaki nyingine za kupata hifadhi katika hoteli hiyo.

“405!” yule mhudulmu akamwambia na Amata akaicha kaunta hiyo na kupandisha kwenda katika gorofa ya 4 chumba namba 5. Akili ya Amata muda wote ilikuwa kwenye hali ya tahadhari sana kwa sababu alijua wazi kuwa si ajabu anafuatiliwa na adui wake. Hakutaka kuiaminisha akili yake

kuwa katika jiji hilo usalama umejaa tele, hapana, alijua, muda wowote, lolote linaweza kutokea. Akajibwaga kitandani na kupitiwa na usingizi.

Dakika kama ishirini baadae, fahamu zake zikarudi taratibu na alipofumbua macho moja kwa moja akatazama mlangoni na kukuta bahasha ikiwa imepenyezwa chini. Amata akajiinua na kuketi vyema kitandani, akaitazama ile bahasha,

akili yake ikazunguka kwa sekunde kadhaa, akainuka na kuiendea lakini kabla hajaiokota, akajipapasa katika nguo yake ya ndani, na kutoa gloves, akavaa katika mikono yake na kuiokota kisha akaichana taratibu. Ndani yake kulikuwa na karatasi moja ya A4, haikuwa nyeupe sana bali iliyofifia kidogo. Akaitoa taratibu na kukutana na maandishi, *'For your eyes only'*. Sentensi hii ikamshtua Amata, akakumbuka

barua aliyopewa na yule kichaa kula Dar es salaam.

Ni yeye tena au? No, huyu si kichaa, kichaa gani anayenifuata kila niendako? Akajiuliza kabla hajaifungua ile bahasha. Alichokiamua ni kutupia bahasha kitandani kisha yeye mwenyewe akaingia maliwato kujiweka sawa. Baada ya kumaliza hayo, akavaa nguo za kazi, jioni hiyo, tayari kuingia kazini. Suruari ya cadet nyeusi na fulana nyeusi

iliyombana sawia na kukijenga kifua chake kipana kionekane wazi katika macho ya wengine, juu yake akavaa kijijaketi cha kijivu juu yake, miwani na saa yake ya kisasa zote zikatiwa mwilini. Kamanda Amata akakamilika, bastola zake zikapachikwa sawia ndani ya kijaketi chake. Sasa akaichukua ile karatasi na kuifungua, tayari kujua nini kipo ndani yake: ilikuwa ramani ya kisiwa, akakiangalia lakini hakuweza

kujua mara moja ni kisiwa gani mpaka alipokutana na maandishi ‘Dassen Island’. Akaendelea kukitalii na kuona alama mbalimbali ambazo ziiwekwa ndani yake, akazielewa na akajua kuwa zina maana sana kwa kazi yake, akaikunja na kuitia mfukoni, kisha akakiacha chumba hicho na kutokomea nje.

* * *

CAPE TOWN

“Mpaka sasa sijapata taarifa yoyote kama kuna mgeni wa kumshuku katika jiji hili,” Margaritha akawaambia wanakikao, ambao walikutana usiku huo katika kasri la Mc Cain.

“Inabidi kuwa makini sana, maana hawa jamaa wajanja, wanaintelijensia wa kukodi watafika usiku huu huu na watatawanyika kwenye kona zao bila kupoteza muda, hivyo

tutegemee matunda mazuri," Mc Cain akawatoa hofu.

Mara simu ya Margaritha ikaita, akaifyatua na kutazama, kulikuwa na picha kama nne hivi za mtu mmoj ambaye alishukiwa kuwa ni mmja wa ajumbe wa mkutano huo kutoka Dar es salaam.

"Naona wameanza kufika!" akawaambia na kuwaonesha ile picha. Yeye pamoja na wenzake wakaichambua ile picha

kujiridhisha kama ni kweli au wamefananisha, mwishowe wakatuma mmoja wa vijana wao kufuatilia kwa makini mpaka hoteli anayofikia mjumbe huyo, ikafanywa hivyo. Kama kuna eneo ambalo lilikuwa na ulinzi mkali wa watu makini ni uwanja wa ndege. Kila mtu mweusi aliyetua kwa ndege alichunguzwa si kwa kushikwa bali kwa kutazamwa tu pasi nay eye kujua kuwa anachunguzwa.

"Tunahisi ndege ya saa tano usiku itakuwa na wageni wetu, maana inatoka Dar es salaam na ni Air Tanzania," ujumbe mmojawapo ukamfikia Margarita.

"Nasubiri matokeo," akajibu.

* * *

Katika Uwanja wa Ndege wa Cape Town, usiku huo, palikuwa na kash kash nyingi, kwanza ulinzi mkali wa askari polisi ambao waliwekwa maalumu kupokea wajumbe hao wa tume

ya upatanishi na kuhakikisha usalama wao. Lakini zaidi ya hapo, makachero wa WP nao walimwagwa kama wapokea mizigo kumbe walikuwa wakichunguza kila apitaye eneo hilo kwa utaalamu wa hali ya juu. Hawakutakiwa kujulikana, walitakiwa kufanya kazi zao kimya kimya. Te daughters waliondoewa Windhoek na kumwagwa Cape Town ili kuongeza nguvu hasa kwenye mahoteli na klabu za usiku.

Kama walivyotoa taarifa, usiku wa siku hiyo ndege ya ATC Boeing Dreamliner ilitua katika uwanja huo ikiwa ni moja ya safari zake za kila wiki kutoka Dar mpaka Cape Town. Macho yote ya kikachero yalitazama kila abiria anayeshuka kwa ukaribu zaidi. Katika abiria wote zaidi ya 200 waliwagundua wawili tu ambao hata hawakutumia nguvu kujificha kwani hata magari yaliyokuja kuwachukua yalikuwa ya Ubalozi wa Tanzania katika

nchi hiyo. Kazi ilikuwa ngumu lakini vijana waliendelea kuhakikisha wanakodoa macho.

Huko katika mahoteli nako, warembo wa The Daughters nao walikuwa wametingwa kuhakikisha kila wanayemshuku wanamchunguza kwa kina kwa kutumia njia mbalimbali za kike. Wengine walikuwa wahudumu mapokezi, wengine wahudumu vyumbani na kadhalika. Kwenye klabu za usiku nako hakukuwa

nyuma, makachero wa siri walikuwepo, wadada wacheza uch* hawakuwa nyuma lakini walikuwa kwa kazi maaluzmu si kunengua tu.

Kama ni kubana njia basi WP walifanikiwa barabara kwa maana hawakuacha hata mwanya wa mshukiwa kuingia, endapo angekwepa hapa, basi angenasa pale, kazi ipo.

* * *

Wakati ulinzi mkali ukiwa umeweka katika Jiji la Cape Town, Kamanda Amata aliingia bila tabu ndani ya hoteli ya Intercontinental katika Jiji la Windhoek ambapo chumba namba 250 kilikuwa kwa ajili ya mkutano wao.

Hakuwa peke yake, katika chumba hicho alikutana na Chiba wa Chiba akiwa tayari katulia mezani na kipakatilishi chake.

“Kuna wengine wawili wanapaswa kuwa hapa ndani ya dakika kumi hizi!” Chiba akamwambia Amata.

“Sawa, ulifika salama lakini?”

“Bila shaka na hapa nasubiri tu kazi ianze, nina uchungu sana na hawa majahili,” Chiba akajibu, “naona umejibadili vya kutosha, hata tukiachana hapa hawa jamaa hawatakukumbuka tena,” akaongeza.

Chiba aliyasema maneno haya baada ya kumwona Amata jinsi alivyojibadili muonekano wake, wote wawili walipaswa kujibadili si tu kuwakwepa adui, bali hata vijana waliojiunga nao kutokea JW, special Force, wasiwatambue uraiani kwa haikutakiwa kuwa hivyo.

“Tumeshawatikisa vya kutosha, nina uhakika sasa wanahaha kutusaka,” Amata akasema huku akikaa kitini.

“Unaambiwa kuna makachero wengi mpaka wa kukodi na wamejiingiza kwenye Nyanja zote ambazo wana wasiwasi kuwa tutazitumia. Laity wangejua kuwa tupo Windhoek wasingejisumbua,” Chiba akajibu.

“Taarifa yoyote…”

“Madam S ataingia Cape Town, kesho asubuhi, Scoba, Gina na Jasmine wameingia usiku huu na wameshatawanyika katika

jiji hilo na kuanza kutega huku na huko," Chiba akajibu.

"Safi sana! Nilijua kwa njia ile, si rahisi kuwagundua, imefaulu, thank God!" Amata akajibu kwa furaha. Wakati huo huo mlango ukagongwa kwa jinsi yake, Chiba akakohoa mara tatu na mlango ukafunguliwa. Kijana mrefu wa kadiri, mweusi mwenye mwili mkakamavu, akaingia, Amata akampa ishara ya kuketi kwenye kiti kingine naye akafanya hivyo.

“Karibu!” Chiba akamkaribisha.

“Asante nimefika!” akajibu.

“ID!” akamwambia.

“Joru! Yaani Joseph Rutashobya!” yule kijana akajibu na kutulia kimya. Kamanda Amata akakaza macho kumwangalia, hakumuuliza lakini alihisi anamkumbuka, akavuta kumbukumbu na baadae akakumbuka ni wapi alimwona, katikati ya Msitu wa Mpumbutu

huko Mashariki mwa nchi ya DRC, akatikisa kichwa juu chini yaani akakubali. Mara tena hodi nyingine ikagongwa, Chiba akakohoa tena na mlango ukafunguliwa. Hapa akaingia kijana mtanashati, hakuonekana mtu wa shari bali umakini wake ulitambulishwa kwa macho yake yanayozunguka harakaharaka. Amata akamsoma na kumgundua kuwa ana uwezo wa mkubwa wa kumsoma binadamu mwingine kwa kumwangalia tu.

Akakaribishwa na kuketi, timu ikatimia.

"ID!" Chiba akauliza.

"Ghost! John Mlolele!" akajibu na kutulia kimya. Kama ungepata nafasi ya kuwatazama watu hawa wane, ungesema Chiba ndo mwenyeji na wengine ni wageni wasiojuana, Joru na Ghost ijapokuwa walitoka kambi moja lakini hawakuonesha kufahamiana kabisa.

“Tupo katika misheni, na misheni hii tunaipa jina *‘Operesheni Mbwa Mwitu’*, inabidi kama inawezekana kuimaliza kabla ya keshokutwa saa nne asubuhi. Na tutaianza kesho mchana mambo yakikaa sawa. Mpango upo hivi, tunaingia Kisiwa cha Dassen kilichopo Afrika Kusini bila mtu kujua, pale tunaenda kuwaokoa ndugu zetu waliwekwa matesoni kwa zaidi ya miaka ishirini sasa, uchunguzi umetuhakikishia kuwa

wapo. Ikitukuta saa nne asubuhi kule basi tuchukulie kuwa peresheni imefeli… sawa?”
Chiba akaeleza.

“Timamu!” Joru akaitika.

Kamanda Amata akatoa ile ramani na kuiweka mezani, wote wakaikodolea macho… “Hapa ndipo tunatakiwa kufika, kisiwa hichi kina nyuma tatu tu, na unaweza kuona hizi alama … najua mnajua maana yake…”

“Ndiyo, ni mabomu yaliyotegwa ardhini!” Ghost akamjibu Amata.

“Yes! Kwa maana hiyo tahadhari inatakiwa, kisiwa ni kidogo na kuna mabomu kama 7000 hivi kukizunguka … hapa kwenye hili jengo ndipo ilipo *target* yetu, kwa hiyo tutapalenga hapa zaidi,” Amata akaeleza.

“Ulinzi ni wastani tu, si wa kutisha kwa sababu wanaamini mitambo zaidi kuliko binadamu,

hivyo tunategemea mitambo mingi ya kielectroniki na binadamu wa chache… tunahitaji shabaha ya hali ya juu ili kutungua vitu kama mbwa au wanyama wengine ambao watahatarisha kazi yetu," Chiba akaongeza.

"Kila kitu sawa?" Amata akauliza.

"Sawa imeeleweka," Ghost akajibu.

“Sasa hapa tunaondokaje na vifaa inakuwaje?” Joru akauliza.

“Kila kitu kipo sawa, tutatoka hapa sasa kuelekea Gobabis, kule tutachukua ndege na kuingia kisiwani,” Amata akaeleza.

“Hatutaonekana kwenye rada? Hawa si wajinga kusema hawana kifaa cha kutuona tukiwa angani. Nilifikiri tutumie boti kuingia…” Chiba akapendekeza.

“Hapana! Kwa kazi hii, ndege ni salama kuliko boti, nitakwambia kwa nini baadae!”

Mipango ikasukwa na kuwekwa sawa, vijana hawa wane wakawa tayari kwa kazi, “Sasa tunakwenda Gobabis, safari yetu itaanzi pale kuelekea Afrika Kusini, sawa?” Amata akawaambia.

“Sawa!” wakajibu.

Kamanda Amata akainuka na kufuatiwa na wengine, wakatoka

na kukifunga chumba hicho huku wakiwa wameacha baadhi ya vitu vyao humo. Wakashuka mpaka kaunta na Chiba akaenda kurudisha funguo akiaga kurudi baada ya siku tano kwa kuwa alikuwa na safari ya kitalii na rafiki zake. Hilo halikuwa na shida kwani katika hoteli hii kinachotakiwa ni pesa tu.

"Welcome brother!" sauti ya dereva wa gari hili la kitalii ilimlaki Amata, si kwamba

hakuwa anamjua kijana huyo, hapana, alimjua vyema na ni yeye aliyefanya mipango yote kumwita aje kwa safari hii. Ni dereva yule ambaye mara ya kwanza aliendesha gari hili hili kwa shinikizo wakati Amata akiwaokoa wajumbe wa Tume ya Upatanishi.

“Najua si mgeni na tunakoenda, sivyo?” Amata akamwambia huku akijiweka sawa kitini.

“Bila shaka, najua kuwa unahitaji kufika Gobby!” akaeleza na kutamka jina la mkoa huo kwa jinsi wanavyolikatisha wao, Gobby yaani Gobabis.

* * *

DAR ES SALAAM…

Katika jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani, Waziri mwenye dhamana alikuwa ameketi kwenye meza kubwa ya afisini kwake huku mbele yake kukiwa na watu wengine

Wazungu ambao walikuwa wametumwa kuhakikisha wanandoka na watu wao ambao wapo katika magereza ya Tanzania. Zaidi yao Kamishina wa Magereza alikuwapo pamoja na viongozi wengine wa ulinzi na usalama.

“Watu wote tayari wapo Dar es salaam katika Gereza la Ukonga!” Kamishna wa Magereza akatoa taarifa kwa Waziri.

“Na mpango wa usafiri ukoje?”

“Watasafiri kwa ndege ya jeshi usiku wa leo, hivyo kufikia kesho saa nne asubuhi watakuwa tayari Afrika Kusini,” akajibu swali la waziri huku akifunga kabrasha lake. Waziri akatoa fomu maalumu za kuachiwa wafungwa magerezani, fomu hizi zilikuwa na picha ya kila mfungwa pamoja na taarifa zake, akawakabidhi wale raia wa Kizungu.

“Hizi ni discharge form, lakini hawa wafungwa bado wapo mikononi mwetu mpaka itakaposainiwa huko kwenye kikao. Wataondoka hapa chini ya ulinzi wa Magereza mpaka watakapokabidhiwa kwa mujibu wa makubaliano,” Waziri akawaeleza wale jamaa, wakasaini zile fomu na kuchukua nakala moja moja huku wakiziacha nyingine, na mashahidi nao wakasaini, kikao hicho kifupi kikaishia hapo. Baada ya kupena

mikono na kupiga picha ya pamoja wajumbe wale wakatawanyika.

603 KJ

Saa 3:00 Usiku

Basi la kubebea wafungwa liliwasili kwatika kambi ya jeshi la wanaanga, airwing, maeneo ya Majumba Sita Ukonga. Kambi hii haikuwa mbali sana na Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa JK Nyerere na pia ni kama kilomita tatu hivi kutoka Gereza la

Ukonga. Likiwa chini ya eskoti ya askari maalum wa Magereza ‘KM’, basi lile likaegeshwa ndani kabisa ya uwanja huo. Askari wenye bunduki wakalizunguka, mwingine akafunua mlango na kuruhusu washuke ndani humo. Wakiwa na minyororo miguuni na pingu mikononi, na minyororo ile yote iliunganishwa na mnyororo mmoja iliwafanya watembee kwa mstari kueleke mahali ambapo dege kubwa la jeshi lilikuwa tayari likiwasubiri.

Ukiachana na marubani katika ndege hiyo, pia kulikuwa na makomandoo wawili na askari wa magereza wawili wenye mafunzo maalum ya kudhibiti wahalifu sugu. Kila mmoja alipketi mahala pake, ndege ile ikaondoka na kuiacha ardhi ya Tanzania.

* * *

Usiku huo huo, Kamanda Amata na kikosi chake wakawasili Gobabis, ambapo walitafuta mahala pa kukaa kwa

muda kama wa saa kumi na mbili hivi ili kuweka mipango yao ya mwisho vizuri.

“Hapa sasa tutachukua ndege jioni ya kesho, kwa hiyo tuna muda wa kama saa sita hivi kupumzika na sita nyingine kujiweka sawa, ukitaka bibi wa Kigoby haya, kazi kwako, ila kumbukeni kuna maradhi…” Amata akawaasa wakati yeye akitoka na kuwaacha hapo.

Katika viunga vya mji huo mdogo, Kamanda Amata akajikuta kwenye baa moja ya kawaida sana, haikuwa ya watu wa hadhi sana, kwa hapa kwetu tungeita kilabu labda. Amata akaingia ndani na kukuta watu wamejaa wakicheza muziki kwa kujiachia. Akapenyapenya mpaka akaifikia kaunta, ijapokuwa watu walijazana lakini alifanikiwa. Akaagiza kinywaji kinachopendwa na wengi katika nchi hiyo, *Windhoek Lager,*

akaletewa, na taratibu akaanza kukimiminia kinywani.

Muziki uliendelea, na watu walizidi kumiminika kwenye kilabu hicho, akiwa anachezea simu yake akahisi kushikwa bega la kulia, mara moja akageuka upande wa kushoto na kugongana macho na Captain Jojina Mamedelo.

“Naona umefika kwa wakati!” Jojina akamwambia Amata.

“Aaa kabisa yaani, na nafurahi kukuona!” Amata akajibu.

“We kweli mgeni, pamoja na ujanja wako umeshindwa kuijua sehemu hii?” Jojina akamtania.

“Ningeshindwa kupajua ningefikaje?” Amata akahoji.

“Swala si kufika, hebu kunywa bia yako umalize tuhame hapa…”

“Unanipeleka wapi? Nyumbani kwako au?” Amata

akaanza maswala yake ya uchokozi.

“Unapenda kwenda nyumbani kwangu ee? Huwa sikaribishi wanaume,”

“Sawa mama, nimemaliza!”

“Haya, twende!”

Amata na Jojina wakapenya tena katika watu wanaocheza muziki mpaka wakaufikia mlango fulani humohumo ndani ya kilabu hicho.

“Huku wapi?” akauliza.

“Tulia mwanaume, uoga tu!” akajibu huku akifungu mlango huo kwa kadi maalumu, baada ya kuingia kwa ndani, Amata akaona maandishi yaliyoandikwa ‘The Magic Cassino’, akakumbuka nje ya kilabu hicho kulikuwa kumeandikwa, ‘The Magic Bar’. Wakaingia kwenye lifti na kuteremka chini kama mita ishirini hivi, wakateremka. Amata alijikuta kwenye ukumbi mkubwa

wenye kila aina ya starehe, watu wengi lakini hawa hawakubanana, kila mmoja alikuwa mahali pake, wengine wakicheza Luck Wheel, wengine Poker na michezo mingine mingi.

“Hapa tunaingia wenye pesa tu!” Jojina akamwambia Amata.

“Sawa wenye pesa!” akamtania.

“Tuketi wapi?” Jojina akauliza huku akiwa ziro distance na Amata.

“We si ndiyo mwenyeji…”

“Haya baba!”

Baada ya kupita hapa na pale, huku akisalimiana na huyu na yule, mwanamke huyu akachukua ufunguo kutoka kaunta na kuingia katika moja ya milango iliyojificha sana ndani ya kasino hilo.

“Karibu!” Jojina Mamedelo, rubani wa kike wa ndege za jeshi na kukodi nchini Namibia, alimkaribisha Amata katika

chumba hicho cha wastani, chenye TV moja redio kubwa yenye muziki mzito, kitanda cha futi tatu na nusu kwa sit na kochi la mtu mmoja huku mbele yake kukiwa na kijimeza chenya kibweta cha sigara.

"Nadhani panatufaa!" Jojina akamwambia Amata.

"Yes!" Amata akajibu, huku akiwasha saa yake na kutembea kona zote za chumba hicho, Jojina hakujua haraka nini

mwenzake anafanya, kumbe yeye alikuwa akichunguza kama kuna vyombo vya kunasa sauti ndani ya chumba hicho.

“Captain Jojina! Nina shida, na ninajua ni wewe tu wa kunisaidia,” Amata akamwambia huku akiketi kitini wakati mwanamke huyo akiwa juu ya kitanda.

“Shida gani?”

“Nahitaji ndege!”

“Ndege!” Jojina akashangaa, “yaani hilo ndo la kunifanya mpaka tuje huku, si ungekuja afisini tu!” akamwambia.

“Hili swala halikutakiwa kuingia ofisini, ndiyo maana nilikwambia tuonane nje ya ofisi…,” Amata akamwambia.

“Nakusikiliza… ndege ipo, we sema unataka kwenda wapi na una shi’ngapi!”

“Kuhusu pesa usijali, cha muhimu nahitaji kuruka saa 11

jioni, kutoka hapa mpaka Kisiwa cha Dassen ni saa ngapi?" Amata akauliza.

"Kisiwa cha Dassen, Afrika Kusini?" Jojina akauliza na Amata akajibu kwa kichwa. Mwanamke huyo akachukua simu yake na kutazama kwenye ramani umbali wa kutoka hapo Gobabis mpaka kisiwani humo. Kisha akaonekana kama anayefikiria kitu… "hivi we

jamaa kwa nini unapenda utani?" akauliza.

"Utani?"

"Ndiyo utani!"

"Utani gani?"

"Wewe unajua kabisa kuwa Dassen hakuna hata barabara ya kutua ndege na nani ataniongoza kule kama si matatizo hayo?" Jojina akauliza vizuri.

"Enhee sasa umefika ninapopataka, sihitaji kutua, we

utaniacha hewani, mi nitashuka kwa parachute…" kamanda akamwambia. Captain Jojina akamkazia macho kijana huyo rijali bila kutetereka wala kupepesa macho.

"… na ujue kuwa sihitaji ndege tu ya kawaida bali ndege maalumu kwa kazi hiyo, nipo na kikosi cha watu wengine watatu, tunahitaji parachutes, na ndege ikiwezekana ya kijeshi…" Amata akamwambia.

“Ndege ya jeshi hutolewa na serikali tu, mimi huwa narusha za kukodi za mtu binafsi, ukitaka hizo hata sasa utapata kwa maana kesho sina safari,” Jojina akajibu. Amata akatulia kimya kwa jozi la sekunde.

“Nahitaji msaada wako, unipe jibu kabla ya masaa matatu kutoka sasa,” Kamanda Amata akamwambia mwanamke huyo ambaye ndiyo kwanza akajitupa kitandani na kubaki kimya.

Huu mtihani sasa! Akawaza.

“Nipe dakika 120, nitakujibu, kama sintopata hiyo ya kijeshi basi nitawapeleka kwa ya kawaida, mtachumpa tu bila shida,” akajibu na kujiinua tena, akaeti kitandani na kuichukua simu yake, akabofya namba fulani na kuiweka sikioni. Simu ilipopokelewa, akaongea kwa lugha ya kwao ambayo Amata alielewa maneno kama matano tu, kisha akakata simu.

“Twende!” akamwambia Amata.

“Wapi?”

“We mpuuzi nini! We umenambia unataka nini?” Jojina akajibu kwa hasira.

“Eeee samahani mama, twende!” Amata akaomba radhi.

* * *

Safari yao ikaishia katika kambi ya jeshi, mwendo kama wa saa moja hivi kutoka mjini

Gobabis. Ilikuwa kambi tulivu sana, haikuwa na kelele wala fujo, nyumba chache zilizojengwa mbalimbali, miti mingi ilizunguka kambi hiyo na kufanya kama kichaka kikubwa. Getini wakaruhusiwa kupita bila taabu, nyumba ya kwanza, ya pili, ya tatu wakaingia na kuegesha gari.

“Vipi mbona usiku?” sauti ikawakaribisha, Amata hakumuona hata anayeongea

yuko wapi, akajikuta tu ameshikwa bega.

"Karibuni," wakakaribishwa na yule jamaa akatangulia ndani. Amata na Jojina wamfuata kwa nyuma mpaka ndani ya nyumba hii. Hakukuwa na vitu vingi zaidi ya meza moja kubwa na viti kadhaa vya bati. Baada ya kusalimiana, Jojina akamweleza yule jamaa kila kitu kuhusu kutaka ndege.

“Captain Jojina! Hivi unajua sheria za jeshi? Na unajua wazi kuwa ndege ya jeshi ni silaha, kuirusha tu inatakiwa idhini ya Mkuu wa Majeshi siyo tu hivi hivi,” yule mtu akasema.

“Comrade!” Amata akaita, na bwana huyo akatega sikio kusikiliza, “najua hatujafahamiana vyema mi na wewe, hata Mkuu wa Majeshi wa hapa akisikia ninahitaji ndege ataidhinisha bila maswali…”

Amata akatamka. Kauli hii ikamshtua hata Captain Jojina, akamkazia macho kijana huyu.

“Ninahitaji ndege ninakwenda kwenye operesheni maalum ya kijeshi…”

“…wewe ni mwanajeshi?” akauliza.

“Ndiyo!” akajibu na kumpa kitambulisho, yule bwana akakipokea na kukitazama, kisha akamrudishia. Akameza funda la mate na kumtazama Jojina…

“umempata wapi huyu, au mmejuana vipi?”

“Alikodi ndege miezi kama mine hivi ilopita na ndipo tulipofahamiana, anaitwa Mr. Spark!” Jojina akaeleza.

“Tulikodi ndege yake kwa kuwa nilikuwa nimetoka kwenye rescue mission ya Kamati ya Upatanishi… na sasa nahitaji ndege kwa sababu nimekuja kufanya operesheni nyingine tuliyoipa jina Operesheni Mbwa

Mwitu…” maneno haya ya kamanda Amata yakaukonga moyo wa yule bwana ambaye ni mkuu wa kambi hiyo ya mafunzo jeshini, hakuwa mgeni wa harakati hii kwani yeye kama mwanausalama alijua fika kuhusu harakati za Tanzania katika kukomboa nchi za Kusini mwa Afrika.

“Kwa hilo, name naunga mkono harakati hizi, kwa nini watunyanyase hawa washenzi?

Nitakupatia ndege kesho, mnataka saa ngapi…?”

“Saa kumi na moja jioni…”

“…sawa, sasa nampa kazi huyuhuyu Captain Jojina,” akamgeukia mwanamke huyo, “sikia Captain, andaa ndege kwa ajili ya mazoezi, hakikisha ina hizo parachutes nne na vifaa vinginevyo,” akarudisha macho kwa Amata, “hilo limepita, kesho hakikisheni saa kumi mpo hapa, mengine niachieni mimi najua

nini nitafanya," akamaliza kusema, baada ya mazungumzo mafupi wakaagana na Amata akarudi mjini. Wakiwa kwenye gari lililokuwa likiendeshwa na Jojina, mwanamke huyo alianza kumhoja Amata maswali mengi kutokana nay ale aliyoyasiki katika mazungumzo yake na mkuu wake.

"Usijali Jojina, yote utayajua, nitakwambia nikirudi kwani sasa

najua itakuwa ndiyo bahati yangu kama ulivyonambia…”

“Hah! Hah! Hah! Hah! Hata sasa ukitaka utapata kwani nimekuhusudu,” Jojina akajibu.

“Sawa, nashukuru!”

* * *

Majira kama ya saa nane usiku, Kamanda Amata aliingia katika chumba walichopiga kambi yeye pamoja na wenzake. Ndani ya chumba hiki aliwakuta wote

wapo macho na chupa kadhaa za pombe zikiendelea kuteketea.

“Bora umerudi, Joru alikuwa na wasiwasi sana nikamwambia mi Kamanda namjua, hawezi kuibwa!” Chiba akasema.

“Aha! Hah! Hah!” wakaangua kicheko.

Amata akajitupa kitini na kujisevia kinywaji kilichokuwa ndani ya bilauri ya Chiba, “kunyweni ila kesho saa nane tutaondoka hapa kuelekea kusini

mwa mji huu wa Gobabis, huko tayari kuna ndege ya jeshi tutaondoka nayo kuelekea Dassen, kila kitu kipo sawa, tutaingiwa kisiwani kwa kutumia parachute na kutua baharini kisha tutapiga mbizi mpaka kisiwani. Kwa hiyo kwa hesabu za haraka haraka tutaingia kisiwani kama saa 1 usiku hivi, na kazi yetu haitachukua muda. Rescue team ipo tayari Cape Town inasubiri simu yetu tu," akawaambia.

“Safi sana! Mi napenda mipango mitamu kama hii… unanikumbusha Comoro mwaka wangu wa kwanza wa kozi hii ya SF, tulishushwa baharini kisha tukaingia kwa kupiga mbizi…” Joru akawaambia huku kinywaji kikiendelea kuteketea.

“Hii ni peresheni ya siri sana vijana, hata wakuu wa usalama huko nyumbani hawajui kinachoendelea, ni Rais peke

yake," Chiba akasema na wote wakatikisa vichwa.

"Ndiyo maana tumekuwa wapole, kwa sababu hata hatujui nini kinaendelea, si tunapelekwapelekwa tu, hata operesheni gani tunaenda kufanya hatuijui, zaidi ya kujua tu Operesheni Mbwa Mwitu," John Mlolele akatamka na wote wakatabasamu.

"Ndiyo, hii peresheni ni secret, nitakuwa nawaambia kile tu

ambacho kinatakiwa kufanywa ndani ya saa moja," Amata akawaambia. Vinywaji vikaendelea kunywewa huku wakiagiza nyama na kuletewa chumbani humo.

SIKU ILIYOFUATA

Saa 8 Mchana:

Mchana wa siku hiyo, wote walibeba vikorokoro vyao na kuiacha gesti hiyo, wakachukua gari la kukodi mpaka katika eneo

ambalo Amata alielekezwa, hapo wakakuta Landrova ya jeshi ikiwasubiri, wakakwea ndani na kuendelea na safari mpaka katika kambi ile ya jeshi ambayo jana yake tu Amata alipelekwa na Jojina.

“Hatuna muda wa kuchelewa, dakika kumi na tano zinazokuja tunaruka, kila kitu kipo ndegeni tutafanya maandalizi huko huko,” mwenyeji wao akawapa taarifa, mara hii Amata

hakumwona yule mkuu wa kambi aliyekutana naye jana, nay eye hakuona haja ya kuuliza, alichofanya ni kufanya kile kilichompeleka.

Walipoingia ndani ya ndege hiyo, walikuta mabegi makubwa manne ya kijeshi, kila moja likiwa limewekwa mahala pake, wakagawana, kila mmoja akaketi karibu na begi lake na kuanza kulichambua ndani. Kabla ndege haijaondoka, Captain Jojina

akajitokeza kutoka katika sehemu ya rubani.

“Flight yetu itachukua saa tatu na nusu, tutaruka juu futi 36000, ndani ya begi hilo kuna kila kitu yaani mavazi, parachute, pia mtapata mitungi ya gesi kwa ajili ya diving, sawa?” akawaambia.

“Sawa!!!” wakajibu na yule mwanamke akaingia tena kwenye kile kisehemu cha rubani na kuwapa ishara ya kufunga mikanda tayari kwa kuruka.

Katika ndege hiyo zaidi ya Amata, Chiba, Joru na John, kulikuwa na wanajeshi wengine watatu kwa ajili ya kusaidia hapa na pale, Jojina alikuwa akisaidiana na kijana mwingine kuiongoza ndege hiyo.

* * *

HOTELI YA JABULHANE CAPE TOWN

"Hata waweke ulinzi vipi, si tunapita tu!" Madam S akamweleza Gina.

“Nilikuwa nina wasiwasi sana kuwa tungegundulika sijui ingekuwaje…”

“Amata ni master plan.. sikutegemea kama angewapa wazo bora kama hili, sasa nasubiri wao waingie, wamesema watnipa ishara wakiingia kwenye anga la Cape Town,” Madam S akasema.

“Naomba Mungu kazi hii iishe salama!” Gina akasisitiza.

“Usijali, hii kazi ni nyepesi sana, haina hata kumwaga damu ila ni kuwatia adabu tu inapobidi,” akaongeza kusema mwanamama huyo, “kesho saa nne mkutano unaanza, muwe makini sana, hawa jamaa wanaweza kuwatumbua hata matumbo,” akamuasa.

“Ndo hivyo, wote tupo standby,” Gina akajibu.

“Mimi nitakuwa ukumbini kwenye kikao, wewe utakuwa nje

ya hoteli ukihakikisha usalama, Jasmine na Scoba watakuwa Rescue Team, na hao walobaki wapo kwenye Operesheni Mbwa Mwitu," akamwambia Gina.

Nusu saa baadae, saa yake ikamfinya kwa nguvu na kuanza kutoa ukulele kama mdudu, akaitazama akagundua kuna kijimkanda chenya ujumbe kikitokeza ndani ya saa hiyo.

“Yes! Here They are!” akakivuta kile kijimkanda na kukichomo.

Tayari tupo juu ya Cape Town tunaelekea Kisiwani Dassen,

tunategemea kutua majini saa kumi na mbili jioni… TSA 1

Ujumbe ule ukakatika hapo, Madam S akatazama saa yake ya kwenye simu, ikamwonesha kuwa ni saa kumi na moja jioni.

* * *

“Unaponambia kuwa hawa jamaa hawajaingia nchini, nashindwa kukuelewa kabisa,” Margaritha Casbarai akamwambia Owen Smith.

“Hatujaona mtu madam, picha tulizonazo, hazijafanana na mtu yeyote, mahotelini kote hakuna taarifa hata za kukosewa tu, hakuna!” Owen akajibu.

“Noooo! Don’t tell me! Hawa watu ni wajanja sana, lazima kujua kuwa tunapambana na

watu wenye weledi wa juu sana katika Nyanja ya ujasusi, nina uhakika wapo," Margaritha akabisha kabisa taarifa ya Owen. Ukimya ukajidai kwa sekunde kadhaa, kisha akavuta hatua na kuketi kwenye kiti chake cha vono.

"Owen!"

"Yes Mom!"

"Hili swala si jepesi jepesi, unajua kuwa ugeni mkubwa upo hapa, hakikisha unapata habari za

hawa watu, pia hakikisha kule kisiwani kupo vizuri, maana tukitoka hapa kesho na watu wetu, tutawapeleka Dassen kwa mapumziko kabla hatuja waingiza uraiani," Margaritha akamwambia kijana huyo.

"Hamna tabu!" akajibu.

Huo ulikuwa mtihani mkubwa sana kwa Owen Smith, alikuwa akijua wazi kuwa kuna watu wamekodiwa kutoka nje kwa ajili tu ya kutambua wote wenye

muonekano wa kikachero, lakini mpaka dakika hiyo nao hawakuwa wametambua yeyote.

Kazi ipo! Owen akawaza na kutia moto gari lake, akapotelea mjini.

* * *

KISIWA CHA DASSEN

Dassen ni kisiwa kidogo kati ya visiwa vingi kando kando ya Jiji la Cape Town, kipo kilomita kama hamsini hivi kutoka katika jiji hilo. Kati ya visiwa vingi

ambavyo makaburu walikuwa wakivitumia kufanya mambo yao ya siri yakiwemo magereza na mengineyo mengi kama kile cha Rhoden ambacho mpigania uhuru, Nelson Mandela na wenzake walifungwa, hiki nacho kiikuwa kimojawapo.

Hakikufikika kirahisi, kulikuwa na njia mbili tu za kukifikia; njia ya boti au helikopta. Katika kisiwa hiki hakukuwa na mtu mweusi, na endapo ungemwona basi ujue ama kaletwa kuuawa au

kuna mateso yanayomkabili. Hakikuwa kisiwa cha mchezo bali ngome ya mateso kwa kila mtu mweusi.

Katika kisiwa hiki kulikuwa na nyumba nne tu, zte za mfuto, yaani si za ghorofa, ardhi iliyokosa mimea ilisambaa pande zote. Katika kingo za kisiwa hicho yaani mita kumi kutoka baharini pande zote kuliwekwa seng'enge maalumu yenye umeme mkali. Kila saa nne usiku,

mbwa wakali wenye mafunzo maalumu walikuwa katika kona tofauti za kisiwa hicho, usingeweza kuwaona kwa sababu hawakuwa wakitoka ovyo ijapokuwa hawakufungwa. Walikuwa mbwa hatari sana kwa mtu yeyote ambaye angekivamia kisiwa hicho pasi na ruhusa. Juu ya nyumba moja kulikuwa na kifaa maalumu ya kutazama kama kuna adui anayekuja katika kisiwa hicho, helikopta na boti zao zote zilikuwa na ishara maalum

ambayo mitambo hiyo ilizitambua.

Kama hakuna kikao au tafrija, basi kisiwa hiki hubakiwa na watu nane tu wanaokitunza ambao huenda mjini kwa shughuli maalumu tu. Moja kati ya majengo hayo lilikuwa ni 'lock up' ndogo ambayo mateso yake hayasemeki. Lock up hiyo ilikuwa chini ya jengo hilo, ilikuwa na vyumba kama kumi na nne hivi vyenye madirisha madogo sana

yanayoweza kukuruhusu kuona mwale wa jua kama yakifunguliwa. Humu ndimo walimoswekwa ndugu zetu, weusi wenzentu, makachero wetu waliokuwa wakiwatetea weusi wenzao katika kuzikomboa nchi za kusini mwa Afrika. Katika jengo lingine kulikuwa na chumba kidogo ambacho kiliwekwa mitambo inayotazama kisiwa kizima ndani na nje pia ndipo rada ile ndogo ilipofichwa. Kwa ujumla nje hakukuwa na

binadamu anayelinda, binadamu wote walikuwa ndani ya majengo hayo.

Hali ya utulivu iliendelea kukiliwaza kisiwa hicho, upepo wa bahari na mawimbi madogo madogo vilikuwa vikipiga hapa na pale. Jioni hii jua lilikuwa likitua taratibu huku mawingu yakiwahi kulificha. Ndani ya chumba kimoja ambacho kulikuwa na mitambo ile kulikuwamo watu wawili wakiwa

wametingwa kutazama luninga hii na ile, mmoja kati yao alikuwa makini sana akifuatilia kitu alichokuwa akikijua yeye.

“Davis! Davis!” akaita.

Davis aiyekuwa kwenye kiti kingine akajisukuma na kuifikia meza ya mwenzi wake huyo, “sema!” akamwambia.

“Listen Carefully,” akamwambia huku akimvalisha vifaa vya kusikiliza masikioni. Davis akatulia kusikiliza mara

akakunja sura, mara akakunjua ilimradi tu alikuwa kama hajielewi, akavua kile kifaa na kumtazama mwenzake.

“Mbona ni sauti za kawaida tu?” akamuuliza.

“Hapana, unajua hapa ndege huwa zinapita mbali sana, lakini tazama hii vibration…” akamwambia na kumwonesha kwenye luninga kubwa pembeni yao iliyokuwa ikionesha michoro mingi ikipitapita. Davis akatikisa

kichwa juu chini kuonesha kuwa amekubaliana na huyo jamaa yake.

“Sasa tufanyeje?” yule jamaa akauliza kwa maana Davis ndiye alikuwa na usemi wa mwisho katika swala kama hilo.

“Subiri tuone uelekeo kama ni huu au vipi!” Davis akatoa ushauri na yule mwenzake akaukubali na kutulia kitini akifuatilia nyendo za ndege hiyo.

* * *

Kamanda Amata, Chiba wa Chiba, Joseph Rutashobya, John Mlolele walikuwa tayari kwa mruko kutoka ndani ya dege hilo na kutua chini tayari kwa uvamizi. Walivaa nguo maalumu za kijeshi zinazotumika kwenye shughuli kama hizi, helmeti vichwani mwao, begi yenye parachute ilikuwa mgongoni mwa kila mmoja huku mitungi miwili ya gesi kwa ajili ya kupiga mbizi iliwatulia. Zaidi ya hapo kila mmoja alikuwa kava viatu

vya kuogelea yaani ‘miguu ya bata’. Kepteni Jojina akatoka kwenye kiti chake na kusogea mpaka kwa vijana hao, mara hii kichwani mwake alikuwa na helmeti maalumu, akasogea karibu na mlango wa nyuma kabisa ambao hutumika kupakilia mizigo, akachukua moja ya mkanda katika nguo yake na kuupachika kwenye hook ya kazi hiyo ambayo iliungwa kwenye bodi ya ndege.

“Aarree yyoouu rreeaaddyy!!” akawauliza kwa kelele.

“Yyyeeessss!!!” wakajibu na kusimama wima, wakasogea mpaka karibu na mlango. Mwanajeshi mwingine aliyekuwepo kwenye ndege hiyo akaufungua mlango na giza la nje likaanza kuonekana.

“Gguuyyss! Kkuummbbuukkeennii kkuuwwaa ssaassaa nnii uussiikkuu, hhaallii yyaa

hheewwaa ssii ssaawwaa nnaa mmcchhaannaa, kkiissiiwwaa kkiippoo Kkuussiinnii, mmuuwwee mmaakkiinnii nnaa mmrruuddii nnaa ddhhaakkaarrii zzeennuu!!" Jojina akawaambia kwa kelele kutoka na mvumo mkali wa upepo na kelele za injini. Jojina akajivuta mpaka alipokuwa amesimama Amata akambusu, "I love you Mr Spark, ukirudi utaikuta zawadi yako," akamwambia kisha akasogea pembeni.

Kikosi cha watu wane kikajitupa nje ya ndege hiyo na kuanza kuyakata mawingu na upepo mkali kuelea duniani na kuliacha lile dege likiendelea na safari. Iliwachukua dakika kama dakika arobaini na tano kufika eneo ambalo wangeweza kufyatua ile miamvuli. Kama walivyokubaliana, Kamanda Amata akatoa ishara na wote wakavuta vibanio vya mabegi yao, miamvuli ikafyatuka na

kuwanya waanze kuelea taratibu kuteremka chini.

Punde si punde, kishindo kikasikika juu ya maji ya Bahari ya Atlantiki, Amata na wenzake wakatua majini na kupiga mbizi huku wakivua yale maparachuti na kuyaacha juu yake. Amata akaitazama saa yake, akaiweka sawa nayo ikamwonesha uelekeo wa Kusini, safari ya maji kwa maji ikaanza kukielekea Kisiwa cha Dassen.

* * *

“Davis! Davis!” yule jamaa akaita tena. Davis akasogea mpaka pale, “vipi?”

“Four Star!” akamwambia, akimaanisha kuwa ameona nyota nne yaani watu au vitu vine vikiwa angani.

“Mbona mi sivioni?” Davia akauliza.

“Nimeviona kabisa hapa yani!” akasisitiza.

“Hebu washa *underwater camera* tujiridhishe,” Davis akamwambia. Camera ambazo zimefungwa chini ya maji zikapewa uhai, zikaanza kugeuka huku na huku zikinasa kila zinachokiona na kupeleka picha hizo mpaka ndani ya kile chumba. Jamaa ndani ya chumba kile akazungushazungusha tufe la kuiongozea kamera hiyo ndogo yanye nguvu lakini hakuona kitu.

“Nimekwambia hakuna kitu, macho yako tu!” Davis akamwambia.

“Hapana, mi si mgeni wa kazi hii, kama hakuna *foreign objects* katika himaya yetu sijui,” akazidi kumwabia Davis ambaye tayari alikwishakuketi kwenye kiti chake akiendelea kufanya kazi nyingine.

* * *

Kamanda Amata aliendelea kuikazia macho ile kamera kule majini huku akiwa juu yake kama

mita tatu hivi. Wakiwa wameshikana mikono kwa mtindo ambao hata ungewaona usingegundua kuwa ni binadamu, waliganda hapo kwa jozi la dakika, kisa Amata akatoa ishara ya kuteremka chini, wakafanya hivyo mpaka usawa wa ile kamera wakaipita kwa ustadi na kuufikia mlango mkubwa wenye tundu la kuweza kupitrisha RAV 4. Kwa ishara ya vidole, Amata akawaamuru kuingia katika tundu hilo, wakaingia kwa zamu na yeye

akawa wa mwisho. Giza kwenye tundu hili lilikuwa totoro, ni vifaa vya kisasa walivyokuwa navyo ndivyo viliwawezesha kuona. Wakaendelea kwenda taratibu bado wakiwa ndani ya maji na kufika mahala ambapo hapakuwa na njia tena ila ngazi mbili zilizokuwa zikielekea juu.

Amata akaonesha ishara ya kuwa wawili waende na ngazi hiyo na wawili wasubiri kujua nini kitatokea. Yeye mwenyewe

akakamata ngazi ile na kukwea juu kidogo kisha akavua madude yake ya hewa kwa kuwa alikuwa tayari kayaacha maji chini, mwisho wa ngazi hiyo kulikuwa na kitu kama mfuniko, akakisukuma taratibu na kuhisi uzito juu yake. Nyuma yake tayari Joru alikuwa amefuatia.

* * *

“Piiiiiip! Piiiiiip! Piiiiiip!” kelele ya alarm ikasikia ndani ya chumba kile walimokuwa akina

Davis. Davisa kwa haraka akakisukuma kiti chake mpaka kwa jamaa yake.

“Vipi?” akauliza.

“Tuna wageni wamekuja kututembela,” akamjibu.

Davis, akajisukuma tena mpaka kwenye meza yake na kuinua mkono wa simu, “Attention please, we have unexpected visitors, be in your position!” akakata simu, akiwa

tayari keshatoa taarifa kwa watu wote walio ndani ya kisiwa hicho.

Yule mwenzake akaminya nobu moja ambayo iliyaondoa maji yote ndani ya ile njia ambayo Amata na wenzake walipita. Kisha akawasha taa kali sana ambazo nazo zimefungwa ndani humohumo, akawasha runinga nyingine kutazama kuna nini au nani katika njia hiyo, hakuona kitu zaidi ya weusi

mzito, akajaribu tena na tena, peupe.

* * *

Mara baada ya kuona maji yale yakivutwa kwa nguvu kutoka ndani njia ile Chiba akamwamuru John Mlolele kukwea ngazi kupandisha juu, nay eye akafuatia lakini akikaribia juu akagundua kuwa ndani humo kuna kamera, akanyofoa waya na kuishia juu ya ardhi ambapo alikutana na bonge la jibwa mithili ya samba

likiunguruma mbele yake, akagwaya na kutazama huku na kule, hakuona mtu. Jibwa namba moja tayari lilikuwa kazini, lilikwishaamuriwa kutoka katika seli yake na kushambulia.

"Chiba yupo matatani!" Joru akamwambia Amata wakiwa wamejificha kwenye pipa kubwa lenye mafuta machafu. Hii ndiyo ilikuwa bahati yao, kwani kwa kulowa mafuta yale ndipo walipompoteza mbwa yule kwa

kushindwa kutambua harufu ya mwanadamu, na kisha mnyama huyo akaenda moja kwa moja kwenye tundu ambalo watu hawa wanaibukia na kukutana na Chiba uso kwa uso.

"John zima taa! Mimi nashambulia mbwa huyu, Joru tulinde," Amata akasema, na wote wakasikia kwa vifaa vyao vya masikioni.

Baada ya kuhesabu mpaka tatu, wakatoka nje, John akiwa

ametulia na Mashine Gun yake, alizitungua taa moja moja kwa ustadi mkubwa akihakikisha kuwa hakuna risasi inayopotea bila kazi. Kamanda Amata alichuma nje na kupiga sarakasi alipotua chini alishuhudia jibwa lie likiwa hewani kumvami Chiba aliyekuwa ameinuka tayari kuokoa maisha yake. Akachomoa bisu lake katika kiatu cha kulia, na kulirusha, shabaha hakikukosea kwani lilididimia

kwenye shingo ya jibwa lile nalo likatua ardhini likitapatapa.

Hakuna sekunde ya kupoteza, Chiba akachomoka na kujificha kwenye jumba moja kando yake, akatazama jinsi nyaya za umeme zilizvyopita na kugundua kuwa huko aliko ndiko kwenye chanzo kikuu cha umeme, power house. Akavuta hatua na kuuendea mlango, kabla hajafanya chochote, akagutushwa na sauti nzito.

“Hapohapo, sintosita kukuua kama utajitikisa kwa namna yoyote ile!” sauti ikamwamuru, Chiba akatulia na mara akahisi domo la bunduki likiwa limetua mgongoni mwake.

Pamoja na taa kuzimwa, Amata alisikia sauti za watu wakija upande huo, mara milio ya risasi ikasikika, akajitupa upande wa pili na kuingia ndani ya kasha kubwa la mbao na kuangukia vitu vigumu vyenye maumbo kama

nazi. Akajaribu kuvipapasa harakaharaka akagundua kuwa kaingia kwenye kasha la kuifadhia mabaki ya binadamu, na haya ni mafuvu ya muda mrefu. Mwili mwake ukamuingia ganzi, akatulia tuli huku akihisi vinyweleo vikimsisimka.

Nishapata laana! Akawaza.

"They were four of them! Find another one!"

Kamanda Amata akasikia sauti hiyo akajua moja kwa moja

wenzake wamekamatwa, kazi ipo. Akasubiri kama dakika kumi hivi, utulivu ukarudi.

"Kill them, leave no one!"

"Noooooooo!!!!!!!"

Sauti hizo zilimfanya Amata ashindwe kuvumilia, moyo wake ukamuuma kusikia kuwa wenzake wapo hatarini kuuawa.

Wacha nife pamoja nao, fight Amata, TSA1! Akajiambia akilini mwake, kisha akavuta pumzi ndefu na kuchomoa Shot Gun

kiunoni mwake, akaruka nje ya kasha lile na kutua kwa kishindo, akajiviringa mpaka kwenye ubavu wa kibanda kimoja kidogo. Akiwa katulia akasikia michakacho ya miguu ya mnyama wa miguu mine. Michakacho ile ikatulia, Amata hakusikia chochote, akatupa jicho huku na huko, hakuona kitu zaidi ya giza na mwanga hafifu wa taa chache.

Nyuma tu ya banda hilo kulikuwa na jibwa kubwa likiwa

linavuta hatua za taratibu kumvamia Amata ambaye bado alikuwa hajaliona. Akatoka pale alipo kwa haraka na kuhamia upande wa pili, kwa kitendo kile akalipotezea shabaha lile jibwa lililokuwa tayari kushambulia. Kamanda Amata akahisi hatari, alipogeuka nyuma tu akakutana uso kwa uso na jibwa hilo ambalo tayari lilikuwa kwenye shambulizi. Hakuwa na jinsi akajikuta akilidaka huku domo lake likiwa tayari kukamata

shingo ya binadamu. Amata akaligeuza na kuanguka nalo chini. Haraka akainuka lakini akasikia maumivu makali mguuni kwake, tayari meno ya mbwa yalikwishazama kwenye nyama ya kigimbi, akajiangusha na kutumia mguu mwingine kulipiga teke kali, lile jibwa likamwachia, akachomoa bisu lake na kulisubiri, lilipotaka kushambulia tena, akalirushia kisu kwa ustadi lakini akashangaa jibwa lile likiepa jisu lile.

“Shabashhh!!!” akatoa unyende na kuvuta hatua kuliendea wakakutana katikati. Pigo moja matata sana likalizimisha bila kelele.

Ndiyo maana uliumbwa mbwa, mbwa we! Akaliambia kimoyomoyo. Muda huo huo akasikia vishindo vya watu wakija upande huo akawasubiri kwa hamu, lakini maumivu ya mguu wake yakawa yanamnyima raha kabisa.

* * *

Watu watatu wakajitokeza wote wazungu, wakasimama wakitazama huku na kule wasimwona Amata. Kisha wagawana mmoja akabaki pale na wawili wakatawanyika mmoja akaenda upande huu wa kibanda na mwingine akaja kulitazama lile jibwa likiwa chini hoi.

Amata akachomoa shot gun yake na kumwaga njugu yule jamaa akaenda chini hana uhai,

akajitokeza na kumtungua mwingine nay eye akaenda chini bila ubishi. Yule wa tatu akafyatua risasi bila kuangalia, tayari Amata alikuwa amehama eneo hilo na kwenda upande mwingine, akaruka na kutua na pigo zito akampeleka yule jamaa chini na kumkaba koo kwa kono lake huku gotile likiwa katika uti wa mgongo jamaa huyo.

"Mko wangapi?" akamwuliza.

“Usitake khujhuaaaa!!!” akajibu huku akikoroma, Amata hakutaka mchezo akamzungusha shingo kwa nguvu na kumwacha marehemu. Akavua kombati lake na kuvua fulana, akaichana katikati na kujifunga mguu wake uliokuwa ukitoka damu, kisha akaishusha suruali vizuri, na kuvaa tena lile kombati lake.

For my people, For my nation! Akarudia kiapo chake cha kazi, akainuka na kuzunguka nyuma ya

banda lile, akagundua kuwa hapo ndipo mitambo mingi ilipo, umeme, simu, na kila kitu, hakupoteza muda, akachukua grunet na kuondoa pini ya usalama akarudi nyuma na kurushia. Mlipuko mkubwa ukatokea, kile kibanda kikasambaratika na kisiwa chote kika wa giza tupu. Amata akakimbia kutoka pale alipo mpaka kwenye moja ya majumba mawili makubwa yaliyopo kisiwani hapo.

* * *

Mitambo ikakatika ghafla ndani ya chumba cha mawasiliano, Davis na jamaa yake wakabaki wameduwaa.

“Tutafanyaje maana ndiyo kwanza nilikuwa nataka kutoa taarifa Cape Town,” mwenzake na Davis akasema.

“Hakuna cha kufanya, ni kuwaua washenzi hawa, twende!” Davis akamwamuru mwenzake, wakachukua bunduki na kutoka

nje, kule wakawakuta mateka wao wamefungwa kamba, lakini wenzao hawakuwaona, giza nalo lilikuwa ni kikwazo kingine kwao. Davis akapita mbinja, ikajibiwa upande wa pili. Mara watu watatu wakaungana nao.

"Hatutakiwi kupoteza muda, Brian na Snardeck, nendeni mkaweke ulinzi shimoni, mkikutana na yeyote hakuna maswali na kumtengenisha mwili na roho yake tu," Davis

akawaambia kisha akamgeukia mwingine.

“Ita mbwa waje wajifaidie nyama ya sokwe!” Davis akasema na mara yule jamaa akapiga kofi mara tatu, mbwa wakubwa weusi, wawili wakafika pale na kuketi wakisubiri amri.

“Ninyi ni nani? Hivi mnajua mnachokifanya?” Davis akawauliza mateka wake.

“Tunajua na tutakifanya!” Joru akajibu.

“Tunawataka ndugu zetu, tumekuja kuwachukua, mtake mistake,” Chiba akaongeza.

“Ndugu! Ninyi mna ndugu hapa?” Davis akang’aka, akapiga kidole chake na wale mbwa wakasimama, akawaamuru wawashambulie mateka wake. Joru alijiandaa tayari kwa kukabiliana na kitisho hicho, wale mbwa walipokuja kasi, kwa miguu yake miwili ingawa alikuwa amefungwa kamba,

akajitutumua na kupiga teke moja zito lililotua barabara kichwani mwa mmoja wa mbwa hao. Akatoa kelele za maumivu lakini bado akatii amri ya mkubwa wake. Akaruka tena kwa minajiri ya kuvamia lakini akiwa juu, Davis akashuhudia mbwa wake wakibwagika chini kama mizigo, wakitapatapa kupigania pumzi ya mwisho.

* * *

Bunduki ya Kamanda Amata ilishawashusha mbwa wale chini, akakutana uso kwa uso na Davis, akajificha nyuma ya jengo.

“Nileteeni roho yake yule!” Davis akaamuru, na wale jamaa wakaanza kumwandama Amata kwa risasi mfululizo. Yeye, Amata akawahi upande wa pili, kupitia dirisha kubwa la kioo akachumba na kujitoma ndani, akaanguka sebuleni na alipotua

akajikuta mbele yam tutu wa bunduki.

“Umejileta mwenyewe, nimesikia sifa zak…!” kabla hajamaliza, pigo la ghafla la Amata likatua mbavuni na kumfanya mtu huyo aliyekuwa akilinda shimo kujikunja na kuangusha silaha yake. ‘Finger’ za Amata zilikuwa zimezama kwenye mbavu za mzungu huyo.

“Im fight for my brothers!!!” akamwambia, “wako wapi,

mmewaweka wapi?" akang'aka. Yule jamaa alipojifanya ubishi tu Amata alikuwa akivuta mbavu huku damu nyingi zikimwagika, vidole vya Amata vilivyovalishwa kucha za chuma zenye ncha kali vilikuwa vimtesa jamaa huyo.

"Down to the hole!" akajibu akimwambia wapo shimoni. Ghafla Amata akamwona jamaa mwingine akiibuka kutoka kwenye ngazi zitokazo upande wa chini, jamaa yule tayari

alikuwa na bunduki mkononi, alichokifanya Amata ni kumsukuma kwa nguvu yule aliyemshika, wakapamiana na kuanguka ngazini, wakaporomoka kurudi chini huku risasi zikifyatuka ovyo.

Kule nje Davis, akamtaka kijana wake mwingine kuchunga mateka, yeye akaelekea ndani kwa tahadhari kuongeza nguvu. Nafasi hiyo ilikuwa ikisubiriwa na Joru kwa muda mrefu sana,

miguu yake mirefu ilimchota ngwala kijana yule aliyekuwa kasimama kama mita mbili hivi kutoka pale walipofungwa kamba. Yule kijana akaenda chini kama mzigo. Chiba kutoka upande wa pili akajirusha kwa ustadi kuja mbele na kitendo hicho kikafanya zile kamba ziachie, alipotua akatua na goti juu ya kolomeo la kiumbe huyo.

"We are free!!" akawaambia huku akiiinuka na kuwasaidia

wenzake hao kutoka mahali hapo. Walipokuwa nje ya kamba, wakatimua mbio kwa tahadhari kuelekea ndani ya jengo lile kubwa.

Ndani ya jengo kulikuwa na mpambano mkali. Amata alikuwa chini akigalagala huku cheko la zarau likimtoka Davis.

“Sifa zako zote leo zitatokea puani,” Davis akamwambia Amata.

“Sasa ujue ndiyo kifo chako kimefika!” Amata naye akamwambia huku akisimama. Kabla hajawa wima Davis, akaruka double ambayo kwa hesabu yake angetua kichwani mwa Amata. Bahati mbaya sana Kamanda alishaijua hesabu hiyo, akaepa kidogo na kumpa pigo moja kwenye korodani, Davis akapiga yowe kali. Amata akasimama na kujirusha kisha akatua chini mzima mzima huku guu lake likikibamiza kwa nguvu

kifua cha mwanaume huyo, akakohoa damu.

“Im fighting for my brothers!” akamwambia kuwa anapigania ndugu zake. Davis kila alipotaka kujibu akajikuata anashindwa.

Wale jamaa kule kwenye ngazi wakapata fahamu na kukurupuka kuanza kurusha risasi ovyo. Amata kwa haraka akachomoa simu ya mkononi ya Davis na kuiweka mfukoni kwake.

“Goodbye white dog!” Amata akamwambia kisha akampa pigo takatifu palepale chini, jamaa akarudisha namba. Amata akainuka haraka na kujibana nyuma ya nguzo. Mlio wa risasi ukasikika kutoka nje na yowe la maumivu likamfikia Amata. Akatamani kujitokeza lakini alijua hapo kuna watu wawili ambao wana silaha. Hana cha kufanya, akaichukua ile simu na kuirusha chini, jamaa mmoja akashtuka na kuiendea, palepale Amata

akaruka na kutua juu yake, akamkamata kwa miguu kama mwewe na kuvingirika naye sakafuni huku tayari bunduki yake keishamnyang'anya na kumtandika yule mwingine na kumwacha mfu.

Akampigiza kichwa chini, "mmebaki wangapi?" akamwuliza.

"Usssiiiinnniiiiuuuue, nitakwambia kila kitu…." Yule jamaa akaanza kulia akitetemeka.

* * *

Kule nje, John alikuwa na hali mbaya baada ya yule jamaa kufyatua risasi kutoka katika bastola yake wakati watatu hawa wakikimbilia ndani. Risasi ile ilimpata John Mlolele katika maeneo ya mgongo na kumbwaga chini vibaya. Joru hakuweza kuvumilia kitendo hicho, akarudi na kutumia bastola ile ile kumfumua kichwa mjinga huyo. Hekaheka za

kumsaidia John zikaanza, wakamvutia pemni na kuanza kumpa huduma ya kwanza. Wakati huo huo, Chiba akachezea simu yake na kuiweka karibu na kinywa chake.

"Rescue mission tafadhali," akairudia sentenzi hiyo kama mara tatu hivi.

"Roger! Roger! Rescue mission, copy and Clear!" sauti ya upande wa pili ikajibu.

* * *

Katika shamba moja kubwa la tajiri wa Kiafrika, Kusini kabisa mwa Cape Town, helkopter moja lilikuwa limeegeshwa njea ya jumba kuu kuu. Ndani ya jumba hilo kulikuwa na watu watatu tu, mzee wa makamo, ambaye ndiye mmiliki wa jumba na chombo hicho, Jasmine na Scoba.

"Tunatakiwa kwenda sasa!" Scoba akawaambia, wote wakainuka, na muda huo tayari saa ilikuwa ikisoma saa kumi

alfajiri. Scoba akisaidiana na yule mzee wakakirusha kile chombo na kukata anga kuelekea Kisiwa cha Dassen.

“Nniinna uucchhuunngguu nnaaoo ssaannaa haawwaa mmbbwwaa!” yule mzee akaongea kwa sauti kutokana na kelele za pangaboi la chombo hicho.

“Kkwwaa nniinnii?” Scoba akauliza kwa mtindo huohuo.

“Wwaammettuutteessaa ssaannaa haawwaa!!!” akajibu wakati mashine ile ikianza kukata bahari ya Atlantiki. Katika siti ya nyuma, Daktari Jasmine alikua ameketi kimya akiangalia maji ya bahari hiyo. Iliwachukua kama nusu saa hivi kukifikia kisiwa hicho.

“Haya tumefika, jiwekeni tayari,” Yule mmzee akawaambia, Scoba akaweka bastola yake sawasawa na kuipachika tena

kiunoni, Jasmini naye akafanya vivyo hivyo.

* * *

Kamanda Amata akaongozwa chini ya jingo hilo na mateka wake huku akiwa mikono juu. Wakashuka ngazi kama nne hivi, kisha wakafika kwenye mlango mmoja wa chuma.

“Fungua!” akamwambia.

“Umefungwa kaka, hapa ni mtu mmoja tu anayeweza kuufungua!”

“Nani?”

“Davis! Huyo jamaa uliyemuua hapo juu, yeye peke yake mkono wake unaweza kusens na kufungua kitasa,” mateka yule akajibu.

“Kwa nini hukunambia tangu kule?”

“Sikujua kama utahitaji kuja huku…” akajibu. Amata akajua tu kuwa mtu huyo anapoteza muda wake bure.

“Simama papa hapa, ukiondoka tu nakuua!” Amata akamwambia na kisha akapanda zile ngazi na kurudi juu. Muda huo huo Chiba akaingia akihema.

“Vipi, mbona unahema?” Amata akauliza.

“Rescue washafika, nimeiona chopa kwa mbali inasogea,” Chiba akamwambia.

“Vyema! Sasa nahangaika kufungua milango ya huko chini nahisi ndiko watu wetu walipo,”

akamwambia, “lakini jificheni kwanza muiangalie hiyo chopa isije kuwa wenye nyumba,” akaongea huku akianza kuuburuza mwili wa Davis akaiushusha ngazi bila huruma mpaka chini, alipofika pale alipomwacha mateka wake alimkuta kasimama vilevile.

“Safi sana! Sasa chukua mkono wa huyu bwege mwnzio ufungue mlango,” akamwambia yule jamaa akafanya alivyoambiwa,

mlango ukafunguka. Korido ndefu yenye giza nene ikamkaribisha. Hkuumiza kichwa, akachomoa kalamu yake yenye tochi upande mmoja na kuiwasha, kisha akamtanguliza mateka wake na kumwamuru afungue kila mlango.

* * *

Huko nje bado Joru alikuwa akihangaika na mgonjwa wakati Chiba akifanya mawasiliano na sehemu tofauti anazozijua yeye.

Hali ya John ilikuwa tete, haikuwa na tumaini la uhai hata chembe, macho yake yalikuwa hayatulii na mara ka mara mboni zake zilijificha juu.

"John! John! Johnnnnnn usife tafadhali!" Joru alijikuta akipiga kelele huku akiendele na huduma hii na ile. Lile Chopa tayari lilikuwa likiteremka taratibu katika uwanja ule, kabla hata halijafika chini, Jasmini tayari alikwisharuka na sanduku lake

maana alikwishaambiwa kuwa kuna mtu mahututi. Haraka akafika pale alipo Joru na kumkuta John akiwa nusu hai nusu mfu, hakupoteza muda, akaanza matibabu yake harakaharaka, akapima mapigo ya moyo, akafanya hiki akafanya kile. Kwenye mkoba wake humohumo akatoa chupa ya maji na kumdunga sindano mshipani.

Scoba akateremka na bunduki mkononi kuweka usalama.

“Scoba, twende bondeni!” Chiba akamwita huku akitangulia ndani ya jengo lile, wakashuka ngazi mpaka chini na kukuta ule mlango wazi.

“Kamanda!!!” Chiba akaita.

“Kaka, njoo upande huu unisaidie!” Amata akamwita Chiba.

Yule mateka alimwongoza Amata mpaka katika vyumba ambavyo kulikuwa wamefungwa watu kwa miaka na miaka.

Chumba cha kwanza chenye mlango wa chuma na kijidirisha kidogo, walimkuta mzee, mwenye nywele ndefu na mdhaifu wa mwili. Amata alisikitika sana mpaka akahisi machozi kumtoka.

"Fungua!" akamwambia mateka wake, naye akafanya alivyoagizwa, Chiba akaungana nao na kuendelea na zoezi hilo. Baada ya dakika kama kumi na tano hivi walifanikiwa kuwapata

watu kumi na mbili. Watu hao walikuwa wamedhoofika sana, hata kutembea kwao ilikuwa shida ikabidi wale wasiojiweza kabisa Amata na Chiba wawasaidie japo kuwashika huku na huku na wengine walioweza kutembea kidogo kidogo wakajitahidi hivyo hivyo.

“Wapendwa! Tunakwenda nyumbani!” Amata akawaambia wale watu, wakajaribu kutabasamu lakini ungeweza

kuona wazi kuwa hata tabasamu kwao ilikuwa shida kutokana na udhaifu waliokuwa nao.

“Siamini! Siamini! Siamini!” mmoja wa wale watu akasema kwa taabu wakati alipofika nje ya jingo lile, “Naenda nyumbani! Ooooh!” akaongeza kusema na furaha yaje haikujificha, wengine hawakusema chochote waliendelea kujivutavuta tu.

Kutoka kwenye ile helikopta, yule mzee akateremka na

kusaidiana na Chiba na Amata kuwachukua watu wale na kuwapakia ndani ya chombo hicho.

“Fanya haraka twendeeee!!!! Mahali si salama hapa!” Chiba akapiga kelele. Wote wakaingia na Amata akawa wa mwisho kuhakikisha kila kitu kimekwenda sawa.

“Hey men, do you leave me alone?” yule mateka wa Amata

akamwuliza mtesi wake kuwa anamwacha?

“Yes we do! This is your home to stay!” Amata akamjibu na kumwambia kuwa hapo ni nyumbani kwake.

Taratibu kile chombo kikaanza kuiacha ardhi huku vumbi likitimka huku na huko.

15

CAPE TOWN

Saa 4:00 asubuhi

Katika hoteli kubwa ya nyota tano iliyopewa jina la Berverly Hill watu walikuwa wamefurika, waandishi wa habari wa TV,

Radio na magazeti. Wageni anuai kutoka nchi mbalimbali walikuwa tayari wameketi katika ukumbi mkubwa wa mikutano, tayari kikao cha upatanishi kilifunguliwa na pande zote mbili zilikuwa ndani ukumbi huo na wasikilizaji kadhaa. Ulikuwa mkutano wa kihistoria ambao wengi walipenda kusikia mwisho wake, kwani waliijua historia ya mkutano huo uliodumu kwa miongo miwili na miaka kadhaa, na kwa kuwa sasa ilikuwa lazima

ifikiwe hatima kwa kuwa tayari taifa la Tanzania lilikubari kutia saini na kuwaachia wafungwa wa kikaburu waliofungwa ndani ya nchi hiyo. Na hii ilitokana na kiminyo ambacho EU iliipa Tanzania kwa miezi michache tu.

Katika upande mmoja kulikuwa kumeketiwa na watu wengine saba, wazungu ambao ngozi zao zilionekana kufifia kwa jua kali ila suti walizovaa

ziliwarudishia heshima kwa namna moja au nyingine.

Miongoni mwa wajumbe kutoka Tanzania, Madam S alikuwa katika kiti kimojawapo, akifuatilia kwa makini majadiliano na mazungumzo hayo yaliyokuwa yakiendeshwa na mjumbe maalumu kutoka Jumuia ya Nchi za Ulaya ambaye yeye alijulikana kuwa mpatanishi asiyeshindwa.

“Baada ya kuzungumza yote haya, basi tufanye lile lililotuleta hapa,” yule bwana akasema na wahudumu watatu wakaleta makabrasha fulani na kuyagawa upande huu na upande ule kwa watu ambao walionekana ndiyo wenye nyadhifa za juu. Uande wa Tanzania alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na upande wa makaburu alikuwa Sir. Mc Cain aliyetinga suti ya gharama sana. Baada ya kabrasha zile kuwekwa mezani, yule bwana akasema

tena, “pande zote mbili hazina budi kukubaliana kwa zoezi hili kabla hatujaweka saini, upande wa kwanza…”

“Tuko tayari, na tuna amani….” Mc Cain akatamka.

“Upande wa pili…”

Yule waziri hakujibu kitu badala yake alikuwa akimwangalia Mc Cain kwa jicho baya, “tunawahitaji watu wetu!” akatamka huku akigonga ngumi mezani na kuuma meno.

“Mjumbe! Serikali yako imekubalia kuwa hakuna watu wenu waliowekwa chini ya ulinzi na jumuia hii, wewe unasemaje unataka watu wako? Unapingana na Rais wako?” yule mpatanishi akamwuliza.

“Najua na ninamtii sana, ndiyo maana nikakubali kuongoza tume hii kuja hapa, nitasaini kwa sababu nimetumwa kufanya hivyo, lakini najua wazi kuwa mna watu wetu ila mnatumia

mabavu yenu kutukandamiza, ninakubali lakini sina amani!" akazungumza na kuvuta lile kabrasha.

Wakati waziri huyo akizungumza hayo, ukumbia mzima ulikuwa kimya kabisa kilichosikika zaidi ya sauti yake ni shata za kamera tu. Alipomaliza kusema hayo makofi mengi yakasikika, na wakati huo huo mwanadada mmoja wa kizungu akaingia katika ukumbi huo kwa

mwendo wa harakaharaka. Huyu alikuwa ni mmoja kati ya wahudumu wa mkutano huo, moja kwa moja akamwendea Margaritha Casbarai na kumnong'oneza jambo. Kwa mtu mwepesi wa kuangalia watu angeshajua jinsi mwanamama huyo alivyochanganyikiwa ghafla, akasimama kitini bila kuambiwa kila mtu akawa anamshangaa.

Upande wa Tanzania, Madam S alikuwa akitazama saa yake kila

wakati kana kwamba ana miadi na mtu muda fulani.

* * *

Kutoka nje ya ukumbi wa hoteli hiyo, kulisikika mngurumo wa helikopta, ndani ukumbi huu haukusikika kwa nguvu sana lakini huko nje ilikuwa ni kizaazaa. Waliokuwa nje ya hoteli wakiwamo askari wa ulinzi na usalama tayari waliinua bunduki zao kukabiliana na lolote linaloweza kutokea.

Scoba aliliteremsha dude hilo lenye sura ya kutisha katikati ya bustani kubwa ya maua, lilipotulia ardhini, Kamanda Amata akawa wa kwanza kushuka huku akichechemea maumivu ya mguu wake, nyuma yake akafuatiwa na Chiba, Joru, Jasmin na wale watu wote waliowachukua katika Kisiwa cha Dassen.

“Nifuateni!” Kamanda Amata akawaamuru huku akitangulia

mbele. Mitutu ya bunduki ilikuwa ikiwatazama. Walipofika mlango mkuu wa kuingia ndani ya hoteli hiyo ndipo kizaakizaa kiauka. Jamii ya watu weusi iliyokuwa hapo ikawa ikishangilia kwa nguvu sana na kuimba nyimbo za ukombozi. Askari watatu wa Kizungu waliokuwa juu ya farasi walizuia mlango ili Amata na watu wake wasipite.

"You are not allowed to enter inside you cockroach!" mmoja

wa wale askari akamwambia Amata aliyekuwa mbele kuwa haruhusiwi kuingia ndani. Kamnda Amata hakujibu kitu badala yake akapiga hatua nyingine kuzipanda ngazi za hoteli hiyo huku akichechemea.

“Huwezi kunipangia jinsi ya kuishi na kufanya nikiwa katika bara langu,” akajibu na kupita kwa nguvu huku watu wakishangilia na kupiga miruzi. Waandishi waliokuwa nje

wakahakikisha wanapata picha za kutosha.

Ndani ya ukumbi nako hali ikabadilika, kelele za vurugu za huko nje zilifanya mkutano usimame kwa sekunde dakika kadhaa baada ya askari walinda usalama kuja ndani na kuhakikisha usalama wa wajumbe wa mkutano huo. Sir Mc Cain akajikuta anapigwa bumbuwazi baada ya kupewa taarifa ya kilichotokea huko Dassen.

Nyimbo zilizkuwa zikiimbwa huko nje ndizo zikampa hasira zaidi na presha ikaanza kushuka.

Madam S akainua mkono wake na kuruhusu saa yake iingize ujumbe.

'Tumewaleta mashujaa, wakoloni wanatuzuia kuingia ndani,'

Ujumbe ule uliishia hapo, Madam S akaukata ule mkanda na kuutia kinywani akitabasamu.

"Our heroes are outside, let them enter!!!" akasema kwa sauti

na upande wa Tanzania wakaanza kushangilia pasi na kujali wapo kwenye kikao nyeti.

"Let them in! Let them in! Let them in! Let them in!" Kelele za wajumbe wa Tanzania zikaufunika ukumbi mzima hakuna aliyeweza kutuliza jazba hizo. Askari wakaingia ukumbini lakini wakshindwa kufanya lolote kwa sababu hawakuruhusiwa kutumia nguvu ndani ya ukumbi huo. Bi Margaritha Casbarai

alikuwa akitetemeka kwa hasira, blauzi aliyovaa ilikuwa imeanza kulowa jasho na kuondoa make up alizojipaka usoni. Sir Mc Cain alikuwa ameketi kimya huku kainamia meza yake. Tayari nyuma ya Mc Cain, Margaritha na yule mpatanishi wa EU walikuwa wamesimama wanadada wawiliwawili nyuma ya kila mmoja. Madam S alipotazama harakaharaka akajua hawa ndiyo 'The Daughters'.

* * *

Nje ya hoteli ile, Kamanda Amata alikuwa amesimama katikati ya mlango wa hoteli hiyo, AK 47 nne zilikuwa zikimtazama yeye, kombati lake lililokuwa limejaa vumbi lilimfanya aonekane kama kinyago, mguu wake uliokuwa umeumia kwa meno ya mbwa ulikuwa bado unamuuma. Hakuongea neno, alinyamaza tu akitazamana na mitutu ya bunduki zile. Unaweza

kufikiri kuwa watu waliambiwa kuwa ni nini kitatokea siku hiyo, lakini hakuna, ilitokea tu.

“Let us in!” Amata akawaambia wale askari huku akizisukuma zile bunduki huku na huku, hatua mbili mbele akakutana na mwanadada aliyevalia suti nzuri ya ofisini, hakumjua haraka lakini akahisi kuwa ni mmoja wa makatibu ndani ya mkutano huo.

“Let them in!” yule mwanadada akatamka na wale askari wakapisha njia. Kelele zikazidi nje ya hoteli ile, Kamanda Amata na watu wake wakapanda ngazi mpaka mpaka ghorofa ya tatu ambako ndiko kulikuwako na mkutano huo, mlango ukafunguliwa wakaingia ndani huku wakipigwa picha na kushangiliwa kwa nguvu na wajumbe wa Tanzania.

Madam S akashindwa kuizuia furaha yake, akatamani akambebe Amata lakini alijikuta hawezi. Kamanda Amata akatembea mpaka kwenye kipaza sauti ambacho ndicho kilituniwa na yule mpatanishi kutoka nchi za Ulaya. Baada ya kusimama tayari mbele ya chombo hicho ukumbi wote ukawa kimya kabisa.

“Tupo hapa, tumefika, lazima tukumbuke kuwa udhalimu haulipwi, kwa nini mliudanganya

ulimwengu kuwa ninyi hamna watu wetu katika magereza yenu ya siri? Hawa ni akina nani?" Amata akang'aka huku machozi yakimtoka. "Sisi siyo wajinga, mwaka 1984 mliua watu wetu saba katika nchi ya Rhodesi, isitoshe mmefanya mambo mengi sana kutudhulumu haki zetu, mkajikosha mbele ya nyuso za walimwengu kuwa ninyi hamna mawaa isipokuwa sisi, mkatuwekea na vikwazo vya kiuchumi ili tuwapatie watu

wenu, kwa nini mliikataa shreia ya kubadilishana wafungwa na mkaamua kutufanyia hivi? Tazama watu wetu, mmewatesa miaka zaidi ya 20, wakikaa kwenye vyumba vidogo vizivyo na hewa ya kutosha, mkiwalisha wadudu na gyakula visivyofaa kwa binadamu. Leo hii aibu imewashuka, wale mlioaminisha ulimwengu kuwa hawapo, na mimi nauambia ulimwengu kuwa hawa hapa, nimewatoa Dassen Island katika mazingira

yasiyosemeka. Tunawashukuru kwa wema wenu, tumewapata watu wetu, chukueni watu wenu, nah ii itawadhihirishia kuwa Tanzania sin chi ya kuichezeachezea, na wale wote waliohusika katika kuwaua wajumbe wa tume ya uatanishi mwaka 184 hatutawaacha salama lazima sheria ifuate mkondo," Amata akamaliza na kushangiliwa na wajumbe wa Tanzania.

Mkutano ukavunjika, kila mmoja akaondoka bila kuaga, hakuna aliyetia saini wala aliyekumbuka kabrasha hilo. Mc Cain akaondoka zake akisndikizwa na wale mabinti. Margaritha alikuwa akimtazama Amata kwa jicho baya.

Code 005! Akawaza na kukusanya makabrasha yake akaondoka. Mjumbe wa EU yeye akachukuliwa kwa ulinzi mkali akaondolewa ukumbini.

Madam S akamkumbatia Amata kwa nguvu huku akitokwa na machozi ya furaha kama si majonzi. Muda huo huo gari aina ya coaster ikawasili huko nje kutoka Ubalozi wa Tanzania, ikawapakia watu wake wote na safari ya kwenda uwanja wa ndege ikaanza, hawakutaka hata kubaki katika nchi hiyo.

"Umetimiza ulichoahidi!" Madam S akamnong'oneza.

“Na hicho ndio kiapo change!” akajibu huku akimwacha bosi wake na kuanza kugombaniwa na watu wale aliowaokoa, wengi walipenda kumjua kuwa yeye ni nani lakini hakuwajibu kitu zaidi ya kuwaambia kuwa yeye ni mpatanishi. Ulinzi mkali uliwaondoa wale watu haraka kuelekea kwenye gari kwamaana hawakutakiwa kuzungumza na vyombo vya habari.

* * *

Kwenye Mercedes Benz moja jeusi lenye milango sita, kulikuwa na watu watatu tu, Mc Cain, Margaritha Casbarai na mtu mwingine mwenye umri mkubwa hivi, na ungemjua tu kwa kuona makwinyanzi ya ngozi yake.

“Mmefanya nini?” akawauliza.

Hakuna aliyejibu zaidi ya ukimya tu.

“Mmenitia aibu sana, sasa tuntazamikaje mbele ya macho ya

dunia?" akaongeza swali. Bado hakuna aliyejibu swali hilo pia, "kila kitu kimeharibika, kila kitu, Dassen imefeli hakuna kiumbe kilichobaki na uhai," akazidi kuwaeleza.

Bi Margaritha Casbarai hakusema kitu akabaki akitetemeka tu huku mashavu yake yakiwa yamemshuka na kuzidi kumzeesha.

"Utusamehe!" Mc Cain akajibu na kubaki kimya tena.

“Swala si kuwasamehe, nataka nijue tutaificha vipi aibu hii mbele ya uso wa kimataifa? Tutajikosha vipi jamii ituelewe!” akalalama.

“Alfa!” Margaritha akaita.

“Usiliite jina langu bila faida, mwanamke mpumbavu wewe!” yule akajibu kwa hasira, “nataka mtekeleze jambo moja tu, na si zaidi ya saa tano kutoka sasa, yule bwana aliyeyafanya yote haya, naihitaji roho yake na hao

wengine wote nataka nisikie, kama ni mlipuko wa ndege, kama ni sijui nini, nataka nisikie sasa," akazungumza kwa hasira. Lile Benzi likaingia ndani ya jingo fulani na kuegeshwa, sakafu ya chini ya gari hiyo ikafunguka na hapo lilipoegeshwa napo pakafunguka, yule mzee akashuka na kufuata ngazi iliyoongoza chini ya jingo hilo, kisha pakajifunga na lile gari vivyo hivyo.

Casbarai na Mc Cain wakatazamana, kisha kila mmoja akashusha pumzi kwa tofauti ya sekunde kama mbili hivi.

“Unajua wajibu wako!” Mc Cain akasema.

“Yes Sir!” Margaritha akajibu.

* * *

Saa saba mchana ya siku hiyo, Watanzania kama ishirini hivi walikuwa ndani ya ndege ya jeshi la Tanzania tayari kwa safari ya nyumbani. Ndani ya ndege hiyo

nyimbo za kishujaa zilikuwa zikiimbwa, watekwa waliokombolewa walikuwa na furaha ya ajabu, waliimba sana, huku Gina akigawa bia za makopo. Madam S alimtazama mmoja wa watu hawa, akaangusha machozi.

“Simbaulanga!” akaita kwa sauti ya chini, mtu mzima yule akainua uso na kumtazama Madam S.

“Unanijua mama?” yule mtu akauliza.

“Naitwa Selina!”

“Selina?”

“Ndiyo, Selina, mwanafunzi wako, chuo cha mafunzo Mbweni…” Madam S akamwambia.

“Selina?!” akamshangaa. Simbaulanga akamkumbuka mwanamke huyu, msichana aliyemfundisha mwenyewe

mafunzo ya ushushushu katika chuo cha Mbweni.

“Nimeteseka sana, miaka 23 tekoni, Selina, kazi hii ni ngumu, si kila mtu anaweza kufanya, lazima ukumbuke kutoa sadaka maisha yako… nilikwambia mwaka ule! Unakumbuka?”

“Nakumbuka!”

“Ulinzi wan chi yetu ni jukumu letu, lazima tuwe tayari kufa na si kutoa siri za taifa letu, nimeteseka sana mimi na

wenzangu, miaka ishirini na tatu, wengine wameuawa kikatili sana, hapa sio wote Watanzania, kati yetu watanzania tupo watano tu, watatu wamekufa uko huko, Mungu awarehemu…”

“Amin!” Madam S akajibu. Mazungumzo kama ya dakika kumi hivi yakafuatia, kisha wakatakiwa kuwa tayari kwa kuruka. Kamanda Amata akasimama alipokuwa baada ya

kupata matibabu kutoka kwa Jasmin.

“Unajisikiaje sasa?” Madam S akamuuliza pindi alipokutana naye katika chumba cha nyuma kabisa cha ndege hiyo ambamo uhifadhiwa silaha na vitu vingine.

“Naendelea vyema, lakini sijamaliza kazi!” akamwambia.

“Kwa hiyo…”

“Narudi Cape Town, nategemea kuja Tanzania baada ya siku tatu nikimaliza kazi

yangu," akamwambia. Madam S akatazama chini kwa sekunde kadhaa kisha akamwangalia kijana huyo mwenye kijiamini kupita kiasi.

"Urudi ukiwa na roho yako!" akamwambia.

"Bila shaka! See you soon!" Kamanda Amata akaaga na kuvaa parachute. Pale aliposimama Madam S palikuwa na swichi maalumu ambayo ukiiminya tu mlango dharula hapo chini

unafunguka na kuruhusu watu kuruka.

"Go!" akamwambia na kuminya ile swichi, Amata akabana mikono yake vyema na kuchomoka kupitia njia hiyo.

* * *

JIONI YA SIKU HIYO HIYO…

Kando kando ya barabara kubwa ya Lower Kroof, kulikuwa na Bungalow kubwa ambalo wenye pesa zao walipenda

kupumzika. Ndani humu kila huduma ilipatikana kadiri ya mahitaji yako. Jioni hii Margaritha Casbarai alikuwa ndani ya bungalow hili kwa mapumziko akitafakari juu ya nini cha kufanya. Hakumwambia mtu yeyote kama anakuja hapa, ilikuwa ni siri yake na walinzi wake wawili ambao ni *The Daughters* tu.

Mwanamke huyu tajiri, alihitaji muda na nafasi ya kutulia ili

kutafakari hasa nini cha kufanya katika kulimaliza sakata hilo. Alihitaji kama saa tatu hivi za kupumzika kwa maana saa mbili usiku wa siku hiyo walitakiwa kukutana na kwa kikao maalumu. Akiwa amelala juu ya maji katika dimbwi kubwa la kuogelea huku wasichana wake wakiwa upande huu na ule kuhakikisha ulinzi, simu yake ya pekee ikaita. Hata kama angezima simu zote hii angeiacha wazi kwani ni simu maalumu na hupigwa na watu

maalumu. Mmoja wa wale binti akaichukua na kutazama kwenye kioo, *'Dutsan'* ikaandika.

"Hello!" sauti ile nzito ikaita, mwanamama huyo mwili ukamsisimka kwa kutekenywa na sauti hiyo, alilijua jina hilo, Dutsan, kilichomchanganya ni kuwa, aliambiwa kisiwa cha Dassen kimeharibiwa hakuna mtu aliyebaki hai, na huyu kijana anakaa huko imekuwaje awe hai.

“Ghost!” akasema kwa sauti ndogo.

“I want to see you, there is your message!” sauti hiyo ikamwambia kuwa kuna ujumbe wake.

“Who are you?” akauliza.

“Dutsan, Im only one escape from Dassen!” akajibiwa kuwa mtu huyo ni pekee aliyetoroka kutoka kisiwani. Casbarai akashusha pumzi, kabla hajajibu chochote, mlango wa bustani hiyo ukafunguliwa, mtu mmoja

akaingia akiwa na bakora ya kutembelea mkono wake wa kushoto huku ule wa kulia ukiwa ndani na simu sikioni mwake. Margaritha akahamaki, hakumjua mtu huyu, kiukweli alikuwa mtanashati, mwenye suti ya gharama, na kofia ya pama kichwani mwake. Wale mabinti wakamfikia ndani ya sekunde mbili tu, hawakutaka kuulizwa wala kuambiwa, michezo waliofanya pale ilikuwa ya kutisha. Kwa kasi ya ajabu

waliazna kumshambulia kwa kipigo mwanaume huyo huku Margaritha akitabasamu na kuvuta bilauli ya mvinyo na kuigigida mafunda makubwa mawili.

Mapigo kadha wa kadha yalimwendea mtu yule lakini cha kushangaza hakuna hata pigo moja lililomfikia mwilini yote aliyapangua kiufundi bila hata kudondosha kofia yake kichwani.

“Hamjui mnachokitaka wanawake!” akawaambia.

Margaritha akatahayari, akaketi vizuri juu ya kile kitanda na kuinua simu yake ili kuomba msaada mwingine zaidi, amechelewa! Pigo moja la kifo likampepesua yule mwanamke akajibwaga chini kama mzigo kimya. Yule wa pili, akadakwa mkono na kuzungushwa kisha ukavunjiliwa mbali, yule mtu kabla hajamwachia, akamweka

sawa na kumtwanga kichwa cha maana, akamtupia majini. Sasa akabaki uso kwa uso na huyo mama mtu mazima aliyekuwa ndani ya bikini akijipumzisha.

"Na hicho kikao watakusubiri wasikuone!" yule mtu akasema, akavua kofia yake na kuondoa sura ya bandia.

"Datsun!" Margaritha akashangaa na kutaja jina hilo.

"Datsun? Niite Amata Ric, Kamanda Amata, mimi ni

kiumbe wa mwisho kuonwa na macho yako… umetesa watu wetu, nimetumwa kuitoa roho yako," Amata akamwambia. Margaitha akaanza kutweta kama mbwa aliyekimbizwa.

"Pliz pliz, nitakupa chochote utakacho kijana, niache hai tafadhali…" akalalama.

"Sijawahi! Kumwacha mdhalimu kama wewe akiendelea kupumua, utalipa roho za watanzania walikufa kwa mkono

wako mwaka 1984 pale Rhodesia. Lazima ujue na ukumbuke kuwa mshahara wa dhambi ni mauti…”

“No no no usiniue nitakupa siri zote utakazo hata mwili wangu chukua,” akaendelea kujibaraguza.

“Siuhitaji mwili wako uliochoka kwa kuchezewachezewa na watu wa ajabu ajabu, kama ni siri zenu zote ninazo, ukibahatika kuwa

hai waambie ndugu zako wa WP kuwa, Kermikov ninae mimi, Bih ameuawa na Kermikov…”
Amata akamwambia huku akiinua ile fimbo yake akaifyatua kwa namna yake na kitu kama msumari kikatoka na kudidimia moyoni mwa mwanamama huyo.

“Shhhh….” Hakumaliza, msumari mwingine ukazama katikati ya paji la uso, akaegemea kitanda chake na kutulia kimya.

Akageuka na kuondoka zake taratibu, nje ya jingo hilo akaingia kwenye gari lake na kuondoka kwa kasi, ile simu akaitupa dirishani kwani mmiliki wake alishafia Dassen, alichokifanya yeye ni kuitumia kwa kupata muelekeo tu wa wapi adui wake alipo.

* * *

HOTELI YA CAPE LOYALE

Ratiba yote aliijua kuwa usiku huo kuna kikao cha dharula

katika hoteli hiyo, mara baada ya kumalizana na Margaritha na kumpumzisha kwa amani. Akilini mwake alipanga tu kuwa atawatikisa kwa kumwondosha mwanamke huyo, na akajua kwa vyovyote vile kikao hicho kitakuwa kichungu kwani mjumbe mkubwa atakutwa amekufa ndani ya dimbwi la kuogelea tena akiwa na bikini. Mpango ulikuwa hivi, baada ya kumaliza kikao chao basi iwe zamu ya kumwondosha

mwingine ili kama kuna ahadi nyingine basi wakutane na hewa.

Alikuwa pale mapema tu, akamwona Mc Caina akiwasili na kuingia katika hoteli hiyo, hakufanya papara, akasubiri kama saa nzima baadae akajua kuwa sasa huko kikao kipo katikati. Kwa mwendo wa taratibu akaliendea gari lile, kwa kutumia kifaa maalumu aliweza kupata codes za kuifunga alam ya usalama ya gari hiyo kisha

akafungua na kuchukua kijichupa chake kidogo, akakifyatua mfuniko na kukirushia ndani kisha akalifunga gari lile. Yeye akarudi garini mwake na kusubiri. Baada ya saa jingine moja aliona watu hao wenye pesa wakitoka na kuchukua magari yao ya kifahari sana na kuanza kuondoka, Mc Cain akiwa mmoja wao. Amata akawasha gari na kumfuata nyuma taratibu kabisa huku akipiga mruzi.

Gari la Mc Cain likaacha barabar kuu na kuingia ile ya Ebenezer kuelekea bandarini, huko likaacha barabara ya bandari na kuchukua ile ya Dock, lakini ghafla, lile gari likasimama na Mc Cain akashuka huku akijikuna kama mtu anayetafuta kitu katika mwili wake. Kamanda Amata akasogea na gari lake taratibu kwa maana alijua tu kuwa kuna sehemu atamkuta anajikuna na kweli ikawa, akamwashia taa na kumpigia

honi, bado mzungu yule aliendelea kujikuna huku tayari keshavua shati. Amata akashuka huku taa za gari lake zikiendelea kummulika, akatembea mpaka pale.

"Is your turn now!" akamwambia akimaanisha kuwa ni zamu yake.

Mc Cain akashtuka na kumtazama mtu huyo aliyevalia suti maridadi n afimbo yake ya kutembelea mkononi.

“Who are you!?” Mc Cain akauliza huku bado akijikuna.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Mimi ni Amata Ric, TSA 1, Code 005,” akamjibu. Mzee yule hata kule kuwasha kukatulia ghafla.

“You?” akauliza huku akimsogelea.

Alipomkaribia, Kamanda Amata akamtandika ngumi moja nzito, ikampeleka hadi kwenye gari lake, akajibamiza na kujikuta amekaa chini, tayari damu puani

zinamchuruzika. Amata akamwendea, kutoka mfuko wake mmoja akachukua gloves na kuvaa, ile fimbo akaibana kwapani. Akamwendea pale alipoketi na kumzaba kofi, kisha akamkamata mkanda wa suruali yake na kumnyanyua kwa kono moja tu mpaka kwenye buti la gari lake akamtuapia ndani na kufunga, kisha akaingia gari na kuondoka kwa kasi.

Kamanda Amata aliendesha kwa kasi kadiri ya dakika thelathini hivi, akawasili anapopataka, akaiacha barabara na kuingia kwenye vichaka kidogo, akashuka na kufungua buti, akamtoa mtu wake na kumtupa chini kando ya barabara.

“Wale jamaa uliowaua kwa amri yako ukiwa waziri kule Rhodesia wamenituma nikutie displini, na wale uliowafunga kule

Dassen kwa kujifanya una mamlaka kuliko dola nao wamenambi nikutenganishe kiungo kimoja baada ya kingine kama kisasi. Na mimi mwenyewe kwa sababu mbwa wako ameniumiza mguu lazima nikuadhibu, maiti yako itaokotwa na wapiti njia asubuhi ya kesho," akamwambia na ghafla akamtandika konde lingine la maana, mtu mzima yule akaenda chini, masikini hakuwa na nguvu ya kujitetea.

“Udhalimu haulipwi! Msalimie mpenzi wako Margaritha…” akamwambia na kisha akachomoa bastola aina ya Magnum 22 na wala hakuifunga kiwambo cha sauti. Akaifyatua bila huruma na risasi moja tu ikakiharibu kichwa cha mtu huyo.

It is accomplished! Akajisemea moyoni mwake akimaanisha yametimia.

Akaingia garini, simu yake ikaita, akainyanyua na kuitazama kiooni, 'Jojina' ikasomeka. Akaiweka pembeni na kuwasha gari kisha akaondoka kwa spidi zote kuelekea uwanja wa ndege kwani tayari *Capt.* Jojina alikwishafika kumchukua kwa ndege ya kukodi.

* * *

"Umefanikiwa?" Jojina akamwuliza wakati tayari ndege

ile ndogo ya kisasa ikiwa hewani ikikata anga kuelekea Namibia.

“Bado kitu kimoja!” akajibu huku akijiweka sawa katika kiti kikubwa akimtazama mwanamke huyo mwenye umbo la Kiafrika haswa akiwa kasimama mbele yake na chupa ya pombe mkononi huku ndege hiyo ikiwa katika *Auto Pilot*.

“Kitu gani?” Jojina akauliza.

“Nitashangaa sana kama ni kweli hukijui, hebu njoo

nikunong'oneze.," akamwambia na mwanamke yule akasogea na kumwinamia, Amata akamshika mabegani na kumvuta chini kwa nguvu, vinywa vyao vikakutana, wakabingirishana kitini huku chupa ile nayo ikijiweka kando kupisha kile kinachoendelea.

MWISHO